

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kwanza – Tarehe 1 Novemba, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Nne wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa wa mwaka 2016(*The Access to Information Bill 2016*);

(ii) Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016*);

(iii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa mwaka 2016 (*The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016*);

(iv) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa mwaka 2016, (*The Chemist Professionals Bill, 2016*);

(v) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania wa mwaka 2016 (*The Agricultural Research Institute Bill, 2016*); na

(vi) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Uvuvi wa Tanzania wa mwaka 2016 (*The Fisheries Research Institute Bill, 2016*).

Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, tayari Miswada hiyo imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Sheria za nchi ambazo sasa zinaitwa:-

(i) Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa Na. 6 ya mwaka 2016 (*The Access to Information Act. No.6, 2016*);

(ii) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Na. 7 ya mwaka 2016 (*The Valuation and Valuers Registration Act, No.7, 2016*);

(iii) Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na. 8 ya mwaka 2016 (*The Government Chemist Laboratory Authority Act, No.8, 2016*);

(iv) Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia Na. 9 ya mwaka 2016, (*The Chemist Professionals Act, No.9, 2016*);

(v) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, Na.10 ya mwaka 2016 (*The Agricultural Research Institute Act, No.10, 2016*); na

(vi) Sheria ya Taasisi ya Uvuvi, Tanzania, Na.11 ya mwaka 2016 (*The Fisheries Research Institute Act, No.11, 2016*).

Waheshimiwa Wabunge, imetolewa leo hii na Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, leo tarehe 1, Novemba 2016. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Hati za kuwasilisha mezani.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:

Taarifa za Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

- (i) Toleo Na. 16 la Tarehe 15/4/2016;
- (ii) Toleo Na. 17 la Tarehe 22/4/2016;

- (iii) Toleo Na. 21 la Tarehe 20/5/2016;
- (iv) Toleo Na. 36 la Tarehe 26/8/2016;
- (v) Toleo Na. 37 la Tarehe 02/9/2016;
- (vi) Toleo Na. 38 la Tarehe 09/9/2016;
- (vii) Toleo Na. 39 la Tarehe 16/9/2016;
- (viii) Toleo Na. 40 la Tarehe 23/9/2016;
- (ix) Toleo Na. 41 la Tarehe 30/9/2016;
- (x) Toleo Na. 42 la Tarehe 07/10/2016; na
- (xi) Toleo Na. 43 la Tarehe 14/10/2016.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Ncho Ofisi ya Waziri Mkuu, sasa namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante sana Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa namuomba Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Sasa namkaribisha Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango.

MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Katibu, tuendeleo.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Viti Maalum.

Na. 1

Makazi Maalum kwa Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Kumekuwa na mauaji ya Watanzania wenye ulemavu wa ngozi kwa muda mrefu sasa ambapo hali hiyo imesababisha wananchi wasamaria wema kuanzisha makazi maalum kwa ajili ya kuwahifadhi.

Je, Serikali inashiriki vipi katika kutoa huduma muhimu ikiwemo kuhakikisha wanapata elimu, matibabu pamoja na *lotion*?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha takriban miaka kumi, kumekuwa na matukio ya vitendo vya kikatili dhidi ya watu wenye ualbino ambavyo vimesababisha baadhi ya wasamaria wema kuanzisha makazi maalum ya kuwahifadhi watu wenye ualbino. Licha ya matukio hayo kupungua, bado kuna makazi yanayotumika kuwatunza watu wenye ualbino kwa sababu mbalimbali zikiwemo sababu za unyanyapaa na taarifa za baadhi ya matukio ya mashambulio japo si mara kwa mara kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita. Makazi hayo yanajumuisha yale yaliyoanzishwa na Serikali na yale yaliyoanzishwa na wasamaria wema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makazi haya, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inawajibika kuhakikisha kuwa watoto wenye ualbino wanapata elimu katika mazingira salama na kadri inavyowezekana kwa kuzingatia hali halisi Serikali itahakikisha watoto hawa wanapata elimu katika mazingira shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matibabu na mafuta maalum ya ngozi, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Tiba za *Ocean Road, KCMC*,

Bugando na wadau wengine imekuwa ikitoa matibabu na mafuta maalum ya kuzuia athari za mionzi ya jua katika ngozi, yaani *sun screen lotion*, kwa watu wenye ualbino. Aidha, Serikali kupitia Bohari Kuu ya Madawa (MSD) imeandaa mkakati wa kusambaza mafuta maalum katika hospitali zote za Wilaya ili kuwasaidia watu wenye ualbino ambapo mafuta hayo yameingizwa katika kundi la dawa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ikishirikiana na wadau wengine imeandaa utaratibu wa kuwapima macho na ngozi watu wenye ualbino na kuwapatia tiba pamoja na ushauri ili wasiathirike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaamini kuwa suluhisho la kudumu la kuondoa vitendo vya ukatili na unyanyapaa dhidi ya watu wenye ualbino nchini ni kutoa elimu ili kubadili fikra potofu kwa jamiii kuliko kunzisha makazi na vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha azma hii, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana mamlaka ya Serikali za Mitaa na wadau wengine imeanzisha kampeni ya kupinga unyanyapaa na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino kwa lengo la kutoa uelewa na kutokomeza imani potofu iliyojengeka miongoni mwa jamii kuhusu watu wenye ualbino.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali la nyongeza.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa makazi haya ya watu wenye ulemavu yako ndani ya Halmashauri, je, Serikali sasa haioni haja Halmashauri ikatenga bajeti ndogo ili iweze kusaidia upatikanaji wa chakula ili wananchi hao wawe na uhakika wa kupata chakula badala ya kusubiri msaada kutoka kwa mwananchi mmoja mmoja? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na jitihada za Serikali za kupambana na mauaji haya. Je, sasa naomba Serikali inihakikishie ina mkakati gani wa haraka kuhakikisha watu hawa wanahudumiwa na vitendo hivi vinakoma ili wananchi hawa waweze kuungana na ndugu zao na jamii ili waweze kushirikiana katika shughuli mbalimbali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Halmashauri, ni kweli, kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu labda nifafanue kwanza; jukumu la kwanza la kumlinda

mtu mwenye ulemavu linaanzia kwenye familia baadaye taasisi, Serikali kwa upande wa Halmashauri ni sehemu ya mwisho kwenye makazi kwa sababu msisitizo uko katika kuishi katika hali ya kuchangamana na wengine na kweli Halmashauri zinaagizwa kuhakikisha kwamba zinatenga bajeti kwa ajili ya kutoa misaada maalum hasa ya makazi na chakula kwa wale wanaohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo ambalo liko wazi kisheria, na tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikitoa maagizo hayo na kwa kutumia fursa hii niwakumbushe wote wanaohusika na Wabunge pia kwa sababu ni Wajumbe katika Mabaraza ya Madiwani ambayo yanahusika kupanga bajeti ya Halmashauri mbalimbali kuhakikisha kwamba wanasimamia bajeti katika Halmashauri zao ili kuhakikisha kwa mba watu wenye ulemavu wanapewa kipaumbele katika masuala mbalimbali si tu ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jitihada maalum, niseme tayari kumekuwa kuna jitihada mbalimbali na hata juzi tu nafikiri, siku ya Ijumaa kwa wale wanaosikiliza habari walisikia kuhusu hukumu nyingine ambayo ilitolewa na Mahakama Kuu - Kagera kwa watu waliofanya tukio mwaka 2008, majina yao siyakumbuki, lakini hizo hukumu zimetolewa na nafikiri katika mwaka huu kumekuwa kuna hukumu zaidi ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba makosa ya mauaji kwa sababu yana adhabu kubwa, kifo ushahidi wake inabidi uwe *watertight* kwa maana hiyo huwezi pia wakati mwingine ukaharakisha kutoa hukumu kwa sababu wengine wanasema kwa lugha ya kingereza *justice rushed is justice buried* na kuna changamoto zingine pia katika kesi hizi. Kuna baadhi ya watu hasa ukizingatia baadhi ya matukio yamekuwa yanafanywa na watu wa karibu katika familia, kumekuwa kuna ugumu wa kupata ushahidi kwa haraka, lakini niseme tu jitihada zinaendelea na zipo ambazo zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote kama nilivyosema, suluhisho la kudumu ni katika kubadilisha tabia na ndio maana siku zilizopita chache katika wiki ya vijana Serikali ilianzisha mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba elimu inatolewa ili tatizo hili liishe na nina imani hili tatizo litakwisha ndani ya muda mfupi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watoto wenye mtindio wa ubongo wamekuwa wakipata matatizo mbalimbali sawasawa na wale watoto wenye ulemavu wa ngozi, hususan suala la haki ya kupata elimu. Naomba nifahamu

Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watoto hawa ili wapate haki ya kupata elimu kwa kuanzisha madarasa maalum au shule maalum walau kwa kila Wilaya ili watoto hawa wapate haki hiyo ya elimu ikiwemo Wilaya yangu ya Babati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba wale watoto wenye *learning difficulties* nachelea kutumia jina mtindio wa ubongo sio wote wanaohitaji kwenda kwenye madarasa maalum. Tutofautishe *normal learning difficulties* na usonji yaani *autism* wako wengine ambao wanaweza wakaanzishwa katika shule za kawaida kabisa na wakafunguka, *actually* kuna taarifa za watu ambao walionekana kama wana *learning difficulties* wakasoma katika elimu shirikishi na wakafaulu mitihani ya darasa la saba na wako wengine *depending on the level* wanaweza wakaishi kwa kusoma na kufanya kazi katika mazingira mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo msisitizo upo katika elimu shirikishi isipokuwa kwa wale ambao kutokana na hali yao basi kuna madarasa maalum ninafahamu kuna shule maalum ambazo zimeanzishwa kwa ajili hiyo na Serikali inafanya jitihada za kutosha ili kuhakikisha kila mtoto anapata elimu kwa sababu tunaamini hali ya ulemavu ni sehemu tu ya mjumuiko wa binadamu kwa hiyo kila mwanadamu ana haki ya kupata fursa sawa na kila binadamu ana namna fulani ya kipaji chake ambacho hakipaswi tu kupuuzwa kwa ajili ya hali ya ulemavu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu unataka kuongezea.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niongezee majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na eneo hili la wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi mpaka sasa hivi Serikali tayari kwa kushirikiana na Halmashauri kumeshakuwa na shule nyingi za watu wenye ulemavu lakini lazima nikiri kwamba kumekuwa na mapungufu katika shule nyingi nilizozitembelea, shule hizo zimekuwa hazipati rasilimali za kutosha pamoja na kuzipitia mara kwa mara, hata pia katika masula ya kibajeti. Lakini Wizara baada ya kutembea tumeshaona hayo mapungufu na sasa hivi mikakati tuliyonayo ni kwanza ni kuziboresha shule zenyewe ikiwemo kuziwekea miundombinu ikiwemo fensi pamoja na majengo, kwa sababu shule nyingi wanazokaa wanafunzi hawa wenye ulemavu ni zile za zamani kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tayari Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu tayari kuna vifaa maalum ambavyo vimeagizwa kwa ajili ya kusaidia hao wanafunzi wenye ulemavu. Lengo ni kuona kwamba wanafunzi hawa wasitengwe wala kubaguliwa lakini wakati huo huo wapewe haki zao za msingi za kusoma kadri inavyostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hayo lakini niseme tu kwamba haitatoshwa kuwa na shule nyingi za watu wenye ulemavu kama hazitapewa huduma inayostahili, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, nafikiri imetoshwa tuendelee na swali la pili, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Jimbo la Dimani.

Na. 2

Umuhimu wa Kubadili Taratibu za Uchaguzi

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliuliza:-

Chaguzi zetu zimekuwa zikikumbwa na matatizo mengi yanayosababisha upotevu wa fedha nyingi za Taifa jambo linaloweza kuepukika kwa faida ya Watanzania mathalani inapotokea mshindi wa uchaguzi wa Jimbo wa chama fulani amefariki hurudiwa badala ya nafasi hiyo kuchukuliwa na mshindi wa pili ndani ya chama hicho.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka utaratibu kuwa pindi mshindi wa jimbo kupitia chama fulani anapofariki mshindi wa pili ndani ya chama apewe nafasi aliyoiacha marehemu badala ya kurudia uchaguzi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka kuondoa utaratibu wa kusimamisha uchaguzi mkuu wakati mgombea anapofariki?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za uchaguzi pamoja na mfumo wa uchaguzi tulionao unamwelekeza mpiga kura kumpigia mtu (mgombea) na siyo chama kama ilivyo katika mifumo mingine ya uchaguzi ya kupigia chama. Hivyo, kwa sasa Serikali itaendelea kutumia utaratibu uliopo, kwa sababu mshindi wa pili atakayechukuliwa kujaza nafasi ya wazi, atakuwa hajachaguliwa na wananchi wote nchini au jimbo au kata husika, bali wanachama wachache wa chama hicho.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya sasa ya Uchaguzi, Sura ya 343 inaelekeza kusimamisha uchaguzi mkuu nchi nzima anapofariki mgombea Urais au Makamu wa Rais. Anapofariki mgombea Ubunge au Udiwani, uchaguzi mkuu nchi nzima huendelea, isipokuwa katika jimbo au kata husika ambayo mgombea amefariki. Hata hivyo, sheria ya uchaguzi inaweza kufanyiwa marekebisho kwa kuzingatia wakati uliopo, mazingira halisi ya nchi, tafiti na tathmini za uchaguzi zinazofanyika na jambo hili linaweza kujadiliwa pia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir swali la nyongeza kama unalo.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake lakini wakati akijibu swali langu alikuwa ameweka wazi kwamba sheria ya uchaguzi inaweza kufanyiwa marekebisho kulingana na wakati uliopo, swali langu kwamba hahisi kwamba sasa wakati wenyewe uliopo ndio huu, na tunapofika mwaka 2020 sheria hii tukaifanyia marekebisho, anasemaje?

Swali la pili, kwa sababu Waziri Mkuu yeye mwenyewe ni Mbunge wa kuchaguliwa na anahisi na anajua ugumu wa gharama katika jimbo, hivi Naibu Waziri si lazima anipe kwa ukamilifu lakini anachoweza kuliambia Bunge hili kiasi ambacho anafikiria hutumika katika kurudia uchaguzi katika majimbo yetu? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu suala la kufanyia marekebisho swali hili lilikuwa lina vifungu (a) na (b) na nilijibu katika kile cha (b) kuhusiana na suala la kusimamisha uchaguzi pale anapofariki mgombea, *of course* hilo liko wazi lakini mwisho wa siku tunaobadilisha sheria ni sisi kama inaona nafaa na wadau watapendekeza basi hilo suala linaweza likaletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama mabadiliko hayo yalikuwa yanahusiana na kubadilisha ule mfumo wa uchaguzi kwamba akifariki mgombea ubunge basi yule aliyekuwa mshindi wa pili katika chama husika anachukua nafasi hiyo, hili si jambo rahisi sana na labda niseme tu ukiangalia *system* za uchaguzi duniani zipo takribani 23 sasa kwa nini nchi moja wakaamua kupigia chama, kwingine wakaamua kupigia mgombea, kwingine wakaamua kupigia orodha ya wagombea iliyofungwa ya chama, kwingine wakaamua kupigia orodha ya wagombea wa chama iliyokuwa wazi, kwingine wakaamua kuchanganya ni swali gumu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu demokrasia yetu inakuwa na kubadilika kwa demokrasia, kubadilika kwa mfumo wa uchaguzi kwa namna moja au nyingine ni sehemu ya historia basi muda utakapofika utatoa majibu sahihi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na swali namba tatu Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini.

Na. 3

Serikali Kutekeleza Ahadi ya Shilingi Milioni 50 kwa kila Kijiji na Mtaa

MHE. STANSLAUS H. NYONGO (K.n.y. MHE. STEPHEN J. MASELE) aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji na mitaa ili kutatua tatizo la ajira na mitaji kwa vijana na kina mama?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 Juni, 2016 wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kuhusu lini ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji itaanza kutekelezwa nilisema kuwa Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 59.5 katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa tayari waraka wa Baraza la Mawaziri utakaoongoza utoaji wa fedha hizo umeshaandaliwa na kujadiliwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu (IMTC) hivi sasa waraka huo unasubiri kujadiliwa na Baraza la Mawaziri ili kuweka mfumo utakaoratibu utoaji wa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Hivyo namuomba Mheshimiwa Mbunge asubiri utekelezaji wake mara baada ya Baraza la Mawaziri kuujadili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahmed Salim swali la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Stephen Julius.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri.

Swali la msingi linauliza kwamba pesa hizi zitaanza kutolewa maana yake toka mpaka sasa ni kwamba uchaguzi umeshapita, mwaka mzima umeisha *quarter* ya kwanza ya bajeti imeisha ni lini? Swali la msingi linauliza.

Swali la pili la nyongeza ni kwamba hili Baraza la Mawaziri litakaa lini kupitisha hii pesa kwa sababu tayari ilishajulikana pesa hizi zinakwenda kwa kila kijiji, ni nini kinakwamisha Baraza hili kukaa na kupitisha pesa hizi au mpango huu ili wananchi waweze kupata hizi pesa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake kauliza ni lini, na katika majibu yangu nimesema kabisa ya kwamba katika bajeti ya mwaka 2016/2017 tayari kiasi cha shilingi bilioni 59.5 zimetengwa kwa hiyo kinachosubiriwa hivi sasa ni waraka ule kupelekwa Baraza la Mawaziri na ukishajadiliwa, baada ya hapo katika jibu langu nimesema utekelezaji utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba jambo hili ni jambo kubwa kidogo na linahitaji maandalizi ya kutosha hasa ukizingatia kwamba tunakwenda kuvigusa takribani vijiji 12,545 vya nchi hii na utaratibu wake huu unawekwa sawa kiasi kwamba tusije tukarudia yale makosa ambayo yalijitokeza pale awali katika usimamizi wa fedha ambao zilitoka ambapo walengwa wale hawakuweza kufikiwa na ndio maana waraka huu unaweka utaratibu mzuri na hatukutaka jambo hili kulifanya kwa uharaka kwa kuzingatia umuhimu wa ukubwa wa jambo hili na ndio maana imeshajidiliwa katika *level* hiyo na mkumbuke kwamba bajeti hii imepitishwa mwezi wa saba tu, kwa hiyo ni miezi mitatu tayari hapa taratibu zimekwisha kuanza nimwondoe hofu kwamba tunalipa uzito mkubwa na baada ya muda sio mrefu waraka huu utajadiliwa na utaratibu utatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Baraza la Mawaziri litakaa, Mheshimiwa Mbunge atupe nafasi tu baada ya kukamilisha taratibu hizi za Bunge hapa natumaini wahusika wa kuandaa utaratibu huu utafanyika na tutarudi tena kwa ajili ya kutoa taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Maswali mengi kuhusu hizi milioni 50 tunaulizwa sisi Wabunge kwenye majimbo yetu. Wakati mwingine tunashindwa kutoa majawabu sahihi kwa sababu Serikali haijatoa taarifa rasmi kuhusu utoaji wa hizi shilingi milioni 50. Je, Mheshimiwa Waziri Serikali iko tayari sasa kwenda *front* na kutangaza kwamba wananchi wasubiri mpaka Baraza la Mawaziri likae ili liweze kutoa utaratibu wa kutoa hizi fedha ili sisi Wabunge tusipate wakati mgumu tunapokuwa Majimboni mwetu kuulizwa suala la shilingi milioni 50? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Waheshimiwa Wabunge wanawakilisha Watanzania na ninajua Watanzania wengi wangependa Ilani hii ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambayo.... (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uendelee, tafadhali naomba mtulie.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ambayo ndio iliwaahidi Watanzania kwamba itatoa shilingi milioni 50 katika kila kijiji, inatakiwa itekelezeke, ninaomba niwahakikishie Watanzania Serikali hii kwanza imeshatenga hiyo bajeti, pili Serikali hii imeshaona umuhimu wa kuanza haraka utekelezaji wa jambo hili, tatu Serikali hii ili kuhakikisha fedha hizo zinawafikia wanyonge sasa imeanza kuweka mfumo mzuri wa kuratibu zoezi hili na mara tu utakapokamilika Serikali hii itawaambia Watanzania ni mfumo gani utakaotumika. Na kwa sababu fedha zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu, fedha hizo tutaanza kuzitoa katika mfumo rasmi utakaowafikia wanyonge ili kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbowe swali la nyongeza.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa imekuwa ni tabia ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutoa ahadi ambazo zinaonekana tamu kwa wananchi wakati wa uchaguzi. Tukikumbuka kwamba katika Awamu ya Nne ulianzishwa mpango wa mabilioni ya Jakaya Kikwete ambao ulikufa bila kueleza Bunge au Watanzania kuwa umekufaje; na kwa sababu sasa hivi ni mwaka mmoja umepita tangu tumemaliza uchaguzi na Baraza la Mawaziri linajua kwamba hadi robo ya kwanza ya mwaka wa fedha ya mwaka 2016/2017 inakwisha kuna Wizara kadhaa hazijapata fedha za maendeleo.

Sasa namuuliza Waziri ni miujiza gani itakayotumiwa na Serikali hii ambayo leo imefilisika ambayo leo imeshindwa kutoa mikopo ya wanafunzi wa chuo kikuu kwa maelfu kwamba inaweza... (Makofi)

WABUNGE FULANI: Aaah!

MWENYEKITI: Naomba utulivu tafadhali.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba bado...

MWENYEKITI: Tafadhali naomba utulivu.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Tulieni niulize swali.

MWENYEKITI: Umeshamaliza swali Mheshimiwa.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Bado.

MWENYEKITI: Basi umalize tafadhali.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nauliza ni miujiza gani Serikali iliyofilisika itakayotumia kutafuta fedha hizi shilingi bilioni 960 badala ya kuwadanganya wananchi? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kalipe Billicanas kwanza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Waheshimiwa basi naomba utulivu tumsikilize kwa hisani yenu nawaombeni.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwanza kwamba Serikali hii haifanyi kazi kwa miujiza, Serikali hii inafanya kazi kwa mpangilio wa bajeti tuliojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na uthibitisho wa kwamba jambo hili litatekelezeka ni kama tulivyoweza kuwashangaza Watanzania kwa kutoa elimu bure kwa mabilioni ya fedha. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyoweza kuwashangaza Watanzania kwa kutekeleza miradi mingine mikubwa na hata ununuaji wa ndege, tulivyoweza kuwashangaza Watanzania kwa utekelezeji wa llani yetu kwa mambo mengine mbalimbali ninaomba niwathibitishie Watanzania fedha hizi zitatolewa na Watanzania watazipata na Serikali hii haitafanya kazi kwa miujiza itafanya kazi kwa mpango wa utekelezaji wa bajeti ya wananchi tuliojiwekea. Na fedha hizo zitafika pia hata katika majimbo ya wapinzani katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa nafikiri majibu yamejitosheleza na inaonesha wazi kwamba Serikali haijafilisika Mheshimiwa Mbowe, kwa hiyo, naomba tuendelee tustahamili. Tunaendelea Waheshimiwa na swali namba nne Mheshimiwa Grace Victor, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Na. 4

Hitaji la Elimu Endelevu kwa Waathirika wa UKIMWI

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y MHE. GRACE V. TENDEGA) aliuliza:-

Mojawapo ya jukumu la Serikali katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni kuhakikisha wanatoa elimu kwa umma na waathirika kupatiwa huduma za matibabu kulingana na masharti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ambalo ndiyo hufadhili huduma hizo kwa takribani 100%.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba huduma hizo zinaendelea kutolewa hata kama msaada kutoka Shirika la Afya Duniani utatetereka?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba huduma za elimu kwa umma na matibabu kwa waathirika wa UKIMWI zinaendelea kutolewa hata pale misaada ya hisani itakapopungua, Serikali tayari imeanzisha Mfuko wa UKIMWI kupitia marekebisha ya Sheria ya UKIMWI Namba 6 ya mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuratibu ukusanyaji fedha za kudhibiti UKIMWI nchini. Hata hivyo, Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) na bajeti za kila mwaka inaendelea kuhakikisha huduma kwa waishio na VVU na elimu kwa wananchi kuhusu UKIMWI inakuwa ajenda muhimu katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Grace Victor, una swali la nyongeza?

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Susan Lyimo. Nashukuru kwa majibu mafupi sana ambayo hayana uelekeo; nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati ya UKIMWI ilipotembelea MSD, pamoja na mambo mengine ilipata taarifa kwamba kuna shehena kubwa sana

ya dawa za UKIMWI ambayo ilikwama bandarini kwa sababu ya kutokulipa VAT, nataka kujua kama dawa zile tayari yameshaondoka bandarini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; natambua kwamba wafadhili wengi walisema watajitoa na hivyo Serikali ikaanzisha Mfuko wa UKIMWI, nataka kujua mpaka sasa hivi mfuko huo una kiasi gani cha fedha hasa ikizingatiwa kwamba wagonjwa hawa au waathirika hawa wakishaanza kutumia madawa wanapaswa kuendelea kuyanywa mpaka mwisho wa maisha yao. Nataka kujua mfuko huo toka umeanzishwa mpaka leo una kiasi gani cha fedha na tusipewe ahadi za uongo kama ambavyo tumesikia?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumtoa hofu kwamba Serikali haishindwi kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI katika nchi hii, lakini ni utaratibu wa kawaida tu wa kujenga mahusiano mema na marafiki ambao wanajitokeza kutusaidia kubeba mzigo mzito wa kutoa huduma za afya kwa watu wetu. Na huu ni utamaduni wa nchi zote duniani na haitarajiwi hata mara moja kwamba itafika siku wataamua ghafla kusitisha misaada hii ambayo wanaitoa kwa wagonjwa wa UKIMWI, lakini kama tutafika huko tayari tumeandaa *fall back position* kwa kuanzisha Mfuko wa UKIMWI anaouzungumzia, na mfuko huo tumeanza kuuwekea bajeti kwenye bajeti hii iliyopita na tumeanza kwa kiwango kidogo cha shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo waweze kuchangia fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye mfuko huo. Na nitoe rai kwake Mheshimiwa Mbunge na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla tujitolee kuchangia Mfuko wetu wa UKIMWI kadri tutakavyoweza na pia hata kuvutia marafiki wawekeze kwenye mfuko huo ili iwe *fall back position* ambayo ina uwezo wa kutosha huko mbeleni kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wetu.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa tunaacha sasa ofisi ya Waziri Mkuu tunaelekea Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Aah, endelea Mheshimiwa kujibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisahau kuhusu shehena ya dawa, hakuna shehena ya dawa mpaka hivi sasa ambayo imekwama popote pale na kwamba dawa zinapatikana nchini kwa asilimia mia moja. Kwa sababu taarifa za dawa za UKIMWI na miradi misonge yote tunazipata kila wiki, kwa *update* niliyonayo kufikia Ijumaa iliyopita hakukuwa na shehena ya dawa iliyokwama bandarini, lakini dawa zote zipo kwenye bohari zetu za mikoa na bohari za kanda kwa kiwango cha asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nizungumzie jambo la kitaalam, tukisema kuna *availability* ya dawa kwa asilimia mia moja, tunamaanisha kwenye Bohari ya Taifa kuna dawa zinazojitosheleza kutumika kwa miezi sita mbele na kwenye bohari za mikoa tuna dawa za kujitosheleza kwa matumizi ya miezi mitatu mbele na kwenye bohari za wilaya tuna dawa za kujitosheleza kwa mwezi mmoja mbele hiyo ndiyo *availability* tunayoizungumzia ya asilimia mia moja, sasa kwenye dawa zote za miradi misonge zikiwemo dawa za UKIMWI tuna *availabaility a hundred percent*.

Na. 5

Matatizo Makubwa ya Maji Mpwapwa

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Vijiji vya Iyoma, Kisokwe, Idilo, Lukole, Lupeta, Bumila, Makutupa, Mkanana, Igoji Kaskazini (Isalaza), Nana, Kisisi, Ngalamilo, Godegoge, Mzogole, Mugoma, Kiegea, Kazania, Igoji Kusini, Chamanda, Simai, Makawila, Iwondo, Lupeta, Gulwe, Majami, Mwenzele na Mlembule katika Wilaya ya Mpwapwa vina matatizo makubwa sana ya maji na hivyo kusababisha wananchi wa vijiji hivyo kutembea umbali wa zaidi ya kilometa tano hadi kumi kutafuta maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima vya maji katika maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.58 kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Kazi zitakazofanyika ni uchimbaji wa visima pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji iliyopo. Vijiji vilivyopo katika mpango ni Iyoma, Mzase, Mima, Bumila, Lukole, Kingiti, Kibakwe, Mbori, Mbuga, Iguluwi, Chogola, Kidenge, Iramba, Mlunduzi na Seluka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazoendelea kwa sasa katika uboreshaji wa huduma ya maji ni utafiti wa maji ardhini na uchimbaji visima virefu katika vijiji vya Mima, Mzase, Bumila na Iyoma. Uchimbaji wa visima virefu katika kijiji

vya Mima na Mzase umekamilika. Kazi ya kuchimba visima virefu katika kijiji vya Bumila na Iyoma unaendelea na utakamilika mapema Novemba, 2016.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa maeneo ambayo ameyataja, kwa mfano Iyoma, Mzase na Bumila kwamba kazi inaendelea. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi kuona kama kazi hiyo imeanza? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mji wa Mpwapwa ni mji wa zamani sana, una zaidi ya miaka 100 sasa tangu mwaka 1905 lakini vyanzo vya maji ni vilevile, kuna maji baridi na kuna maji ya chumvi, na kuna maeneo ambayo wanaweza wakachimba visima vya maji tukapata maji baridi ili wananchi wa Mpwapwa waweze kupata maji baridi. Je, Serikali iko tayari kutuma watafiti waende waanze kufanya utafiti ili kuongezea visima vya maji kwa Mji wa Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, ambaye mimi namwita greda la zamani lakini makali yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niko tayari, tena hata kipindi hiki cha Bunge tunaweza tukatoka Mpwapwa ni karibu hapa tukaenda kutembelea hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika suala zima la kufanya utafiti, ni kweli, ukiangalia Mji wa Mpwapwa siku ile tumekwenda pamoja Mheshimiwa Mbunge, chanzo cha maji sasa hivi kimeelemewa na hata ile changamoto kubwa ni kwamba uharibifu wa mazingira ndiyo umekuwa ukiathiri sana suala zima la maji yanayopatikana katika Mji wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hivi sasa kuna watu wako *site* wanafanya utafiti maeneo mbalimbali lakini kwa uzoefu wako uliokuwa nao na kwa kushirikiana na watafiti hawa kuangalia jinsi gani tutafanya kwa pamoja kama Serikali, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Lubeleje, katika safari yetu ya pamoja tutaangalia, tutaonana na wataalam wa maji katika ofisi yangu kama sehemu ya awali. Mwisho wa siku ni kwamba watu wa Jimbo lako la Mpwapwa, lakini Halmashauri yote ya Mpwapwa kwa ujumla waweze kupata fursa ya maji kama Mbunge wao anavyowapigania.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Jimbo la Mpwapwa linafanana kabisa na Jimbo la Mbulu Vijijini kwa ukosefu wa maji kwa eneo kubwa mno, je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuja kuviangalia hivi vijiji na kata za Labay, Bisigeta, Maretadu, Endamilay, Endahagichan, Bashnet na Dinamu, ili kuzipatia visima virefu na wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini kupata maji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi, nilifika kwa Mheshimiwa Mbunge takribani wiki nne zilizopita kutembelea katika jimbo lake. Nipende kumpongeza kwa harakati kubwa sana anazozifanya na mwezake Mbunge wa Mbulu Mjini. Naomba nikiri wazi kwamba kweli kuna changamoto ya maji na kwa sababu mpango wetu wa Serikali sasa hivi ndani ya miaka mitano kujielekeza tunahakikisha kwamba Mpango wa Maji katika Awamu ya Pili unafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba niseme kwamba tutafanya kila liwezekanalo kutumia wadau mbalimbali kupitia bajeti hizi tulizokuwa nazo lakini kutumia fursa nyingine mbalimbali tunazozipata, lengo kubwa na ushahidi niliyouona nilivyofika *site* nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutashirikiana kwa pamoja kwa kadri iwezekanavyo kwa ajili ya wananchi wa Mbulu Vijijini.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa tatizo la maji lililopo Jimbo la Mpwapwa linaonesha uhalisia wa ukosefu wa maji Tanzania nzima likiwepo Jimbo la Tarime Mjini, na kwa kuwa maji safi na salama ni muhimu kwa afya za binadamu; ni lini sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaona kuna umuhimu wa kuwapatia maji wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini maji safi na salama kwa kutekeleza bajeti ambayo tuliipitisha hapa, ambayo bado hamjaanza kuitekeleza mpaka sasa hivi, ili wananchi wa Tarime Mjini na Tanzania kwa ujumla waweze kupata maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema ni kweli, tatizo la maji sio Tarime tu, ni nchi nzima, na ndiyo maana katika mipango ya Serikali tumejielekeza jinsi gani tutafanya kuhakikisha tatizo la maji tuweze kulipunguza. Hata sasa hivi katika halmashauri zetu ukiangalia, takribani shilingi bilioni 25 zimepelekwa ili miradi ya maji iweze kufanyika katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba sisi dhamira yetu ya dhati ni kuhakikisha katika bajeti ta mwaka huu ambayo Serikali inafanya mpango, utaratibu mzuri wa kupeleka hizi fedha, utafikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Matiko asiwe na hofu katika hili, tutasimamia bajeti za Halmashauri, lengo letu ni kwamba ile bajeti ya karibu halmashauri zote na TAMISEMI, zaidi ya shilingi trilioni 6.4 ziweze kutekelezeka

katika mwaka huu wa fedha. Na hili ni wazi kwa sababu mchakato wa ukusanyaji wa mapato unavyoendelea Serikali tuta-pump hizo pesa lakini sisi tuliopewa dhamana ya kusimamia tutahakikisha tunasimamia wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Na. 6

Kituo cha Afya – Laela

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Kituo cha afya kilichopo Laela kinategemewa na Kata za Lusaka, Kasanzama, Laela, Mnokola, Miangalua na Kaoze; kutokana na kupanuka kwa kasi kwa mji huo na ongezeko la watu wanaohudumiwa katika kituo hicho, kimesababisha upungufu wa dawa, wataalamu na vifaa tiba.

(a) Je, ni lini Serikali itakipa kituo hicho hadhi ya Hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini kituo hicho kitapatiwa gari la wagonjwa?

(c) Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam wa kutosha, vifaa tiba na dawa za kutosha katika kituo hicho?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Kituo cha Afya Laela hakina miundombinu inayokidhi sifa za kuwa hospitali, kazi inayofanyika kwa sasa ni upanuzi wa miundombinu ya kituo hicho ambapo tayari jengo la upasuaji wa dharura kwa mama wajawazito limekamilika pamoja na wodi ya mama wajawazito na wodi ya wagonjwa waliofanyiwa upasuaji. Aidha, mpango wa muda mrefu katika eneo hilo ni kujenga Hospitali ya Wilaya kukidhi mahitaji ya matibabu kwa wagonjwa wanaotembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za rufaa kwa wagonjwa wanaohudumiwa katika kituo hicho kwa sasa zinatolewa kupitia magari ya kawaida ya Halmashauri kutokana na ukosefu wa gari la kubebea wagonjwa. Ni matarajio ya Wizara kwamba Halmashauri itaweka kipaumbele katika kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ununuzi wa gari la wagonjwa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watumishi katika Kituo cha Afya Laela ni tisa kati ya 45 wanaohitajika. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri imepewa kibali cha kuajiri watumishi wapya wapatao 42 ambapo baadhi yao watapelekwa kituoni hapo. Kuhusu dawa na vifaa tiba, kituo kimetengewa bajeti ya shilingi bilioni 9.3 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia.

WABUNGE FULANI: Ooooh!

MWENYEKITI: Mwenyewe yupo haya, swali la nyongeza fupi tafadhali. Aliyeuliza swali naomba aulize swali la nyongeza.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ina vituo vya afya vitano ambavyo havina magari ambavyo ni Laela, Kayengeza, Msanadamungano, Mpuwi na Milepa, na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imejitahidi sana katika kuweka bajeti kwa mwaka 2013/2014, 2014/2015 ili kukabiliana na adha hii lakini Serikali haijatoa fedha ili halmashauri iweze kununua magari hayo. Sasa Serikali inaithibitishiaje halmashauri kwamba ikitenga fedha inaweza kuipatia ili iweze kununua magari kukabiliana na tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia tatizo la msongamano wa wingi wa wagonjwa katika Kituo cha Afya Laela, na amezungumzia utatuzi wa tatizo hilo kwa mpango wa muda mrefu, wakati kwa sasa tatizo hilo ndiyo lipo na ni kubwa sana kutokana na wingi wa watu na kupanuka kwa mji mdogo. Nataka Serikali inieleze, kwa sasa inafanyaje mpango wa dharura ili kuokoa wananchi wanaosongamana katika kituo cha afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mchakato wa bajeti unaokuja, naomba ninyi anzeni tu ule mchakato wa awali wa kuhakikisha kwamba mnatenga ile bajeti halafu sisi tutasimamia jinsi gani katika Bajeti ya mwaka 2017/2018 hilo gari liweze kupatikana, yaliyopita si ndweli tugange yajayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msongamano wa sasa tulionao katika hospitali, nakumbuka Mheshimiwa Mbunge tulikuwa pamoja pale katika eneo lako. Kwanza wasiofahamu jimbo la Mheshimiwa Malocha, liko kama

mbalamwezi hivi ambao mwezi mchanga, ambayo kuna watu wengine wanatoka maeneo ya Pembe mbali sana kuja katika Hospitali ya Sumbawanga. Kwa hiyo, mwenyewe nime-verify lile tatizo, ni tatizo la msingi na hili naomba nimwelekeze RAS wetu wa Mkoa wa Rukwa kwamba aangalie jinsi gani kwanza kama mpango wa haraka kuhakikisha eneo hili linapata angalau huduma katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni kweli, wananchi wa Mheshimiwa Malocha pale wakitoka kule Pembe mpaka kufika hapa kama mgonjwa anaweza akafariki. Kwa hiyo, naomba nikwambie ofisi yetu itawasiliana na ofisi ya mkoa pale tuangalie mipango mikakati ya haraka kuwasaidia wananchi wa eneo lako ilimradi waweze kupata huduma ya afya kama ilivyokusudiwa na Watanzania wengine.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia kwa vile nilishamtaja.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuwa swali la msingi hapa ni kituo cha afya; na kwenye Jimbo la Vunjo, Kata ya Marangu Magharibi yenye vijiji saba haina kituo cha afya wala zahanati hata moja, na mpaka sasa Mbunge kwa kushirikiana na wananchi wa kijiji cha Kitowo na Kiraracha tumeweza kufanikisha shilingi milioni 20, na KINAPA wanatupatia shilingi milioni 53 na tunategemea kujenga kwa shilingi milioni 200, *commitment* ya Serikali itatoa mchango gani ili Kata ya Marangu Magharibi, hasa Kijiji cha Kiraracha waweze kupata huduma ya afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwapongeze kwa ile *initial stage* ya wananchi wako, mmefanya *resource mobilization* pale mmeweza kupata karibu shilingi milioni hiyo ishirini na kwa ajili ya jambo hilo, nililizungumza katika vipindi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwanza tumefanya tathmini ya nguvu za wananchi katika maeneo mbalimbali, kuna maboma mengi sana yamejengwa lakini yamefika katikati hayajakamilishwa, ndiyo maana tumewaagiza Wakurugenzi wote wa maeneo mbalimbali kuangalia zile juhudi ambazo wamefanya katika eneo lao, ili mradi katika bajeti hii ya mwaka wa fedha inayokuja tuhakikishe kwamba ajenda ya kwanza ni kukamilisha maboma na maeneo yote. Tukifanya hivi yale maboma ambayo yapo katika *stage* mbalimbali tutakuwa tumesaidia sana kuwapa *support* wananchi, lakini hali kadhalika tutakuwa tumejenga vituo vingi vya afya na zahanati tutapunguza tatizo la afya katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo nikushukuru katika hilo. Serikali *commitment* yetu ni kwamba tumeshafanya hilo zoezi liko katika *ground* linaendelea na katika mchakato wa bajeti hiyo ni *priority* yetu katika mpango wa fedha wa mwaka 2017/2018.

Na. 7

Usambazaji wa Maji Safi na Salama katika Mkoa wa Geita

MHE. UPENDO F. PENEZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusambaza maji katika Kata za Kasamwa, Shiloleli, Bulela, Nyarugusu, Bukeli na maeneo mengine ya Wilaya ya Geita na Mkoa wa Geita kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 imepanga kutumia shilingi milioni 593.14 kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika Kata za Kasamwa, Shiloleli, Bulela, Nyarugusu na Bukolina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa miundombinu ya maji kwa kutumia chemchemi ya Mawemeru katika Kata ya Nyarugusu; uchimbaji wa visima virefu katika Kata ya Bulela na Shiloleli na kuboresha miundombinu ya maji iliyopo katika kata ya Kasamwa na Kanyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa mzima wa Geita Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji ambazo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Fedha hizo zitatumika kujenga miradi ya maji 22 ili kuboresha huduma ya maji kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Upendo swali la nyongeza kama unalo.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri suala zima la miundombinu; Mheshimiwa Rais alivyokuwa na ziara Mkoani Geita alitoa ahadi kwa wananchi wa Kasamwa kwa ajili ya kuwachangia pesa kujenga bwawa au lambo kama tunavyoweza kuliita. Lakini kazi iliyofanyika ni chini kabisa ya viwango na maji yale ni machafu, wananchi hawawezi kuyatumia. Na katika majibu yako pia katika hizi pesa ambazo zimetajwa hapa tumepata taarifa katika Kamati zetu kwamba Serikali haina pesa ya kutoa kwa ajili ya miradi ya maji katika sehemu nyingi hapa nchini.

Sasa naomba Serikali itoe tamko kwa wananchi ambao wana wasikiliza leo kwamba Serikali hii ina mkakati gani wa kuhakikishia wananchi kwamba wanapata maji safi na salama ambao wananchi wengi ambao ni wanyonge shida yao ni maji na sio *bombardier*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali pili Mheshimiwa Rais Magufuli aliweza kutoa ahadi kwa wananchi wa Geita kuweza kuwapatia magwangala, lakini katika eneo la Nyarugusu ni kati ya maeneo ambayo yameathirika sana kutokana na uchenjuaji wa dhahabu na wananchi katika maeneo hayo hawana maji salama kutokana kwamba vyanzo vingi vimeathiriwa na *mercury*.

Serikali inatoa tamko gani kwamba pamoja na shughuli za magwangala ambazo Rais amezitoa kwamba wananchi wa Geita watapata maji salama ili waweze kuendelea na maisha yao? Ahsante (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema kwamba Mheshimiwa Rais ametoa ahadi pale, lakini kazi inaendelea chini ya kiwango. Naomba nikuhakikishie kwamba tarehe 27/08 nilikuwa katika Mkoa wa Geita na nilifanya harambee kubwa pale tulipata karibuni *1.4 billion* kwa ajili ya madawati katika Mkoa wa Geita. Hata hivyo, katika sekta ya maji kwa sababu ni kipaumbele changu, nilitembelea maeneo mbalimbali ikiwepo Chato na mradi mwingine nikazindua lakini na mradi mwingine ambao ulikuwa watu wamefanya mambo ya ovyo na kuunda kamati. Na hivi sasa tutaenda kuchukua hatua stahiki kwa wale watu wote waliokiuka utaratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikwambie ni *commitment* ya Serikali kama sehemu ambayo umefanya ubadhirifu na mambo ya hovyoy tutaenda kuyasimamia. Nikwambie kama kamati sasa hivi timu niliyounda tayari taarifa ipo mezani kwangu tunaenda kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya wananchi. Kuna mradi mmoja wa Changolongo ambao umefanyika mambo ya ovyo, watu hawakufanya mambo sawasawa hata hiyo tunaenda ku-cross check. Lengo letu ni kwa wananchi wa Mkoa wa Geita na Mikoa na mingine waweze kupata huduma ya maji na hatutokuwa na masihara hata kidogo kwa watu ambao wanachezea kwa makusudi nguvu yoyote ya Serikali inayopelekwa halafu watu wakafanye mambo ya ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie *commitment* yetu ipo hapo na Mkoa wa Geita tunaenda kuchukua hatua, lakini naomba niwaombe radhi sana kwa wale watu ambao hata wakiwa ndugu zenu tukiwachukulia hatua tunaacha sasa naomba tusileteane vi-memo tunaenda kuwachukulia hatua watu waliokiuka taratibu za manunuzi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; suala la kwamba kuna *mercury* wananchi wa Nyarugusu wanahakikishiwa vipi? Ni kwamba ni *commitment* ya Serikali na ndio maana hata nilipofika kule niliwaambia wataalam wetu wajiongeze. Haiwezekani Mkoa wa Geita ambao kuna Ziwa Victoria kila sehemu unakoenda unakuta maji wananchi wanakosa fursa ya maji. Tukawaambia kwamba waje na mpango jinsi gani tutafanya Mkoa mzima wa Geita kutumia fursa ya Ziwa Victoria badala ya kuchimba *borehole*, tupate vyanzo vya maji mbadala kutumia Ziwa Victoria na hili niliwaagiza wataalam wetu na hilo wanalifanyia kazi. Na nimewaambia nataka tulione katika mpango wa bajeti wa mwaka huu wa fedha unaokuja, lengo kubwa wananchi wapate fursa ya maji katika maeneo yao. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana, naona jibu limejitosheleza tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 8

Watumishi Hewa

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu suala la watumishi hewa limekuwa likiathiri sana uchumi wa Taifa na kwa kuwa waliohusika wengi wao ni maafisa na watumishi wa Serikali.

Je, Serikali inasema nini juu ya wale waliohusika kurudisha nyuma maendeleo ya nchi kwa njia hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 25/10/2016 Serikali imechukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa umma 1,663 kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao walibainika kusababisha uwepo kwa watumishi hewa kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ni watumishi wa umma 16, kwa upande wa Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali ni watumishi

wa umma tisa, kwa Sekretarieti za Mikoa ni watumishi wa umma wa sita, Mamlaka za Serikali za Mitaa watumishi wa umma 1,632 inayofanya jumla ya watumishi 1,663.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii inajumuisha kuwasilishwa kwa masuala yanayohusu baadhi ya watumishi hawa katika vyombo vya ulinzi na usalama ambapo kufikia tarehe 25/10/2016 jumla ya watumishi wa umma 638 wamefunguliwa mashitaka polisi, watumishi 50 wanafanyiwa uchunguzi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na watumishi wa umma 975 mashtaka yao yamefikishwa kwenye mamlaka zao za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hizi Serikali inaendesha ukaguzi wa mara kwa mara kwa mfumo wa taarifa za kiutumishi au *Human Capital Management Information System* na maafisa wanaobainika kuhusika au kusababisha kuwepo kwa watumishi hewa katika taasisi au mamlaka zao wanachukuliwa hatua za kinidhamu kama vile kuwafungia dhamana na uwezo wa kuingia na kufanya kazi katika mfumo huo na hatua nyingine za kinidhamu. Nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maida, swali la nyongeza.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa wanavyojitahidi na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa kuhusiana na kadhia hii au suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Katika uhakiki unaondelea kuchukuliwa hadi tarehe aliyoitaja Mheshimiwa Waziri ni hasara kiasi gani Serikali imepata hadi kufikia tarehe hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; pamoja na mikakati ambayo Serikali imekuwa ikichukua kuhusiana na watumishi pamoja na maafisa waliohusika na swala hili. Serikali itambue kwamba kuna udhoroteshaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyokuwa inakwama pamoja na ukosefu wa madawa pamoja na ufinyu wa bajeti uliokuwa unajitokeza.

Je, Serikali inaweza kukubaliana na mimi kwamba pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa kwa watumishi kwamba iwepo adhabu ya kurudisha fedha ambazo walizipoteza? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mara nyingi tumekuwa tukitoa takwimu mwezi hadi mwezi endapo watumishi hao hewa wasingeondolewa kwa mwezi husika wangeisababishia hasara kiasi gani? Niseme tu kwamba hadi sasa tumeshaondoa watumishi hewa 19,629 ambao endapo wangeendelea kubaki katika orodha ya malipo ya mshahara kwa mwezi husika mmoja wangeisababishia Serikali hasara ya shilingi 19,749,737,180, hiyo ni kama wangebaki kwa mwezi mmoja husika bila kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nitoe labda takwimu ya Halmashauri mojawapo. Ningeweza kutaja kwa ujumla wake maana yake tuliomba takwimu lakini sijapiga mahesabu kwa jumla kwa haraka. Nikianza na Kinondoni tangu ambavyo wameondoa watumishi hewa waliondoa watumishi hewa 107 na kwa kiasi cha fedha ambacho walilipwa watumishi hao ni shilingi bilioni 1.279. Nikija kuchukua kwa Halmashauri ya Kishapu watumishi 73 wamelipwa shilingi milioni 543. Kwa hiyo, ambacho naweza kusema ni kwamba endapo wangeendelea kubaki kwa kweli ni gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili ni mikakati gani ambayo Serikali inachukua kuhakikisha kwamba pamoja na watumishi hawa hewa kuondolewa basi wanarejesha fedha. Nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge kama nilivyotoa takwimu kwa wale ambao tayari mashauri yao yamefikishwa mahakamani wametakiwa pia aidha kulipa faini lakini pamoja kurejesha fedha na endapo watahindwa kufanya vyote viwili basi watapata kifungo jela. Na kesi mbalimbali zimekuwa zikiendelea; tayari kesi 38 zilishamalizika mahakamani, tayari kuna majalada mengine ya uchunguzi 126 yanaendelea, lakini vilevile bado tunaendelea kuhakikisha kwamba tunakamilisha na wote walioshiriki basi wanafikishwa katika vyombo vya kisheria. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na kufanya kazi nzuri ya kupatikana kwa wafanyakazi hewa ambao takribani wataokoa zaidi ya shilingi bilioni kumi na Serikali inapaswa ijazie hizo nafasi kutokana na watumishi wengine. Lakini walio wengi ni wale wanavyuo ambao sasa wanakwenda kuanza vyo, lakini mpaka leo tunavyozungumza hawajapata mikopo wanahangaika. Je, kuendelea kutokuwapa mikopo hatuoni kwamba tunaweza tukazalisha hewa nyingine zaidi? Sasa Serikali iseme mpango mzima kwa nini mpaka leo mikopo ya wanafunzi baadhi hawajapata? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imekuwa ikisisitizwa katika nyakati tofauti tofauti ni kwamba kimsingi fedha kwa ajili ya mikopo kwa awamu hii zilishatolewa jumla ya shilingi bilioni 80 na tayari bajeti yake ipo sawa. Suala lililokuwa limetucheleweshwa lilikuwa ni suala la uhakiki kwa misingi kwamba watu wanaohitaji mikopo sio wote watakaoweza kupata kwa sababu fedha ambayo inatolewa ni kwa ajili ya watu wale ambao hasa wana uhitaji wa kupita wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivyo nina maana kwamba tumeangalia mikopo tu, lakini Serikali kupitia Wizara ina majukumu mengine makubwa sana ya kuangalia mfano tumeona vijana wetu wengi walikuwa wanakaa katika maeneo ambayo walikuwa wakijipangia wenyewe, mabweni yalikuwa yanakuwa hayapo, vitendea kazi vingine vilikuwa viepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyoangalia katika utoaji wa elimu tunaangalia Nyanja zote na haswa katika kuona kwamba elimu inatolewa kwa kiwango kinachostahili na kwa haki inayostahili mwanafunzi kuipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo wale wote ambao wanastahili kupata mikopo kutokana na uhitaji uliopimwa, mikopo yao itapatikana, lakini hata hivyo lazima tuzingatie kwamba mikopo hiyo inamfikia mlengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini ndani ya wiki hii tutakuwa tumefikia mahali pazuri zaidi. Ahsante *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nafikiri imeeleweka ingawa swali limeingia sio moja kwa moja, lakini naomba Serikali ilete kauli ya Bodi ya Mikopo ili Bunge nafikiri litaweza kufahamu vizuri zaidi. Mheshimiwa Waziri tunategemea kwamba mtaleta hiyo Kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tuendeleo na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano sasa namuita Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka.

Na. 9

Tatizo la Mawasiliano Wilaya ya Liwale

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijiji vya Mlembwe, Kimambi, Lilombe, Mirui, Mpigamiti, Kikulyungu na Mtungunyu vinapata miradi ya mawasiliano ya simu za mkononi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha usikivu hafifu wa matangazo ya Redio Tanzania (TBC – Taifa) katika Wilaya ya Liwale?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Mlembwe, Lilambwe, Mirui, Mpigamiti na Mtungunyu vimo katika orodha itakayofikishwa huduma ya mawasiliano na kampuni ya simu ya Halotel katika Awamu ya Nne inayotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2017. Aidha, kijiji cha Kikulyungu katika Kata ya Mkutano kitafikishiwa huduma ya simu na kampuni ya simu ya *TTCL* kupitia mradi wa Awamu ya Kwanza B, kwa jumla ya ruzuku ya dola za Kimarekani 143,280. Mradi huu unategemewa kukamilika mwezi Machi, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji Tanzania lina mitambo ya kurushia matangazo ya redio katika Mkoa wa Lindi kwa kutumia mitambo yake iliyopo Nachingwea eneo la Songambe na Lindi eneo la Kipihe. Hivi sasa mitambo ya redio ya masafa ya kati kilowati 100 iliyopo eneo la Songambe Wilayani Nachingwea haifanyi kazi kutokana na uchakavu. Mitambo ya Lindi eneo la Kipihe ni ya *FM* ambayo ni kilowati 2. Hali hii inasababisha maeneo mengi ya Mkoa wa Lindi na Mtwara kutopata usikivu mzuri wa matangazo ya redio ikiwemo Wilaya ya Liwale na mengine kutopata matangazo kabisa. Mitambo uliopo Kipihe, Lindi una uwezo wa kurusha matangazo katika maeneo ya Lindi Mjini na baadhi ya maeneo ya Lindi Vijijini. Shirika limeandaa mpango mahsusi wa kupanua usikivu nchi nzima ambao utekelezaji wake utategemea upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kujenga mitambo yenye uwezo wa kurusha matangazo maeneo yote yaliyoathirika na kutofanya kazi kwa mtambo wa Nachingwea wa kilowati 100. Mpango wa muda mrefu ni kuhakikisha kuwa TBC inanunua mitambo inayolingana na teknolojia ya kisasa katika tasnia ya utangazaji. Mpango huu utahusisha pia maeneo mengine ya nchi ambako mitambo ya masafa ya kati haifanyi kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya kutia matumaini. Lakini nataka ieleweke kwamba Wilaya ile ya Liwale ipo mbali sana na makao makuu ya Mkoa, Wilaya ya Liwale haina usafiri, haina barabara za kutosha yaani za kuaminika, Wilaya ya Liwale haina mtandao wa simu unaoaminika, Wilaya ya Liwale haina usikivu wa redio. Sasa muone jinsi Wilaya hii ilivyo kisiwani, hawa ni miongoni mwa walipa kodi wa nchi hii, sijui kama kodi zao watanufaika nazo

vipi? Nashukuru kwa jibu la kwanza nimepata *timeframe* na mimi nitafuatilia kuhakikisha hii *timeframe* inafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa swali la pili napata wasiwasi, nimepata tu majibu ya moja kwa moja. Nahitaji kujua ni lini Redio Tanzania itasikika Liwale? Hapa nimepewa tu majibu ya jumla jumla. Mwisho kabisa hapa amesema kwamba mpango wa muda mrefu sasa hata huo mpango wa muda mfupi nao haujatajwa, huo ni wa lini? Naomba nipatiwe majibu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Nape.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba usikivu wa Redio Tanzania kwenye maeneo mengi ya nchi yetu umekuwa na shida, na itakumbukwa wakati wa bajeti hapa tulionesha karibu nusu ya Wilaya za nchi yetu zilikuwa matangazo hayafikiki, na tulieleza kwamba hii ilitokana na kuhama kutoka kwenye mfumo wa zamani kwenda kwenye mfumo mpya; na mfumo mpya kwa kweli kwa hali ilivyo unahitaji uwekezaji mkubwa. Tulipoleta hapa mapendekezo na bajeti ikapitishwa, na tuliorodhesha wilaya ambazo tutakwenda awamu kwa awamu tukiboresha usikivu. Na Mikoa ya Kusini, ikiwemo Lindi na Mtwara ambapo Wilaya ya Liwale ni mojawapo ni katika Wilaya ambazo kipaumbele chake kipo na kwa bajeti hii iliyopitishwa tunaendelea na ukarabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea tayari tathmini imeshafanyika na uwekezaji katika eneo hilo baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo unaendelea, na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Liwale haitategemea mitambo iliyopo Lindi Mjini ambapo kwa kweli ni mbali kama alivyosema, badala yake tunawekeza kuunganisha Liwale, Nachingwea pamoja na Masasi na Newala ili tupate usikivu wa ukanda ule wa juu.

Na. 10

Daraja la Magara na Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Kumekuwa na ahadi za viongozi wa juu hususan Marais za kujenga daraja la Magara pamoja na barabara ya Mbuyu wa Mjerumani kwa kiwango cha lami na usanifu wa daraja na lami ya zege sehemu ya mlimani hasa ikizingatiwa kuwa ukosefu wa daraja na jiografia ya Mlima Magara kuwa hatarishi sana hasa kipindi cha mvua.

(a) Je, ni lini ahadi hiyo ya viongozi wetu wa Kitaifa itatekelezwa?

(b) Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kujenga barabara ya lami yenye urefu wa kilometa tano katika Mji wa Mbulu itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuunganisha Mji wa Mbulu na barabara Kuu ya Babati – Arusha katika eneo la Mbuyu wa Mjerumani. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Magara lenye urefu wa mita 84. Taratibu za kumpata mhandisi mshauri wa kusimamia ujenzi wa daraja hili zinaendelea. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), inafanya maandalizi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa daraja la Magara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya shilingi milioni 300 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja la Magara na shilingi milioni 455 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege (*rigid pavement*) kwenye Mlima Magara katika barabara ya Mbuyu wa Mjerumani hadi Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kutekeleza ahadi za viongozi wa Serikali kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ikiwemo ahadi ya ujenzi wa barabara ya lami katika Mji wa Mbulu yenye urefu wa kilometa tano.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nichukue nafasi hii kuuliza maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa kilio cha barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu ni ya muda mrefu na kwa kuwa barabara hii ndiyo inaunganisha Mji wa Babati na Mji wa Arusha kwa ajili ya wananchi wa Mbulu na kwa kuwa taarifa anayosoma Mheshimiwa Naibu Waziri ni taarifa aliyoandikiwa; wakati wa bajeti tulikubaliana fedha zote, karibu shilingi bilioni moja na milioni 200 zitumike kujenga daraja la Magara, na kwa sasa fedha zinazozungumzwa, shilingi milioni 300, ni hela ndogo sana.

Je, ni lini Naibu Waziri au Waziri mwenyewe mwenye dhamana ya Wizara hii atafanya ziara kujionea hali halisi ya mateso wanayopata wananchi wa Mji wa Mbulu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni katika uwanja wa Mbulu Mjini, aliahidi kuweka kilometa tano za lami katika Mji wa Mbulu kutokana na Mji wa Mbulu kuwa Mji mkongwe sana na kwa kuwa Rais aliahidi kwamba ahadi hii itatekelezwa katika bajeti ya mwaka 2015/2016.

Je, ni kitu gani kilipelekea ahadi ile isitekelezwe mpaka leo? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nitakuwa nimefika katika hiyo barabara na nitakujulisha lini, lakini kwa vyovyote itakuwa ni kabla ya mwezi Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ni suala la ukosefu wa fedha ndilo lililosababisha kipindi kilichopita kilometa tano za barabara hiyo zilizoahidiwa zisijengwe.

Naomba tu nikuhakikishie kwamba tunachukua kwa umuhimu mkubwa na tutaitekeleza hii ahadi ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne pamoja na wakati huo alikuwa Waziri wa Ujenzi walizitoa, nikuhakikishie kwamba tutazitekeleza.

Na. 11

Uhitaji wa Mahakama ya Mkalama

MHE. ALLAN J. KIULA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na kuteua Mahakimu wa Wilaya?

(b) Je, kwa nini Serikali isiridhie Mahakama ya Mwanzo iliyopo ifanywe kuwa Mahakama ya Wilaya?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wilaya ya kiutawa nchini inatakiwa kuwa na Mahakama ya Wilaya. Kutokana na utaratibu huu Serikali imekuwa ikijitahidi kwa kushirikiana na mahakama kuhakikisha kuwa wilaya zinazoanzishwa zinakuwa pia na huduma ya mahakama. Vigezo vinavyotumika kuanzisha mahakama katika eneo lolote ni pamoja na:-

- (i) Hati ya kisheria ya kuwepo kwa Wilaya, Mkoa au Kata;
- (ii) Umbali wa upatikanaji wa huduma za mahakama;
- (iii) Idadi ya wakazi wa eneo hilo;
- (iv) Uwepo wa huduma nyingine za Kiserikali kama Polisi na Magereza;
- (v) Upatikanaji wa rasilimali fedha, watu na miundombinu mingine kama viwanja na majengo; na
- (vi) Aina ya shughuli za kiuchumi na kijamii za eneo hilo zinazovuta aina fulani ya mashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto ya kukidhi baadhi ya vigezo nilivyoainisha hususan miundombinu, bado kuna Wilaya ambazo zinapata huduma ya mahakama kupitia Wilaya nyingine. Kwa sasa jumla ya Wilaya 21 nchini zinapata huduma ya mahakama kupitia Wilaya nyingine ikiwemo Wilaya ya Mkalama inayohudumiwa na Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imepanga kujenga jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, Mahakama imeomba kupatiwa kiwanja katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, bado mipango ya upatikanaji wa kiwanja hicho haijakamilika. Tunaiomba Halmashauri kupitia kwa Mheshimiwa Mbunge waweze kutupatia kiwanja hicho mapema ili kutuwezesha kujenga mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila ngazi ya mahakama ina mipaka yake kwa mujibu wa sheria na kanuni na hivyo kila moja inahitajika. Hivyo, hatuwezi kubadilisha Mahakama ya Mwanzo kutumika kama ya Wilaya. Aidha, kutokana na udogo wa jengo la Mahakama ya Mwanzo iliyopo sio rahisi kwa jengo hilo kutumika kwa Mahakama ya Wilaya na ya Mwanzo. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mkalama kuwa wastahimilivu wakati tunasubiri kujenga mahakama yao ya Wilaya.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuahidi kwamba mwaka wa fedha 2017/2018 tutaanza kujengewa mahakama, lakini cha pili nimhakikishie kwamba kiwanja atapata, kiwanja kipo. Sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wananchi wa Mkalama wanapata adha kubwa na wanakwenda kilometa zaidi ya 100 kupata huduma hiyo Kiomboi, katika kipindi hiki cha mpito haoni umuhimu wa kuanzisha mahakama ya Wilaya ya mpito kwa maana kwamba hiyo mahakama ya Wilaya iliyopo inaweza kuhamishiwa katika mahakama iliyopo Gumanga au Iyambi, takribani kilometa 15, ambazo kilometa 15 ni ndani ya kilometa zinazokubalika ili wananchi waanze kupata huduma hiyo wakati wakisubiri hilo jengo jipya na la kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Waziri atakuwa tayari kutembelea Wilaya ya Mkalama katika kipindi hiki cha Bunge, maana tukitawanyika hapa tunakuwa hatuonani tena, ili aweze kujionea uhitaji wa Mahakama ya Wilaya na aone viwanja vilivyopo kwa wingi na huduma nyingine za Mahakama za Mwanzo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze na suala la kutembelea MkaLama, Mheshimiwa Kiula nakuhakikishia mkipata kiwanja, kama unavyosema mmepata, lakini chenye nyaraka zote, hata kesho mimi nakuja na nitajitahidi nije na viongozi wa Mahakama kuwathibitishia wananchi kuwa tumedhamiria kuwamalizia tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naelewa *pressure* aliyonayo Mheshimiwa Kiula kuwapunguzia adha wananchi wa Wilaya mpya ya Mkalama. Namuomba Mheshimiwa avute subira, hiyo mikakati ya mpito haitakuwa na tija sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili yasijitokeze maswali mengine ya nyongeza, nimeona Wabunge wengi wamesimama, naomba niwatulize Waheshimiwa Wabunge wote kuwa katika mwaka huu wa fedha Mfuko wa Mahakama umetengewa jumla ya shilingi bilioni 46.76 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo, lakini katika fedha hiyo ujenzi wa mahakama ni shilingi bilioni 36; kwa hiyo ukiunganisha na pesa tuliyokuwa nayo mwaka 2015/2016 ya shilingi bilioni 12.3 tuna shilingi bilioni 48.3 kwa ujenzi wa mahakama. Fedha hizi zitatumika kujenga mahakama 40 nchini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ujenzi kwa mwaka 2015/2016 na 2016/2017 kwa fedha hii niliyoitamka itakuwa kama ifuatavyo ili Waheshimiwa Wabunge msisumbuke kusimama tena. Tunajenga Mahakama Kuu mpya nne katika Mikoa ya Mara, Kigoma, Dar es Salaam na Arusha.

Tunajenga Mahakama za Mikoa sita za Hakimu Mkazi, katika Mikoa ya Simiyu, Geita, Katavi, Njombe, Songwe na Lindi. Mahakama za Wilaya tunajenga 14 ambazo ni Bunda, Kilindi, Bukombe, Chato, Makete, Ruangwa,

Kondoa, Kasulu, Nkasi, Sikonge, Chamwino, Namtumbo, Nyasa na Hanang.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama za Mwanzo vilevile tunajenga mpya 16, tena katika kipindi kifupi. Tunajenga Mwanga, Makuyuni (Arusha), Ludewa Mjini, Longido, Lukuledi (Mtwara), Gairo (Morogoro), Nangaka (Nanyumbu), Makongorosi sasa hivi iko Mbeya, Ulyankulu (Tabora), Sangabuye (Nyamagana), Telati (Simanjiro), Mtowisa (Sumbawanga), Uyole (Mbeya), Kibaya (Kiteto), Mgandu (Wanging'ombe) na Chanika (Dar es Salaam).
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwamba katika ujenzi wa mahakama hizi, Mahakama kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi na Baraza la Taifa la Ujenzi watatumia ujenzi wa gharama nafuu, lakini majengo yatakuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetumia teknolojia hii mpya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Kibaha ambayo wengi mmeiona tena kwa gharama ndogo ya asilimia 40 chini ya bei ya kawaida ya hizi *conventional methods* tena kwa kipindi kifupi cha miezi mitatu tu na kwa kiwango kikubwa cha ubora wa jengo. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa nashukuru naona imetosheleza. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Waitara Mwita Mwikabe, Mbunge wa Ukonga.

Na. 12

Gharama za Upimaji Kuwa Juu

MHE. MWITA M. WAITARA aliuliza:-

Suala la Mpango Miji ni jema na mtu aliyepimiwa ardhi na kupata hati ya eneo lake huweza kutumia hati hiyo kukopa kirahisi lakini gharama za kupima ardhi ni kubwa sana kiasi kwamba wananchi walio wengi wanashindwa kupima maeneo yao.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kupunguza gharama za upimaji ardhi ili wananchi wengi zaidi waweze kupima maeneo yao na kuyaongezea thamani?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 12 la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa ardhi hapa nchini unafanywa na Wapima wa Ardhi wa Serikali walioajiriwa na Serikali na Wapima Binafsi walioajiriwa na Bodi ya Wapima Ardhi na kupewa leseni za biashara ya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Serikali, gharama za upimaji rasmi kwa sasa ni shilingi 300,000 kwa hekta ya shamba moja na kiwanja kimoja. Gharama hizi zilipunguzwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo kabla ya hapo zilikuwa shilingi 800,000 kwa hekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa za upimaji zinatokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Halmashauri nyingi hazijajengewa uwezo wa wataalam na vifaa na jukumu la kuajiri wataalam na kununua vifaa ni la Halmashauri yenyewe hivyo upungufu wa vifaa pamoja na wataalam ni mkubwa kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kwamba gharama za vifaa vya upimaji ni kubwa sana na upatikanaji wa seti moja ya kawaida ya upimaji kwa kutumia darubini ni shilingi milioni 18 kwa seti moja na GPS ni shilingi milioni 48. Ukubwa huu wa gharama na vifaa husababisha wapima wengi kutokuwa na uwezo wa kununua vifaa na hivyo kutegemea kukodi kwa gharama kubwa hivyo kufanya pia upimaji kuwa ghali ili kuweza kurejesha gharama za vifaa kwa sababu ni vya kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na ongezeko la gharama za upimaji nchini, Serikali ina mpango wa kusogeza huduma zote zinazotolewa Wizarani kwenda kwenye kanda. Hatua hii itawezesha kanda hizo kujengewa uwezo na hivyo kuchangia kupunguza gharama. Katika kuzijengea uwezo, Serikali inategemea kununua vifaa vya upimaji katika mradi wa *World Bank* na kuvigawa katika kanda zake ambavyo vitasaidia Halmashauri katika kanda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nitoe rai kwa Halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya upimaji pamoja na kuajiri wataalam wa kutosha katika kada hii ya upimaji na wengine wa sekta ya ardhi ili kuondokana na gharama kubwa za kukodisha vifaa hivyo kutoka katika taasisi binafsi. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Wa....

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Waitara, jina hili inabidi ulifahamu, jina rahisi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ameandika mwenyewe hapa kwamba gharama za upimaji ni shilingi 300,000 lakini mimi niliwaita hawa wahusika nikataka wanipimie eneo langu ambalo halifiki ekari mbili, wakafanya tathmini na wakaniambia nataka nilipe shilingi milioni tano, kwa hiyo nikapiga mahesabu wananchi wangu ambao wananzunguka pale Kivule na maeneo mengine wanawezaje kumudu hizo gharama kubwa za kupimiwa maeneo yao?

Kwa hiyo naomba kwanza anisaidie, gharama nilizopewa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ni milioni tano kwa eneo langu chini ya ekari mbili, yeye anasema hekta moja ni shilingi 300,000, na nini kauli yake sasa kwa maana ya maelekezo nchi nzima juu ya hili la upimaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba mimi nimeuliza swali langu ni hatua gani za dharura kwa sasa kwa sababu migogoro mingi ya ardhi iliyopo nchi nzima ni kwa sababu maeneo hayo kwa sehemu kubwa hayajapimwa na ikiwemo Dar es Salaam na watu wanasogeza mawe, kunakuwa na ugomvi mkubwa na kuna kesi nyingi katika mabaraza ya ardhi. Sasa nikataka mkakati wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema wana mpango wa kusogeza huduma, sasa naomba anisaidie, huu mpango walionao kuna bajeti yoyote ambayo imetengwa? Kwa sababu wakisema halmashauri inunue vifaa hivi ambavyo yeye mwenyewe amesema ni gharama, kama Waziri anakiri kwamba gharama ya vifaa vya upimaji wa ardhi ni kubwa Halmashauri ambayo haina fedha na imeomba fedha kutoka kwenye Bunge hili na Serikali hawajapeleka mpaka leo, hali ni mbaya, wao Serikali kwa maana ya hii Wizara wanasaidia nini katika mpango wa dharura kwa sasa ili huduma hizi ziweze kupatikana katika maeneo husika? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza maswali mawili, jambo la kwanza amesema, nimetaja kwamba gharama za upimaji ni 300,000 kwa hekta. Naomba niseme hizo ndizo gharama sahihi ambazo tulipitisha hapa kwenye kikao baada ya kupunguzwa ile awali iliyokuwa shilingi 800,000 na Bunge hili lilipitisha baada ya Mheshimiwa Waziri kuleta katika bajeti yake na kuomba ipunguzwe. Sasa kama

Manispaa inatozo lingine tofauti na wewe ni mmojawapo katika Manispaa hiyo, ni vizuri pia kujua kwa sababu *officially* tunachojua na kiko katika maandishi ni shilingi 300,000 lakini kama Halmashauri huwa wana mipango yao kule kutegemeana na Baraza lenyewe la Madiwani wameridhia nini katika lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu kuna mambo mengine ambayo yanafanyika ndani ya Halmashauri kutegemeana na mamlaka walizonazo, lakini katika *rate offial* zilizoko ni shilingi 300,000 kwa hekta moja na ni shilingi 300,000 hiyo hiyo kwa kiwanja kimoja. Sasa pengine itabidi tuwasiliane kuweza kujua kwanini wanatoza shilingi milioni tano kwasababu zipi za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ameongelea habari ya harakati zipi za dharura ambazo tunazifanya ili kupunguza hilo na ni bajeti gani imetengwa. Naomba niseme; bajeti tuliyopitisha hapa Wizara ilileta bajeti ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya kununua vifaa hivyo na tayari mchakato wa kununua umeshaanza na kwa sababu uko chini ya Benki ya Dunia ambao ndio wafadhili, mchakato ndani ya Wizara tumeshamaliza, tunachosubiri tu ni ile *no objection* kutoka Benki ya Dunia, wakishapitisha sisi hatuna tatizo kwasababu tayari ipo na tulisema itakwenda katika kanda zote nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, harakati za dharura ambazo tunafanya sisi ndiyo katika hizo lakini bado tulishasema kuna makampuni zaidi ya 58 ambayo yapo na Halmashauri inaweza kuyatumia, Wizara imesharidhia yafanye kazi hiyo ili kuondokana na tatizo hili. Kama Wizara tunafanya kazi ya urasimishaji katika maeneo ambayo hayako vizuri, kwahiylo hilo naweza kujibu kuwa ndizo hasa harakati zetu tunazofanya kuhakikisha tatizo hilo linaondoka.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini.

Na. 13

Hitaji la Umeme

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Mtambula, Idunda, Maduma, Kiyowela na Idete ili wananchi waweze kufaidika na huduma hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa ya kiti chako, niombe dakika moja niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kabla sijajielekeza kwenye kujibu maswali yaliyoulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge jinsi ambavyo walijitoa kwenye msiba mzito wa mama yangu uliotokea wiki tatu zilizopita, nawashukuru sana na ningependa kwa ruhusa yako kwa uwakilishi wa Waheshimiwa Wabunge niwatambue wachache walioweza kufanikiwa kufika Chato kwa ajili ya msiba, lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ridhaa hiyo. Baada ya kusema hayo Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na madini, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kufikisha umeme nchi nzima ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijiji vya Mufindi Kusini. Vijiji vya Kata ya Idete, Idunda, Kiyowela, Maduma pamoja na Mtambula vitapatiwa umeme kupitia mradi kabambe wa REA Awamu ya Tatu unaoanza Disemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo nilivyovitaja vya Wilaya ya Mufindi itahusisha itahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *kilovolt* 33 yenye urefu wa kilometa 242, ujenzi wa njia ya msongo wa *kilovolt* 0.4 yanye urefu wa kilometa 81, ufungaji wa *transformer* 24 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 3,533. Kazi inatarajiwa kuanza mwezi huu wa Disemba, 2016 na kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 11.92. (*Makofi*)

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina maswali mawili tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; katika upelekaji wa umeme vijijini, REA wanapeleka kwa kufuata barabara na kwenye *centres*, lakini unaweza ukaona kwamba kwenye shule za msingi, sekondari, vituo vya afya na zahanati kule umeme haupelekwi. Sasa Naibu Waziri naomba anihakikishie wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kwenye maeneo haya niliyotaja kama watapewa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti la pili, namuomba Naibu Waziri, kwa majibu haya aliyoeleza vizuri, kwa programu ya awamu ya tatu ambayo inaanza, je, utakuja lini Mufindi ukafanya mkutano angalau hata mmoja kuongea na wale wananchi? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba mradi kabambe wa REA Awamu ya Tatu utapeleka umeme katika maeneo yote ya taasisi ikiwemo shule za msingi, sekondari, hospitali na katika taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Kigola, jimbo lako la Mufindi Kusini, maeneo yote niliyoyataja ikiwemo pia katika vijiji vyako vya Mbaramaziwa, Tambarang'ombe kwenda mpaka Tengereo mpaka kule Kilowelo vitapelekewa umeme kwenye taasisi nilizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala lake la pili, kwamba ni lini sasa tutatembelea katika maeneo yale? Nimhakikishie Mheshimiwa Kigola; kwanza kabisa nikupongeze umeshaanza kuchimba visima kwa ajili ya kuhitaji umeme. Napongeza sana kwenye Kitongoji chako cha Msumbiji umeshaanza kujenga, lakini pale Idambaravumo pia umeshaanza kujenga na pia unatarajia kupeleka umeme pale *Kilowelo centre*, na pia kwenye vijiji vyako vingi sana ikiwemo kama nilivyosema pale Kisaula tutakupelekea mashine ya umeme, lakini pia kwenye vijiji vyako vingine mbali na vijiji na Kitongoji cha Msumbiji na pale Changarawe kwa Mheshimiwa Kigola kwa vijiji vyako 47 vilivyobaki vyote vitapata umeme wa uhakika.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Kwa kuwa tatizo linalowakabili wananchi wa Mufindi Kusini linafanana sana na wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini; nilitaka kusikia kauli ya Waziri, katika kata ya Migua, jimbo la Nzega Mjini, Kata za Mwanzoli, Mbogwe, maeneo ya Bulunde pamoja na Kashishi yote haya yalikuwa yapekelewe umeme kwa miradi ya MCC na miradi hii imefutwa. Je, Naibu Waziri anasema kauli gani kuwaambia wananchi wa jimbo la Nzega wa maeneo haya juu ya upatikanaji wa uhakika wa umeme katika maneo niliyoyataja? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipende tu kusema wazi kwamba miradi yote iliyokuwa chini ya MCC ambayo haikuendelea sasa itapelekewa umeme kwa bajeti ambayo tumeipitisha kupitia mradi wa REA wa Awamu ya Tatu ikiwemo pamoja na vijiji kwa Mheshimiwa Bashe alivyovitaja kwenye jimbo lake. Lakini niseme tu, kijiji cha Kashishi tulishaanza kufanyia survey lakini pia vijiji vya Mbogwe na vingine

vya karibu tulishaanza kuvifanyia survey na vyote vitapelekewa umeme kwenye kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako mimi nitatembelea kwa Mheshimiwa Kigola mara tukimaliza Bunge, pia nitatembelea kwa Mheshimiwa Bashe na maeneo mengine kuhakikisha maeneo yote yanapata umeme.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

Na.14

Usambazaji wa Umeme Nchini

MHE. HUSSEIN N. AMAR aliuliza:-

Serikali imekuwa na ahadi nyingi, nzuri za kutekeleza katika kusambaza umeme kwenye maeneo mengi ya nchi yetu.

(a) Katika Wilaya ya Nyang'hwale ni vijiji vitatu tu vya Nyang'hwale, Nyarubele, Busegwa na Makao Makuu ya Wilaya ambavyo vina umeme; je, katika bajeti ijayo ni vijiji vingapi vya Jimbo la Nyang'hwale vitapatiwa umeme?

(b) Je, kwa nini nguzo haziletwi Kharumwa wakati wateja wengi tayari wamefanya wiring kwenye nyumba zao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vijiji 61 katika jimbo la Nyang'hwale vitapatiwa umeme katika utakekezaji wa mradi kabambe wa REA Awamu ya Tatu. Kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolt 33 yenye urefu wa kilometa 50, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolt 0.4 yenye urefu wa kilometa 372 na ufungaji wa transformer 24 pamoja na kuunganishia umeme wateja wa awali 3,578. Kazi hizi zitaanza mwezi Disemba mwaka huu na kukamilika mwaka wa fedha 2019/2020. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 6.23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kharumwa ambacho ni makao makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale tayari kimepatiwa umeme na kazi ya kupeleka nguzo inaendelea. Hata hivyo TANESCO inakamilisha kazi za kuunganishia

umeme wateja wapya wa Kharumwa kadri maombi yataavyofikiwa. Mpaka mwisho wa mwezi wa Disemba mwaka huu vijiji vya Kharumwa vitakuwa vimepata umeme.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya matumaini kwa wananchi wa jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika kijiji cha Busorwa pameshasimikwa nguzo, nyaya zimetandazwa na *transformer* zimeshafungwa takribani zaidi ya miezi minane, kwa nini umeme kijiji cha Busorwa haujawashwa?

Na kwa kuwa kuna baadhi ya vijiji kama vile Izunya, Nyashilanga, Nyamikonze, Nyijundu nguzo na nyaya za umeme zimeshatandazwa lakini *transformer* hazijafungwa. Ni lini *transformer* hizo zitafungwa ili umeme huo uweze kuwashwa na kuweza kuchochea maendeleo katika vijiji hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Naibu Waziri nakuomba baada ya Bunge hili tuongozane pamoja mimi na wewe ukaone mradi huu unavyosuasua ili uweze kuleta changamoto ili mradi huu uweze kwenda haraka ili wananchi wa jimbo la Nyang'hwale waweze kupata maendeleo kupitia umeme, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika Jimbo la Nyang'hwale ni vijiji vitatu tu ambavyo vimeshaunganishiwa umeme, na nitoe masahihisho kidogo, Mheshimiwa na wala siyo vijiji 61, vijiji 62 mbavyo bado kwenye jimbo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Busorwa ambacho tayari kina *transformer* na tayari kina nyaya zimeshafungwa kulikuwa na shida ndogo tu ya vikombe ambavyo vilikuwa havijakamilika, na hivi leo vimekamilika kesho saa tisa mchana Mheshimiwa Hussein wanakuwashia umeme pale Busorwa na mtapata umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini vijiji alivyovitaja vitapata umeme. Ametaja vijiji vitatu lakini kuna vijiji 66 ambavyo vimepatiwa kwa nusu lakini vijiji 40 vikiwemo vijiji vya Busorwa kama ulivyotaja, Kakora, Kanegere, Nyamitongo, Nyabushishi, Nyaruzugwa, Nyaruyeye na Izuguna bado havijapatiwa umeme, kwa hiyo vyote tunavipelekea umeme kama ambavyo nimetaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongezana naye, kwa idhini yako kama ningepeta nafasi ningependa kwenda kushuhudia vijiji vitano ambavyo amevitaja vya Nyashilanga, Nyamikonze na Izunya ambavyo vitawashwa umeme Ijumaa ijayo. Lakini kwa ridhaa yako niombe kuongozana nawe Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili ili tukawashe umeme kwenye vijiji vyako kama ambavyo nimekusudia, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Mbunge wa Kahama Mjini.

Na.15

Kuingia Ubia Katika Ununuzi wa Vifaa Tiba

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA aliuliza:-

Hospitali nyingi nchini ikiwemo zilizo katika mji wa Kahama zina upungufu mkubwa wa vifaa tiba kama *x-ray* na *ultra-sound*. Nchi ya Kenya baada ya kutambua changamoto ya upungufu wa vifaa tiba ilitunga sera kuhusu kampuni binafsi kuingia ubia na hospitali kununua vifaa tiba na kugawana mapato yanayotokana na vifaa hivyo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiga mfano huo mzuri wa Kenya ili kunusuru maisha ya wagonjwa wetu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya inatambua *modules* mbalimbali na Serikali inaendelea kuangalia ni kwa jinsi gani inaweza kuzitumia katika eneo hilo. Aidha, Serikali inaendelea kununua vifaa na vifaa tiba na kusambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya kulingana na uhitaji wa eneo husika. Sanjari na hilo, tunaendelea kuangalia mikataba hii ya kampuni binafsi ni kwa jinsi gani tunaweza kuichukua na kuitekeleza katika kusaidia upatikanaji wa vifaa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vyetu vya kutolea huduma za afya hapa nchini.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu yasiyoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za vipimo ni kubwa mno kwa wananchi wetu maskini ambao tunawawakilisha. Nafikiri ni vizuri Waziri akatamka ni lini ataruhusu watu binafsi kuweka x-ray na vipimo vingine kwenye hospitali za binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii x-ray ziko madukani, Waziri yuko tayari kwenda kufunga hospitali ya mtu lakini hayuko tayari kuamrisha x-ray zilizoko madukani ziende kwenye hospitali za Serikali ili zihudumie wananchi wetu wanaokufa kila siku.

Kama kwa nchi nzima suala hili haliwezekani, namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri lifanyiwe majaribio kwenye Halmashauri ya Mji wa Kahama ambapo hospitali hiyo inahudumia zaidi ya Halmashauri 15 ikiwemo na Halmashauri ya kwake mwenyewe. Naomba majibu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba kwa swali lake la nyongeza na nimpongeze kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya kuwahudumia wananchi wa jimbo lake la Kahama Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubunifu anaouzungumzia wa kutumia watu binafsi kutekeleza miradi mbalimbali ya kufunga vifaa na vifaa tiba vya kutolea huduma za afya hususani vya uchuguzi wa magonjwa kama x-ray na *ultra-sound* kwenye hospitali za Serikali ni ubunifu ambao tunaukubali. Anasema ni lini mimi nitaruhusu kwenye Wizara yetu; napenda kumtaarifu tu kwamba Serikali tayari inaruhusu ubia wa sekta binafsi na Serikali (*Public Private Partnership – PPP*) na ina sheria mahususi ambayo ilitungwa na Bunge hili miaka kadhaa iliyopita kwa hivyo siyo jambo jipya; sema *modality* ya mikataba hii iweje na nani afunge lini na mkataba na nani na kwa sababu zipi ndizo taratibu ambazo tunazitazama siku hata siku na tunazitazama kwa kesi kadri zinavyokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kama Halmashauri ya Kahama Mjini inapenda kufanya mikataba ya namna hiyo Mheshimiwa Mbunge azungumze na wataalam kwenye Halmashauri yake, wafuate taratibu za ndani ya Serikali za kuingia mikataba ya *PPP* ili waweze kupata vibali kutoka Hazina, Wizara ya Afya na TAMISEMI waweze kutekeleza mipango hiyo ila ni jambo ambalo tunalikubali.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tumemaliza muda wetu wa maswali.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MBUNGE FULANI: Mwongozo Mwenyekiti.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mwongozo Mwenyekiti.

MWEYEKITI: Tafadhali naomba mkae tuna matangazo kwanza Mwongozo baadae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Okay.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nitaanza na matangazo ya wageni walioko Bungeni asubuhi hii, ambapo tunaye mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Balozi wa Rwanda nchini Tanzania, Mheshimiwa Eugene S. Kayihura. Mheshimiwa Balozi karibu sana.

Wageni wengine ni Wageni watano wa Mheshimiwa Freeman Mbowe ambao ni viongozi na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wanaotokea jijini Dar es salaam ambao ni Mheshimiwa Fredrick Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu, wengine ni Profesa Abdallah Safari, Profesa Mwesiga Baregu pamoja na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi/Vigelegele)*

Wageni wengine ni wageni wa Wabunge wa Wanawake Tanzania (TWPG) ambaye ni Mheshimiwa Getrude Mongella. Mheshimiwa Getrude ni Rais Mstaafu wa Bunge la Afrika, karibu sana. *(Makofi/vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Na wale sio Mawaziri Wakuu.

MWENYEKITI: Wageni wengine ni wageni kumi kutoka Bunge la Zimbabwe ambao ni Wajumbe wa Umoja wa Wabunge Wanawake kutoka Bunge la Zimbabwe *(Zimbabwe Women Parliamentary Caucus)* ambao ni Mheshimiwa Paulina Mpariwa, Kiongozi wa msafara, Mheshimiwa Melody Dziva, Mheshimiwa Metrine Mudau, Mheshimiwa Dorothy Mangami, Mheshimiwa Sabina Thembani, Mheshimiwa Alice Chimbudzi, Mheshimiwa Ethel Mabhugu. Wengine ni Mheshimiwa Margaret Matienga, Mheshimiwa Christine Mafoko na Mheshimiwa Fari Hondonga. Karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu.

Matangazo mengine ni tangazo la Mwenyekiti wa Ibada, Mheshimiwa Anna Lupembe, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa makanisa ya CCT kwamba wahudhuri ibada katika jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili leo Jumanne tarehe 1 Novemba, 2016 mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge. Aidha, wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma watahudhuria Ibada hiyo.

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo 1 Novemba, 2016 saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Msekwa C.

Tangazo lingine ni kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Suzan Lyimo anawatangazia Wabunge wanawake wa TWPG kuwa leo tarehe 1 Novemba, 2016 kutakuwa na seminar kwa ajili ya Wabunge wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi mkubwa wa Msekwa kuanzia saa saba mchana na msemaji mkuu katika semina hiyo atakuwa Mama Balozi Getrude Mongella. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumemaliza matangazo.

Kwanza Waheshimiwa Wabunge nafikiri mlikuwa mnapiga makofi mengi, nilishasema kwamba Mheshimiwa Lowassa ni Waziri Mkuu Mstaafu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hukusema.

MWENYEKITI: Nilitamka lakini mlikuwa mnapiga makofi mengi, kwa hiyo natamka rasmi kwamba ni Waziri Mkuu Mstaafu. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sumaye....

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Wote wawili niliwataja, na naomba...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo si kazi yako, endelea, wasikubabaishe.

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba tuendeleo nimeshayamaliza hayo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mheshimiwa pale, Mheshimiwa Kangi Lugola na ninyi huku wawili haya. Mheshimiwa Lwakatare na Mheshimiwa Mtolea. Wawili huku na wawili huku. Tunaanza na Mheshimiwa Ahmed.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama hapa kwa Kanuni ya 69, kwamba Mbunge anaweza kutoa hoja ya dharura baada ya kipindi hii cha asubuhi cha maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na majibu kutoka Serikali ambayo kwa kweli mimi binafsi nayaona hayaniridhishi kwenye suala zima la Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bandari hoja kubwa pale ni kwamba tumekuwa tunapoteza mapato makubwa sana. Mapato yale yangeweza kufanyiwa kazi vizuri, yangeweza kurekebishwa ili sasa wale ambao walikimbia kutumia bandari yetu waweze kurudi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya dharura kwamba tuahirishe shughuli zote za Bunge ili tuweze kujadili hoja hii na kuishauri Serikali namna bora na nzuri ya kuweza kurudisha *confidence* kwa wale ambao walikuwa wanaitumia bandari yetu ya nchi jirani waweze kuja kuitumia na mapato ya Serikali yaweze kiurudi kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kutoa hoja.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo chini ya Kanuni 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa Elimu anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo linalohusu masuala ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, macho yangu na masikio yangu yameshuhudia maelezo aliyokuwa anayota Mheshimiwa Naibu Waziri kana kwamba jambo hili la mikopo ya elimu ya juu ni jambo ambalo ni la kawaida hivi, halina uzito wowote, ilhali hali ya utoaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wetu imekuwa na matatizo makubwa, na mpaka sasa tunavyozungumza wanafunzi wengi hawajapa mikopo licha ya Serikali kuendelea kutoa kauli kwamba wako mbioni kujaribu kutoa mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili ni jambo linalohitaji uharaka, kwa nini kiti chako kisiombe Wizara ya Elimu waletе kauli Bungeni hapa kesho kwa maana ya *timeframe* ya kesho ili masuala haya yazungumzwe Bungeni hapa, na endapo itaonekana kwamba Wabunge wanahitaji kuyajadili basi suala hilo liweze kujadiliwa hapa Bungeni, vinginevyo tunakwenda kuua elimu ya nchi yetu kwa sababu wanafunzi ambao wanatoka vijijini ambako ni watu maskini, wanafunzi wanatoka shule za kata wanapata wengine *division one form six* wana matokeo mazuri lakini wamekosa mikopo awamu hii ya Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba uielekeze Serikali kesho ilete kauli yake hapa ya masuala ya utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Nimeshaona mmeunga mkono. Haya, Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimesimama hapa kwa Kanuni ya 68(7) kwa kuheshimu muda ulivyotutupa mkono naomba nisisome, lakini kinachonifanya niombe Mwongozo hapa ni kusiginwa kwa Kanuni ya 37(2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 37(2) inasema nakala za Matoleo yote ya Gazeti pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita zitawasilishwa Bungeni na Waziri na kugawiwa kwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matoleo ya Magazeti ambayo leo Serikali imeyawasilisha hapa Bungeni hatujapata nakala zake, jambo hili limekuwa likijirudia mara kwa mara. Toka nimekuwa Mbunge wa Bunge hili la Kumi na Moja sijawahi kuona Kanuni hii ikiheshimiwa na Serikali. Sasa naomba Mwongozo wako ni kwanini Serikali inachagua Kanuni za kuzifuata na Kanuni nyingine inazisigina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo. *(Makofi)*

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesimama kwa Kanuni ya 47(3) kuomba mjadala ulioko mbele yetu uahirishwe ili tuweze kujadili jambo halisi na la dharura ambalo linatokea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ya leo nimepokea simu kutoka Tarime, hospitali hazina dawa, kituo cha afya, Nyamongo watu wamepata matatizo pale mgodini wamekimbizwa pale hakuna dawa na watu wanakufa ovyo na Serikali iko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niliomba Wabunge waniunge mkono kwa sababu hili ni jambo la Kitaifa. Tujadili uhai wa watu wetu waliotutuma hapa kwasababu hakuna dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimepokea miongozo hiyo minne.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti ulisema utanipa nafasi kuomba mwongozo, tafadhali naomba sana.

MWENYEKITI: Nilisema wawili huku, wawili huku, kwa hiyo Mheshimiwa Heche amesha wasilisha.

MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti nilitaja Waitara.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bado Haonga hapa.

MWENYEKITI: Naanza na Mwongozo wa Mheshimiwa Ahmed huyo kuhusu suala la bandari. Mwongozo wangu ni kwamba suala hili liko kwenye Kamati ya PAC na itabidi tsubiri taarifa kutoka Kamati hiyo PAC kwa hiyo tutasubiri taarifa hiyo. Baadae tutaweza kujadili suala hilo.

Lakini kuna suala la Mheshimiwa Kangi Lugola kuhusu mikopo ya elimu ya juu tayari nimeshaiagiza Serikali iweze kuleta kauli yake kuhusiana na suala hili, kwa hiyo hilo tayari limeshaeleweka.

Kuhusu Mwongozo wa Mheshimiwa Mtolea, hilo nimelichukua kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1) na 68(10) nitalitolea Mwongozo wake baadae lakini pia na hili suala la Mheshimiwa Heche sioni kama ni dharura kwa sasa hivi kwa hivyo litatolewa Mwongozo wake baadae.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea maelekezo ya kiti chako ya kuleta taarifa kuhusiana na Bodi ya Mikopo na ni lazima tukaiandae taarifa ambayo itatosha kuwasilishwa Bungeni na tutawasiliana na Ofisi yako ili tuweze kuiwasilisha.

Kuhusu suala la magazeti tuliyoyasoma hapa asubuhi, tumeshawasilisha Ofisi ya Bunge, na kazi ya Serikali ni kuyawasilisha Ofisi ya Bunge na Ofisi ya Bunge itachukua hatua ya pili, na inawezekana tayari yameshawekwa kwenye *pigeonholes* kwa hiyo sisi kazi yetu ni kuwasilisha kwa barua, na ninayo kumbukumbu ya barua ambayo tumeitumia kuwasilisha magazeti hayo kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaheshimu maagizo yako na tutayatekeleza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, naomba sasa Hoja ya Kutengua Kanuni.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkutano wa Tano wa Bunge umepangwa kufanyika kwa siku tisa za kazi kuanzia tarehe 1 Novemba, 2016 hadi tarehe 11 Novemba, 2016 na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) kwa siku zisizopungua tano Bunge linatakiwa kukaa kama Kamati ya Mipango, kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata; na kwa kuwa Kanuni ya 28(15) inaelekeza kwamba Bunge halitaendelea na shughuli zake siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko; na kwa kuwa shughuli zilizopo haziwezi kufanyika kwa ufanisi na kukamilika ndani ya muda wa siku tisa zilizotengwa kwa ajili ya Mkutano huu.

Hivyo basi Mheshimiwa Mwenyekiti ili kuliwezesha Bunge kutekeleza kazi zake kiufanisi na kuweza kumaliza shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano wa Tano, Kamati ya Uongozi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 31 Oktoba, 2016 iliafiki kwamba Kanuni ya 94(1) na Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, tole la Januari 2016 zitenguliwe kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 94(1) itenguliwe ili Bunge litumie siku tatu kukaa kama Kamati ya Mipango badala ya siku tano zilizotakiwa na Kanuni hii, Kanuni ya 28(15) itenguliwe ili Bunge likutane siku ya Jumamosi tarehe 5 Novemba, 2016 isipokuwa siku hiyo Bunge litaanza saa tatu asubuhi hadi saa nane mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

MWENYEKITI: Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa mwaka 2017/2018 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2017/2018 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na hivyo kuweza kukutana katika Mkutano huu wa Tano wa Bunge la Kumi na Moja ili kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 ambayo ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) ambao una dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa ushirikiano wao waliotupatia wakati wa kujadili mapendekezo haya. Maelekezo

na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa majadiliano yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha maandalizi ya Mpango na Mwongozo kufikia hatua hii ya kuyafikisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuipatia Kamati hii ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake na kuzingatia maelekezo yanayotolewa katika hatua mbali mbali za uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya ushauri mzuri na maoni ya Kamati maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambayo yatazingatiwa katika maandalizi ya Mpango wa 2017/2018 na Mwongozo ni yafuatayo:-

(i) Umuhimu wa kushirikisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo ya Taifa;

(ii) Maendeleo ya viwanda vidogo vidogo (*SIDO*) na maeneo ya *EPZA* na *SEZ* yapewe msukumo ili kuiwezesha nchi kuingia haraka katika uchumi wa viwanda;

(iii) Kuweka mfumo wa kulinda masoko ya bidhaa za ndani;

(iv) Kuchagua miradi michache ya kipaumbele kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti;

(v) Kukamilisha miradi ya maji na umwagiliaji kabla ya kuanza miradi mipya; na

(vi) Kuendelea na Mpango wa kurasimisha biashara na mali za wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Doto Mgosha James kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya mapendekezo na Mpango ninayoyawasilisha sasa. Aidha, tunawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, sekta binafsi na wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango yao katika kukamilisha mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Jodeph Magufuli, lakini pia Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kutoa pole kwa ndugu, jamaa na

marafiki waliopatwa na janga la tetemeko la ardhi lilitokea katika Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza na Mara Septemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha yamezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi; hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja, maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naomba tafadhali utulivu Bungeni mnazungumza sana kwa sauti.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: ...Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na malengo endelevu sanjari na makubaliano ya kikanda, baina ya Tanzania na nchi nyingine na makubaliano ya kimataifa yaliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha na malengo ya uchumi jumla:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2017, asilimia 7.9 mwaka 2018 na asilimia 8.2 mwaka 2019;

(ii) Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia 5 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Kuwa na Pato ghafi la Taifa la shilingi trilioni 123.9 mwaka 2017/2018; shilingi trilioni 139.7 mwaka 2018/2019; na shilingi trilioni 165.4 mwaka 2019/2020;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 14.6 ya Pato la Taifa mwaka 2017/2018; asilimia 15.5 mwaka 2018/2019 na asilimia 15.8 mwaka 2019/2020;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 26.6 ya Pato la Taifa mwaka 2017/2018, asilimia 26.5 mwaka 2018/2019 na asilimia 25.5 mwaka 2019/2020;

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha muda wa kati misingi ya mpango na bajeti yatakuwa ni pamoja na amani, usalama, utulivu na utangamano wa ndani na katika nchi jirani kuendelea kuimarishwa na kudumishwa, viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, mfumuko wa bei, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii kuendelea kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia uchumi wa dunia kuendelea kuimarika na kutengemaa, bei za mafuta katika Soko la Dunia hazitaongezeka, hali ya hewa nchini na katika nchi jirani kuwa nzuri, mahusiano na nchi jirani, kikanda na kimataifa kuendelea kuwa mazuri mapoja na kuwepo kwa sheria na taratibu wezeshi kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kidogo kuhusu mwenendo wa uchumi. Katika nusu ya kwanza (Januari hadi Juni) ya mwaka 2016, Pato ghafi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 52.7 ikilinganishwa na shilingi trilioni 45.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Aidha, katika kipindi hicho ukuaji halisi wa uchumi ulifikia asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Na matarajio ni kufikia ukuaji wa asilimia 7.2 katika mwaka huu wa 2016. Mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 6.5 Januari, 2016 hadi asilimia 5.5 Juni, 2016 na umeendelea kupungua zaidi hadi asilimia 4.5 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ukwasi kwenye uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha sambamba na sera thabiti za fedha katika kusimamia mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa hali ya ukwasi inaendana na mahitaji halisi ya kiuchumi. Hadi mwezi Septemba, 2016 ukuaji wa ujazi wa fedha katika tafsiri pana (M3) uliongezeka kwa shilingi bilioni 913 hadi kufikia shilingi bilioni 22,194.8 sawa na ukuaji wa asilimia 4.3. Katika kipindi kama hicho mwaka uliopita ujazi wa fedha uliongezeka kwa shilingi bilioni 3007.5 hadi kufikia shilingi bilioni 21, 281.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi umeendelea kuongezeka kulingana na mahitaji halisi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ambapo kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2016 mikopo iliongezeka kwa shilingi bilioni 1,744 hadi kufikia shilingi bilioni 16, 622.8 sawa na ukuaji wa asilimia 11.7. Katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia mikopo iliongezeka kwa shilingi bilioni 2,935.8 hadi kufikia shilingi bilioni 14,878.8 sawa na ukuaji wa asilimia 24.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kibenki imeendelea kukua katika kipindi cha mwaka unaoishia Septemba, 2016, na takwimu za awali za tathmini ya hali ya mabanki yetu zinaonesha kuwa mabanki yetu ni imara na salama yakiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Hadi mwezi Septemba, 2016 kulikuwa na jumla ya mabanki na taasisi za fedha zinazosimamiwa na benki kuu zipatazo 66 zenye matawi 783 nchini kote.

Kiwango cha mitaji ikilinganishwa na mali iliyowekezwa (*total capital to total risk weighted assets and of balance sheet exposure*) kilikuwa asilimia 19.08 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 12. Kiwango cha mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa

na viwango vya amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi (*liquidity assets to demand liabilities*) kilifikia asilimia 34.18 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ubora wa rasilimali za mabanki ulipungua kidogo kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu kufikia asilimia 9.06 ya mikopo yote mwezi Septemba 2016 ikilinganishwa na asilimia 6.71 mwezi Septemba 2015. Hata hivyo ubora wa rasilimali za benki nyingi uliendelea kubaki ndani ya ukomo wa asilimia tano na benki ambazo bado zina kiwango cha juu zaidi ya asilimia tano zinatakiwa kuchukua jitihada za kuhakikisha kuwa ubora wa rasilimali zao unaimarika na kubaki ndani ya kiwango cha asilimia tano kinachotakiwa na benki kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mauzo na bidhaa na huduma kutoka nje katika kipindi kinachoishia Julai 2016 ilikuwa dola za Kimarekani milioni 9,810.4 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 9,128.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Kwa upande mwingine thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ilipungua kwa asilimia 18.3 kutoka dola za Kimarekani milioni 13,569 Julai, 2015 hadi dola za Kimarekani milioni 11,003.4 Julai, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya fedha za kigeni imebaki kuwa imara ikiwa na dola za kimarekani milioni 4,096.0 kufikia mwisho wa Septemba 2016, ambao ni uwezo wa kutosheleza uagizaji nje wa bidhaa na hudumu kwa kipindi cha miezi minne bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya uwekezaji wa moja kwa moja nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Taifa lilifikia dola za Kimarekani milioni 18,614.93 sawa na ongezeko la asilimia 9.76 kufikia Juni 2016, ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 16,959.47 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya iliyochukuliwa kugharamia miradi ya maendeleo na hasa ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, barabara na madaraja. Maelezo kuhusu mwenendo wa uchumi yapo katika aya ya 12 hadi ya 19 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nieleze maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni miradi ya kielelezo. Miradi hii itajumuisha makaa ya mawe Mchuchuma, chuma Liganga, kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge* na matawi yake, kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi mkoani Lindi, uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi, uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini, kusomesha vijana katika stadi maalum hasa mafuta na gesi, uhandisi na

huduma za afya, uanzishwaji wa Mji wa Kilimo wa Mkulazi, ununuzi na ukarabati wa meli kwenye Maziwa Makuu, ujenzi wa barabara za Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310) lakini pia barabara ya Masasi - Songea – Mbamba Bay (km 868.7).

Pili ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda. Miradi itakayozingatiwa ni pamoja na uendelezaji wa maeneo ya viwanda vidogo – *SIDO* katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha; uendelezaji wa eneo la viwanda *TAMCO*, *EPZA* na *SEZ*, Bandari Kavu (Pwani), Mradi wa Magadi Soda Bonde la Engaruka, kufufua kiwanda cha *General Tyre*, Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga na uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda hasa vile vinavyotumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni kufungamanisha maendeleo ya uchumi, na maendeleo ya watu, na katika eneo hili kipaumbele ni kitakuwa katika elimu na mafunzo ya ufundi, afya na maji kama ilivyoainishwa katika aya ya 28 mpaka 30 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji, na maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na kuendelea na miradi iliyoanza kutekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, miradi itakayotekelezwa chini ya utaratibu wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Maelezo ya kina kuhusu mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yapo katika aya ya 30 na 31 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa. Maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, utawala bora na utawala wa sheria, miradi katika maeneo ya misitu, ardhi, nyumba na makazi lakini pia madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe maelezo kuhusu Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18. Mwongozo huo unawaelekeza Maafisa Masuuli masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa mipango na bajeti za mafungu yao. Maelezo ya mwongozo yanajumuisha utekelezaji wa Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015 na kanuni zake, usimamizi na uhibitaji wa matumizi, ulipaji na uzuiaji wa ongezeko la madeni ya Serikali, ukusanyaji wa mapato, mfumo wa bajeti wa mwaka 2017/2018 na mfumo wa utoaji taarifa za utekelezaji. Aidha, Mwongozo unatoa mapendekezo ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mwongozo wa mwaka 2017/2018 ni mwendelezo wa utekelezaji wa maelekezo ya msingi yaliyotolewa na Serikali katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha. Baadhi ya maelekezo hayo ni pamoja na mapato yote kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo kufuta utaratibu wa *retention*, kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na kudai stakabadhi kwa bidhaa na huduma zilizotolewa; ukusanyaji wa kodi ya majengo kusimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kutumia taasisi za umma katika huduma za bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi (*courier services*), matangazo na usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhakiki watumishi wote ili kuondokana na watumishi wanaolipwa bila kustahili, ununuzi wa bidhaa na huduma kwa pamoja kutoka kwa wazalishaji au watengenezaji ili kupata nafuu ya bei, kutenga bajeti na kulipa michango ya Serikali katika mashirika ya kimataifa na kikanda kupitia Hazina, kufanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, na kugharamia uendeshaji wa elimu ya msingi bila malipo kuanzia Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze mapendekezo ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za bajeti kwa mwaka 2017/2018 ambazo nimekwisha zieleza sura ya bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 32.946 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Hata hivyo, kiasi hiki ni makisio ya awali ambapo makisio ya mwisho yatapatikana baada ya kukamilika kwa tathmini ya nusu mwaka 2016/2017 pamoja na taarifa ya Kikosi Kazi cha Maboresho ya Kodi kinachojumuisha wadau mbalimbali wakiwemo sekta binafsi na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 20.872 sawa na asilimia 63 ya mahitaji yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 18.097 sawa na asilimia 89 ya mapato ya ndani. Mapato yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 2.022 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 753.3. Serikali inategemea kukopa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 900 sawa na shilingi trilioni 2.080 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara na shilingi trilioni 4.434 ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shilingi trilioni 1.859 sawa na asilimia 1.5 ya Pato la Taifa ni mikopo mipya ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vilevile washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 3.7, kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 496.3 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (*GBS*), shilingi trilioni 2.821 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya

maendeleo na shilingi bilioni 382.4 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisékta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 32.946 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 19.782 zitatengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi trilioni 7.206 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma na shilingi trilioni 9.723 kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa lililoiva. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi trilioni 13.164, sawa na asilimia 40 ya bajeti yote, ambapo fedha za ndani ni shilingi trilioni 9.96 sawa na asilimia 76. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.343 ikilinganishwa na mwaka huu wa fedha.

Maelekezo ya kina kuhusu maboresho ya ya mfumo wa kibajeti na uandaaji wa mipango na bajeti kwa mwaka ujao wa fedha yako katika aya 40 hadi 50 na aya ya 52 hadi 54 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhamisha shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujumuisha mahitaji ya kuhamia Dodoma katika mipango na bajeti kwa kuzingatia ratiba iliyotolewa na Serikali. Mipango ya ujenzi wa majengo na miundombinu ya Serikali yaliyopangwa kujengwa Dar es Salaam ihamishiwe Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo na miundombinu yoyote inayotegemewa kujengwa Dodoma ni lazima ipate idhini kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya ukomo wa bajeti kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa vitatolewa kwa kuzingatia vigezo vya ugawaji rasilimali na vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018 na Mwongozo huu. Aidha, hakutakuwa na nyongeza ya ukomo wa bajeti nje ya viwango vitakavyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/2018 yanapatikana katika aya ya 55 hadi ya 68 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018 na ambao nimeuelezea kwa kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii pamoja na vitabu vya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka ujao wa fedha na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA
TAIFA KWA MWAKA 2017/2018 NA MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO
NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.
- 2. Mheshimiwa Spika**, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na hivyo kuweza kukutana na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18. Mapendekezo ya Mpango ni ya mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) wenye dhima ya *“Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”*.
- 3. Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18, yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha hatua za maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo. Maoni ya Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Bajeti yatakayozingatiwa katika kukamilisha Mpango na Mwongozo ni pamoja na:

(i) Kushirikisha Sekta Binasi katika utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo;

(ii) Kuwezesha nchi kuingia haraka katika uchumi wa viwanda kwa kupitia maendeleo ya viwanda vidogo vidogo – SIDO, kuboresha maeneo ya EPZA na SEZ;

(iii) Kuweka mfumo wa kulinda masoko ya bidhaa za ndani;

(iv) Kuchagua miradi michache ya kipaumbele kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti;

(v) Kukamilisha miradi ya maji na umwagiliaji kabla ya kuanza miradi mipya; na

(vi) Kuendelea na Mpango wa kurasimisha biashara na mali za wanyonge.

4. Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb), na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Doto Mgosha James kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii na Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo. Aidha, tunawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo huu.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Mhe. Kassim M. Majaliwa, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, na Watanzania wote kwa ujumla kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopatwa na janga la tetemeko la ardhi lilitokea katika Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza na Mara Septemba 2016. Wapo wananchi waliopoteza maisha, waliojeruhiwa na kuharibikiwa na mali zao kutokana na janga hilo. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa waliojeruhiwa na wafiwa wote na kuwatakiya afya njema.

6. Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliojitoa kwa hali na mali katika kuchangia wahanga wa tukio hilo. Ni heshima yangu kutambua michango ya Waheshimiwa Wabunge, Jumuiya ya Wafanyabiashara Nchini, Waheshimiwa Mabalizi, Wawakilishi wa Mashirika ya Umma na ya Kimataifa, Makampuni, Taasisi za Dini, Wafanyakazi wa Serikali, Watu Binafsi, Mashirika yasiyo ya Serikali, Vikundi Mbalimbali na Mtanzania

mmoja mmoja. Michango hiyo imetumika na kuendelea kutumika kuleta nafuu kwa wahanga wa tukio hilo. Tunawashukuru sana kwa ushirikiano na uzalendo wa hali ya juu walioonesha katika tukio hilo.

7. Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 yamezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015; Maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) sanjari na makubaliano ya kikanda, makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na makubaliano ya kimataifa yaliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SHABAHA NA MISINGI YA MPANGO NA BAJETI

8. Mheshimiwa Spika, katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/18 Serikali inatarajia kusimamia mambo muhimu kama ifuatavyo:

Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla

9. Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha muda wa kati (2017/18 – 2019/20) ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2017, asilimia 7.9 mwaka 2018 na asilimia 8.2 mwaka 2019;

(ii) Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia 5.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Kuwa na Pato ghafi la Taifa la Shilingi trilioni 123.9 mwaka 2017/18, Shilingi trilioni 139.7 mwaka 2018/19 na Shilingi trilioni 165.4 mwaka 2019/20;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 14.6 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18, asilimia 15.5 mwaka 2018/19 na asilimia 15.8 mwaka 2019/20;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 26.6 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18, asilimia 26.5 mwaka 2018/19 na asilimia 25.2 mwaka 2019/20;

(vi) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 4.5 katika kipindi cha muda wa kati;

(vii) Kuwa na kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 15.0 mwaka 2017/18, asilimia 14.0 mwaka 2018/19 na asilimia 13.1 mwaka 2019/20;

(viii) Kuwa na nakisi katika urari wa malipo ya kawaida (*current account balance including transfers*) wa asilimia 6.3 ya Pato la Taifa katika kipindi cha muda wa kati; na

(ix) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4) katika kipindi cha muda wa kati.

Misingi ya Mpango na Bajeti

10. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha muda wa kati (2017/18-2019/20), misingi ya mpango na bajeti ni pamoja na:

(i) Amani, usalama, utulivu na utangamano wa ndani na nchi jirani vitaendelea kuimarishwa na kudumishwa;

(ii) Viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, mfumuko wa bei, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii vitaendelea kuimarika;

(iii) Uchumi wa Dunia kuendelea kuimarika na kutengemaa;

(iv) Bei za mafuta katika soko la Dunia hazitaongezeka;

(v) Hali ya hewa nchini na katika nchi jirani kuwa nzuri;

(vi) Mahusiano na nchi jirani, kikanda na kimataifa kuendelea kuwa mazuri; na

(vii) Kuwepo kwa sheria na taratibu wezeshi kwa uwekezaji.

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/18

11. Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutoa maelezo kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18. Mapendekezo haya yanahusisha tathmini ya mwenendo wa uchumi na ustawi wa jamii, Hali ya Viwanda, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16 na maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/18.

TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI

12. Mheshimiwa Spika, katika nusu ya kwanza (Januari hadi Juni) ya mwaka 2016, Pato ghafi la Taifa lilikuwa Shilingi trilioni 52.7 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 45.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Aidha, katika kipindi hicho ukuaji halisi wa uchumi ulikuwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Shughuli zilizokuwa na ukuaji mkubwa

katika kipindi hicho ni pamoja na: Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo (asilimia 17.4); Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 13.7); Habari na Mawasiliano (asilimia 13.0); na Huduma za Fedha na Bima (asilimia 13.0). Shughuli zilizokuwa na ukuaji mdogo ni Huduma za Chakula na Malazi (asilimia 0.6) na Usambazaji Maji Safi na Udhhibiti Maji Taka (asilimia 0.9). Ukuaji huu unajenga msingi wa kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2016.

13. Mheshimiwa Spika, Pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 1,918,928 sawa na Dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015. Tanzania inaendelea kuwa na kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu ambapo inakadiriwa kuwa na watu milioni 50.1 mwaka 2016 na milioni 63 ifikapo mwaka 2025. Malengo ya Dira ya maendeleo ya Taifa ni kuwa na Pato la wastani la kila mtu la Dola za Kimarekani 3,000 ifikapo 2025. Hivyo, juhudi za makusudi zinahitajika ili kufikia malengo ya Dira ya kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kati ifikapo 2025.

14. Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 6.5 Januari 2016 hadi asilimia 5.5 Juni 2016 na kupungua zaidi hadi asilimia 4.5 Septemba 2016. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na fedha, kushuka kwa bei za bidhaa kwenye soko la Dunia hususan bei za mafuta ya petroli na kasi ndogo ya ongezeko la bei kwa bidhaa za chakula nchini. Matarajio ni kubaki na mfumuko wa bei katika kiwango cha tarakimu moja kwa kuongeza uzalishaji hususan wa chakula na kuimarisha sera za fedha na bajeti.

15. Mheshimiwa Spika, kiwango cha riba za amana za muda maalum kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 9.19 Julai 2015 hadi asilimia 9.97 Julai 2016. Aidha, kiwango cha riba za amana za mwaka mmoja kiliongezeka hadi asilimia 12.40 Julai 2016 kutoka asilimia 10.50 Julai 2015. Vile vile, wastani wa kiwango cha riba za mikopo kwa kipindi cha mwaka mmoja kilipungua kutoka asilimia 14.31 Julai 2015 hadi asilimia 13.31 Julai 2016. Tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.81 Julai 2015 na kufikia asilimia 0.9 Julai 2016. Mwenendo huu wa viwango vya riba unaonesha kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kufanya biashara na ushindani nchini hivyo kuvutia zaidi uwekezaji wa Sekta Binafsi.

16. Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje katika kipindi kinachoishia Julai 2016 ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 9,810.4 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 9,128.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ilipungua kwa asilimia 18.3 kutoka Dola za Kimarekani milioni 13,569 Julai 2015 hadi Dola za Kimarekani milioni 11,003.4 Julai 2016 kufuatia kupungua kwa uagizaji wa bidhaa hususan bidhaa za ukuzaji mitaji na thamani ya mafuta. Kutokana na mwenendo huu wa uuzaji

na uagizaji wa bidhaa nje, urari wa malipo ya kawaida uliimarika kutoka nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 4,778.9 Julai 2015 na kuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 1,866.1 Julai 2016.

17. Mheshimiwa Mwenyekiti, Akiba ya fedha za kigeni imebaki kuwa imara, ikiwa ni Dola za Marekani milioni 4,096.0 kufikia mwisho wa Septemba 2016, ambao ni uwezo wa kutosheleza uagizaji nje wa bidhaa na hudumu kwa kipindi cha miezi 4. Kuongezeka (kutotetereka) kwa Akiba ya Fedha za Kigeni kunatokana na manunuzi yanayofanywa na Benki Kuu ya Tanzania kutoka kwenye soko la ndani la fedha za kigeni na mashirika ya umma.

18. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2015/16, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilibaki kuwa imara hususan katika kipindi cha pili cha mwaka 2016/17. Kiwango cha ubadilishaji wa Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani kilipungua thamani kwa wastani wa asilimia 3.5 Juni, 2015, ambapo Juni 2016 kasi ya kupungua kwa thamani ilikuwa wastani wa asilimia 0.1. Kati ya Januari hadi Julai 2016 thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani ilishuka kwa kasi ndogo kutoka wastani wa Shilingi 2,172.38 kwa Dola moja Januari 2016 hadi wastani wa Shilingi 2,180.54 Julai 2016. Hali hii ilichangiwa na usimamizi madhubuti wa uchumi uliofanywa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania, kupunguzwa kwa matumizi ya Serikali na kutoterereka kwa akiba ya fedha za kigeni.

19. Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa (likijumuisha deni la ndani na nje) lilifikia Dola za Kimarekani milioni 18,614.93 sawa na ongezeko la asilimia 9.76 kufikia Juni 2016, ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 16,959.47 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya iliyochukuliwa kugharamia miradi ya maendeleo hususan ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, barabara na madaraja.

UTEKELEZAJI WA WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2015/16

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

20. Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/16 ni pamoja na kukamilika kwa:

(i) Ujenzi wa km 382.9 za barabara kuu na ukarabati wa km 82.4 kwa kiwango cha lami;

(ii) Ujenzi wa madaraja ya Kigamboni, Maligisu, Nango, Mbutu na Ruhekei katika barabara kuu;

(iii) Ujenzi wa barabara na miundombinu ya mabasi ya mwendo kasi katika Jiji la Dar es Salaam (BRT Phase I, km 20.9) na huduma zinatolewa kwa wananchi kuanzia Mei 2016;

(iv) Awamu ya Pili ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (km 25,954) na kusambazwa katika mikoa 24 Tanzania Bara;

(v) Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam (km 542) na ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi katika maeneo ya Madimba na Songosongo;

(vi) Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi vya Somanga – Fungu na Kinyerezi;

(vii) Usimikaji wa mitambo minne (4) ya kufua umeme Kinyerezi I yenye uwezo wa kuzalisha MW 150 na kuanza uzalishaji wa umeme;

(viii) Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini (REA Turnkey Phase II) na hivyo kuunganisha wateja 61,023 wa awali kati ya wateja 250,000;

(ix) Ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Iramba – Majita, Msangamkuu – Msemo, Ilagala – Kajeje, Igogo na Swea – Mwanza na ujenzi wa maegesho ya muda katika eneo la Magogoni - Dar es Salaam na Mbegani - Bagamoyo;

(x) Mradi wa Maji wa Ruvu Chini (Pwani); ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa km 55.3 kutoka kwenye mtambo Ruvu juu hadi matenki ya Chuo Kikuu cha Ardhi – Dar es Salaam; upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu pamoja na ulazaji wa mabomba kutoka Mlandizi hadi Kimara; Miradi mipya 1,160 ya maji ya vijiji 10 katika vijiji 1,206 yenye vituo 28,499 vya kuchotea maji katika Halmashauri 148; uchimbaji visima 11 mkoani Tabora; upanuzi wa huduma ya maji safi katika manispaa ya Dodoma na mji wa Singida;

(xi) Ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kiwanda cha Viuadudu Kibaha - Pwani na ujenzi wa barabara za kuingia kiwandani kwa kiwango cha lami (mita 400);

(xii) Kutoa mafunzo katika fani za mafuta na gesi kwa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 159. Kati ya wanafunzi hao, 124 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 35 wanagharamiwa na Washirika wa Maendeleo;

(xiii) Kutoa mikopo na ruzuku kiasi cha Shilingi bilioni 467.43 kwa wanafunzi 124,243 wa elimu ya juu ikilinganishwa na lengo la wanafunzi 101,129;

(xiv) Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na nyumba za walimu katika shule za sekondari 264; na

(xv) Kukamilika kwa ujenzi wa chuo cha mafunzo ya ufundi cha Wilaya ya Makete (Makete District Vocational Training Centre).

21. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2015/16 yapo katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 (**Sura ya Tano**).

HALI YA VIWANDA

22. Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005 na 2013, mauzo ya bidhaa Duniani yalikuwa kwa wastani wa asilimia 7.5. Biashara ya bidhaa Duniani ilikua na kufikia zaidi ya Dola za Kimarekani trilioni 17, ambapo asilimia 83.0 ilitokana na bidhaa za viwandani. Bidhaa za viwandani kwa nchi za viwanda ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 5.2 katika kipindi hicho na kufikia Dola za Kimarekani bilioni 8,929 mwaka 2013. Karibu asilimia 58 ya mauzo ya bidhaa za viwandani Duniani yalikusishia bidhaa zinazotumia teknolojia ya kati na juu kama vile mitambo ya kemikali na bidhaa zake, vifaa vya mawasiliano na magari.

23. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya mwisho ya Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya Mwaka 2013, Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda (vikubwa na vidogo) 49,243 ambapo, viwanda vikubwa vilikuwa 1,322 (asilimia 2.7) na vidogo ni 47,921 (asilimia 97.3). Sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani (manufacturing) iliongoza kuwa na idadi kubwa ya viwanda 48,474 (asilimia 98.4) ikifuatiwa na uchimbaji madini na mawe 391 (asilimia 0.8). Aidha, shughuli nne (4) za uzalishaji zilichangia asilimia 52.8 ya idadi ya viwanda nchini ambavyo ni bidhaa za chakula, 19,696 (asilimia 40.0), bidhaa za nguo 13,392 (asilimia 27.2), samani 6,823 (asilimia 13.9) na bidhaa za chuma isipokuwa mitambo na vifaa 3,805 (asilimia 7.7). Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kuwa na idadi kubwa ya viwanda (vikubwa na vidogo) ambapo kati ya viwanda vikubwa 1,322 ilikuwa na viwanda 389 (asilimia 29.4), ukifuatiwa na Manyara 167 (asilimia 12.6), Arusha 89 (asilimia 6.7) na Kilimanjaro 66 (asilimia 5.0). Idadi kubwa ya viwanda 41,919 (asilimia 85.1) ina wafanyakazi mmoja hadi wane (1 – 4) na viwanda vichache 6,002 (asilimia 12.2) vina wafanyakazi watano hadi tisa (5 - 9).

24. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu hali ya viwanda Kimataifa na Kitaifa yapo katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 (**Sura ya Tatu**)

MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2017/18

25. Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/18 yamezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/18 yamegawanyika kama ifuatavyo:-

Miradi ya Kielelezo

26. Mheshimiwa Spika, Miradi hii ni mahsusi, kwa maana ya ukubwa wa uwekezaji na matokeo yake katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango. Miradi hii itajumuisha:- Makaa ya Mawe Mchuchuma; Chuma Liganga; ujenzi wa Reli ya Kati kutoka Dar – Tabora - Kigoma (km 1,251) kwa *Standard Gauge* na matawi yake ya: Tabora – Isaka – Mwanza (km 379); Isaka – Rusumo (km 371); Kaliua – Mpanda - Karema (km 321); Keza – Ruvubu (km 36); na Uvinza - Kilelema kuelekea Musongati (km 203); kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi mkoani Lindi; uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi mkoani Tanga, Bagamoyo, Kigoma, Ruvuma na Mtwara; uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini; kusomesha vijana katika stadi maalum (mafuta na gesi, uhandisi na huduma za afya); uanzishwaji wa mji wa Kilimo wa Mkulazi; ununuzi na ukarabati wa meli kwenye Maziwa Makuu; ujenzi wa barabara za Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310) na Masasi - Songea – Mbamba Bay (km 868.7).

Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

27. Mheshimiwa Spika, miradi itakayozingatiwa ni pamoja na: mradi wa Magadi Soda (Bonde la Engaruka); Kufufua Kiwanda cha General Tyre; Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO; uendelezaji wa maeneo ya viwanda vidogo – SIDO katika mikoa ya Morogoro, Dar es salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha; Bandari kavu (Pwani) na mradi wa bomba la Mafuta kutoka Uganda hadi bandari ya Tanga.

Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Maendeleo ya Watu

28. Mheshimiwa Spika, katika **Elimu na Mafunzo ya Ufundi** maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Elimu msingi bila malipo; kujenga na ukarabati miundombinu ikiwemo madarasa, maabara, umeme, vyoo na maji kwa ajili ya elimu ya awali, msingi na sekondari; kuhakikisha upatikanaji wa madawati na walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi na hisabati; ujenzi na ukarabati wa karakana za kuandaa wanafunzi kwa njia ya vitendo katika vyuo vya ufundi nchini; ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu katika taasisi za elimu ya juu na vyuo vya ufundi na

ualimu; kupanua matumizi ya TEHAMA katika vyuo vya elimu ya juu na ufundi nchini; na kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuongeza uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi.

29. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Afya na Ustawi wa Jamii**, maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuboresha Hospitali za Rufaa na mikoa kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa; kuimarisha upatikanaji wa huduma za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati; kuongeza udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza; kuimarisha huduma za kinga na magonjwa yasiyoambukiza; kupunguza vifo vya watoto na kina mama vinavyotokana na uzazi; na kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kwa jamii hususan vijana.

30. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **maji**, maeneo ya kipaumbele ni pamoja na kulinda, kuendeleza na kusimamia vyanzo vya maji nchini pamoja na kudhibiti ubora wa maji; kuboresha usambazaji wa maji katika miradi ya kitaifa, makao makuu ya wilaya na miji midogo; kuboresha uwezo wa usambazaji wa maji safi na udhibiti wa maji taka na usafi wa mazingira; kupanua usambazaji wa maji vijijini; kuboresha usambazaji wa maji Dar es Salaam; na kujenga mabwawa katika mikoa yenye ukame pamoja na mkoa wa Dar es Salaam.

Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

31. Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuendelea na miradi iliyoanza kutekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2016/17, ikiwa ni pamoja na: nishati; kilimo cha mazao; mifugo; uvuvi; maji; umwagiliaji; miundombinu ya reli na barabara; ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) kwenye makutano ya barabara za jiji la Dar es Salaam; madaraja; bandari; kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga; usafiri wa majini; na miundombinu ya TEHAMA.

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kutekeleza miradi chini ya utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa kufua umeme Kinyerezi III MW 300; mradi wa mabasi ya mwendokasi Dar es Salaam awamu ya II, III na IV zenye jumla ya km 60; kiwanda cha kuzalisha madawa muhimu na vifaa tiba na mradi wa barabara ya tozo Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200).

Maeneo Mengine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa

33. Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayozingatiwa ni pamoja na: kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma; miradi katika maeneo ya wanyamapori; misitu; mazingira na mabadiliko ya tabianchi; ardhi, nyumba na makazi; madini; ushirikiano wa kikanda na kimataifa; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; utawala bora na utawala wa sheria; kuwezesha uanzishwaji wa kanzidata ya miradi ya maendeleo katika ngazi zote; na kujenga uwezo katika idara zinazohusika na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18

34. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18. Mwongozo huo unawaelekeza Maafisa Masuuli masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa mipango na bajeti za mafungu yao. Maelekezo ya Mwongozo yanajumuisha utekelezaji wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; usimamizi na udhibiti wa matumizi; ulipaji na uzuiaji wa ongezeko la madeni ya Serikali; ukusanyaji wa mapato; mfumo wa bajeti wa mwaka 2017/18; na mfumo wa utoaji taarifa za utekelezaji. Aidha, Mwongozo unatoa mapendekezo ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/18.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO KWA MWAKA 2015/16

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Serikali iliandaa na kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali yaliyotolewa kwenye mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali. Maelekezo hayo ni pamoja na: kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima; kudhibiti ongezeko la madeni; na kusimamia ununuzi wa umma ili kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika.

36. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maelekezo hayo umewezesha kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia Shilingi trilioni 14.139 sawa asilimia 101 ya lengo la Shilingi trilioni 13.998. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi yalikuwa Shilingi trilioni 12.525 sawa na asilimia 101.3; mapato yasiyo ya kodi yalikuwa Shilingi trilioni 1.188 sawa na asilimia 106.8; na mapato ya halmashauri yalikuwa Shilingi bilioni 425.9 sawa na asilimia 81.6. Mafanikio hayo yalitokana na Maafisa Masuuli kuzingatia maelekezo ya kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato, kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na kuimarisha usimamizi wa mashirika yanayotoa michango na gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Maafisa Masuuli walizingatia maelekezo ya Mwongozo katika kudhibiti matumizi kwa: kupunguza safari za nje zisizo za lazima na maadhimisho ya sherehe mbalimbali; kufanya mikutano katika kumbi za Serikali; na kudhibiti posho zisizokuwa za lazima. Aidha, fedha zilizopatikana kutokana na hatua hizo zilitumika katika shughuli mbalimbali zikiwemo ujenzi wa barabara ya Ali Hassan Mwinyi (Morocco – Mwenge, km 4.3) na barabara ya Mwanza (Ghana Quarters – Airport, km 9.15); ununuzi wa vitanda kwa ajili ya Hospitali ya Taifa Muhimbili; ununuzi wa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI; na ununuzi wa madawati kwa ajili ya shule za msingi ambapo pia wadau na wananchi wamechangia juhudi za Serikali. Utekelezaji wa hatua zilizoinishwa katika Mwongozo kwa mwaka 2015/16 uliwezesha Serikali kutekeleza majukumu ya msingi na hivyo kuboresha huduma za kijamii na kukuza uchumi.

CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/16 NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

38. Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na: uwezo wa kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi kwenye mipaka ya nchi; kuendelea kukua kwa sekta isiyo rasmi na ugumu wa kukusanya kodi; kupatikana kwa wakati kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kutoka nje; mahitaji makubwa yasiyowiana na mapato; kuongezeka kwa madeni ya ndani; kubadilika kwa masharti na sera za upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; na ushiriki mdogo wa Sekta Binafsi kutokana na mazingira yasiyo wezeshi kwa uwekezaji na uendeshaji biashara.

39. Mheshimiwa Spika, mikakati ya kukabili na changamoto hizo ni pamoja na: kuimarisha doria na upelelezi katika mipaka, bandari na bandari bubu kupitia Kikosi Kazi cha Kuzuia Magendo; kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuzuia mianya ya ukwepaji kodi; kuhakiki madeni na kutekeleza mkakati wa kuyalipa; kuendelea na jitihada za kurasimisha sekta isiyo rasmi; kurahisisha masharti ya leseni za biashara na uwekezaji nchini; kuendelea kuimarisha soko la ndani la hati fungani za Serikali ili kuvutia ushiriki wa wawekezaji wengi; kukamilisha zoezi la kufanyiwa tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa; kufanya mapitio ya mkakati wa pamoja wa misaada na kuandaa mpango mpya wa mahusiano na washirika wa maendeleo; na kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji ili kuchochea uwekezaji kwa Sekta Binafsi.

MWONGOZO WA MWAKA 2017/18

40. Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Mwaka 2017/18 ni mwendelezo wa utekelezaji wa maelekezo ya msingi yaliyotolewa na Serikali katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17. Baadhi ya

maelekezo hayo ni pamoja na: mapato yote kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo kufuta utaratibu wa 'Retention'; kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na kudai stakabadhi kwa bidhaa na huduma zilizotolewa; ukusanyaji wa kodi ya majengo kusimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; kutumia Taasisi za Umma katika huduma za bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi (courier), matangazo na usafiri; kuhakiki watumishi wote ili kuondokana na watumishi wanaolipwa bila kustahili; ununuzi wa bidhaa na huduma kwa pamoja/wingi (*in bulk*) kutoka kwa wazalishaji au watengenezaji ili kupata nafuu ya bei; kutenga bajeti na kulipa michango ya Serikali katika mashirika ya kimataifa na kikanda kupitia Hazina; kufanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma; na kugharamia uendeshaji wa elimu msingi bila malipo kuanzia Januari 2016.

MFUMO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18

41. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za bajeti kwa mwaka 2017/18, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi trilioni 32.946 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Hata hivyo, kiasi hiki ni makisio ya awali ambapo makisio ya mwisho yatapatikana baada ya kukamilika kwa tathmini ya nusu mwaka, 2016/17 pamoja na taarifa ya Kikosi Kazi cha Maboresho ya Kodi kinachojumuisha wadau mbalimbali wakiwemo Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

42. Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Shilingi trilioni 20.872 sawa na asilimia 63 ya mahitaji yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya Shilingi trilioni 18.097 sawa na asilimia 87 ya mapato ya ndani. Mapato yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 2.022 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni Shilingi bilioni 753.3. Serikali inategemea kukopa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 900 sawa na Shilingi trilioni 2.080 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara na Shilingi trilioni 4.434 ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva. Aidha, Shilingi trilioni 1.859 sawa na asilimia 1.5 ya Pato la Taifa, ni mikopo mipya ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vile vile, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia Shilingi trilioni 3.700. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 496.3 ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (*GBS*), Shilingi trilioni 2.821 ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 382.4 ni misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kissekta.

43. Mheshimiwa Spika, Maelezo ya kina ya Sura ya Bajeti 2017/18 yapo katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 (**Sura ya nne, Jedwali Na. 4.1**).

44. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2017/18 Serikali inapanga kutumia jumla ya Shilingi trilioni 32.946 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni 19.782 zitatengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi trilioni 7.206 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi za Umma na Shilingi trilioni 9.723 kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa lililoiva. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi trilioni 13.164, sawa na asilimia 40 ya bajeti yote, ambapo fedha za ndani ni Shilingi trilioni 9.960 sawa na asilimia 76. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.343 ikilinganishwa na mwaka 2016/17.

MAELEKEZO YA MWONGOZO KWA MWAKA 2017/18

Maboresho ya Mfumo wa Kibajeti

45. Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika mfumo wa kibajeti ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi. Maboresho makubwa yaliyofanyika ni pamoja na kuandaliwa na kupitishwa kwa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni za Bajeti za mwaka 2015. Hivyo, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuendelea kuzingatia Sheria ya Bajeti pamoja na Kanuni yake wakati wa uandaaji na utekelezaji wa Mipango na Bajeti.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuandaa bajeti kwa kuzingatia Programu (*Programme Based Budget - PBB*) ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa umma. Mabadiliko haya yanatokana na maboresho mbalimbali yanayofanyika katika taasisi za kimataifa zinazosimamia masuala ya bajeti na fedha za umma. Mfumo huu utanza kwa hatua ya majaribio katika Wizara nane (8) ambazo ni: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; na Wizara ya Nishati na Madini. Mfumo huu unawataka Maafisa Masuuli wa Wizara za majaribio kuainisha bajeti zao kwa utaratibu wa programu na kwa kuzingatia miongozo na viwango vya kimataifa. Aidha, Maafisa Masuuli wa mafungu haya wanatakiwa kuandaa bajeti kivuli za mafungu yao kwa kuzingatia malengo ambayo yataonesha matokeo na viashiria vya kiutendaji vitakavyotumika kupima matokeo ya utekelezaji wa programu hizo.

47. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015 Serikali ilitoa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma ambapo mafunzo ya mwongozo huo kwa watendaji wa mafungu mbalimbali yamefanyika mwaka 2016. Mwongozo huo, unatoa maelekezo mbalimbali ikiwemo: uibuaji na uchambuzi; ugharamiaji; utekelezaji; usimamizi; ufuatiliaji na tathmini; pamoja na usimamizi wa kanzidata ya miradi ya uwekezaji wa umma. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa

kuzingatia Mwongozo huo na kuhakikisha wanajenga uwezo wa wataalam kulingana na mahitaji ya mafungu yao.

Uandaaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2017/18

48. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinaelekeza kuundwa kwa Kamati za Bajeti katika Serikali na taasisi zake ili kurahisisha maandalizi ya mipango na bajeti. Kamati za Bajeti zinaelekezwa kutekeleza majukumu yao katika uandaaji wa mipango na bajeti kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 17(3) ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Aidha, Maafisa Masuuli wa Taasisi na Wakala wa Serikali wanaelekezwa kuzingatia Nyaraka za Msajili wa Hazina katika uandaaji wa mipango na bajeti zao.

49. Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa Mipango na Bajeti ya Muda wa Kati (MTEF) na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango wiki ya tatu ya Februari, 2017 kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaagizwa kuandaa na kuwasilisha makadirio yao Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) wiki ya kwanza ya Februari, 2017 baada ya kupitishwa na Mamlaka husika na baadaye kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha rasimu ya mipango na bajeti katika Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma SURA 105.

50. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya majumuisho ya bajeti za Mafungu na kuwasilisha kwenye ngazi za maamuzi za Serikali. Aidha, Mafungu yataandaa Randama za bajeti zao na kuwasilisha kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta wiki ya tatu ya Machi, 2017 na wiki ya kwanza ya Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi na kuandaa mapendekezo yatakayowasilishwa Bungeni. Majumuisho ya bajeti yatawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kuanzia wiki ya pili ya Aprili, 2017 hadi wiki ya nne ya Juni, 2017. Utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya mwaka 2017/18 utanza tarehe 1 Julai, 2017 hadi tarehe 30 Juni, 2018.

51. Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamisha shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujumuisha mahitaji ya kuhamia Dodoma katika mipango na bajeti kwa kuzingatia ratiba iliyotolewa na Serikali. Mipango ya ujenzi wa majengo na miundombinu ya Serikali iliyopangwa kujengwa Dar es salaam ihamishiwe Dodoma. Aidha, ujenzi wa majengo na miundombinu yoyote inayotegemewa kujengwa Dodoma ni lazima upate idhini kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

52. Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa utafanywa kwa pamoja baina ya Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Msajili wa Hazina na wadau wengine. Taasisi zote za Serikali zinaagizwa kuandaa na kuwasilisha mipango na bajeti zao Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi kwa mujibu wa Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala tano (5) ngumu na laini za rasimu ya mipango na bajeti zao kwa ajili ya uchambuzi wa kitaalamu. Vile vile, zinapaswa kuwasilisha nakala tatu (3) za mipango na bajeti iliyosainiwa kwa mamlaka husika. Mikoa na Halmashauri zinapaswa kuwasilisha nakala tatu (3) za MTEF zilizosainiwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Pia, Taasisi za Umma zinatakiwa kuandaa na kuwasilisha mipango na bajeti na kuwasilisha nakala tatu (3) zilizosainiwa kwa Wizara zinazoratibu bajeti zao na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ili kuweka ufafanuzi na uwazi katika zoezi la uchambuzi wa bajeti, majadiliano yataendeshwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16;

(ii) Kupitia mapato na matumizi ya kipindi cha nusu mwaka wa 2016/17, changamoto na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo;

(iii) Kanuni za uandaaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/18 (MTEF) kama ilivyoelekezwa katika Sura ya Tano ya Kiambatisho cha Mwongozo;

(iv) Vipaumbele vilivyotolewa katika Mwongozo na ukomo wa bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;

(v) Kuwasilisha mipango na bajeti iliyoandaliwa kwa Mfumo wa Utengaji Bajeti wa Kimkakati (*Strategic Budget Allocation System – SBAS*) kwa upande wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na *PlanRep* kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(vi) Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015; na

(vii) Maelekezo ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni yake ya mwaka 2015, Nyaraka za Msajili wa Hazina, pamoja na Nyaraka na Miongozo mingine ya Serikali.

54. Mheshimiwa Spika, kuhusu uingizaji wa takwimu za bajeti katika Mfumo wa Malipo (*IFMS*), kulingana na ratiba ya maandalizi na uchambuzi wa bajeti, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kukamilisha kwa wakati zoezi la kuingiza takwimu za bajeti kwenye mfumo wa malipo na kuhakikisha usahihi wa takwimu hizo;

(ii) Kuzingatia Mfumo wa Kimataifa wa mwaka 2014 wa Takwimu za Kifedha za Serikali (*GFS Codes*) toleo la mwaka 2014 na za miradi (*Project Codes*) kama ilivyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;

(iii) Kutumia vizio vilivyokubalika na vinavyotolewa katika mfumo wa *SBAS* na *PlanRep*; na

(iv) Kuweka makadirio sahihi ya gharama za kodi ya pango, umeme, maji na simu.

MAELEKEZO YA UANDAAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

55. Mheshimiwa Spika, viwango vya ukomo wa bajeti kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa vitatolewa kwa kuzingatia vigezo vya ugawaji rasilimali na vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 na Mwongozo huu. Aidha, hakutakuwa na nyongeza ya ukomo wa bajeti nje ya viwango vitakavyotolewa. Kwa msingi huo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia ukomo wa viwango vya bajeti vilivyoidhinishwa kwa mwaka 2017/18.

56. Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mikakati na hatua za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kama ilivyoainishwa katika Sura ya Nne ya Kiambatisho cha Mwongozo huu. Jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato yote ya Serikali ni la Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakusanya mapato kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango na kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti zitakazoidhinishwa katika mafungu yao. Vile vile, Taasisi na Wakala za Serikali zinaelekezwa kuendelea na akaunti zao za mapato zilizopo Benki Kuu ya Tanzania na kuwa na akaunti ya matumizi katika benki za biashara. Ili kutimiza lengo hili, Taasisi na Wakala zote zinatakiwa kuwasilisha mapato yote katika akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania ndani ya saa 24 baada ya kukusanywa.

57. Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha kutoka akaunti za mapato zilizo Benki Kuu ya Tanzania kwenda kwenye akaunti za matumizi za Taasisi zilizo katika benki za biashara utazingatia Mpango wa Mtiririko wa Fedha wa bajeti iliyoidhinishwa. Fedha kwa ajili ya matumizi ya Taasisi na Wakala za Serikali zitasimamiwa na Msajili wa Hazina kulingana na Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha na bajeti iliyoidhinishwa.

58. Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuweka mazingira wezeshi katika kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuainisha vyanzo vyote vya mapato kama moja ya mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato;

(ii) Kuhakikisha kuwa majengo yote yanathaminihwa kulingana na bei halisi ya soko. Aidha, majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa viwango vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Zoezi hili lifanyiwe kwa kipindi cha mpito wakati zoezi la uthamini wa majengo hayo likikamilishwa;

(iii) Kupima na kuainisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa Hati miliki ya ardhi;

(iv) Urasimishaji wa biashara ili kupanua wigo wa kodi;

(v) Kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(vi) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(vii) Kuingia mikataba na wazabuni, makandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za EFD;

(viii) Kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kujipanga upya;

(ix) Kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango; na

(x) Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vituo vya ukusanyaji wa mapato kama vile bandari, viwanja vya ndege na mipakani.

59. Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa utaratibu wa kupata mikopo kwa miradi mipya na inayoendelea uzingatie Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134 kama ilivyorekebisha mwaka 2004. Kwa

Mamlaka za Serikali za Mitaa, mapitio ya mkopo yatazingatia Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, SURA 290.

Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kupata idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango kabla ya kukopa kama ilivyobainishwa katika Kifungu Na. 60(4) na 62(b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

60. Mheshimiwa Spika, kuhusu ulimbikizaji wa madeni ya ndani, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia Kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na Waraka Na. 4 wa Mwaka 2014 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni. Kutokana na hali hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa;

(ii) Kuhakikisha kwamba hakuna madeni mapya yanayozalishwa;

(iii) Kubainisha madeni yaliyopo na kuhakikisha yanaingizwa kwenye hesabu za majumuisho za Serikali;

(iv) Kuingiza matumizi yote kwenye Mfumo wa Malipo wa IFMS; na

(v) Kuhakikisha madeni yote yamehakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na kuingizwa kwenye hesabu za fungu husika (*Financial Statement*).

61. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kudhibiti madeni sanjari (*contingent liability*) hususan yenye dhamana ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mikataba inayoweza kusababisha madeni. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia madeni sanjari yote katika maandalizi ya bajeti zao.

62. Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti matumizi, Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutekeleza hatua zifuatazo bila kuathiri ubora wa huduma zinazotolewa:

(i) Kuhakikisha mikataba inayoingiwa na Serikali na taasisi zake inakuwa katika Shilingi za Kitanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara za kimataifa;

(ii) Kuendelea kupunguza gharama na matumizi yasiyokuwa ya lazima ikiwemo sherehe za kitaifa, posho za vikao, uchapishaji wa fulana, kofia, mikoba, safari za nje, mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na ununuzi wa samani kutoka nje;

(iii) Kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya bodi, mafunzo, warsha na semina inafanyika katika kumbi za Serikali na Taasisi za Umma;

(iv) Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma na zile ambazo Serikali inamiliki hisa katika kununua huduma kama vile bima, huduma za fedha, usafirishaji wa barua, wavuti, simu, mizigo na vifurushi, matangazo na usafiri. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia unafuu na ubora wa huduma zinazotolewa na taasisi hizo;

(v) Kuhakikisha Mashirika ya Umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali;

(vi) Kudhibiti ununuzi wa bidhaa, huduma na ujenzi kwa lengo la kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha ya ununuzi inapatikana kwa kutumia utaratibu wa *Force account*, ununuzi wa bidhaa ya pamoja/wingi, ushindani na kupitia masoko ya ndani;

(vii) Kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia inayopunguza matumizi ya nishati na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipia ankara hizo zinatumiwa kama ilivyokusudiwa;

(viii) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo ya umeme, maji na simu ili kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;

(ix) Kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa kulipa watumishi wanaostahili pekee;

(x) Kutumia utaratibu wa ununuzi wa nyumba kwa utaratibu wa kulipia kwa awamu (mortgage financing arrangement) hususan kwa majengo ya balozi na wawakilishi walioko nje ya nchi badala ya utaratibu wa kupanga;

(xi) Kudhibiti safari za nje ya nchi na ukubwa wa misafara;

(xii) Kuhakikisha ununuzi wa magari inafanyika kwa pamoja kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) baada ya kupata kibali cha ununuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(xiii) Kuthibiti utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi waliokidhi vigezo pekee ndio wananufaika na mikopo hiyo; na

(xiv) Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kufanikisha mawasiliano katika Ofisi za Serikali, hususan katika kipindi cha mpito cha Serikali kuhamishia shughuli za Makao Makuu Dodoma.

63. Mheshimiwa Spika, Maafisa Masuuli wanapaswa kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti ya mwaka 2017/18 na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika ipasavyo. Ili kufanikisha lengo hili, kila Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinasisitizwa kutenga fedha za kutekeleza vipaumbele kwenye masuala mtambuka. Vipaumbele hivyo ni pamoja na masuala ya kijinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kuweka kipaumbele katika masuala yote yanayohusu watu wenye mahitaji maalum hususan ajira, afya, elimu, na ujenzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kutekeleza maboresho ya masuala mtambuka ambayo ni ya muhimu katika utawala bora, uboreshaji wa huduma na uwajibikaji. Maboresho haya yanajumuisha: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma (*PSRP*), Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa (*LGRP*), Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (*LSRP*), Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFMRP*), Maboresho ya Sekta ya Fedha (*SGFRP*), Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (*BEST*), na Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Rushwa (*NACSAP*). Maboresho mengine ya kuzingatia ni pamoja na Udhibiti wa Fedha Haramu, Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi, Mfumo wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini zenyewe (*APRM*), na Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu. Hivyo, kila taasisi inapaswa kuzingatia majukumu yake na kuhakikisha inatenga fedha za kutekeleza kwa ukamilifu maboresho yanayozihusu.

65. Mheshimiwa Spika, katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, Serikali itaendelea kutenga Shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kupitia Mfuko ambao utakuwa wa Mzunguko (*Revolving Fund*). Mfuko huo utasimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kutekelezwa na Halmashauri za Wilaya. Katika ngazi ya kijiji, Mfuko utasimamiwa na Kamati ya Mfuko ya Kijiji. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia kuwa miradi/biashara itakayofaidika inachaguliwa kwa kuzingatia vigezo na masharti ya Mfuko.

66. Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa mali za umma, Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi wa mali za umma zilizo chini ya sekta zao. Aidha, wanapaswa kupanga na kutenga fedha za kuhakiki, kupima, kuweka mipaka na kurasimisha umiliki wa mali za umma kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utoaji taarifa. Mali hizo ni pamoja na viwanja vya Serikali, maeneo ya wazi, viwanda, shule, vyuo vikuu, hospitali, vituo vya afya, zahanati, jeshi na vyombo vya usalama na mashamba ya umma. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Halmashauri wanapaswa kuwezesha umiliki wa mali hizo.

67. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi katika utaratibu wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Sheria ya PPP Na. 18 ya Mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2014. Ili kukuza utekelezaji wa miradi ya PPP, vipaumbele vitatolewa kwa miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinatakiwa kukamilisha upembuzi yakinifu ili kuwezesha miradi hiyo kupitia mfumo wa PPP. Katika kuanzisha miradi ya PPP na kujenga uwezo wa kitaasisi, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye Mfuko wa Uwezeshaji wa PPP.

68. Mheshimiwa Spika, kuhusu maelekezo mahsusi kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa katika **Aya Na. 52** ya Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

69. Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji na tathmini utafanyika ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utekelezaji kulingana na thamani halisi ya fedha za umma zinazotumika. Kwa msingi huu Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo, programu na shughuli zote za Serikali zinabuniwa vizuri, kupangwa kwa mtiririko na kutenga fedha kwa kuzingatia mipango na bajeti iliyoidhinishwa.

70. Mheshimiwa Spika, taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (kwa Taasisi za Umma) zikiwa katika nakala ngumu na laini. Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuwasilisha taarifa hizo kwa mujibu wa muundo uliooneshwa katika Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

HITIMISHO

71. Mheshimiwa Spika, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

72. Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau wote na wananchi wanaoendelea kuchangia masuala mbalimbali ya mipango na bajeti ya Serikali. Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha za kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwezesha ushiriki mkubwa zaidi wa Sekta Binafsi

na wananchi hususan katika maeneo ambayo yatakuza viwanda na maendeleo ya watu nchini.

73. Mheshimiwa Spika, hotuba hii pamoja na vitabu vya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz) na Tume ya Mipango (www.mipango.go.tz).

74. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kutoa maoni na kushauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2017/18 na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18.

75. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hoja imeungwa mkono. Sasa tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili aweze na yeye kuleta maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusiana na Mpango wa Serikali wa Taifa. *(Makofi)*

MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, Kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imeusoma na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 iliyotayarishwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa muhtasari, mapendekezo hayo yanatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma namna bora ya kuandaa na kutekeleza mipango na bajeti itakayoendana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) ambayo ni kuwa na viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa misingi ya uchumi; kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu; kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na usimamizi wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mapendekezo haya yanaelekeza vyombo husika utaratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mipango na Bajeti zao ili kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za Serikali, kwa kuzingatia miongozo ya kisheria pamoja na namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa rasilimali fedha kugharamia miradi ya maendeleo; kutoa mwongozo wa kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali, sekta binafsi na wadau wengine; pamoja na mapitio ya ukuaji wa uchumi jumla kwa kuzingatia utekelezaji wa Sera ya Fedha na Kodi tukielekea mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonyesha kwamba katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016 (Januari hadi Juni) pato halisi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 23.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Sekta zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 17.4) na uchimbaji madini na mawe (asilimia 13.7). Aidha, shughuli zilizokuwa na ukuaji mdogo ni pamoja na huduma za chakula na malazi (asilimia 0.6) pamoja na usambazaji maji safi na udhibiti wa maji taka. Mwenendo wa mfumuko wa bei umekuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ingependa kutoa angalizo kuhusu kushuka kwa wastani wa pato kwa kila mtu katika dola za Kimarekani kutoka dola za Kimarekani 1,047 mwaka 2014 hadi dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015 ambako kunaelezwa kuwa kulitokana na kushuka kwa thamani ya shilingi. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani iliendelea kupungua katika kipindi chote cha mwaka 2015 na nusu ya kwanza ya mwaka 2016. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,179.0 Julai, 2016 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,086.4 Julai, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri zinazochukuliwa na Serikali katika kuongeza Pato la Taifa na kupunguza mfumuko wa bei, Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa katika eneo hili hasa katika upatikanaji wa vyanzo vipya vya mapato. Serikali imekuwa ikitegemea mapato yake kwa kuibua vyanzo vya mapato ya ndani zaidi kuliko kuangalia vyanzo vingine ambavyo ni *Non Tax Revenue* vitakavyosaidia kugharamia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuona kodi zinazobuniwa zinasaidia kuongeza hali ya uzalishaji, ujasiriamali na uwekezaji na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Aidha, ukuaji wa uchumi ujielekeze zaidi katika kuongeza kipato kwa Mtanzania na hivyo kufikia malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo kuwa ifikapo mwaka 2025 pato la kila Mtanzania liwe limefikia dola za Kimarekani 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa na hatimaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015. Sheria hii na Kanuni zake zitasaidia kuhakikisha usimamizi na uwajibikaji katika hatua zote za mchakato wa bajeti unazingatiwa.

Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mfumo wa Programu wa Kibajeti ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kuanzisha utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha Awamu ya Nne. Mifumo hii kwa ujumla itasaidia sana kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Baada ya pongezi hizi, Kamati ingependa kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu mwongozo na kutayarisha Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/2018 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, makisio ya awali ya Bajeti ya Serikali yanaonyesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 32.946 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo kati ya fedha hizo shilingi trilioni 20.872 sawa na asilimia 63 ya bajeti yote zitatokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kuwa Serikali imepanga kuongeza mapato yake ya ndani hasa yale yatokanayo na kodi kwa kupanua wigo wake wa kukusanya kodi kwa kuja na vyanzo vipya ambavyo havitakuwa kero kwa wafanyabiashara na wananchi wote kwa ujumla ili kuweza kufikia lengo la mapato yatokanayo na kodi iliyoongezeka kwa asilimia 16.532 kutoka shilingi trilioni 15.105 mwaka 2016 hadi shilingi trilioni 18.097 mwaka 2018. Aidha, pamoja na hatua hii muhimu, ni vema Serikali ikajielekeza katika kuangalia pia vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kugharamia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa Serikali imepanga kukopa ndani kiasi cha shilingi trilioni 6.28 ambayo ni sawa na 1.5% ya Pato la Taifa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 14.49 ukilinganisha na kiwango cha mkopo wa ndani kilichokopwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 cha shilingi trilioni 5.37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haipingani na mpango wa Serikali kukopa kiasi cha shilingi trilioni 2.080 ambayo ni sawa na dola za Kimarekani milioni 900 kutoka katika vyanzo vyake vya nje ili kugharamia utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo. Kamati ingependa kuishauri Serikali kupunguza kukopa zaidi katika vyanzo vya ndani na badala yake ikope vyanzo vya nje kwa sababu kwa kufanya hivyo inafanya sekta binafsi na wananchi kushindwa kukopa kwa sababu taasisi za kifedha zinapenda kuikopesha Serikali zaidi kwa kuwa hakuna *risk* yoyote katika ukusanyaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka zoezi la *sovereign rating* ili kuiwezesha kukopa zaidi kutoka katika vyanzo vya nje ili kuiwezesha kugharamia miradi yake ya maendeleo na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango cha fedha itakachokopa katika vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali kuanzisha utaratibu wa Wizara, Taasisi na Mashirika yote ya Umma kutakiwa kuwasilisha Benki Kuu mapato yao yote yanayokusanywa ndani ya saa 24 baada ya kukusanya. Lengo la utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kuwa na udhibiti wa fedha za umma. Utaratibu huu pia utaiwezesha Serikali kujua ina fedha kiasi gani zilizokusanywa wakati wote. Hata hivyo, Kamati ingependa kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka haraka iwezekanavyo fedha za matumizi ya Wizara, Taasisi na Mashirika hayo kadri ya mipango kazi inavyoonyesha na kadri walivyopitishiwa na Bunge katika bajeti zao ili kuepuka kukwamisha utekelezaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza kuwa itaendelea na utaratibu iliouanzisha katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 wa ukusanyaji wa kodi ya majengo kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa jambo hili kwa TRA kuanza kukusanya katika maeneo machache. Hii itaiwezesha TRA kujipanga vizuri kabla ya kuanza kukusanya mapato yote. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum utakaoanisha namna TRA watavyoendelea kukusanya katika maeneo yaliyosalia.

Aidha, Kamati ingependa kurudia ushauri wake iliutoa mwaka jana kwa Serikali kuhusu majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini kukusanya viwango vya kodi vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Vilevile katika ufanyaji tathmini, Serikali izingatie hali ya uchumi wa eneo husika, thamani ya ardhi na thamani ya nyumba yenyewe katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Serikali Dodoma kutoka Dar es Salaam. Aidha, Serikali imeainisha namna itakavyotekeleza jambo hili kwa awamu katika muda mfupi na muda wa kati, hivyo kutoa fursa kwa Wizara husika kujipanga na kuwezesha utekelezaji wa uamuzi huu. Pamoja na nia hii nzuri ya Serikali, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha za matumizi mengineyo kwa mafungu husika ili kuweza kugharamia mpango huu vizuri hasa kwa upande wa malipo ya stahili za watumishi watakaohamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo umeainisha mikakati na hatua mbalimbali za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Mikakati hiyo ni pamoja na kupitia upya ada, tozo na ushuru ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo ya uchumi na ya kijamii;

kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na maelekezo ya Serikali kwa Wizara na Taasisi zake. Hata hivyo, msisitizo zaidi uwekwe katika kukamilisha mifumo ya usimamizi na malipo ya fedha kwa njia ya kieletroniki ili kuongeza na kufuatilia mapato yanayokusanywa na Taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeainisha namna itakavyoshirikiana na sekta binafsi katika kuibua na kugharamia miradi kwa utaratibu wa ushirikiano baina yake na sekta ya binafsi. Pamoja na kwamba kuna ongezeko la mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje na ile ya ubia, bado kuna ushiriki hafifu wa sekta binafsi katika kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na miradi mingi kutokidhi vigezo vya PPP vilivyowekwa na Serikali. Kamati inaona hali hii imechangiwa na kutokuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara, uhaba wa miundombinu, uwepo wa kodi zinazobadilika mara kwa mara, urasimu wa upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji na uwezo mdogo wa kifedha na taaluma kwa sekta binafsi za ndani.

Kamati ingependa kuona kuwa mwongozo huu unasimamia kikamilifu katika kuondoa matatizo hasa ukizingatia kuwa tunaelekea katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye lengo la kuhakikisha kwamba tunakuwa na uchumi imara wenye uwezo wa kuhimili ushindani kupitia ukuaji wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuiwezesha sekta binafsi kutoa mchango wake unaostahili katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba msukumo wa kipekee kwa Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhusu ujenzi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya rasilimali watu; Kamati ingependa kuona ni kwa namna gani mwongozo huu wa maandalizi wa Mpango na Bajeti umejielekeza katika kuhakikisha unatanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi wa viwanda hasa katika sura zifuatazo:-

(i) Kwanza kuandaa mpango mkakati wa kuanzisha, kukuza, kuviendeleza na kuvilinda viwanda nchini;

- (ii) Kukuza na kuendeleza viwanda vyenye uzalishaji mkubwa, wa kati na mdogo, ikiwa pamoja na uanzishwaji wa viwanda vipya;
- (iii) Kuboresha miundombinu ya kukuza Sekta ya Viwanda hasa kwa upande wa maji, barabara na umeme;
- (iv) Kurekebisha sheria, tozo na ada mbalimbali zitakazoweza uvutiaji wa uwekezaji wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo;
- (v) Kurekebisha Sheria za Ardhi ili kuruhusu uwekezaji mkubwa katika kilimo pamoja na kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji ili kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa malighafi za viwanda;
- (vi) Kuhakikisha kuna uhakika wa upatikanaji wa masoko ya bidhaa zitakazozalishwa na viwanda vyetu nchini;
- (vii) Kusimamia upatikanaji wa wataalamu wa viwanda wa daraja la juu, kati na la chini ili kuongeza ufanisi wa uzalishaji viwandani katika sekta mbalimbali za viwanda; na
- (viii) Kuhamasisha utafiti na matumizi ya teknolojia bora itakayolinda afya ya mlaji na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018. Mapendekezo haya yanalenga kutoa Mwongozo wa Kutayarisha Mipango ya Maendeleo ya Wizara, Taasisi za Serikali na sekta binafsi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Kwa kuzingatia mapendekezo haya, Kamati ingependa kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaiunga mkono Serikali kuchagua vipaumbele vichache vitakavyotekelezwa kwa kipindi husika. Lengo la kuchagua vipaumbele vichache ni kuwezesha rasilimali chache zilizopo zilete tija na matokeo chanya.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2017/2018 yanazingatia kuondoa changamoto zilizojitokeza kwenye kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017.

Aidha, kwa sasa Serikali inaandaa bajeti kwa kuzingatia Mfumo wa Programu ili kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika kutoa huduma kwa umma. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha programu hizi ambazo zimeanza kwa majaribio katika Wizara sita zinashabihiana na vipaumbele tulivyojiwekea katika mapendekezo ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote inayotaka kupiga hatua za haraka kiuchumi ni sharti iwekeze vya kutosha katika viwanda. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo na kuja na mikakati thabiti itakayoweza nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mpango huu yamelenga kutekeleza mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka, Mradi wa Kufufua Kiwanda cha *General Tyre*, uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo (*SIDO*), uendelezaji wa sekta za nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi pamoja na mafuta ya alizeti nchini pamoja na ubainishaji wa mnyororo wa thamani wa zao angalau moja kwa kila Halmashauri. Hata hivyo, ukifuatilia kwa makini mapendekezo yaliyopitiwa yamekuwa yakijirudia bila utekelezaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa mapendekezo ya mpango huu yaonyeshe mkakati na muda wa kukamilisha miradi hii ikiwemo upatikanaji wa fedha za kumaliza miradi husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana katika nchi yoyote kama rasilimali watu itakuwa haijaelimishwa vya kutosha na haina afya bora.

Kamati inaunga mkono Mpango wa Serikali wa kuboresha elimu na mafunzo ya ufundi kwa kuimarisha mifumo na miundombinu katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo. Vilevile Kamati inaunga mkono kujenga, kukarabati na kuboresha Hospitali za Rufaa na upatikanaji wa maji safi na salama na kuondoa majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya muda wa kati na muda mrefu ili kutatua changamoto inayoweza kujitokeza kwa ongezeko la wanafunzi wanaopata nafasi za kujiunga katika vyuo vya elimu ya juu. Suala la mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu imeonekana kuwa ni changamoto kutokana na; kwanza, wigo kuwa mdogo, vigezo kutozingatiwa na kukosekana kwa ufuatiliaji kwa waliokopa mikopo hiyo. Upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mikopo unaongezeka kwa kuongeza wigo na kuzingatia vigezo vya wahitaji ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata mikopo. Aidha, Serikali ihakikishe inaweka utaratibu wa kufuatilia wakopaji kupitia vitambulisho vya Taifa ili waliokopa warejeshe na hivyo kufanya mikopo hiyo kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 wakati wa majadiliano ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 kulikuwa na kilio kikubwa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu upungufu mkubwa wa zahanati na vituo vya afya hapa nchini. Serikali iliahidi Bunge lako kwamba italifanyia kazi suala hili kwa kufanya tathmini ya kina ili kujua mahitaji halisi pamoja na gharama ya ujenzi wake. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali

imekamilisha tathmini yake na itakuja na mpango mahsusi wa utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya afya kila kata na zahanati kila kijiji na kuujumuisha kwenye Mpango wa Maendeleo unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliamua kutenga shilingi milioni 50 kwa kila kijiji, mitaa na shehia kwa upande wa Zanzibar kama Mfuko wa Uwezeshaji kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia ushirika wa kuweka na kukopa. Mwaka 2016/2017 Serikali ilianza kutekeleza mpango huu kwa kutenga shilingi bilioni 56 pekee ili kuipa nafasi ya kuweza kuandaa utaratibu utakaofaa wa namna ya ugawaji wa fedha hizo, pamoja na usimamizi wake. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha maandalizi ya utaratibu huo na kuanza kutenga kiasi cha shilingi bilioni 200 kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2017 ili kuweza kukamilisha upelekaji wa fedha hizo kwenye maeneo husika katika kipindi cha miaka minne iliyosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoiwezesha sekta binafsi kuwekeza pamoja na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji, barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika, kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji, kuweka sheria za fedha na kodi zinazotabirika, kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda na kunakuwa na sheria bora za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuchagua miradi mikubwa ya kielelezo na kulinda bajeti zake. Utekelezaji wa miradi hii mahsusi unalenga kufanikisha utekelezaji wa Mpango na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Miradi hiyo ni ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Makaa ya Mawe na Chuma ya Liganga na Mchuchuma ni moja ya miradi mikubwa ya kielelezo iliyopangwa kutekelezwa. Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma utakapokamilika utawezesha uzalishaji wa megawati 600 ambazo zitasaidia sana kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme nchini. Mradi wa Chuma wa Liganga utakaozalisha chuma utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa kutoa malighafi ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na chuma kama vile nondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu mkubwa wa miradi hii, mipango ya utekelezaji wake imekuwa ya kusuasua sana. Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la kutolipa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuhamishwa katika maeneo miradi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuweka muda maalum wa ulipaji wa fidia pamoja na kukamilisha mazungumzo yake kuhusu mkataba wa mauziano ya umeme utakaozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya njia madhubuti ya kuiwezesha nchi kuingia haraka katika uchumi wa viwanda ni kupitia uwekezaji katika maendeleo ya viwanda vidogo vidogo, kuboresha uwekezaji katika maeneo ya *Export Processing Zone*, pamoja na Maeneo Maalum ya Uwekezaji yaani *Special Economic Zone*. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka uendelezaji wa maeneo haya likiwemo lile la Bagamoyo kwa kukamilisha ulipaji fidia wa eneo la uwekezaji na kuanza utekelezaji wa mradi wenyewe. Aidha, Serikali itenge maeneo mengine kila Mkoa na kuyapanga kulingana na mazao au bidhaa zitakazozalishwa katika Mkoa husika na kuyaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ulipaji wa fidia wa eneo la Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini na inaiomba iharakishe katika utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuboresha miundombinu ya usafirishaji kwa kujenga reli ya kati kwa *standard gauge*, kujenga barabara za lami pamoja na kufufua shirika letu la ndege kwa kuweza kununua ndege mbili mpya pamoja na kuendelea kuboresha shirika letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inapenda kutoa ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iziongezee mtaji Benki ya *TIB* na *TADB* ili ziongeze uwezo wake wa kuwakopesha wajasiriamali na wakulima.

(ii) Pia Serikali iweke kodi kubwa kwa bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa ndani ya nchi ili kuvilinda viwanda vyetu vya ndani; na pia Serikali ichague maeneo machache ya miradi ya maendeleo ya kipaumbele ambayo itaweza kuyakamilisha kwa muda mfupi.

(iii) Kamati pia inapendekeza Serikali ilipe fidia maeneo ambayo itaweka viwanda vikubwa na miradi mikubwa ya kilimo na pia ipange maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*. Napenda kuhitimisha kwa kukushukuru wewe pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa miongozo yao ambayo wamekuwa wakitupatia Waheshimiwa Wabunge.

Napenda pia kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Naibu wake Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Pia nawashukuru wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege kwa ushirikiano mkubwa ambao wameutoa ambao wamewezesha taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo kwa umuhimu, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretarieti ya Idara ya Kamati ya Bajeti kwa kuhudumia vyema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (Makofi)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO
WA MAENDELEO WA TAIFA PAMOJA NA MWONGOZO WA KUTAYARISHA
MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya bajeti imeusoma na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 iliyotayarishwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa muhtasari Mapendekezo hayo yanatoa maelekezo kwa Maafisa Masuhuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma namna bora ya kuandaa na kutekeleza mipango na bajeti itakayoendana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21); ambavyo ni kuwa na viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa misingi ya uchumi; kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu; kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji pamoja na usimamizi wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mapendekezo haya yanaelekeza vyombo husika utaratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini za Mipango na Bajeti zao ili kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za Serikali, kwa kuzingatia miongozo ya kisheria; pamoja na namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa rasilimali fedha kugharamia miradi ya maendeleo; kutoa mwongozo wa kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na wadau wengine; pamoja na mapitio ya ukuaji wa Uchumi Jumla kwa kuzingatia utekelezaji wa sera za fedha na kodi tukielekea mwaka 2017/18.

2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016

Mheshimiwa Spika, Takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonyesha kwamba, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016 (Januari hadi Juni) Pato Halisi la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 23.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Sekta zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 17.4) na uchimbaji madini na mawe (asilimia 13.7). Aidha, shughuli zilizokuwa na ukuaji mdogo ni pamoja na huduma za chakula na malazi (asilimia 0.6) pamoja na usambazaji maji safi na uthibiti wa maji taka. Mwenendo wa mfumuko wa bei umekuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa kutoa angalizo kuhusu kushuka kwa wastani wa pato kwa kila mtu katika Dola za Kimarekani kutoka Dola za Kimarekani 1,047 mwaka 2014 hadi Dola za Kimarekani 966.5 mwaka 2015 ambako kunaelezwa kuwa kulitokana na kushuka kwa thamani ya shilingi. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani iliendelea kupungua katika kipindi chote cha mwaka 2015 na nusu ya kwanza ya mwaka 2016. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,179.0 Julai 2016 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,086.4 Julai 2015.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri zinazochukuliwa na Serikali katika kuongeza Pato la Taifa na kupunguza Mfumuko wa bei; Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa katika eneo hili hasa katika upatikanaji wa vyanzo vipya vya mapato. Serikali imekuwa ikitegemea Mapato yake kwa kuibua Mapato ya Ndani zaidi (*Tax Revenue*) kuliko kuangalia vyanzo vingine vya mapato (*Non Tax Revenue*) vitakavyosaidia kugharamia Bajeti ya Serikali. Ipo haja ya kuona kodi zinazobuniwa zinasaidia kuongeza ari ya uzalishaji, ujasiriamali na uwekezaji na hivyo kuongeza Pato la Taifa, Aidha, ukuaji wa uchumi ujielekeze zaidi katika kuongeza kipato kwa Mtanzania na hivyo kufikia malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo kuwa ifikapo mwaka 2025 pato la kila mtanzania liwe limefikia Dola za Kimarekani 3,000.

3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/18

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa na hatimaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015. Sheria hii pamoja na Kanuni zake vitasaidia kuhakikisha usimamizi na uwajibikaji katika hatua zote za mchakato wa bajeti unazingatiwa. Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mfumo wa Programu wa Kibajeti ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kuanzisha utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha awamu ya nne. Mifumo hii kwa ujumla itasaidia sana kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Baada ya pongezi hizi, Kamati ingependa kutoa maoni/ ushauri na mapendekezo kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Mwaka 2017/18 kama ifuatavyo;

3.1 Makisio ya awali ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18

Mheshimiwa Spika, makisio ya awali ya Bajeti ya Serikali yanaonyesha kuwa jumla ya shilingi **trilioni 32.946** zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 ambapo kati ya fedha hizo shilingi **trilioni 20.872** sawa na **asilimia 63** ya bajeti yote zitatokana na mapato ya ndani. Kamati inaamini kuwa, Serikali imepanga kuongeza mapato yake ya ndani hasa yale yatokanayo na kodi kwa kupanua wigo wake wa kukusanya kodi kwa kuja na vyanzo vipya ambavyo havitakuwa kero kwa wafanyabiashara na wananchi wote kwa ujumla ili kuweza kufikia lengo la mapato yatokanayo na kodi lililo ongezeko kwa **asilimia 16.532** kutoka shilingi **trilioni 15.105** mwaka 2016/17 hadi shilingi **trilioni 18.097** mwaka 2017/18. Aidha pamoja na hatua hii muhimu ni vema Serikali ikajielekeza katika kuangalia pia vyanzo vingine vya mapato (*Non Tax Revenue*) vitakavyosaidia kugharamia Bajeti ya Serikali.

3.2 Mwenendo wa Mikopo

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonyesha kuwa Serikali imepanga kukopa ndani kiasi cha shilingi **trilioni 6.28** (trilioni 4.435 kulipia hati fungani na dhamana zilizoiva na shilingi **trilioni 1.859** ambayo ni sawa na **1.5%** ya Pato la Taifa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo) kwa mwaka 2017/18. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 14.49** ukilinganisha na kiwango cha mikopo ya ndani iliyokopwa katika mwaka wa fedha 2016/17 cha shilingi **trilioni 5.37**. Kamati haipingani na mpango wa Serikali wa kukopa kiasi cha shilingi **trilioni 2.080** (Dola za Kimarekani 900) kutoka katika vyanzo vyake vya nje ili kugharamia utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo. Kamati ingependa kuishauri Serikali kupunguza kukopa zaidi katika vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa, ukopaji mkubwa wa ndani unapunguza uwezo wa wafanyabiashara, wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kuweza kukopa katika Taasisi za Fedha hapa nchini. Taasisi za Fedha zinaona ni salama zaidi kuikopesha Serikali kuliko wananchi ili kupunguza 'risk' zinazojitokeza katika ukusanyaji na usimamizi wa mikopo hiyo. Ili kutatua changamoto hii ni vema Serikali ikatumia nafasi yake ya uwezo wa kukopa nje ya nchi ili kugharamia miradi itakayoleta matokeo ya haraka ya kiuchumi yenye *multiplier effect*. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka zoezi la *Sovereign Rating* ili kuiwezesha kukopa zaidi kutoka katika vyanzo vya nje ili iweze kugharamia miradi yake ya maendeleo na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango cha fedha itakachokopa kutoka katika vyanzo vya ndani.

3.3 Uwasilishaji wa Mapato ya Serikali kwenda Benki Kuu (BOT)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuanzisha utaratibu wa Wizara, Taasisi na Mashirika yote ya Umma kutakiwa kuwasilisha Benki Kuu mapato yao yote wanayoyakusanya kila baada ya masaa 24 baada ya kukusanya. Lengo la utaratibu huu ni kuiwezesha Serikali kuwa na udhibiti wa fedha za umma. Utaratibu huu pia utaiwezesha Serikali kujua ina fedha kiasi gani zilizokusanywa wakati wowote. Hata hivyo Kamati inapenda kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka haraka iwezekanavyo fedha za matumizi ya Wizara, Taasisi na Mashirika hayo kadiri ya mipango kazi inavyoonyesha na kadiri walivyopitishiwa na Bunge katika bajeti zao ili kuepuka kukwamisha utekelezaji. Aidha Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Mwongozo au Utaratibu wa kubakisha fedha (*Retention*) kwenye baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali zenye uhitaji wa fedha hizo kwa shughuli maalumu kwa mujibu wa Sheria husika.

3.4 Kodi ya Majengo

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kuwa itaendelea na utaratibu iliouanzisha katika mwaka wa fedha wa 2016/17 wa ukusanyaji wa kodi ya majengo kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa jambo hili kwa TRA kuanza kukusanya katika maeneo machache. Hii itaiwezesha TRA kujipanga vizuri kabla ya kuanza kukusanya maeneo yote. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum utakao oneshwa namna TRA watavyoendelea kukusanya katika maeneo yaliyosalia (Manispaa, Halmashauri na Miji Midogo). Aidha, Kamati ingependa kurudia ushauri wake ilioutoa mwaka jana kwa Serikali kuhusu majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini kukusanya viwango vya kodi vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Vile vile katika ufanyaji tathmini, Serikali izingatie hali ya uchumi wa eneo husika, thamani ya ardhi na thamani ya nyumba yenyewe katika eneo husika.

3.5 Serikali kuhamia Makao Makuu Dodoma

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Serikali - Dodoma kutoka Dar es salaam. Aidha, Serikali imeainisha namna (utaratibu na ratiba) itakavyotekeleza jambo hili kwa awamu katika muda mfupi na wa kati na hivyo kutoa fursa kwa Wizara husika kujipanga na kuwezesha utekelezaji wa uamuzi huu. Pamoja na nia hii nzuri ya Serikali, Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha za matumizi mengineyo (O.C) kwa mafungu husika ili kuweza kugharamia mpango huu vizuri hasa kwa upande wa malipo ya stahili za watumishi watakaohamishwa. Kamati inatoa pendekezo hili kwa sababu Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 kuwa fedha za matumizi mengineyo (O.C) zimepungua kutoka **shilingi trilioni 2.547** zilizopitishwa mwaka 2016/17 hadi **shilingi trilioni 2.214** zinazopendekezwa kwa mwaka 2017/18.

3.6 Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Mwongozo umeainisha mikakati na hatua mbalimbali za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Mikakati hiyo ni pamoja na kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii, kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato. Kamati inakubaliana na maelekezo ya Serikali kwa Wizara na Taasisi zake, Hata hivyo msisitizo zaidi uwekwe katika kukamilisha mifumo ya usimamizi na malipo ya fedha kwa njia ya vifaa vya kielektroniki ili kuongeza na kufuatilia mapato yanayokusanywa na Taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali. Aidha Serikali iendelee kuhamasisha na kuongeza matumizi ya mashine za EFD na wananchi kwa ujumla kudai risiti halali pale wanaponunua bidhaa. Maeneo yenye mianya ya upotevu wa fedha kama vile uwepo wa bandari bubu na biashara za magendo kupitia mipaka yetu yadhhibiwe kikamilifu ili kuongeza upatikanaji wa mapato ya Serikali.

3.7 Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha namna itakavyoshirikiana na Sekta binafsi katika kuibua na kugharamia miradi kwa utaratibu wa Ushirikiano baina yake na Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Pamoja na kwamba kuna ongezeko la mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje na ile ya ubia, bado kuna ushiriki hafifu wa sekta binafsi katika kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na miradi mingi kutokidhi vigezo vya PPP vilivyowekwa na Serikali. Kamati inaona hali hii imechangiwa na kutokuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na

ufanyaji biashara; uhaba wa miundombinu (barabara, maji na umeme); uwepo wa kodi zinazobadilika mara kwa mara; urasimu wa upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji; na uwezo mdogo wa kifedha na taaluma kwa sekta binafsi za ndani. Kamati ingependa kuona kuwa mwongozo huu utasimamia kikamilifu katika kuondoa matatizo haya ukizingatia kuwa tunaelekea katika utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye lengo la kuhakikisha tunakuwa na uchumi imara wenye uwezo wa kuhimili ushindani kupitia ukuaji wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Serikali imepanga kuongeza ushiriki wa Sekta binafsi katika kutekeleza Mpango wa maendeleo wa Taifa kutoka shilingi trilioni 6.8 mwaka 2016/17 hadi shilingi trilioni 7.4 mwaka 2017/18. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa ushiriki wa Sekta binafsi bado ni mdogo. Kamati inaishauri Serikali kupunguza kiwango ambacho imekiweka kama mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18. Kamati inaishauri Serikali iboreshe mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuiwezesha Sekta Binafsi kutoa mchango wake unaostahili katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

3.8 Kuimarisha uchumi kupitia Sekta ya Viwanda

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba msukumo wa kipekee kwa Serikali ya awamu ya Tano ni kuhusu ujenzi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya rasilimali watu '*Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development*'. Kamati ingependa kuona ni kwa namna gani mwongozo huu wa maandalizi ya Mpango na Bajeti umejielekeza katika kuhakikisha unatanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi wa viwanda hasa katika sura zifuatazo:-

- kuandaa mpango mkakati wa kuanzisha, kukuza, kviendeleza na kuvilinda viwanda nchini;
- kukuza na kuendeleza viwanda vyenye uzalishaji mkubwa, wa kati na mdogo; ikiwa pamoja na uanzishwaji wa viwanda vipya;
- kuboresha miundombinu ya kukuza sekta ya viwanda hasa kwa upande wa maji, barabara na umeme;
- kurekebisha Sheria, tozo na ada mbalimbali zitakazoweza uvutiaji wa uwekezaji wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo;
- kurekebisha Sheria za Ardhi ili kuruhusu uwekezaji mkubwa katika kilimo pamoja na kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji ili kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa malighafi za viwanda;

- kuhakikisha kuna uhakika wa upatikanaji wa masoko ya bidhaa zitakazozalishwa na viwanda vyetu nchini;
- Kusimamia upatikanaji wa wataalamu wa viwanda wa daraja la juu, kati na la chini ili kuongeza ufanisi wa uzalishaji viwandani katika sekta mbalimbali za viwanda;
- kuhamasisha utafiti na matumizi ya teknolojia bora itakayolinda afya ya mlaji na mazingira;

4.0. MAONI NA USHAURI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2017/18. Mapendekezo haya yanalenga kutoa mwongozo wa kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21). Kwa kuzingatia mapendekezo haya, Kamati ingependa kutoa maoni na ushauri ufuatao;

4.1. Ujumuishwaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Mwaka unaoendelea

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiunga mkono Serikali kwa kuchagua vipaumbele vichache vitakavyotekelezwa kwa kipindi husika. Lengo la kuchagua vipaumbele vichache ni kuwezesha rasilimali chache zilizopo zilete tija na matokeo chanya. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Mwaka 2017/18 yanazingatia kuondoa changamoto zilizojitokeza kwenye kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17. Aidha, kwa sasa Serikali inaandaa bajeti kwa kuzingatia Mfumo wa Programu (Programme Based Budget –PBB) ili kutekeleza Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika kutoa huduma kwa umma. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha program hizi ambazo zimeanza kwa majaribio katika Wizara sita zinashabihiana na vipaumbele tulivyojiwekea katika mapendekezo ya mpango huu.

4.2. Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

Mheshimiwa Spika, Nchi yoyote inayotaka kupiga hatua za haraka kiuchumi ni sharti iwekeze vya kutosha katika viwanda. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua hilo na kuja na mikakati thabiti itakayowezesha nchi yetu kufanya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wetu wana mitaji midogo na hawana teknolojia ya hali ya juu, hivyo viwanda vidogo vidogo ni moja ya suluhisho

muhimu la kuweza kuongeza ushiriki wao katika mageuzi ya viwanda katika nchi yao. Viwanda vidogo vitakavyoanzishwa na wajasiriamali wetu siyo tu vitaliingizia Taifa mapato kupitia kodi bali vitaongeza ajira, vitatumia malighafi zinazozalishwa hapa hapa nchini pamoja na kupunguza au kuacha kabisa kuagiza nje ya nchi bidhaa ambazo ni rahisi kuzalishwa hapa nchini kwa mfano samani, vibiriti, siagi, jibini, *tomato/chili sauce*, *toothpick*, vijiko, sahani, sufuria n.k. Jambo la msingi ni kuunganisha mnyororo mzima wa uzalishaji kuanzia kwa mzalishaji wa malighafi kwenda kwa wazalishaji katika viwanda vidogo na mwisho kwa mlaji/mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango huu yamelenga kutekeleza mradi wa Magadi Soda katika bonde la Engaruka, mradi wa kufufua kiwanda cha General tyre, uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo- SIDO, uendelezaji wa Sekta za nguo na mavazi, ngozi na bidhaa za ngozi pamoja na mafuta ya alizeti nchini pamoja na ubainishaji wa mnyororo wa thamani wa zao angalau moja kwa kila Halmashauri. Hata hivyo, ukifuatilia kwa makini mapendekezo yaliyopita yamekuwa yakirudia rudia bila utekelezaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa mapendekezo ya mpango huu yaonyeshe mkakati na muda wa kukamilisha miradi hii ikiwemo upatikanaji wa fedha za kumaliza miradi husika.

4.3. Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu

Mheshimiwa Spika, Hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana katika nchi yoyote kama rasilimali watu itakuwa haijaelimishwa vya kutosha na haina afya bora. Kamati inaunga mkono Mpango wa Serikali wa kuboresha elimu na Mafunzo ya ufundi kwa kuimarisha mifumo na miundombinu katika shule za Awali, Msingi na Sekondari na vyuo. Vilevile Kamati inaunga mkono kujenga, kukarabati na kuboresha Hospitali za Rufaa na upatikanaji wa maji safi na salama na kuondosha maji taka.

Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya muda wa kati na muda mrefu ili kutatua changamoto inayoweza kujitokeza kwa ongezeko la wanafunzi wanaopata nafasi za kujiunga katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Suala la mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu imeonekana kuwa ni changamoto kutokana na kwanza wigo kuwa mdogo, vigezo kutozingatiwa na kukosekana kwa ufuatiliaji kwa waliopokea mikopo hiyo. Upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa Upatikanaji wa mikopo unaongezeka kwa kuongeza wigo na kuzingatia vigezo vya wahitaji ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata mikopo. Aidha, Serikali ihakikishe inaweka utaratibu wa kufuatilia wakopaji kupitia vitambulisho vya Taifa ili walio kopa warejeshe na hivyo kufanya mikopo hiyo kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana wakati wa majadiliano ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 kulikuwa na kilio kikubwa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu upungufu mkubwa wa Zahanati na Vituo vya Afya hapa nchini. Serikali iliahidi Bunge kwamba italifanyia kazi suala hili kwa kufanya tathmini ya kina ili kujua mahitaji halisi pamoja na gharama ya ujenzi wake. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali imekamilisha tathmini yake na itakuja na mpango mahsusi wa utekelezaji wa ujenzi wa Vituo vya Afya kila Kata na Zahanati kila kijiji na kuujumuisha kwenye Mpango wa Maendeleo unaokuja.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kutenga shilingi milioni 50 kwa kila Kijiji, Mitaa na Shehia kwa upande wa Zanzibar kama Mfuko wa Uwezeshaji (*Revolving Fund*) kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia ushirika wa kuweka na kukopa. Mwaka 2016/17 Serikali ilianza kutekeleza mpango huu kwa kutenga shilingi **bilioni 59** pekee ili kuipa nafasi ya kuweza kuandaa utaratibu utakaofaa wa namna ya ugawaji wa fedha hizo, pamoja na usimamizi wake. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha maandalizi ya utaratibu huo na kuanza kutenga kiasi cha shilingi **bilioni 200** kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 ili kuweza kukamilisha upelekaji wa fedha hizo kwenye maeneo husika katika kipindi cha miaka minne iliyosalia.

4.4. Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji na ushiriki wa Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoiwezesha Sekta binafsi kuwekeza pamoja na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege), kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika, kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji, kuweka sheria za fedha na kodi zinazo tabirika (zisizo badirika mara kwa mara), kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda na kunakuwa na sheria bora za ajira.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo unaonesha kuwa ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza mpango wa mapinduzi ya viwanda nchini utachukua miaka mingi sana kufikia malengo yake ama isiyafikie kabisa. Duniani kote, hakuna nchi yeyote inayoweza kupiga hatua za Kiuchumi bila ya kuwa na msukumo mkubwa katika uwekezaji wa viwanda kupitia sekta binafsi hasa tukizingatia inachangia kuongeza mapato na ajira katika uchumi. Mapendekezo ya Mpango yaagize mambo yatakayo fanyika katika kuweka mazingira wezeshi yatakayo wezesha Sekta Binafsi kufanya kazi yake. Maeneo muhimu ni yenye viashiria vya kufanya biashara kama vile kufungua au kufunga biashara, upatikanaji wa Vibali vya biashara, upatikanaji mikopo, kulinda wawekezaji, ulipaji kodi, mauzo ya ndani na nje ya nchi na utekelezaji wa mikataba ya

biashara. Ripoti ya Benki ya dunia ya Kufanya Biashara ya mwaka 2015 (*Doing Business Report 2015*) inaonyesha Tanzania tunashika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 duniani na inashika nafasi ya 15 kati ya nchi 47 za kusini mwa Jangwa la Sahara katika jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Tupo nyuma sana! Ili tuweze kuvutia wawekezaji wengi katika viwanda ambavyo tunatarajia kuvianzisha ni lazima tuwe na mkakati madhubuti wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

4.5. Miradi Mikubwa ya Kielelezo

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuchagua miradi mikubwa ya kielelezo (*Flagship projects*) na kulinda bajeti zake (*ringfence*). Utekelezaji wa Miradi hii mahsusi unalenga kufanikisha utekelezaji wa Mpango na kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Miradi hiyo ni ifuatayo;

4.5.1 Mchuchuma na Liganga

Mheshimiwa Spika, Miradi ya makaa ya mawe na chuma ya Liganga na Mchuchuma ni moja ya miradi mikubwa ya kielelezo iliyopangwa kutetelezwa. Mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma utakapokamilika utawezesha uzalishaji wa **MW 600** ambazo zitasaidia sana kupunguza tatizo la upatikanaji wa umeme nchini. Mradi wa chuma wa Liganga utakaozalisha chuma utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa kutoa mali ghafi ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na chuma kama vile nondo. Pamoja na umuhimu mkubwa wa miradi hii mipango ya utekelezaji wake imekuwa ya kusuasua sana. Kumekuwa na tatizo la muda mrefu la kutolipa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuhamishwa katika maeneo miradi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuweka muda maalum (*timeframe*) wa ulipaji wa fidia pamoja na kukamilisha mazungumzo yake kuhusu Mkataba wa Mauziano ya umeme utakaozalishwa (PPA).

4.5.2. Maeneo Maalum ya Uwekezaji na Viwanda vidogo vidogo

Mheshimiwa Spika, Moja ya njia madhubuti ya kuiwezesha nchi kuingia haraka katika uchumi wa viwanda ni kupitia uwekezaji katika maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, kuboresha uwekezaji katika maeneo ya *Export Processing Zones - EPZ* pamoja na Maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zones – SEZ*). Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka uendelezaji wa maeneo haya likiwemo lile la Bagamoyo SEZ kwa kukamilisha ulipaji fidia wa eneo la uwekezaji na kuanza utekelezaji wa mradi wenyewe. Aidha, Serikali itenge maeneo mengine kila Mkoa na kuyapanga (*Classify*) kulingana na mazao au bidhaa zitakaozalishwa katika Mkoa husika na kuyaendeleza kwa kuyawekea miundombinu kama vile maji, umeme na barabara/reli ili kurahisisha uwekezaji katika maeneo hayo.

4.5.3 Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ulipaji fidia kwa wananchi waliopisha mradi huu. Hata hivyo Kamati inasikitishwa na muda mrefu unaochukuliwa na Serikali katika uendelezaji wa eneo hili muhimu. Kamati inasisitiza juu ya Serikali kuona umuhimu wa kuhakikisha malengo ya mradi huu yanatimizwa kwa kuzingatia kuwa mwekezaji wa awali kutoka China alikwisha ondoka. Hivyo, ni wakati sasa wa Serikali kuhuisha mazungumzo ili mwekezaji mpya apatikane kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi huu.

4.5.4. Uboreshaji wa Miundombinu ya Usafirishaji

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kuboresha miundombinu ya usafirishaji kwa kujenga reli ya kati kwa *standard gauge*, kujenga barabara za lami na kuboresha shirika la ndege la Taifa (ATCL) kwa kuweza kununua ndege mbili mpya pamoja na kuendelea kuboresha usimamizi wa Shirika.

Mheshimiwa Spika, Reli ya TAZARA ina uwezo mkubwa wa kubeba mizigo, kwa kuwa reli hiyo ina viwango vya ratili 80 lakini bado haijaweza kuleta manufaa kwa kiwango kinachopaswa. Reli hiyo imeshindwa kujiendesha kibiashara kutokana na baadhi ya wadau wa nchi jirani kutoitumia kabisa. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Zambia kuendelea kuelimisha wadau husika kuhusu ubora wa Reli hiyo ili kurejesha imani kwa watumiaji na hivyo kuweza kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mipango mizuri ya Serikali ya kuendelea kujenga barabara za lami katika maeneo mbalimbali nchini, Kamati inaona ni vema Serikali ikaweka mkazo zaidi katika kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo ya kimkakati ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwenye maeneo husika. Kwa mfano barabara kuelekea katika Mbuga na Hifadhi za wanyama hasa zilizopo mikoa ya kusini mwa nchi yetu, za maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi, zile zinazoelekea kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na kwenye miradi mikubwa ya kimkakati bado hazijatumika ipasavyo katika kuchangia kukuza uchumi wa nchi yetu. Umarishaji wa barabara kwenye maeneo haya ya kimkakati yataiwezesha Serikali kupata fedha zaidi na hivyo kuendelea kuboresha miundombinu katika maeneo mengine yaliyobakia.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na nchi yetu kuwa na fursa nzuri za kijiografia, bado hatujaitumia fursa hiyo ipasavyo. Kumekuwepo na hatua nzuri zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha bandari ya Dar es salaam, juhudi hizo hazitoshelezi kuwezesha nchi yetu kuwa “gateway” katika ukanda huu wa Afrika mashariki na Kati kama ilivyo kwa jiji la Hongkong kwa upande wa Asia ya Mashariki. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka ukarabati na ujenzi wa gati 13 na

14, uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji katika bandari pamoja na kuboresha mfumo mzima wa kuhudumia wateja ili kutoa fursa kwa nchi jirani kutumia bandari yetu ili kukuza uchumi wa nchi yetu.

4.6. Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati inapata shaka ni namna gani Serikali imejipanga katika kutekeleza Mipango yake kikamilifu. Takwimu zinaonyesha kwamba katika mipango yote iliyopita kuanzia ule wa 2011/12-2015/16; miradi mingi haijaweza kutekelezwa kwa ukamilifu. Bado kuna tatizo kwa upande wa Serikali katika kupata fedha za kugharamia miradi husika, pia ushiriki mdogo wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi hiyo ambayo Serikali ilitegemea kupata mchango mkubwa kutoka kwao.

4.7. Maoni ya jumla

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsusi, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla yafuatayo;

- Serikali iziongezee mtaji Benki ya TIB na TADB ili ziongeze uwezo wake wa kuwakopesha wajasiriamali na wakulima.
- Pamoja na kutambua kuwa Dunia sasa ipo katika mfumo wa soko huria, nchi zote duniani zimekuwa na utaratibu wa kulinda masoko ya bidhaa zake. Serikali iweke mkakati kuhakikisha bidhaa ambazo si za lazima sana au bidhaa ambazo zinaweza kutengenezwa hapa nchini kama vile toothpick, maziwa, nyama, tomato sauce, samaki, unga wa mahindi na ngano, mchele n.k haziingizwi nchini kwa kuweka kodi kubwa ya uingizaji wa bidhaa hizo.
- Serikali ichague maeneo machache ya miradi ya maendeleo ya kipaumbele ambayo itaweza kuyakamilisha kwa kuzingatia uwezo wake wa fedha ili iyakamilishe hayo kwa ukamilifu ndipo indelee na maeneo mengine badala ya kuwa na miradi mingi sana na hivyo kufanya utekelezaji wake kuwa mgumu.
- Serikali ifanye mazungumzo na wamiliki wa viwanda vyote vilivyokufa ili kuona namna bora ya kuvifufua kwa viwanda vinavyoweza kufufuliwa.
- Kamati inaunga mkono mpango wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kutoa mikopo ya muda mfupi, kati na mrefu katika Sekta ya Kilimo pamoja na kugharamia miundombinu ya umwagiliaji, huduma za maghala na usafirishaji. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati maalum wa kuandaa mashamba makubwa na madogo kwa kuyapima ili kuweza kuwavutia wawekezaji na kuondoa migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikitokea mara

kwa mara katika maeneo mengi kwa wananchi kuvamia mashamba yaliyotelekezwa.

- Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na umwagiliaji ishirikiane na Sekta Binafsi kuanzisha minada ya mazao ya biashara kama vile Chai ili kurahisisha upatikanaji wa soko kwa wakulima wetu.
- Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa baadhi ya kodi na tozo zilizopo katika sekta ya kilimo. (Mfano kuna tozo zipatazo 37 katika zao la chai pekee.)
- Serikali ilifanyie marekebisho ratiba yake ya uandaaji wa mpango wa maendeleo wa Taifa, 2017/18 ili kuwezesha ufanisi wa kutoa mapendekezo ya mpango kwa mwaka husika.
- Serikali ikamilishe haraka mpango wake wa kurasimisha biashara na mali za wanyonge ili kuziongezea thamani, kuwawezesha waweze kukopa katika taasisi za kifedha lakini pia kuwezesha Serikali kukusanya kodi.
- Kamati imegundua kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa Sare za Askari wetu. Kamati inaona ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili Serikali iliwezeshe kifedha Jeshi la Magereza ili liweze kuboresha viwanda vyake vya kuzalisha nguo (Sare) na viatu. Viwanda hivi vizalishe sare za majeshi yote, sare za shule za Serikali za Msingi, sekondari na Vyuo vya Ufundi, Sare za Manesi na madaktari pamoja na Sare za wafungwa.
- Kamati inashauri, kwa kuwa NSSF ilishawekeza dola za Kimarekani milioni kumi (10) katika kiwanda cha General Tyre basi wapewe nafasi ya kukiendeleza kiwanda hiki. Serikali iwakutanishe General Tyre, TIB na NSSF ili waone namna bora ya kukifufua kiwanda hiki
- Kamati inashauri NDC iruhusiwe kukopa au kushirikisha na Mifuko ya Hifadhi ya jamii au Benki za ndani kama CRDB, TIB ili kwa pamoja wawekeze katika mradi wa Kuhusu Kiwanda cha magadi Soda.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia Wabunge. Namshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa

Mwaka pamoja na mwongozo kwa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu masuala hayo mawili muhimu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat S. Kandege, Mb - M/Kiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jitu V. Soni, Mb
5. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
6. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
7. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
8. Mhe. Maria Ndila Kangonye, Mb
9. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
10. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
15. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
16. Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
17. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
18. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
19. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
20. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
21. Mhe. David Ernest Silinde, Mb

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretariati ya Idara ya Kamati ya Bajeti kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Hawa A. Ghasia, Mb

MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

01 Novemba, 2016

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Sasa tunamkaribisha Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ili naye aweze kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

MHE. HALIMA J. MDEE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya na uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Tano wa Bunge tukiwa salama. Aidha, nawapongeza viongozi wakuu wa CHADEMA na UKAWA kwa ujumla, kwa kazi kubwa wanayofanya kutetea na kulinda misingi ya demokrasia hapa nchini ambayo kwa sasa ipo katika majaribu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018 uliopo mezani, napenda niweke *record* sawa kuhusu uwasilishwaji wa mpango. Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Katiba, Sheria na hata Kanuni za Bunge katika uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa utekelezaji hafifu wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaelekeza kwamba Bunge litakaa kama Kamati ya Mpango katika Mkutano wake wa mwezi Oktoba – Novemba kila mwaka ili kujadili na kuishauri Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata; Kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaelekeza kwamba Mapendekezo ya Mpango pamoja na Makisio ya Bajeti yatawasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Februari kila mwaka au kama Bunge halipo kwenye Mkutano katika mwezi wa Februari, basi katika wiki ya kwanza ya Mkutano huo utakapoitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mgongano wa wazi kati ya Kanuni za Bunge na Sheria ya Bajeti kuhusu uwasilishwaji wa Mpango na Makisio ya Bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata. Uzoefu unaonyesha kwamba pale kunapotokea mgongano kati ya kanuni na sheria, sheria ndiyo husimama; lakini kwa hapa Bungeni mambo yamekuwa tofauti kwa sababu sheria imewekwa kando na badala yake Kanuni za Bunge ndiyo zimesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizingatia makatakwu ya kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti, mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yalitakiwa yawasilishwe Bungeni katika Bunge la Januari na Februari. Mantiki ya Sheria ya Bajeti hapa, kwa mujibu wa kifungu cha 21(3) cha sheria hiyo, ni kutoa mwanya wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoendelea (*current financial year*) na makisio ya hali ya uchumi kwa miaka

mitatu ya fedha inayofuatia. Ili tathmini hiyo iweze kutoa mwanga wa mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti, basi angalau iwe ni tathmini ya robo ya pili au nusu ya kwanza ya mzunguko wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, tathmini iliyowasilishwa hapa ni tathmini ya robo ya kwanza ya mzunguko wa bajeti ambayo inaishia tarehe 30 Septemba. Robo ya pili inayoishia tarehe 30 Disemba, haijaguswa kabisa kutokana na ukweli kwamba hatujafika huko. Kutegemea tathmini ya robo ya kwanza ambayo utekelezaji wake ni chini ya robo kwa ajili ya kufanya makisio ya miaka mitatu mfululizo ni kutumia vibaya maudhui ya tathmini na faida zake katika kusaidia kufanya makisio ya bajeti za miaka mitatu inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninaposoma hotuba hii sasa hivi, hata hiyo tathmini ya robo ya kwanza ni siri ya Serikali peke yake kwa sababu hata Kamati ya Bajeti ya Bunge haijapata. Kwa hiyo, tunajadili kitu ambacho Mheshimiwa Dkt. Mpango na wenzake wanajua, lakini Kamati mahususi ya Bunge haijui Serikali ime-*perform* vipi katika robo hii ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mgongano huo wa Kanuni za Bunge na Sheria ya Bajeti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwako wewe Mwenyekiti ukiwa unamwakilisha Mheshimiwa Spika, kuiagiza Kamati ya Kanuni kufanya marekebisho ya Kanuni ya 94(1) ili izingatie matakwa ya kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge kwa manufaa ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi mbovu unavyochangia kuyumba kwa uchumi. Licha ya mbwembwe nyingi za Serikali ya Awamu ya Tano, inayotokana na chama kilichokaa madarakani toka mwaka 1961 tumeshuhudia Serikali iliyotengeneza watumishi hewa ikisitisha ajira kwa kigezo kuwa inafanya uhakiki wa watumishi wake. Jambo hili limepelekea kuyumba kwa uchumi kwa baadhi ya familia ambazo zina watu wenye sifa ya kuajiriwa katika sekta ya umma kama vile walimu, manesi na madaktari. Kusimamishwa huku kwa ajira kumefanya nguvu kazi iliyokuwa na uwezo wa kuzalisha kuishi kama ombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Serikali hii ikiwaumiza sana wafanyabiashara wakubwa na wa kati kwa kukamata mali zao kama Mheshimiwa Rais alivyofanya kwa kukamata mali za mfanyabiashara kwa Kitanzania Salim Bakhresa. Sukari yake ilishikiliwa na Serikali bila kutoa sababu zozote zile na Mheshimiwa Rais aliamua kuiachia sukari hiyo bila kutoa sababu zozote za maana kwa umma. Hali iko hivyo kwa wafanyabiashara wengi sana ambao akaunti zao benki zimeshikiliwa na Serikali bila kuelezwa sababu, jambo

ambalo linapelekea kuporomoka kwa uchumi kwa kasi katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wale wote waliokuwa wanahusika kwa namna moja au nyingine kuhujumu uchumi, lakini tunapinga kwa nguvu zote kwa dola kutumia mamlaka yake kuonea au kunyanyasa wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao kwa kufuata sheria na taratibu za nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia vilevile sekta ya kilimo ambayo imeathirika sana hasa kutokana na uamuzi wa Benki Kuu kuzuia baadhi ya benki kukopesha wakulima kama ilivyofanya kwa Benki ya Maendeleo kwa hoja kuwa kama wakiendelea kukopesha miradi ya kilimo, kuna hakuna uhakika wa mikopo hiyo kurejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Magufuli tumeshuhudia sekta ya hoteli na utalii iko ICU na hasa kutokana na uamuzi wa Serikali kuanzisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye huduma zote za utalii huku jirani zetu Wakenya wanaojua kujiongeza wakizifuta. Jambo ambalo limepelekea kushuka kwa idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu na hivyo kufanya hoteli zilizokuwa zinafanya biashara ya utalii pamoja na makampuni yaliyokuwa yakijihusisha na biashara ya utalii kwa ujumla kuteketea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mitaa hasa Majiji, zimeathirika sana kutokana na uamuzi wa Serikali kuamua kukusanya kodi ya majengo kupitia TRA badala ya Halmashauri ambazo awali zilikuwa zikifanya jukumu hilo. Ni muhimu Bunge hili Tukufu likaelewa kwamba Serikali iliipoka mamlaka TRA miaka miwili iliyopita baada ya *poor performance*, imerudisha kwenye Halmashauri, zimeanza kufanya vizuri, Serikali imepoka, leo ni mwezi wa nne Halmashauri haijakusanya mapato, TRA haijakusanya mapato, tunategemea Halmashauri zetu tunaziendeshaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia sekta ya afya imekuwa ikizorota kwa kasi kubwa licha ya porojo zinazopigwa nje na ndani ya Bunge.

Hivi karibuni tumeshuhudia ukosefu mkubwa wa madawa, chanjo na vifaa tiba katika hospitali zetu mbalimbali hapa nchini. Hali hii imepelekea wananchi kupoteza maisha kutokana na kukosekana kwa dawa na kundi la watoto limeathirika sana kutokana na kukosekana kwa chanjo kwenye hospitali zetu. Huku tukishuhudia mgongano wa kauli kati ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Waziri akidai dawa ziko tele, huku boshi wake akisema hali ni tete. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia sekta ya elimu ikizidi kwenda mrama baada ya Serikali ya matukio kudandia hoja ya elimu bure bila kuwa na maandalizi ya kutosha na ya kuweza kutekeleza ajenda hiyo.

Hali katika shule za umma imekuwa mbaya sana kutokana na Serikali kushindwa kupeleka fedha za uendeshaji kwenye shule hizo na hivyo kufanya suala zima la elimu ya msingi na sekondari kuwa katika hali mbaya na huenda baada ya muda mfupi ujao shule hizi zinaweza kuanguka kutokana na kukosekana kwa fedha za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kwenye maandiko ya Mpango Serikali inajitapa kwamba itaendelea kutoa ruzuku ya uendeshaji (*capitation*) ya shilingi 1,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi, ya awali ama shule maalum na shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa sekondari wa kutwa na bwani; ukweli ni kwamba fedha inayotengwa kwa wastani huwa ni shilingi 1,000 kwa shule za msingi na shilingi 7,000/= kwa shule za sekondari, huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Septemba 2016, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kugharimia elimu bure kiasi cha shilingi bilioni 18.7 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 15.7 kinatakiwa kupelekwa Halmashauri na shilingi bilioni tatu zinatakiwa kupelekwa NECTA kwa ajili ya fidia ya mitihani. Kwa mujibu wa tovuti kuu ya takwimu huria ya Serikali, takwimu za mwezi Machi, 2016 zinaonesha kuwa Serikali ina jumla ya shule za msingi 16,084 zenye jumla ya wanafunzi milioni 8.3 kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi za idadi ya wanafunzi, maana yake ni kuwa Serikali imetenga kiasi cha shilingi 1,800 kwa mwezi kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi. Sasa fikiria shilingi 1,800 kwa mwezi, sijui inakuwaje. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Serikali ambayo mgombea wake wa Urais wakati akiomba kura aliwaahidi Watanzania kwamba hakuna mwanafunzi atakayekosa mkopo wa elimu ya juu, huku akiwashangaa watangulizi wake kwa kushindwa kulitafutia ufumbuzi na kudai eti yeye ndio mwarobaini wa tatizo, ikiwanyima mkopo wanafunzi 27,053 katika vyuo vikuu mbalimbali nchini kwa mwaka huu wa masomo huku wanafunzi waliopata mikopo wakiwa 20,183 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Watanzania wanaisoma namba! Tuliposema tuanze kuujenga UKUTA kuzuia udhalimu unaoendelea katika nchi yetu, kuna ambao hawakutuelewa. Mkono wa chuma unagusa mmoja baada ya mwingine, ninaamini tutaelewana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Serikali ya CCM ikijitapa kutumbua majipu iliyoyatengeneza yenyewe kwa mbwembwe nyingi; kumbe nyuma ya pazia Serikali hiyo hiyo inayalipa majipu hayo mishahara pamoja na marupurupu mengine kama kawaida. Mwezi Septemba kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kilitengwa kwa ajili ya kuwalipa viongozi ambao walitumbuliwa kikiwemo kiasi cha shilingi milioni 196 kama posho ya usumbufu. Mimi natoka Manispaa ya Kinondoni, tunalipa Wakurugenzi wawili. Kwa hiyo, muache mbwembwe wakati kwenye uhalisia hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano yaanza na mdororo wa uchumi; sindano hizo, vumilieni. Ni bahati mbaya kwamba Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yanaletwa mbele ya Bunge hili kujadiliwa na kupitishwa wakati ambapo hali ya uchumi wa nchi yetu ikiwa imeporomoka vibaya ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tu tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani. Kwa mujibu wa Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Tanzania iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania Septemba, 2016, imeonesha kuwa hali ya uchumi wa Taifa inaenda mwendo wa kusuasua karibu katika sekta zote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo inaonesha kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2016, ukuaji wa Pato la Taifa unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 5.7 kipindi kama hicho mwaka 2015. Kuporomoka huku hakujawahi kufikiwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwani takwimu zinaonesha kuwa katika robo ya kwanza tangu mwaka 2011, ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa kama inavyoonekana kwenye mabano, 2011 (7.9%); 2012 (7.1%); 2013 (6.3%); 2014 (8.3%) na 2015 (5.7%). Taarifa hiyo inaonesha kuyumba kwa uchumi katika sekta zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo itolewayo na mabanki ya biashara kwenye sekta binafsi, imeendelea kushuka katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016 na kuwa shilingi trilioni 1.1 ama shilingi bilioni 1,167.2 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 1,577.5 la mwaka 2015 katika kipindi kama hicho. Hii maana yake ni kuwa sekta binafsi imenyang'anywa au imekosa takribani bilioni 410 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016. Hali hii imepelekea mzunguko wa sarafu na noti mikononi mwa wananchi kushuka kutoka 18% mwezi Disemba, 2015 hadi kufikia 6.7% mwezi Julai, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amana za wateja katika mabanki zilipungua kutoka shilingi trilioni 20.5 mwezi Disemba 2015 hadi 20.2 mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miezi sita ya kwanza ya mwaka 2016, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje ilipungua kwa asilimia 61.7 na kufikia nakisi ya dola za Kimarekani milioni 970

kutoka nakisi ya dola za Kimarekani milioni 2,532. Hali kadhalika Deni la Taifa limeendelea kuongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Benki Kuu ya Tanzania inatoa takwimu hizi za kiuchumi zinazoonesha kuwa uchumi unasuasua, Serikali kupitia TRA imekuwa ikijigamba kwamba makusanyo ya mapato yameongezeka na kwamba uchumi uko imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti mdogo wa kiuchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba mapato ambayo TRA inasema yameongezeka ni hewa; hii ni kwa sababu bandari ambayo ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya mapato ya Serikali imekumbwa na mtikisiko mkubwa kutokana na mizigo iliyokuwa inaingia kupitia bandari hiyo kushuka kutoka tani 25,000 kwa siku hadi tani 5,000 kwa mujibu wa taarifa za Kamati ya Viwanda na Biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoipa kiburi TRA na kujigamba kwamba mapato yameongezeka ni ujanja wa kuwalazimisha wafanyabiashara na kulipa kodi ya mbele, kabla ya muda wa kulipa kodi hiyo kufika. Imebainika kwamba kama mlipa kodi analipa kodi ya mwezi, sasa TRA inamshawishi kulipa kodi hiyo kwa miezi sita au mwaka bila kujali *stability* ya mapato ya mlipa kodi huyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno rahisi ni kwamba sasa Serikali inakopa kodi ya wananchi. Kwa hiyo, inaonekana kuwa makusanyo ni mengi lakini kimsingi ni makusanyo ya miaka ama miezi ya mbele na siyo mwaka huu wa fedha. Kwa hali hii, sina hakika hiyo miaka ya mbele tutakuwa na makusanyo gani na sijui tutakuwa na akiba kiasi gani kuweza kuendesha nchi ama itakuwa ujanja ujanja wetu wa kuongeza kodi na kuumiza wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalowafanya TRA wafikiri mapato yameongezeka ni kitendo cha kukusanya maduhuli, yaani mapato yasiyokuwa ya kodi ya Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali na kuyaingiza moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali yaani Hazina, tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo mamlaka husika zilikuwa zinakusanya zenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwa wazi na kuwaambia wananchi ukweli kuliko kuwadanganya kuwa mapato yameongezeka wakati hali ya maisha inazidi kuwa ngumu. Aidha, Serikali izingatie demokrasia na utawala wa sheria. Hii misuli ya Serikali ya kutoa matamko kila kukicha na kukandamiza shughuli za kikatiba za kisiasa za Vyama vya Upinzani vinawatisha wawekezaji wakubwa na hivyo kuwafanya wazuie

mitaji yao kuingia kwenye mzunguko kwa hofu kwamba pengine kutatokea machafuko ya kisiasa halafu wakapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuporomoka kwa shehena ya *transit* katika Bandari ya Dar es Salaam. Hakuna mashaka tena kwamba shehena ya mizigo bandarini imepungua sana, hivyo kuathiri mapato ya Serikali. Majibu ya Serikali katika hoja hii ni kwamba wafanyabiashara wakwepa kodi wamekimbia bandarini kutokana na kubanwa na Serikali na hoja nyingine kwamba mizigo ya *transit* imekuwa haivuki mipakani na hivyo kubakishwa hapa hapa nchini kwa matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu tajwa hapo juu zina ukweli wake, lakini kwa kiwango fulani, siyo kwa asilimia mia moja. Kuna sababu nyingine ambazo zinalalamikiwa kama chimbuko kwa bandari yetu kukimbiwa; na kama hatua zisipochukuliwa na tukiendelea kujidanganya, athari itakuwa kubwa sana. Sababu zinazotajwa na wadau wakuu wa Bandari ni pamoja na zifuatazo:-

Mosi, uanzishwaji wa himaya ya forodha kati Tanzania na DRC; hii ina maana shehena yote ya DRC ushuru ukusanywe wakati shehena hiyo ikiwa Bandari ya Dar es Salaam. Baadhi ya wafanyabiashara wanaona kitendo cha ushuru kukusanywa huku wanaweza kupata hasara mara mbili kwa sababu watakuwa wamelipa kodi, lakini vilevile kuna uwezekano mkubwa mizigo isifike huko inakoenda.

Pili, uanzishaji wa Sheria ya Kutoza VAT katika huduma ya shehena ya *transit* inayopita katika bandari na mipaka ya Tanzania, kuna ongezeko la asilimia 18, kinyume kabisa na Mkataba wa Vienna (*Program of Action for Landlocked Developing Countries for the Decade 2014 – 2024*) ambapo Tanzania ni *signatory*.

Tatu, tozo za *storage* na *customs warehousing rent*, hiki ni kitu kimoja lakini wameweka majina mawili tofauti ilimradi mtu alipe mara mbili bila sababu ya msingi.

Nne, Taasisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa shehena za kikemikali inatoza tozo kubwa kuliko nchi nyingine. Tanzania inatoza dola moja hadi mbili za Kimarekani kwa kila tani moja ya shehena kulingana na aina ya kemikali. Kama kuna shehena ya tani 30,000 ina maana italipiwa zaidi ya dola 30,000 za Kimarekani. Nchi nyingine kama Afrika Kusini wanatoza kwa kila *bill of lading* dola 100 tu.

Tano, muda mdogo wa bidhaa ya mafuta kukaa bandarini (*wet cargo*). *South Africa* inatoa siku 180, *Msumbiji* inatoa siku 90, Tanzania inatoa siku 30. Siku 30 kiutendaji kwa vyovyote vile hazitoshi kusafirisha mzigo.

Sita, ongezeko la gharama za vibali vya usafirishaji kwenda nchi jirani kwa malori ya Tanzania; *TRA* imepandisha toka dola za Kimarekani 12 mpaka dola za Kimarekani 200 kwa kila lori. Hii ina maana kama mtu ana lori 100 atatakiwa alipe dola 20,000 kwa kibali tu, ni sawa sawa na shilingi milioni 44. Saba, kila *container* moja la futi 40 lina ongezeko la gharama ya dola za Kimarekani 180.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwenendo huu ni wazi kwamba wafanyabiashara wengi wataikimbia bandari yetu. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu mikakati ambayo inafanya kulipatia ufumbuzi jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa za Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti wa mwaka 2017/2018 iliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, Deni la Taifa likijumuisha deni la ndani na la nje lilifikia dola za Kimarekani milioni 18, sawa na shilingi trilioni 40, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9.8 kufikia Juni, 2016, ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 16, sawa na shilingi trilioni 37 katika kipindi kama hicho mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo deni hili litajumuishwa na madai ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yanayokadiriwa kufikia trilioni tatu na deni la nje la sekta binafsi ambalo linakadiriwa kufikia dola za Kimarekani trilioni mbili, jumla ya Deni la Taifa litakuwa dola za Kimarekani milioni 23, sawa na shilingi trilioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni hili la sugu na linazidi kukua kutokana na ukweli kwamba kile kinachoitwa kulipwa kwa Deni la Taifa, siyo kulipa kwa lengo la kupunguza deni, bali ni kupunguza makali ya kudaiwa kwa kulipia gharama za kusogeza mbele deni. Ukweli huu unadhihirika na maandiko ya Serikali inayoonesha kwamba kwa mwaka 2015/2016 malipo ya Deni la Taifa yalifikia shilingi trilioni 4.9 ambapo malipo ya shilingi trilioni nne yalikuwa malipo ya deni la ndani na shilingi bilioni 980 yalikuwa ni malipo ya deni la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za kulipa deni la ndani yaani shilingi trilioni nne kamili zinazodaiwa kulipwa, shilingi trilioni tatu zilikuwa ni kwa ajili ya kuahirisha deni lililoiva na shilingi trilioni moja ilikuwa ni kulipa riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida kwa Serikali kubadilisha takwimu za uhimilivu wa Deni la Taifa ili kujipa uhalali wa kuendelea kukopa. Ikumbukwe kwamba wakati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete anaingia madarakani mwaka 2005, Deni la Taifa lilikuwa shilingi trilioni saba; miaka 11

baadaye chini ya utawala huu huu wa CCM, Deni la Taifa limeongezeka mpaka shilingi trilioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya marejeo ya kina ya Mpango wa Maendeleo ambayo inaonyesha juu ya tathmini ya uhimilivu wa Deni la Taifa iliyofanyika Septemba, 2015 ilionyesha kuwa deni hilo ni himilivu na kwamba viashiria vya deni vinaonesha kuwa thamani ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 20 kwa mwaka ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka mmoja baadaye, Serikali hiyo hiyo ya CCM kupitia Taarifa ya Mwongozo wa Kutayarisha Mpango wa Bajeti ya mwaka 2017/2018 iliyotolewa na Wizara ya Fedha ikizungumzia uhimilivu wa deni, imenukuu ripoti ileile ya tathmini ya mwezi Septemba, 2015 na kusema kwamba Deni la Taifa ni himilivu kwa kuwa thamani ya sasa ya Deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 36 kwa mwaka ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, ukomo ni upi hasa; ni asilimia 50 au ni asilimia 74? Ni nani anaweka ukomo wa kukopa? Ni sisi kama nchi ama ni Benki ya Dunia? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu ya Tanzania ya viwanda yageuka kiini macho. Kauli mbiu ya Tanzania na viwanda ndiyo iliyotawala sera za mgombea Urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2015. Kauli mbiu hiyo imechukuliwa kama ilivyo na kuwa kauli mbiu ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017 – 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa ujasiri kwa sababu katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mzunguko wa bajeti (Julai hadi Septemba), kati ya shilingi bilioni 40 zilizotengwa kwa ajili bajeti ya maendeleo, hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa viwanda. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Sekta ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2016 iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa robo ya kwanza yote ya mzunguko wa bajeti imeisha hakuna hata senti moja iliyotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya viwanda, Serikali hii inakuwa na ujasiri gani wa kutumia tathmini hiyo ya kushindwa katika Mapandekazo ya Mpango wa Maendeleo 2017/2018? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu iingie kama ilivyo na ijibiwe kwa ufasaha. Porojo tumeshazichoka sasa. Ahsante sana. (Makofi)

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2017/18 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Inatolewa chini ya Kanuni ya 94(5) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote afya na uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa tano wa Bunge tukiwa salama. Aidha, nawapongeza viongozi viongozi wakuu wa CHADEMA na UKAWA kwa jumla kwa kazi kubwa wanayofanya ya kutetea na kulinda misingi ya demokrasia hapa nchini ambayo kwa sasa ipo katika majaribu makubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapandelezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 uliopo mezani; napenda niweke rekodi sawa kuhusu uwasilishwaji wa Mpango. “Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Katiba, Sheria na hata Kanuni za Bunge katika uwasilishaji wa Mapandelezo ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa utekelezaji hafifu wa Mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, wakati Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaelekeza kwamba Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango katika mkutano wake wa mwezi Oktoba – Novemba kila mwaka ili kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapandelezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata; kifungu cha 21(2) cha Sheria ya bajeti ya mwaka 2015 kinaelekeza kwamba mapandelezo ya Mpango pamoja na makisio ya bajeti yatawasilishwa katika mkutano wa Bunge wa mwezi Februari kila mwaka au kama Bunge halipo kwenye mkutano katika mwezi wa februari basi katika wiki ya kwanza ya mkutano huo utakapoitishwa.

Mheshimiwa Spika, huu ni mgongano wa wazi kati ya Kanuni za Bunge na Sheria ya bajeti kuhusu uwasilishwaji wa Mpango na makisio ya bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata. Uzoefu unaonyesha kwamba pale kunapotokea mgongano kati ya kanuni na sheria; sheria ndio husimama, lakini kwa hapa Bungeni mambo yamekuwa tofauti kwa sababu sheria imewekwa kando na badala yake Kanuni za Bunge ndio zimesimama.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia makatawa ya kifungu cha 21(2) cha sheria ya bajeti, mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yalitakiwa yawasilishwe katika Bunge la Januari – Februari. Na mantiki ya sheria ya bajeti hapa;kwa mujibu wa kifungu cha 21(3) cha sheria hiyo, ni kutoa mwanya wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoendelea (current financial year)na makisio ya hali ya uchumi kwa mika mitatu ya fedha inayofuatia. Na ili tathmini hiyo iweze kutoa mwanga wa mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti basi angalau iwe ni tathmini ya robo ya pili au nusu ya kwanza ya mzunguko wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge, tathmini iliwasilishwa hapa ni tathmini ya robo ya kwanza ya mzunguko wa bajeti ambayo inaishia tarehe 30 Septemba. Robo ya pili inayoishia tarehe 30 Disemba, haijaguswa kabisa kutokana na ukweli kwamba hatujafika huko. Kutegemea tathmini ya robo ya kwanza ambayo utekelezaji wake ni chini ya robo kwa ajili ya kufanya makisio ya miaka mitatu mfululizo ni kutumia vibaya maudhui ya tathmini na faida zake katika kusaidia kufanya makisio ya bajeti za miaka mitatu inayofuata.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mgongano huo wa Kanuni za Bunge na Sheria ya bajeti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwako wewe Mheshimiwa Spika, kuiagiza Kamati ya Kanuni kufanya marekebisho ya Kanuni ya 94(1) ili izingatie matakwa ya kifungu cha 21 (2) cha Sheria ya bajeti ya 2015 kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge kwa manufaa ya wananchi.

2. UNGOZI MBOVU UNAVYOCHANGIA KUYUMBA KWA UCHUMI

Mheshimiwa Spika, licha ya mbwembwe nyingi za Serikali ya awamu ya Tano ,inayotokana na Chama kilichokaa madarakani toka mwaka 1961 **tumeshuhudia;**

- i) 'Serikali iliyotengeneza watumishi hewa' ikisitisha ajira kwa kigezo kuwa inafanya uhakiki wa watumishi wake ,jambo hili limepelekea kuyumba kwa uchumi kwa baadhi ya familia ambazo zina watu wenye sifa ya kuajiriwa katika sekta ya umma kama vile waalimu,manesi na madaktari. Kusimamishwa huku kwa ajira kumewafanya nguvu kazi iliyokuwa na uwezowa kuzalisha kuishi kama ombaomba !
- ii) Serikali hii ikiwaumiza sana wafanyabiashara wakubwa na wa kati kwa kukamata mali zao kama Rais alivyofanya kwa kukamata mali za mfanyibiashara kwa kitanzania Salim Baharesa ,sukari yake ilishikiliwa na serikali bila kutoa sababu zozote zile na Rais aliamua kuachia sukari hiyo bila kutoa sababu zozote za maana kwa umma. Hali iko hivyo kwa wafanyabiashara

wengi ambao akaunti zao Benki zimeshikiliwa na Serikali bila kuelezwa sababu, jambo linalopelekea kuporomoka kwa uchumi kwa kasi katika taifa letu.

Kambi rasmi inaunga mkono hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wale wote waliokuwa wanahusika kwa namna moja au nyingine kuhujumu uchumi, lakini tunapinga kwa nguvu zote kwa dola kutumia mamlaka yake kuonea au kunyanyasa wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao kwa kufuata sheria na taratibu za nchi!

- iii) Sekta ya kilimo imeathirika sana hasa kutokana na uamuzi wa Benki kuu kuzuia baadhi ya Benki kukopesha wakulima kama ilivyofanya kwa Maendeleo Benki kwa hoja kuwa kama wakiendelea kukopesha miradi ya kilimo hakuna uhakika wa mikopo hiyo kurejeshwa.
- iv) Sekta ya Hoteli na utalii iko ICU na hasa kutokana na uamuzi wa serikali kuanzisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye huduma zote za utalii jambo ambalo limepelekea kushuka kwa idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu na hivyo kufanya hoteli zilizokuwa zinafanya biashara ya utalii pamoja na makampuni yaliyolikuwa yakijihusisha na biashara ya utalii kwa ujumla.
- v) Serikali za mitaa zimeathirika sana kutokana na uamuzi wa serikali kuamua kukusanya kodi ya Majengo kupitia TRA badala ya Halimashauri ambazo awali zilikuwa zikifanya jukumu hilo, na hasa ikizingatiwa kuwa uamuzi huu ulifanyika baada ya bajeti za Halimashauri kupitishwa na TAMISEMI na kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato ya Halimashauri husika. Ni mwezi wa nne sasa toka uamuzi huu ufanywe na serikali na kuthibitishwa na Bunge TRA haijaweza kukusanya kodi husika! Halmashauri ziko katika ukata Mkubwa sababu ni moja ya vyanzo vinavyotegemewa kwa shughuli za Maendeleo!
- vi) sekta ya afya imekuwa ikizorota kwa kasi kubwa .Hivi karibuni tumeshuhudia ukosefu mkubwa wa madawa, chanjo na vifaa tiba katika Hospitali zetu mbalimbali hapa nchini.Hali hii imepelekea wananchi kupoteza maisha kutokana na kukosekana kwa dawa na kundi la watoto limeathirika sana kutokana na kukosekana kwa chanjo kwenye hospitali zetu. Huku tukishuhudia mgongano wa kauli kati ya waziri wa afya na Makamu wa Rais. Waziri akidai dawa ziko tele....huku boshi wake akisema hali ni mbaya!
- vii) Sekta ya elimu ikizidi kwenda mrama baada ya Serikali ya matukio kudandia hoja ya elimu bure bila kuwa na maadalizi ya kutosha na ya kuweza **kutekeleza** ajenda hiyo.Hali katika shule za umma imekuwa mbaya sana kutokana na serikali kushindwa kupeleka fedha za uendeshaji kwenye shule hizo na hivyo kufanya suala zima la elimu ya msingi na Sekondari kuwa katika hali mbaya na huenda baada ya muda mfupi ujao shule hizi zinaweza kuanguka kutokana na kukosekana kwa fedha za uendeshaji.

viii) Wakati kwenye maandiko ya mpango Serikali inajitapa kwamba itaendelea kutoa ruzuku ya uendeshaji (capitation) ya shilingi 10,000/= kwa kila Mwanafunzi kwa shule za Msingi /awali/maalum na shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa sekondari wa kutwa na bweni. Ukweli ni kwamba kwa kipindi kiasi kinachotolewa kwa wastan huwa ni shilingi 1000 kwa shule za msingi na shilingi 7,000/= kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2016, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kugharimia elimu bure kiasi cha shilingi **18,777,000,000** ambapo kiasi cha shilingi **15,714,000,000** kinatakiwa kupelekwa Halimashauri na shilingi **3,063,000,000** zinatakiwa kupelekwa NECTA kwa ajili ya fidia ya mitihani. Kwa mujibu wa tovuti kuu ya takwimu huria ya serikali (www.pendadata.go.tz) takwimu za mwezi machi 2016 zinaonyesha kuwa serikali ina jumla ya shule za msingi 16,084 zenye jumla ya wanafunzi **8,340,128** kwa nchi nzima.

Kwa takwimu hizi za idadi ya wanafunzi maana yake ni kuwa serikali inatenga kiasi cha shilingi **1,884/=** kwa mwezi kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi .

ix) Tumeshuhudia, serikali ambayo Mgombea wake wa Urais wakati akiomba kura aliwaahidi watanzania kwamba hakuna mwanafunzi atakayekosa mkopo wa elimu ya juu, huku akiwashangaa watangulizi wake kwa kushindwa kulitafutia ufumbuzi huku akidai yeye ndio mwarobaini wa tatizo, ikiwanyima mkopo wanafunzi **27,053!** katika vyuo vikuu mbalimbali nchini kwa mwaka huu wa masomo. Huku Wanafunzi waliopata Mikopo wakiwa **20,183 tu!!!!**. Hakika watanzania 'wanaisoma namba' Tuliposema tuanze kuujenga ukuta kuzuia udhalimu unaoendelea katika nchi yetu kuna ambao hawakutuelewa... Mkono wa chuma unagusa mmoja baada ya mwingine!

Aidha ikumbukwe kuwa, serikali inadaiwa na vyuo mbalimbali nchini kiasi cha **shilingi bilioni 60.798** ambazo ni fedha za ada za wanafunzi walizokopeshwa lakini serikali haikupeleka mkopo huo kwenye vyuo husika kwa mwaka wa masomo 2015/16. Jambo hili linahitaji kufuatiliwa kwa kina kwani likiachwa kama lilivyo litasababisha vyuo kushindwa kujiendesha kwani na kugharimia gharama nyingine za uendeshaji

x) Tumeshuhudia Serikali ya CCM ikijitapa kutumbua 'majipu' iliyoyatengeneza yenyewe kwa mbwembwe nyingi, kumbe nyuma ya pazia serikali hiyo hiyo inayalipa 'majipu hayo' mishahara pamoja na marupurupu mengine kama kawaida! Mwezi Septemba kiasi cha **shilingi 2,199,740,340** (bilioni 2.1) zilitengwa kwa ajili ya kuwalipa viongozi ambao "walitumbuliwa" kikiwemo kiasi cha **shilingi 196,842,000** kama posho ya usumbufu.

3. SERIKALI YA AWAMU YA TANO YAANZA NA MDORORO WA UCHUMI

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya kwamba mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/18 yanaletwa mbele ya Bunge hili kujadiliwa na kupitishwa wakati ambapo hali ya uchumi wa nchi yetu ikiwa imeporomoka vibaya ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tu tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani.

Kwa mujibu wa Taarifa Kuhusu Hali ya Uchumi wa Tanzania iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania Septemba, 2016 imeonyesha kuwa hali ya uchumi wa taifa inaenda mwendo wa kusuasua karibia katika sekta zote hapa nchini.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa Katika robo ya kwanza ya mwaka 2016, ukuaji wa Pato la Taifa unakadiriwa kukukua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 5.7 kipindi kama hicho mwaka 2015

Kuporomoka huku hakujawahi kufikiwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwani takwimu zinaonyesha kuwa katika robo ya kwanza tangu mwaka 2011 ukuaji wa pato la Taifa ulikuwa kama inavyoonekana kwenye mabano , 2011 (7.9), 2012 (7.1), 2013 (6.3), 2014 (8.2) na 2015 (5.7)

Kwa mujibu wa ripoti hiyo shughuli zilizochangia ukuaji huu wa uchumi kwa kiasi kikubwa ni pamoja na kilimo (asilimia 11.7), biashara (asilimia 10.6), uchukuzi (asilimia 10.1), sekta ya fedha (asilimia 10.1) na mawasiliano (asilimia 10.0). Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi katika robo ya kwanza ya mwaka 2016 ni sekta ya fedha (asilimia 13.5), mawasiliano (asilimia 13.4), na utawala wa umma (asilimia 10.2) pamoja na taarifa hiyo kuonyesha kuwa uchumi unaimarika lakini wakati huohuo taarifa hiyo imeonyesha kuyumba kwa uchumi katika sekta zifuatazo;

i. Mikopo itolewayo na mabanki ya biashara kwenye sekta binafsi, imeendelea kushuka katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016 na kuwa Shilingi **bilioni 1,167.2**, ikilinganishwa na ongezeko la Shilingi **bilioni 1,577.5** la mwaka 2015 katika kipindi kama hicho. Hii maana yake ni kuwasekta binafsi imenyanganywa au imekosa takribani shilingi **Bilioni 410.3** katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016. Hali hii imepelekea mzunguko wa sarafu na noti mikononi mwa watu kushuka kutoka asilimia 18.8 Disemba 2015 na kufikia asilimia 6.7 Mwezi Julai, 2016.

ii. Amana za wateja katika mabanki zilipungua kutoka shilingi trilioni 20.52 mwezi Desemba 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 20.24 mwezi June 2016.

iii. Katika miezi sita ya kwanza ya mwaka 2016, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*)

ilipungua kwa asilimia 61.7 na kufikia nakisi ya dola za Kimarekani milioni 970.4, kutoka nakisi ya dola za Kimarekani **milioni 2,532.5** mwaka 2015. Kupungua huko kulitokana zaidi na ongezeko la thamani ya bidhaa za viwandani, mapato yatokanayo na utalii na huduma za usafirishaji nje ya nchi, pamoja na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi hususan bidhaa za mitaji, na bidhaa za matumizi ya kawaida katika kipindi hiki

iv. Hadi mwezi June 2016, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Kimarekani milioni 3,870.3 ambazo zinatoshesha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 4 tu, hali ambayo hairidhishi hata kidogo kwa taifa ambalo halijatoka vitani nahii imeendelea kusababisha kushuka kwa dhamani ya shilingi nchini

v. Deni la Taifa limeendelea kuongezeka kwa kasi

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ya Benki Kuu inaendelea kuonyesha kwamba; **shughuli za uchumi zinazohusu wananchi masikini zimeshuka kutoka kasi ya ukuaji ya 10.20% katika robo ya mwisho ya mwaka 2015 mpaka 2.7% katika robo ya kwanza ya mwaka 2016**, ikiwa ni punguzo la 8% ndani ya kipindi kisichozidi miezi sita. Hii ina maanisha kwamba Wananchi wetu wanazidi kuzama kwenye dimbwi la umasikini na ufukara kwa kasi kubwa tangu awamu ya tano ya Serikali ya Chama Mapinduzi iingie madarakani/

Mheshimiwa Spika, wakati Benki Kuu ya Tanzania inatoa takwimu hizi za kiuchumi zinazoonesha kuwa uchumi unasuasua; Serikali kupitia TRA imekuwa ikijigamba kwamba makusanyo ya mapato yameongezeka na kwamba uchumi uko imara.

Mheshimiwa Spika, kwa utafiti mdogo wa kiuchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba; mapato ambayo TRA inasema yameongezeka ni hewa. Hii ni kwa sababu bandari ambayo ndio chanzo kikuu cha Mapato ya Serikali imekumbwa na mtikisiko mkubwa kutokana na mizigo inayoingia kupitia bandari hiyo kushuka kutoka tani hadi 25,000 kwa siku hadi tani chini ya 5,000 kwa siku. (- Rejea taarifa za TRA zinazoonyesha tozo mbali mbali kama ilivyoonyeshwa katika kurasa za mbele)

Mheshimiwa Spika, kinachoipa kiburi TRA na kujigamba kwamba mapato yameongezeka ni ujanja wa kuwalazimisha wafanyabiashara na walipa kodi wengine kulipa kodi ya mbele kabla ya muda wa kulipa kodi hiyo kufika. Imebainika kwamba kama mlipa kodi analipa kodi ya mwezi; sasa TRA inamshawishi kulipa kodi hiyo kwa miezi sita au mwaka bila kujali 'stability' ya mapato ya mlipa kodi huyo. Hali kadhali mlipa kodi anayetakiwa kulipa kodi yake kwa mwaka sasa analazimika kulipa kodi hiyo kwa miaka mitatu au mitano kwa mkupuo mmoja. Kwa maneno rahisi ni Kwamba sasa **Serikali**

inakopa kodi kwa wananchi. Hivyo inaonekana kuwa makusanyo ni mengi lakini kimsingi ni makusanyo ya miaka ya mbele, na sio ya mwaka huu wa fedha. Kwa hali hii sina hakika hiyo miaka ya mbele tutakuwa na makusanyo gani na sijui tutakuwa na akiba kiasi gani kuweza kuendesha nchi.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine linalowafanya TRA wafikiri mapato yameongezeka ni kitendo cha kukusanya maduhuli (mapato yasiyo ya kodi) na kuyaingiza moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Hazina) tofauti na ilivyokuwa hapo kabla.

Mheshimiwa Spika, Majigambo yote hayo ya Serikali na vyombo vyake vya ukusanyaji mapato kwamba mapato yameongezeka ni hila ya kuwahadaa wananchi ili Serikali hii ya awamu ya tano ipate uhalali kwa wananchi lakini kimsingi mapato yameshuka kwa kiwango kikubwa sana jambo ambalo pia limesababisha fedha kupotea katika mzunguko wake.

Mheshimiwa Spika, nyote ni mashahidi kwamba miezi michache iliyopita Rais alisema kwamba kuna watu wameficha fedha majumbani ndio maana fedha hazipo katika mzunguko. Aidha, Rais alitishia kuchapisha noti mpya ili hao walioficha fedha wapate hasara. Huo ni ushahidi kwamba hakuna fedha, na sababu yake kubwa ni kwamba hakuna mzunguko wa biashara na hivyo hakuna mapato. Sasa Serikali ituambie hayo mapato inayosema yameongezeka yametoka wapi ikiwa fedha imepotea kwenye mzunguko?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwa wazi na kuwaambia wananchi ukweli kuliko kuwadanganya kuwa mapato yameongezeka wakati hali ya maisha inazidi kuwa ngumu. Aidha, Serikali izingatie demokrasia na utawala wa sheria. Hii misuli ya Serikali ya kutoa matako kila kukicha na kukandamiza shughuli za kikatiba za kisiasa za vyama vya upinzani vinawatisha wawekezaji wakubwa na hivyo kuwafanya wazuie mitaji yao kuingia kwenye mzunguko kwa hofu kwamba pengine kutatokea machafuko ya kisiasa halafu wakapata hasara. Hivyo Rais, na vyombo vyake vya dola wajitazame upya mienendo yao katika kuendesha Serikali – yamkini mienendo hiyo ndiyo imepelekea anguko hili la uchumi wa nchi yetu.

4. KUPOROMOKA KWA SHEHENA YA TRANSIT KATIKA BANDARI YA DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Spika, hakuna mashaka tena kwamba shehena ya mizigo bandarini imepungua sana hivyo kuathiri mapato ya serikali. Majibu ya serikali katika hoja hii ni kwamba, wafanyabiashara wakwepa kodi wamekimbia bandarini hapo kutokana na kubanwa na serikali na hoja nyingine ni kwamba mizigo ya transiti imekuwa haivuki mipakani na hivyo kubakishwa hapa hapa nchini kwa matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Spika,sababu tajwa hapo juu zina ukweli wake kwa kiwango fulani,lakini sio sahihi kwa 100%. Kuna sababu nyingine ambazo zinalalamikiwa kama chimbuko kwa bandari yetu kukimbiwa, na kama hatua zisipochukuliwa na tukiendelea kujidanganya, athari itakuwa kubwa sana: Sababu zinazotajwa na wadau wakuu wa Bandari ni Pamoja na :

- 1) Uanzishwaji wa himaya ya forodha kati Tanzania na DRC. Ina maana shehena yote ya DRC ushuru ukusanywe wakati shehena hiyo ikiwa bhandari ya Dar es salaam. Baadhi ya wafanyabiashara wanaona wanaweza pata hasara iwapo mzigo hautaweza fika DRC.
- 2) Uanzishaji wa sheria ya kutoza VAT katika huduma ya shehena ya Transiti inayopita katika bhandari na mipaka ya Tanzania mfano. Wharphage, storage, customs rent, stevedoring ,transport shipping line delivery nk.....katika kila huduma ,kuna ongezeko la 18% kinyume kabisa na Mkataba wa Viena Program OECD Organisation for economic cooperation ambao Tanzania ni Signatory.Kwa mfano kwa tozo ya wharphage peke yake, wakati bandari ya Mombasa wanatoza dola 70 za kimarekani kwa makasha ya futi 20,bandari ya Dar es salaam tunatoza dola 240. Halikadhalika wakati Mombasa wanatoza dola 105 (Import Transit) kwa makasha ya futi 40, Dar es salaam tunatoza dola 420.¹
- 3) Tozo za storage na customs warehosung rent (Hiki ni kitu kimoja lakini wameweka majina mawili tofauti ilimradi mtu alipe bila sababu ya msingi.
5. Taasisi ya Mkemia Mkuu wa serikali kwa shehena za kikemikali inatoza tozo kubwa kuliko nchi zingine. Tanzania inatoza dola 1 hadi 2 za kimarekani kwa kila tani moja ya shehena kulingana na aina ya kemikali. Kama kuna shehena ya tani 30,000 ina maana italipiwa zaidi ya dola 30,000 za kimarekani. Nchi nyingine kama Afrika Kusini wanatoza kila Bill of Lading dola 100 tu.
6. Muda mdogo wa bidhaa ya mafuta kukaa bandarini (wet cargo). South Africa inatoa siku 180, Msumbiji inatoa siku 90 , Tanzania siku inatoa 30. Siku 30 kiutendaji, kwa vyovyote hazitoshi kusafirisha mzigo.
7. Ongezeko la gharama za vibali vya usafirishaji kwenda nchi Jirani kwa malori ya Tanzania. TRA imepandisha toka dola zakimarekani 12 mpaka dola 200 kwa kila lori.

¹ Taarifa ya Mwenendo wa Uingizaji wa Mizigo iendayo nchi jirani kupitia Bandari ya Dar es salaam . TRA Makao Makuu, Dar es salaam.

8. Kila container moja la futi 40,lina ongezeko la gharama ya dola za kimarekano 180.

Mheshimiwa Spika,kwa mwenendo huo ni wazi kwamba wafanyabiashara wengi wataikimbia bandari yetu. Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge hili mikakati ambayo inafanya kulipatia ufumbuzi jambo hilo.

5. DENI LA TAIFA

Mheshimiwa Spika,taarifa za Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/18 iliyotolewa na Wizara ya fedha na Mipango, Deni la Taifa likijumuisha deni la ndani na la nje) lilifikia dola za kimarekani milioni 18.614 (sawa na shilingi trillion 40.9) ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9.8 kufikia Juni, 2016; ikilinganishwa na dola za kimarekani milioni 16.9 (shilingi trillion 37.180) katika kipindi kama hicho mwaka 2015.**(ongezeka la shilingi trillion 3.72 katika kipindi cha mwaka 1)**

Mheshimiwa Spika, endapo deni hili litajumuishwa na madai ya mifuko ya hifadhi ya jamii (yanayokadiriwa kufikia trillion 3.2) na deni la nje la sekta binafsi la dola za kimarekani 2.829.3 (shilingi trillion 2.8) **jumla ya Deni la taifa litakuwa Dola za kimarekani milioni 23.093 katika kipindi hicho, sawa sawa na shilingi za kitanzania trillion 50.8.**

Mheshimiwa Spika, deni hili la sugu linazidi kukua kutokana na ukweli kwamba kile kinachoitwa kulipwa kwa deni la Taifa, sio kulipa kwa lengo la kupunguza deni,bali ni kupunguza makali ya kudaiwa kwa kulipia gharama za kusogeza mbele deni!Ukweli huu unadhihirika na maandiko ya serikali inayoonyesha kwamba kwa mwaka 2015/16, malipo ya deni la Taifa yalifikia shilingi **trillion 4.996!**ambapo malipo ya shilingi trillion 4.015 yalikuwa malipo ya deni la ndani na shilingi bilioni 980 yalikuwa ni malipo ya deni la nje.

Mheshimiwa Spika,kati ya fedha za deni la ndani (trillion 4.015) zinazodaiwa kulipwa, shilingi **trillion 3.006 zilikuwa ni kwa jili ya 'kuahirisha deni'** lililoiva na shilingi **trillion 1.009 ilikuwa ni malipo ya riba!**²

²Uk.15

6. UHIMILIVU WA DENI LA TAIFA

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa serikali kubadilisha takwimu za uhimilivu wa deni la Taifa ili kujipa uhalali wa kuendelea kukopa! Ikumbukwe kwamba wakati Mhe Jakaya Mrisho Kikwete anaingia madarakani kupitia CCM, mwaka 2005 deni la Taifa lilikuwa shilingi za kitanzania Trillion 7 tu... Miaka 11 baadae chini ya utawala huu huu wa CCM, deni la Taifa limeongezeka na kufikia shilingi trillion 50!!

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya ya marejeo ya kina ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano (Comprehensive Review Report for Tanzania Five years Development Plan 2011/12 -2015/16) uk. 15 juu ya³ tathmini ya uhimilivu wa deni la taifa (debt sustainability assessment) iliyofanyika septemba 2015 **ilionyesha kuwa deni hilo ni himilivu** na kwamba viashiria vya deni vinaonyesha kuwa thamani ya deni la nje kwa **pato la Taifa ni 20.9% kwa mwaka ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 50%.**

Mheshimiwa Spika, mwaka mmoja baadae, Serikali hiyo hiyo ya CCM kupitia Taarifa ya mwongozo wa kutayarisha mpango wa bajeti ya mwaka 2017/18 iliyotolewa na wizara ya fedha mwezi oktoba 2016, ikizungumzia uhimilivu wa Deni la imenukuu ripoti ile ile ya tathmini iliyofanyika mwezi septemba 2015 na kusema kwamba deni la taifa ni himilivu kwa kuwa thamani ya sasa ya deni la serikali kwa pato la Taifa ni 36.8 % kwa mwaka ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 74% !! Kambi ya rasmi ya upinzani inaitaka serikali ilieleze Bunge lako ni ukomo ni upi haswa? Asilimia 50% au 74% ? Na ni nana anaweka ukomo wa kukopa, ni sisi kama nchi au Benki ya dunia?

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukopaji wa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara unaonekana kuendelea, kwani taarifa zinaonyesha kwamba katika bajeti ya mwaka 2017/18 serikali inatarajia kukopa mikopo ya kibiashara licha ya kukiri katika maandiko yake kwamba kuongezeka kwa kasi kwa thamani ya deni dhidi ya Pato la Taifa tokea mwaka 2010 ni kielelezo cha uwezo mdogo wa kiuchumi wa kulipa.⁴

7. MATAKWA YA KIKATIBA KUHUSU MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Januari, 2016 Bunge hili limekaa kama Kamati ya Mipango, ili kukidhi matakwa ya ibara ya 63(3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

³Ministry of Finance and Planning, January, 2016

⁴Comprehensive Review Report for Tanzania Five year Development plan 2011/2012-15/16 pg. 15

Tanzania kwa kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, matakwa ya ibara ya 63(3) (c) ambayo Bunge hili linatakwia lifuate linapokaa kama Kamati ya Mipango ni Bunge kutekeleza madaraka yake, kwa kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ilipoleta mbele ya Bunge hili Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/17 – 2020/21, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliibua hoja ya kuitaka Serikali kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo kama ibara ya 63(3) (c) ya Katiba inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani iliibua hoja hii kwa nia njema ya kuisaidia Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kisheria wa utekelezaji wa Mpango huo kwa kudhibiti mianya yote inayoweza kukwamisha utekelezaji wa mpango huo ili Serikali ifikie malengo iliyokusudia kuyafikia katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa iliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya umuhimu wa kutekeleza matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango, ilitokana na ukweli kwamba; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2011/12 – 2015/16 ulishindwa kufikia malengo yake kwa takriban asilimia 50 kutokana na kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wake na hivyo kusababisha mambo kufanywa hovyohovyoy bila utaratibu.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana Serikali haikuona haja ya kuheshimu matakwa ya Katiba na kama desturi yake ikatumia vibaya wingi wa wabunge wa chama tawala kuupitisha Mpango ule bila kuitungia sheria ya utekelezaji. Ukiukaji huo wa Katiba ulifanyika pia wakati wa kupitisha mpango wa taifa wa maendeleo wa mwaka; kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya awamu ya tano imeanza vibaya mhuhula wake wa uongozi kwa kuivunja Katiba ya nchi. Iianza kwa kukanyaga uhuru na haki za msingi za wananchi za kutoa maoni yao, kupata habari, kukusanyika, kushiriki mikutano halali ya kisiasa, kutumia fedha za umma bila idhini ya Bunge na sasa imeanza kukwepa agizo la wazi kabisa la Katiba la kutunga sheria ya kusimamia mpango wowote utakaotekelezwa katika Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, hii si dalili nzuri hata kidogo kwa utawala huu wa awamu ya tano; na ni kiashiria cha kushindwa kwa Mpango wa Taifa wa Maendeleo unaopendekezwa kwa kuwa hakutakuwa na mwongozo wowote wa kisheria wa kusimamia utekelezaji wake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini inapuuza Katiba ya nchi kwa kukwepa kwa makusudi kuleta muswada wa sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo?

8. MISINGI YA KIBAJETI KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali umuhimu wa uwepo wa sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango, jambo jingine muhimu ni uwepo wa bajeti ya uhakika ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa tathmini ya Mpango wa kwanza wa Maendeleo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema kwamba; moja ya sifa kubwa ya Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) ilikuwa ni kuweka msingi wa kibajeti ulioitaka Serikali kutenga asilimia 35 ya Mapato yake ya ndani kwa ajili ya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo. Mpango huo ulisema hivi: nanukuu, **“kwa kuelewa kuwa wakati wote kutakuwa na miradi ya uwekezaji nje ya mpango, serikali, kuanzia sasa, itakuwa inatenga asilimia 35 ya makadirio ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo kila mwaka”** mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba Mpango huo haukutungiwa sheria ya utekelezaji kama Katiba ya nchi inavyoelekeza; Serikali ilijificha katika kichaka cha udhaifu huo; na matokeo yake kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango huo, Serikali haikuwahi hata mara moja kutenga asilimia 35 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuna wakati mwingine haikutenga hata senti moja. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2012/13 Serikali haikutenga fedha yoyote kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Serikali kugoma kutoa asilimia 35 ya mapato yake ya ndani kutekeleza miradi ya maendeleo, miradi mingi ya maendeleo haikukamilika hadi mwisho wa muda wa utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na aibu ambayo Serikali iliipata kwa miaka yote mitano ya utekelezaji wa Mpango huo kwa kushindwa kutekeleza utaratibu iliyojiwekea yenyewe wa kutenga asilimia 35 ya Mapato yake ya ndani kugharamia mpango wa Maendeleo; safari hii Serikali imefuta kabisa utaratibu huo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 –

2020/21) na kwa maana hiyo utaratibu huo hautakuwepo tena katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, tafsiri rahisi ya uamuzi wa Serikali hii ya CCM inayojinasibu kwa kauli ya hapa kazi tu kufuta msingi wa kibajeti wa kugharamia mpango wa maendeleo kila mwaka kwa kutenga asilimia 35 ya mapato yake ya ndani ni hofu ya kushindwa kutekeleza commitment hiyo kama ambavyo ilishindwa kufanya hivyo katika Mpango uliomaliza muda wake; lakini pia ni kukwepa kuwajibika au kuwajibishwa na Bunge kwa hofu hiyo hiyo ya kushindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17 – Mpango ambao unaendelea kutekezwa hivi sasa; Serikali ilisema kwamba ilitenga shilingi trilioni 11.82 sawa na asilimia 40 ya bajeti yote kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo; lakini ukisoma kitabu cha Matumizi ya Fedha za Maendeleo (Public Expenditure Estimates Development Votes) VOLUME IV, fedha zilizotengwa ni shilingi trilioni 10.511. Katika hali hiyo, ni lazima kuwe na sheria itakayoibana Serikali kutekeleza kile inachoahidi hasa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ambao unatumia fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 Serikali imesema pia kwamba itaendelea na dhana ya kutenga asilimia 40 ya Bajeti yake kugharamia Mpango; akini imekwepa kueleza ni kaisi gani katika hiyo asilimia 40 kitakuwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kiwango cha fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia Mpango kiwekwe bayana kwa sababu Maendeleo ya nchi yataipimwa kwa uwezo wa nchi yenyewe kugharamia miradi yake ya maendeleo kwa kutumia fedha zake za ndani na sio kwa kutumia fedha za nje.

9. BAJETI HEWA NA UTEKELEZAJI HEWA WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, wakati bajeti kuu ya serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 inawasilishwa hapa Bungeni, Kambi Rasmi ya Upinzani ilibaini mapungugu makubwa katika bajeti hiyo, na kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba bajeti hiyo ilikuwa ni **'bajeti hewa'** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa ushahidi wa kuthibitisha jambo hilo kwa kuonyesha jinsi ambavyo takwimu zilizoandikwa kwenye vitabu vya bajeti zilivyokuwa zikitofautiana kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, kitabu cha Mapato ya serikali katika mwaka wa fedha 2016/17 (Volume 1 'Financial Statements and Revenue estimates' for the year 1st July ,2016 to 30th June 2017) kilionyesha kuwa mapato yote ya serikali yaani mapato ya kodi , yasiyokuwa ya kodi ,mikopo na misaada ya kibajeti itakuwa jumla ya shilingi Trilioni 22.063.

Mheshimiwa Spika, wakati jumla ya makusanyo yote ya Serikali kwa mwaka 2016/17 ni trilioni 22.063; kitabu cha matumizi ya kawaida, (Volume II: Estimates of Public Expenditure Consolidated Fund Services for the year 1st July, 2016 to 30th June, 2017 na kitabu cha matumizi ya maendeleo Volume IV Public Expenditure Estimates Development Votes (part A) kama vilivyowasilishwa Bungeni, vinaonyesha kuwa matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge ni jumla ya shilingi Trilioni 23.847; kwa mchanganuo kwamba: Fedha za Matumizi ya Kawaida (Volume II) ni shilingi 13,336,042,030,510 wakati fedha za Miradi ya Maendeleo (Volume IV) ni shilingi 10,511,945,288,575.

Mheshimiwa Spika; kwa kifupi, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Serikali imepanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 22.063 ila imepanga kutumia shilingi trilioni 23.847, kiasi ambacho ni zaidi ya mapato yake kwa shilingi trilioni 1.783

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni kichekesho kitupu. Hii ni kwa sababu ukiosoma ukisoma sura ya bajeti iliyowasilishwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango utaona kwamba jumla ya makusanyo yote ni shilingi trilioni 29.539 na matumizi yote ni shilingi trilioni 29.539 lakini takwimu zilizoandikwa kwenye vitabu vya mapato na matumizi ni tofauti kama nilivyoonyesha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko huo wa takwimu za bajeti: kwamba Serikali itakusanya trilioni 29.5 na kutumia trilioni 29.5 lakini kwenye vitabu inaonekana itakusanya trilioni 22.063 na kutumia trilioni 23.8 ndio kunaifanya Kambi Rasmi ya Upinzani kuiita bajeti hiyo kuwa ni **'bajeti hewa'** na kwamba mkanganyiko huo ndio kiashiria cha kwanza kikubwa; kwamba bajeti hiyo haitekelezeki. Kutotekelezeka kwa bajeti tafsiri yake ni kutotekelezeka kwa miradi ya maendeleo na ndio kufeli kwenyewe kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Aidha, sababu nyingine inayoifanya bajeti hiyo kuwa hewa ni kwa na vyanzo hewa vya mapato. Kwa mfano, kuingiza malipo ya kiinua mgongo cha wabunge ambacho kinatakiwa kulipwa mwaka 2020 kwa mujibu wa sheria na kukifanya kuwa chanzo cha mapato katika mwaka huu wa fedha 2016/17, hakuna jina lingine la kukiicha chanzo hicho cha mapato isipokuwa ni **'chanzo hewa cha mapato'** kwa kuwa fedha hiyo itapatika mwaka 2020 wakati wabunge watakapolipwa kiinua mgongo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na vyanzo hewa vya mapato ambavyo vimepelekea kuwa na bajeti hewa, basi tutegemee pia kwamba utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo nao utakuwa hewa. Na kama tunatumia bajeti hewa kufanya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaofuata na makisio ya bajeti kwa miaka mitatu mfululizo inayofuata, kuna hatari kubwa ya kuishia kuwa na Mpango dhaifu na makisio hewa ya bajeti kwa miaka mitatu inayofuata.

10. MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA NA SEKTA YA KILIMO

Mheshimiwa Spika, sekta ya Kilimo ni miongoni mwa maeneo ambayo hayajawekewa mkazo kabisa na yamepuuzwa na serikali ya CCM. Sekta hii imekuwa ikidumaa siku hadi siku na katika hali ya kutia aibu hali ni mbaya kuliko hata ilivyokuwa wakati nchi inapata uhuru! Ni muhimu serikali ikaelewa kwamba bila kuwekeza katika kilimo, itakuwa ni ndoto wananchi wetu kutoka kwenye lindi la umasikini. Kama kilimo hakikaendelezwa ina maana kwamba inamaanisha kwamba maisha ya 75% ya watazania iko matatani! Ripoti zinaonyesha kwamba Shughuli za kiuchumi za kilimo zilikuwa kwa kasi ndogo ya asilimia 2.3 mwaka 2015 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2014. Licha ya kuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa kuchangia kwa asilimia 29.0 kwa mwaka 2015 zikifuatiwa na shughuli za ujenzi (13%), biashara na matengenezo (10.7%) na ulinzi na utawala 6.4%.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kwanza wa Maendeleo wa miaka mitano (2011-16)⁵ lengo lilikuwa kukuza shughuli za kilimo kwa wastani wa 6%, kiwango hiki kiliwekwa baada ya lile lengo la awali la 10% kuishia kwenye makaratasi. Kutokana na uwekezaji duni, kikaambulia kukua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 3.4 tu! Na Mapitio ya mwenendo wa uchumi 2016/17 yanaonyesha kwamba sekta hii muhimu imeporomoka mpaka kufikia 2.3%!

Mheshimiwa Spika, baada ya serikali kushindwa vibaya kwenye Kilimo, sasa imekuja na hoja ya serikali ya viwada. Ni muhimu ikaeleweka kwamba Maendeleo ya sekta moja inategemea ukuaji wa sekta nyingine. Viwanda sio mbadala (Substitutive) wa Kilimo, bali ni sekta mbili zinazotegemeana. Viwanda /Kilimo haviwezi kukua bila kukuza / kuboresha sekta hizi mbili kwa pamoja. Kama Kilimo kitachukuiwa kuwa ni 'moyo' wanachi, basi viwanda itakuwa ni 'ubongo'.

Mheshimiwa Spika, tusitegemee miujiza kama kwa miaka mitatu mfululizo kati ya kiasi cha shilingi 2,710 (shilingi trillion 2.7) kilichopangwa katika mpango kama kichocheo cha kufufua sekta hii muhimu, kiasi kilichopitishwa (approved budget) ni shilingi 371 bilioni (13.71%), na kiasi cha pesa kilichotolewa (actual budget released) ni shilingi bilioni 250.12 tu! sawa na 9.23% ya mahitaji yote.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Mpango, hauonyeshi dalili ya kulifanyia kazi hili! Uchumi unaonekana kukua kwa tarakimu, bila kuzalisha ajira nyingi wala kupunguza umasikini kutokana na ukweli kwamba Sekta zinazokuwa kwa kasi

⁵ibid

ni zile zinazotumia machine na mitambo. Sekta hizi haziajiri wafanyakazi wengi kama zile zinazotumia misuli mfano Kilimo, uvuvi na ufugaji. Sekta hii inatoa soko kwa sekta nyingine kama vile viwanda , fedha, usafirishaji na biashara. Pia hutoa malighafi kwa sekta nyingine kama viwanda na huingiza fedha nyingi za kigeni. Kwa ufupi ni sekta yenye muingiliano mkubwa na sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika,Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) akitoa utangulizi katika semina ya waheshimiwa wabunge kuhusu kuanzishwa kwa TADB alisema: *“ili Tanzania ifanikiwe katika kupunguza umasikini na kujenga uchumi wa viwanda , ni lazima ifanye mapinduzi kwenye sekta ya Kilimo”*. Ni ukweli unaouma kwamba viwanda haviwezi kuwepo bila malighafi.Bado uzalishaji kwa eneo ni mdogo,miundombinu kama barabara za vijijini,umwagiliaji na masoko ni duni, uwezo wa kupata fedha kutoka vyombo vya fedha ni mdogo,masoko ni shida ,halikadhalika uwezo wa kuongeza thamani kwa bidhaa za kilimo ni mdogo. Wakulima wadogo, kimsingi ndio wanalisha Taifa hili? Serikali imewekeza nini kwao ili kuwawezesha kuzalisha Zaidi na kuongeza kipato!!

Mheshimiwa Spika,zilianzishwa programu kadhaa kama vile TAFSID-Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan, SAGCOT- Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania ambazo lengo lilikuwa ni kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara kwa kuhusisha sekta binafsi jambo ambalo lingekuwa nguzo muhimu wa kuubadilisha uchumi wa Tanzania kutoka kutegemea kilimo na kuwa nchi ya viwanda. Mipango hii imebaki kwenye makaratasi...japo chama ni kile kile, kila Rais anayeingia,anakuja vipaumbele vyake kwa kadiri akili yake inavyomuongoza!

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ilianzishwa **Benki ya Maendeleo ya kilimo**.Benki hii ilianzishwa kwa lengo la kuiwezesha Tanzania kufikia mapinduzi ya kilimo. Uanzishwaji wa bank hii ilikuwa moja ya maazimio kumi ya KILIMO KWANZA yaliyofikiwa mwaka 2009 (Miaka 7 iliyopita). Na ilikuwa shughuli ya pili kwa umuhimu (Baada ya shughuli ya 1 ya “kuongeza bajeti ya Serikali kwa ajili ya Kilimo kwanza “)Kati ya shughuli 15 za nguzo ya pili ya Kilimo Kwanza ilidhamiriwa ilidhamiriwa TADP ianzishwe ikiwa na mtaji wa dola za kimarekani milioni 500 (kipindi kile shilling bilioni 800, sasa hivi Trilion 1.1)....Fedha hizo zingepatikana iwapo serikali ingetenda bilioni 100 kila mwaka Lengo likiwa ni kukopesha wakulima wadogo wadogo kwa masharti na riba nafuu!! Mpaka nasoma hotuba hii, benki hii muhimu ilipewa shilingi bilioni 60 tu mwezi April 2015. Na inasemekana kama hatua zisipochukuliwa haraka,kwa mgao huu itakapofika 2020 banki hii itashindwa kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mwendelezo wa mipango yetu kama nchi limekuwa ni tatizo kubwa sana, hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa maendeleo ya nchi na wananchi wake.

11. KAULI MBIU YA “TANZANIA YA VIWANDA’ YAGEUKA KIINI MACHO

Mheshimiwa Spika,Kauli mbiu ya ‘Tanzani ya Viwanda’ ndio iliyotawala sera za Mgombea Urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. Kauli mbiu hiyo imechukuliwa kama ilivyo na kuwa Kauli Mbiu ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa 2016/17 hadi 2020/21.

Mheshimiwa Spika,Kambi Rasmi ya Upinzani haikosoi kuweka viwanda kama kipaumbele cha Mpango kwa kuwa viwanda vitatoa ajira kwa watanzania walio wengi na hivyo kukuza pato la mtu mmoja mmoja (per capita income) ambalo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa ujumla. Jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inashangazwa nalo ni kwamba zile mbwembwe na mihemko ya kwenye kampeni za Urais kwamba Tanzania itakuwa ya viwanda zimeyeyuka na nchi sasa imekosa kabisa mwelekeo kuhusu uhuishaji wa sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa ujasiri kwa sababu katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biasharia kwa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mzunguko wa bajeti (Julai hadi Septemba, 2016), kati ya shilingi bilioni 40 zilizotengwa kwa ajili bajeti ya maendeleo, hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa viwanda. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Sekta ya Viwanda na Biasahara na Uwekezaji kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2016 iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara mwezi Oktoba, 2016.

Mheshimiwa Spika, Ikiwa robo ya kwanza yote ya mzunguko wa bajeti imeisha na hakuna hata senti moja iliyotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya viwanda, Serikali inakuwa na ujasiri gani wa kutumia tathmini hiyo ya kushindwa katika mapandekazo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/18?

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza hapo wali; sekta ya viwanda ikikuwa kwa viwango vinavyokusudiwa itapanua wigo wa ajira kwa vijana wa Tanzania. Hata hivyo, licha ya uhalisia huo, bado Serikali haijatilia mkazo miradi inayozalisha ajira kwa wingi. Kwa mfano taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango miradi itakayozingatiwa, ukiifanyia tathmini; ni mirandi ambayo siyo “labour intensive”, hivyo upatikanaji wa ajira bado utakuwa wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba Serikali ilikwisha ainisha maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya uzalishaji bidhaa kwa mauzo ya nje ya nchi, lakini hadi sasa maeneo hayo bado Serikali haijamaliza kuyalipia fidia toka kwa wamiliki. Na kwa yale ambayo tayari fidia imekamilika ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji bado haijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kituo kikubwa cha biashara cha KURASINI LOGISTIC CENTRE cha ubia kati ya Tanzania na China (EPZ), ambapo tumefanya ulipaji fidia mkubwa kwa kuhamisha watu toka eneo husika lakini katika vipaumbele haioneshi. Jambo hili linatuonesha kwamba mradi huo unapingana na dhana nzima ya Tanzania ya Viwanda kwani kuruhusu mradi huo kuendelea ni sawa na kusaini mkataba wa EPA kati ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, kufunguliwa kwa kituo hicho maana yake ni kwamba Tanzania itakuwa nchi ya wachuuzi wa bidhaa kutoka uchina na hivyo sisi kama nchi “industrialization” haitofanikiwa kwani kutokana na kiwango cha teknolojia walichonazo wachina katika uzalishaji viwandani hatutaweza kuzalisha bidhaa za kuweza kushindana na bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ya Viwanda haitapatikana kwa kauli mbiu za Viongozi bali itapatikana kwa sera madhubuti ambayo inaelekeza uwepo wa utawala bora katika sekta husika (rasilimali watu), mazingira wezeshi kwa uanzishaji wa viwanda pamoja na mgawo wa upendeleo wa rasilimali fedha kwa sekta husika. Aidha, kuandika nyaraka ni jambo moja na utekelezaji way yale yaliyomo kwenye nyaraka hizo ni jambo lingine. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda tujiulize ni kwa kiwango gani matakwa hayo yametokelezwa?

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Biashara; Taarifa ya Benki ya Dunia ya Mwelekeo wa Ufanyaji Biashara Tanzania kwa mwaka ujao 2017 inaonesha kuwa Tanzania imeboresha mazingira ya biashara kutoka nchi ya 139 hadi ya 132. Hata hivyo; yapo mazingira ambayo yanaifanya Tanzania kuendelea kuwa nyuma katika uwekaji wa mazingira wezeshi ya biashara hasa katika uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizotolewa katika taarifa hiyo ni mfumo wa kodi mgumu na usiotabirika ambapo wawekezaji ambao wanategemea kuja nchini wanashindwa kupima na kufanya tathmini yao kuhusu masuala yote ya kodi kabla ya kuleta mitaji yao nchini. Aidha, ufanyaji wa biashara nje ya mipaka yetu imetajwa kuwa ni changamoto ambayo inarudisha nyuma mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, imeonekana pia kuwa hakuna uhakika wa kuwalinda wawekezaji waliopo nchini. Changamoto hii si ya kupuuza kwa sababu toka serikali ya awamu ya tano iwepo madarakani, kwa kauli na matendo imeonesha kutowathamini wawekezaji waliopo nchini. Pamoja na changamoto ya baadhi ya mikataba katika sekta mbalimbali kuwa mibovu, ni ukweli pia kuwa ni serikali hii ya CCM ambayo ilishiriki kuingia kwenye mikataba hiyo na Rais wa sasa akiwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa miaka ishirini.

Mheshimiwa Spika, ni vema taratibu zikafuatwa katika kuboresha mifumo na si kauli za kubeza wawekezaji na kusema nchi ilikuwa na ufidia wakati Rais wa sasa hajashuka toka mbinguni kama malaika na kinyume chake alikuwa sehemu ya serikali hiyo. Kambi ya Upinzani kwa miaka mingi tumetoa maoni ya kuhakikisha kuwa mazingira ya biashara ni wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na wa nje wanafanya biashara zao na serikali inanufaika na uwepo wao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangaa kuona serikali hii ya hapa kazi ikijigamba kuwa inaipeleka nchi kuwa ya viwanda wakati biashara ya kimataifa imedorora na mfumo wa kodi umekuwa ni mgumu zaidi. Hii ni tofauti na nchi jirani ya Kenya ambayo ni miongoni mwa nchi kumi duniani zilizoboresha mazingira yake ya biashara.

12. NISHATI YA UMEME NA UCHUMI WA VIWANDA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mapendeko ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2017/18, sekta ya viwanda ndio kipaumbele cha Mpango kwa ajili ya kukuza uchumi wa viwanda. Hata hivyo, ukuaji wa sekta ya viwanda unategemea sana ukuaji wa sekta ya nishati – na hasa nishati ya umeme ili viweze kufanya kazi na kuzalisha kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutegemeana huku kati ya sekta ya viwanda na sekta ya nishati, Serikali hii ya awamu ya tano haikulipa uzito stahiki sula la nishati ya umeme katika ukuaji wa viwanda nchini. Sekta ya nishati imewekwa kama kipaumbele cha mwisho katika mapandokezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba; Kama Serikali ina nia thabiti ya kuhuisha viwanda katika nchi yetu; basi azma hiyo iende sambamba na uboreshaji wa miundo mbinu ya umeme ili kuwe na umeme wa uhakika wa kuweza kuendesha viwanda na kukidhi matumizi mengine ya wananchi. Kambi Rasmi inatoa angalizo hili kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia umeme wa mgawo kabla hata ya kufanya mapinduzi ya viwanda; sasa baada ya viwanda hivyo vinavyosemwa kujengwa na kuanza kufanya kazi hali itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na Donna Peng & Rahmatallah Poudineh wa Oxford Institute for Energy Studies ya mwaka 2016; juu ya Bei Endelevu ya Umeme Tanzania (*Sustainable Electricity Pricing for Tanzania*) ni kwamba upungufu wa umeme nchini unatokana na upotevu wa umeme unaotokea katika usafirishaji na usambaza wa umeme. Taarifa hiyo inaonyesha pia kwaamba upotevu mkubwa wa umeme unatokea kwenye usambazaji, ambapo na uchakavu wa miundombinu ya umeme, mipango ya

uzambazaji ya umeme isiozingatia mahitaji ya uwekezaji wa baadye ndiyo chanzo kikubwa cha upotevu huo.

Mheshimiwa Spika, kutoakana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza bayana katika mapendekezo ya Mpango wa maendeleo wa 2017/18 namna itakavyokabiliana na tatizo la upungufu wa umeme nchini ili kukidhi mahitaji ya nishati inayohitajika viwandani na kwa matumizi ya wananchi majumbani.

13. MISINGI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 yanaeleza kwamba katika kipindi cha 2017 – 2019/20 misingi ya mpango na bajeti ni pamoja na amani, usalama, utulivu na utangamano wa ndani na nchi jirani kuendelea kuimarishwa na kudumishwa.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kisiasa yaliyopo sasa hapa nchini ya Serikali kuzuia washindani wa kisiasa kufanyakazi za siasa ni ishara tosha kwamba mpango wa bajeti umejengwa kwenye msingi ambao tayari una ufa. Nchi hii ni ya watanzania wote na Katiba ya nchi inatambua uwepo wa siasa za ushindani. Siasa za ukosoaji na kukubali kukosolewa ndio msingi wa maendeleo. Hoja ya msingi ni kama wadau wa ndani hawaridhiki, je sifa za watu wa nje zinafaida gani?

Mheshimiwa Spika, tunu ya amani na utulivu, usalama na utangamano wa ndani vinajengwa juu ya msingi wa haki, uhuru na usawa miongoni mwa wananchi. Tunu hizo zinaimarishwa kunapokuwa na Serikali inayozingatia misingi ya kidemokrasia na utawala wa sheria katika kutekeleza majukumu yake. Inapotokea dola kutaka kuwa juu ya sheria na kuongoza kwa matamko ya mkuu wa Serikali, basi misingi hiyo ya kidemokrasia na utawala wa sheria inakuwa imevunjwa. Hali hiyo ni hatari kwa kuwa aliyenyimwa haki atakapoidia ataonekana kwamba ni mkorofi na kwa hiyo kutakuwa na hali ya uhasama kati ya vyombo vya dola na wananchi wanaodai haki.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka rekodi sawa kuhusu mambo yafuatavyo:

- i. Umma ndio wenye madaraka ya mwanzo na mwisho kuhusu hatima ya nchi yao na Serikali itapata uhalali na madaraka yake kutoka kwa wananchi. Na hili ni takwa la kikatiba.
- ii. Nguvu na Mamlaka ya Umma vitajenga na kudumisha Demokrasia kuendana na katiba.
- iii. Nguvu na Mamlaka ya Umma ndiyo msingi wa kuhoji na kuwajibisha uongozi uliochaguliwa kwa uhuru na kwa haki.

- iv. Nguvu na Mamlaka ya Umma ndiyo chombo cha kuwaamsha, kuwahasisha, na kuwaelimisha Watanzania waimiliki, waitawale, wailinde, waiendeshe na waiendeleze nchi kwa ubunifu ili wanufaika nayo.

Mheshimiwa Spika napenda kumaliza hotuba yangu kwa kusema kwamba ni aibu kubwa kwa Serikali kupanga mipango ambayo inashindwa kuitekeleza. Kupanga ni kuchangua, hivyo Serikali iwe inapanga mipango ambayo ni realistic na ilete miswada hapa bungeni ya kusimamia utekelezaji wa mipango hiyo vinginevyo hotuba zetu zitaendelea kuwa hivi hivi na hatuataifika ndoto ya taifa – ndoto ya kuondokana na umasikini na kuwa nchi ya watu wenye kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

Halima James Mdee (Mb)
**WAZIRI KIVULI NA MSEMaji MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

1 Novemba, 2016.

MWENYEKITI: Ahsante Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Katibu, tunaendelea.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa
Kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango
na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2017/2018**

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa tunaanza sasa uchangiaji. Tunaaza na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango kwa uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo. Nampongeza kwa kutuletea vipaumbele vilevile kama vilivyokuwa mwaka 2016/2017 kujenga msingi wa uchumi wa viwanda, kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na usimamizi wa utekelezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *commitment* ya kuendelea kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya nchi na hii inaonesha kielelezo cha uendelevu wa mpango yetu, kielelezo cha sera zinazotabirika na kielelezo cha mipango imara. Kwa hiyo, namshukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi alipoonyesha katika kitabu hiki cha mapendekezo mkakati wa ufuatiliaji na tathmini chini ya uratibu wa Tume ya Mipango ambao umewekwa vizuri sana. Napongeza lakini natoa rai kwamba yale mazuri ambayo yalikuwa yanatekelezwa na ule Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, yaingizwe katika huu Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ili kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti nimeshituka kidogo niliposoma tathmini ndogo iliyoko kwenye kitabu cha mapendekezo hasa kuhusu hali ya viwanda ya sasa (*status*). Tuna viwanda vikubwa 1,322, tuna viwanda vidogo 47,921, takwimu ni nzuri. Hata hivyo tatizo nimeliona kwenye viwanda vikubwa vya uzalishaji yaani *manufacturing industries* viko 998; lakini kati ya hivyo 998 asilimia 53 ya viwanda hivyo viko katika mikoa mitatu tu ya Dar es Salaam, Arusha na Kagera. Sasa hii mimi nimeona kwamba kwa kweli uwiano wa uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji nchini hauko vizuri. Naomba huko tuendako ili kusudi hii *status* iweze kubadilika, huko tuendako tuzingatia uwiano wa maendeleo ya nchi yetu kwa kuzingatia kwamba viwanda vya uzalishaji vinahitajika hata katika mikoa ambayo sasa hivi haina hivyo viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nije sasa kwenye miradi ya kipaumbele. Nimeisoma, ni mizuri na ninatoa maoni kidogo katika miradi ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa au *standard gauge* ni mradi muhimu sana. Juhudi ambazo zimeshaanza za kutafuta fedha kwa ajili ya mradi huu naomba zisilegezwe; zifuatiliwe kwa ukamilifu wake ili kusudi hii reli ijengwe kama ambavyo inaonekana katika mapendekezo. Umuhimu wake unaonekana kutokana na matokeo ya kiuchumi yatakayopatikana. Kwanza, ujenzi wa reli ya kati utashusha gharama za usafiri na usafirishaji ambazo ndizo kiini kikubwa cha kupanda gharama za maisha. Mfano, gharama za kusafirisha mbolea, gharama za kusafirisha mafuta ya *petrol* na *diesel* zitapungua kwa kiasi kikubwa na hivyo kupunguza bei ya *petrol*, bei ya *diesel* na bei ya pembejeo na hiyo itasababisha maisha yawe nafuu kwa wananchi. Kwa hiyo, mradi huo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji barabara za lami, viwanja vya ndege, tunahitaji kuboresha barabara za changarawe na hili niliwekee msisitizo kwenya maeneo yangu ya Jimbo. Barabara ya Tabora – Ipole – Mpanda ambayo sasa hivi inajengwa, mkazo uwekwe, barabara ile ikamilike kwa ajili ya

kunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Katavi. Barabara ya Ipole - Rungwa inaunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mbeya. Naomba katika kipindi hiki cha mwaka 2017/2018 ianze kujengwa; na barabara ya kutoka Chunya – Ifigi – Mkiwa, kipindi cha mwaka 2017/2018 barabara hii nayo ikamilike kwa sababu hapo kuna uchumi mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ni muhimu sana. Imetajwa miradi ya maji kwa ujumla jumla, sasa mimi nakwenda kwenye *specific* ili Mawaziri husika wa sekta husika wazingatie wakati watakapokuwa wanaweka maoteo ya bajeti rasmi kwa ajili ya kuingia kwenye rasimu ya mpango wenyewe, naomba sana mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ufike Sikonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *status* ya sasa hivi wametangaza kandarasi tatu. Kuna *lot* inatoka Solwa mpaka Nzega; kuna *lot* inatoka Nzega mpaka Igunga; na kuna *lot* inatoka Nzega mpaka Tabora Mjini. Ile *lot* ya kutoka Tabora Mjini mpaka Sikonge haijatangazwa. Naomba wakati wa bajeti utakapofika, Waziri wa Maji asimamie hilo ili *lot* ya kutoka Tabora Mjini mpaka Sikonge ionekane kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018; vinginevyo kwa kweli tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wa Sikonge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mapendekezo ya jumla kuhusu afya; lakini nilitegemea kuona mkakati wa kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata, unakuwa wazi katika huu mpango. Nimesoma maelezo, yako jumla jumla sana, naomba tuwe *specific*; zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata ni sera ya Serikali na ni sera ya nchi yetu. Kwa hiyo, naomba sana iwe *specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu mpango kwenye sekta ya kilimo. Sisi Sikonge hatuwezi kuzungumzia kilimo bila kuzungumzia tumbaku. *Status* ya sasa hivi kwa mwaka 2016/2017; hawa ndugu zetu makampuni yanayonunua tumbaku, yameshusha makisio kwa zaidi ya asilimia 50, maana yake nini? Maana yake ni kwamba kijiji ambacho kilikuwa na wakulima 300 wa Tumbaku mwaka huu hawataweza kulima wote 300, watalima labda wakulima 100. Ina maana wengine hata wakulima hawana pa kuuza.

Naomba sana Serikali kwanza kwa mwaka huu iwe macho kuhusu haya makampuni ili yafanyike marekebisho ya makusudi, lakini kwenye mpango wa 2017/2018 matatizo kama yaliyotokea mwaka huu naomba yasijitokeze kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mwongozo wa Uandaaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018, naunga mkono na ninaipongeza Serikali kwa kuendelea na vigezo vya asilimia 40 kwamba itumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo na asilimia 60 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa kweli huo ndiyo msingi ambao utaendeleza pale ambapo tumeanza mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono vigezo hivyo vikuu vya ugawaji wa rasilimali kwa sababu nchi yetu itaendelea kuweka uzito unaostahili kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vigezo vikuu vya OC, napendekeza viwe ni pamoja na idadi ya miradi ya maendeleo inayosimamiwa na taasisi husika ili miradi hiyo utekelezaji wake usimamiwe vizuri na ulingane na thamani ya fedha itakayotumika. Kama idadi ya miradi ya maendeleo haitakuwa miongoni vya vigezo vya kugawa OC, basi tutakuwa tunatekeleza miradi ambayo haisimamiwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile upo umuhimu wa kupitia upya vigezo vya kisékta ili kulingana na wakati uliopo ziandaliwe; maana yake hivi vigezo ambavyo viko kwenye hivi vitabu viliandaliwa kipindi kirefu sana, mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana vigezo hivyo vifanyiwe mapitio ili vilingane na wakati wa sasa. Mfano, ruzuku katika sekta ya maji kwa sasa inahitaji kigezo cha idadi ya watu tu wanaokaa vijijini, lakini kwa sasa hivi kuna wakazi wengi katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ambayo ndiyo imejitokeza hivi karibuni. Mimi naomba vigezo hivi vifanyiwe mapitio ili kusudi vilingane na mahitaji ya wakati wa sasa maana yake ni vya muda mrafu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni machache tu, ni hayo, nawapongeza sana Serikali, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana mchangiaji wetu. Kwa vile muda hauwezi kutosheleza kuendelea na wachangiaji wengine, naomba niwataje tu hawa ambao tutaanza nao jioni. Wa kwanza ni Mheshimiwa Jumanne Kishimba, mwingine ni Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Wilfred Lwakatara pamoja na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

Sasa Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kufikia hapa tumeweza kukamilisha shughuli zetu za asubuhi ya leo hadi mchana. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.52 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE -KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na wachangiaji wetu na tunaanza sasa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na baadaye Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ajiandae.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri, vilevile nitakuwa mkosa fadhila nikianza kuchangia Mpango bila kwanza kuishukuru Serikali kwa jitihada wanazoendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu; Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa; na Baraza la Mawaziri lote kwa jitihada wanazoendelea kuzifanya kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Kagera na janga la tetemeko la ardhi lililotupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wabunge wote kwa kuguswa na kwa mchango wenu mlioutoa katika kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Kagera. Pia niishukuru Serikali kwa jitihada za kidharura ambazo wanaendelea kuzifanya kuwasaidia wananchi wa Wilaya

ya Karagwe kwa janga la njaa lililotupata lililosababishwa na ukame wa muda mrefu ambao haujawahi kutokea katika historia ya Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali, nipende kuiomba Serikali ili kuwaondoa wananchi wa Karagwe kutoka kwenye utegemezi wa kuomba chakula Serikalini, Serikali ishirikiane na mimi na Waheshimiwa Madiwani kuhakikisha tunajenga mpango mkakati wa kati na wa muda mrefu wa kuwasaidia wananchi wa Karagwe kutoka kwenye utegemezi wa kuomba chakula, kwenda kwenye kujitegemea kama tulivyokuwa kabla ya kupata janga la njaa ambalo limesababishwa na ukame na ukame umesababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali ituletee chakula chenye bei ya ruzuku haraka iwezekanavyo ili wananchi wengi wa Karagwe waweze kupata chakula, hasa maharage na mahindi, Serikali ituletee mbegu za mazao yanayostahimili ukame, taarifa tumeshaiwasilisha kwenye Kamati ya Maafa ya Taifa. Naiomba Serikali iifanyie kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itusaidie kutatua migogoro ya ardhi, hasa migogoro mikubwa. Kuna mgogoro wa Kihanga ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja alipokelewa na halaiki kubwa ya wananchi wa Karagwe na akaiagiza Serikali ifanye haraka iwezekanavyo kuhakikisha zile hekta 2,000 ambazo wananchi wa Kihanga walihadiwa toka NARCO ziende kwa wanakijiji, lakini mpaka hivi sasa maelekezo haya hayajafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itusaidie, pori la akiba la Kimisi usimamizi wa kisheria umekuwa siyo usimamizi wa kisheria, umekuwa ni *double standard*, kuna mifugo mingi inatoka sehemu mbalimbali za nchi, kuna mifugo kutoka nchi za jirani iko Kimisi, lakini mimi na Waheshimiwa Madiwani tumekuwa tukiwaambia wananchi wetu wa Karagwe kwamba lazima watii utawala wa kisheria na ng'ombe wao wasiingie mle Kimisi, sasa kinachoendelea ni *double standards*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kama lile pori la akiba la Kimisi wameshindwa kulitumia kwa tija na kwa kufuata misingi ya sheria, basi lirudishwe kwa wananchi kupitia Halmashauri ili katika Baraza la Madiwani tukae na kupanga matumizi bora ya kutumia hili eneo kwa kuzingatia sasa hivi Karagwe tuna tatizo la ukame, tunahitaji ardhi ya ziada kwa ajili ya kulima na kufuga. Kwa hiyo, niombe sana Serikali, tengeni eneo la pori la akiba la Kimisi angalau wananchi wangu wa Karagwe wapate eneo la kulima na kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe Serikali itusaidie, tuna Kata sita ambazo zina maji ya kutosha, tuwasaidie wananchi wa Karagwe waende kwenye kilimo cha kujitegemea. Serikali ilete wataalam waangalie ni namna gani tunaweza tukafanya kilimo cha umwagiliaji katika Kata ya Bugene, Kanoni, Kamagambo, Boranyange, Nyakakika na Lugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie mapendekezo ya Mpango. Hapa kikubwa sana, hasa ni kuangalia katika vile vipaumbele vinne. Napenda kuishauri Serikali mwisho wa siku tutapimwa ni namna gani maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu vimefungamana. Sasa, katika hili bahati mbaya sana tumekuwa tukitumia GDP kama kigezo cha kuangalia uchumi wa nchi unakuaje, siyo Tanzania tu ni dunia nzima. Bahati mbaya sana, kupima GDP kama kigezo cha maendeleo siyo kipimo kizuri kwa sababu ukiangalia ukuaji wa uchumi kwa takwimu tu hali yake haifanani na hali ya mtaani. Matokeo yake, taarifa zinakuwa zina takwimu nzuri lakini hali ya maisha ya wananchi haibadiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali katika Mpango wa kuwa na uchumi wa kati ifikapo 2025, katika malengo ya kuwa na uchumi wa viwanda, nirudie kwa mara nyingine; tujikite kwenye shughuli ambazo zinawahusisha Watanzania wengi na si shughuli nyingine bali ni Sekta ya Kilimo na Mifugo, ujasiriamali mdogo na wa kati, pamoja na mnyororo wa mazao yaani *value chain* ya mazao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Serikali itajikita katika maeneo haya matatu, kilimo na mifugo, biashara ndogo na kati na *value chain* ya mazao, tutakuwa tumewagusa Watanzania wengi zaidi ya asilimia 70 na tutakuwa tunakwenda kwenye mwelekeo mzuri wa kufikia uchumi wenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, lakini tukiendelea kusaidia zile sekta ambazo *multiply effect* yake ni ndogo, kusema ukweli inaweza kufika 2025 bado tukawa tunaulizana maswali magumu humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuisitiza sana, kwenye upande wa *value chain* ya mazao lazima tuangalie ni namna gani tunawasaidia wananchi wa Tanzania kutoka pale walipo hata kama ni hatua ndogondogo lakini ni hatua ambazo zinamsaidia kila Mtanzania kukuza kipato chake popote alipo katika shughuli hizi ambazo anajishughulisha nazo. Baada ya ku-focus katika hivi vipaumbele vitahakikisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu vinafungamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hili lazima tuweke mazingira wezeshi, mikopo ya bei nafuu katika hizi sekta ambazo nimezitaja. Kwa mfano; tuna Benki ya Maendeleo ya Kilimo; mpaka hivi sasa ina bilioni 60 tu. Ukiangalia kwa vitendo kama kweli tunataka kusaidia kilimo na mifugo kwa kuwapatia

wananchi wetu mikopo ya bei nafuu, lazima tuiwezeshe Benki ya Maendeleo ya Kilimo ipate mtaji wa kutosha iwasaidie wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna VICOBA Vijijini na Mjini kuna SACCOS, tuzisaidie zipate mitaji ya bei nafuu ili ziweze kukopesha vijana na akinamama vijijini na mjini ili waweze kutumia mitaji hii kufanya shughuli ambazo wanajishughulisha hata kama ni kidogo lakini *multiply effect* yake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatuwezi kupata maendeleo endelevu katika mpango wetu wa kuwa na uchumi wa kati kama hatuwekezi kwenye rasilimali watu. Niipongeze Wizara kwa kuliona hili katika mapendekezo ya mpango, lakini hii haitoshi. Kwa mfano, hivi sasa kuna wanafunzi wengi sana Vyuho Vikuu wanasubiri kupewa mikopo Serikalini, sasa tukifanya kwa vitendo kuonesha namna gani tunawekeza katika rasilimali watu tunatakiwa tuhakikishe katika Taasisi zetu za Vyuho Vikuu ili Taifa na *work force* ambayo tunaiandaa tunaiwezesha kupata mikopo ili waweze kusoma na tuweze kutumia hii *work force* kusaidia uchumi wetu na kusaidia kwenda kwenye malengo ya uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma taarifa ya ndugu zetu wa Upinzani. Niwapongeze, wana mapendekezo mazuri, lakini katika taarifa yao wamesahau ku-acknowledge kwamba Serikali yoyote makini kuna *transition period*. Toka Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikijipanga kuhakikisha inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama tulivyowaahidi wananchi na Watanzania wana imani sana na Serikali ya Awamu ya Tano, watupe muda tunajipanga, Serikali ni sikivu na naamini kabisa tutawavusha Watanzania kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Lwakatare ajiandae.

MHE. STANLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika huu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri na mipango mizuri niliyoiona katika maelezo yake na hotuba yake. Vilevile naipongeza Kamati husika nao wametoa mapendekezo mazuri tunawapa pongezi sana kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwamba Serikali inakwenda kuongeza kiwango cha Bajeti kutoka trilioni 29.5 kwenda kwenye trilioni 32.9. Nawapongeza sana kwa mawazo mazuri na mipango hii mizuri, kwa sababu hii ni ishara kwamba Serikali ya CCM imejipanga sawasawa kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi wake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu bure bila malipo, umeme vijijini, barabara za vijijini, maji safi na salama na huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi na changamoto nyingi ambazo zimeonekana katika Bajeti ambayo imepita, hivyo tunavyo-focus kwenda kwenye Bajeti hiyo kubwa ni lazima basi Serikali iwe na mikakati mizuri na mipango ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na vyanzo vizuri vya kuweza kupata pesa ili tuweze kukamilisha yale malengo tunayoyahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017, ambayo ndiyo tunaendelea nayo sasa hivi tuko katika *quarter* ya pili, kwa maana ya kwamba *quarter* ya kwanza tumeimaliza tunakwenda kwenye *quarter* ya pili leo ni tarehe moja ina maana tuna mwezi mmoja wa *quarter* ya pili. Tukitazama ni kwamba pesa za maendeleo zimekwenda kidogo sana, hii ni kwa sababu pengine kuna mikakati fulani haikukaa sawa, basi hili tunaomba lisijitokeze tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kwenye mwaka mpya wa fedha na tumeweka makadirio makubwa ya kiasi hicho cha shilingi 32.9 trilioni inabidi tujifunge kibwebwe kwelikweli kuhakikisha kwamba tunaongeza mapato ambayo yataweza kuwezesha bajeti hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuchangia kwenye masuala ya fedha. Pamoja na kwamba tunakwenda katika mkakati na mpango huu, kuna tatizo kubwa limejioneshwa katika taasisi mbalimbali za kifedha. Kulikuwa kuna tatizo la kupeleka pesa ambalo Mheshimiwa Mpango naye ni shahidi, ni kwamba waliamua kupeleka pesa kwenda *BOT* yaani *Central Bank* kutoka kwenye taasisi kubwa za kifedha, kwa mfano *NSSF* na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa mabwana walikuwa wanapeleka pesa kwenye hizi *commercial banks* mara ya kwanza, kwa mfano, *NSSF* walikuwa wanapeleka mabilioni mengi kwenye hizi *commercial banks* na kule *commercial banks* walikuwa wanalipa *interest* kwa maana ya kwamba walikuwa wanawalipa kila mwezi kiasi fulani cha fedha ambazo hawa *NSSF* walikuwa wanaweza na wao sasa kutumia pesa zile za *interest* kuweza kuwalipa wateja wao, kwa maana ya zile *benefits* wanapojiondoa kwenye mafao. Sasa unapoziondoa zile pesa kupeleka *Central Bank* ina maana kwamba ile biashara umeiondoa kwa hawa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kunakuwa na *impact* nyingine kwenye *commercial bank* kwa sababu wanakuwa wamekosa pesa, sasa hivi na wao nao wanakosa pesa ya kuwakopesha wateja wao. Unapowakosesha pesa ya kuwakopesha wateja wao yaani wafanyabiashara, hizo benki na zenyewe zinakufa kwa sababu zinashindwa kupata *interest* kutoka kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huu naomba Serikali itazame kwa macho mawili huu mpango, iweze kubadilisha, kurudisha zile pesa kwenye *commercial banks*. Unavyoziondoa ina maana kwamba hizi benki za kibiashara unaziua na kwamba zisiwe na uwezo tena wa kukopesha wateja wao. Hivyo basi tunaomba Serikali itazame upya, kwa sababu kwa kupeleka pesa kule ina maana kwamba benki isingekufa na Serikali ingeendelea kupata pesa pale inapohitaji pesa, lakini mnapopeleka *Central Bank* ina maana kwamba mnakwenda kuziweka kwenye *shelf* hizi pesa, zinakosa mzunguko, hakuna anayelipa *interest* na mwisho wa siku tunashindwa kupeleka pesa kwenye maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la bandari. Suala la bandari tunalipigia kelele kwenye mambo makubwa mawili tu. Jambo la kwanza ni VAT kwenye *auxiliary services on transit goods*. Sisi Tanzania tumesaini mkataba wa Vienna, tulisaini mkataba wa *World Trade Organisation (WTO)*, mteja anayepita Tanzania au raia wa nchi nyingine anayepita Tanzania anapopewa huduma au anaponunua kitu, unapokwenda nchi nyingine yoyote wewe kama ni mgeni ukinunua hata shati, unapotoka kama ulilipa VAT unarudishiwa! Kwa nini tunaweka VAT kwenye mizigo ya watu wanaokwenda nje? Kwa nini tunakwenda kinyume na mikataba? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukosa hivi ni kwamba tunaweka mazingira magumu, hawa wafanyabiashara wa Congo na sehemu zingine tunawa-charge hizi VAT, matokeo yake ile VAT inakwenda kwa wateja wao. Mwisho wa siku wanakwenda kwenye bandari zingine, wanaamua kwenda Mombasa, wanakwenda Beira kwa sababu kuna charge kubwa inayochajiwa katika Bandari yetu. Tunaomba hiyo VAT iondolewe. Tuliyaungumza kwenye mpango wa mwaka 2016/2017 na nalirudia leo katika huu Mpango wa 2017/2018, ondoeni! Tunazidiwa na bandari za majirani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine katika bandari tumezunguka tumeliona, kuna kitu kinaitwa *single customer territory*, huo mkataba ni tatizo. Tulioingia mkataba ni nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Congo haipo kwenye huu mkataba. Sisi tumesaini, tumewahi, tumeingia kwenye huu mkataba leo Wakongo wanachajiwa kodi kwenye bandari ya Dar es Salaam, risk ya mteja anapochajiwa mzigo wake Dar es Salaam, mfano mafuta amechajiwa Dar es Salaam, akatembea katikati gari likapata ajali, mafuta yakamwagika yule

mteja anapata hasara mara mbili kwa sababu anakuwa amenunua, hasara na amelipa kodi, hasara mara ya pili, tuna kiherehere gani cha kwenda kusaini hiyo mikataba? Matokeo yake hawa wateja wanahama wanakwenda Beira, wanakwenda Mombasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari iji-assess upya, Serikali iangalie bandari ina matatizo yapi na isitoshe bandari iwe na kitengo cha *marketing*, waweze kufanya *research* na kugundua ni nini tatizo limewafanya wateja wa Congo na sehemu zingine waondoke? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mawili yamefanya wale watu wanaofanya biashara ya *copper* badala ya ku-*export* mzigo katika bandari ya Dar es Salaam wana-*export* kupitia bandari ya Beira. Meli kubwa hawawezi wakaja Dar es Salaam kama hawana uhakika wa kushusha mzigo na kupakia mzigo. Hizi *shipping* zinataka uhakika wa kushusha mzigo na kupakia mzigo, wasipokuwa na uhakika wa kupakia mzigo wa ku-*export* maana yake ni kwamba wataleta mizigo mingine kwa gharama kubwa kufidia ile mizigo wanayoikosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ondoeni hizi sheria tuziangalie upya. Kwa kufanya hivi tumeondoa wafanyabiashara wakubwa. TATOA wana magari 26,000; magari asilimia 60 yamepaki ambayo ni magari 15,000 ina maana kuna madereva 15,000 wamesimama hawana kazi, utingo 15,000 wamesimama hawana kazi, vipuri hawauzi, wenye matairi hawauzi, ina maana wale wafanyabiashara wa mafuta hawauzi mafuta, mama ntilie anakosa biashara, mwenye *guest* anakosa biashara, mwenye *M-PESA* anakosa biashara. Maana yake tumedhibiti mapato ya milioni 600 halafu tukazuia *circulation* ya bilioni sita, *what are we doing?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kilimo na hasa kilimo cha pamba, kuna mpango wa C2C naomba uzingatiwe, tuna soko kubwa sana la nguo Afrika Mashariki, tuna nchi tano, Tanzania yenyewe tu ina watu karibu milioni 50 sasa, ukienda na nchi zingine tuna watu zaidi ya milioni 100, hawa watu wote wanavaa nguo kutoka China, wanavaa nguo kutoka India na sehemu zingine, Tanzania tuna uwezo wa kulima pamba ya kutosha, tuna uwezo wa kufungua viwanda vya nguo na hivi viwanda vya nguo vikaweza kuzalisha nguo za kutosha kuuza soko la *East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tusitegemee mtu binafsi atajenga kiwanda cha nguo. Kiwanda cha nguo ni jambo ambalo Serikali inatakiwa i-*intervene* iingie kwenye ku-*invest* kwenye viwanda vikubwa kwa kufanya *spinning*, kutengeneza vifungo, kutengeneza *ribbons*, kutengeneza vitu mbalimbali ambavyo vinaunda nguo, pawe na *industry* ya *textile* maalum kwa soko la Afrika Mashariki, tuende huko. Tukishafanya vile ina maana kwamba

tutakuwa na soko la uhakika na kuweza ku-export nguo zetu katika soko la *East Africa* na mkulima wa pamba, pamba yake itauzika na mkulima wa pamba atapata soko la uhakika kuliko sasa hivi mnavyotwendesha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa viwanda napenda kumalizia, kuna watu wanaitwa *TEMDO*. *TEMDO* wana teknolojia ya kutengeneza mitambo midogomidogo ambayo inaweza ikamsaidia mwananchi wa kawaida, tukawa na viwanda vidogovidogo hata vya ndani, mtu akawa na kiwanda kidogo cha kukamua alizeti, kiwanda kidogo cha kutengeneza soksi, kiwanda kidogo cha kutengeneza bidhaa ndogondogo ambazo ni *highly consumed* katika market yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kwamba, tukiwawezesha hawa ndiyo tutaweza kupata uchumi wa viwanda, lakini leo *TEMDO* hawapewi hela, leo tumekwenda kwenye *quarter* ya pili, *TEMDO* hata senti tano hawajapewa, wakati wanatakiwa wanunue vipuri, wanunue *spare* mbalimbali waweze kuvumbua zile teknolojia na kuwauzia watu wengine waweze kufyatua mashine mbalimbali ndogondogo kwa ajili ya viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuwabebe akinamama, tubebe vijana, tunataka kwenda kuwapa milioni 50 ya mitaji, lakini kama tutawapa mitaji kwa maana ya kuchuuza, kuchukua bidhaa moja iliyotengenezwa yaani *finished product* kwenda kwenye soko lingine kila mtu anafanya, tunataka twende kwenye uchumi wa uzalishaji, uchumi wa kila mtu aweze kuzalisha kuondoa *state* moja ya bidhaa ya kilimo, kwenda kwenye *new state*, haya ndiyo yanayoweza yakatuondoa, bila hivyo hatuwezi kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, tuangalie kodi hizi ndogondogo ambazo ni kero zimezungumzwa katika bajeti iliyopita, lakini bado kodi ndogondogo ni kero. Tumehesabu kodi zinazochajiwa ndogondogo ziko kodi zaidi ya 41 tumeziona ziko wazi, tuziondoe hizi kodi zinawafanya watu waweze kurudi nyuma, zinawafanya watu wasiweze kwenda mbele. Tunaomba hizi kodi ziangaliwe upya, tunapokwenda katika mkakati huu na mpango wa mwakani ina maana tuhakikishe kwamba tunaziondoa kodi ambazo ni kero, tunakwenda kwenye kodi chache zinazoweza kumwinua mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wananchi wa kawaida wapewe mikopo midogomidogo ili waweze kujinasua pale walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na baadaye Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Janet Mbene wajiandae.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami pia nitumie fursa hii kushukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wote, Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wabunge wa CHADEMA na UKAWA pia Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na pia Chama changu na hususan Mjumbe wa Kamati Kuu, Mheshimiwa Lowassa. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Abdallah Bulembo wa CCM, pia taasisi za ndani na nje ya nchi, makampuni mbalimbali, Mabalizi na watu binafsi ambao kwa kweli walitukimbilia katika Mkoa wetu wa Kagera kuweza kutoa misaada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Waziri Mkuu, pamoja na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge, Mwenyekiti wa NCCR pamoja na Mawaziri mbalimbali wa Wizara nyingi ambao walitukimbilia katika Mkoa wetu kwa ajili ya kuangalia kwa karibu lile janga lililotupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako na kupitia kwa Baraza la Mawaziri, Mawaziri waliopo hapa na hususan Waziri Mkuu niombe wamfikishie ujumbe Mheshimiwa Rais kwamba kutofika kwake katika Mkoa wetu na kuangalia majanga na kuhudhuria msiba ambao kimsingi unamhusu sana, niseme kabisa bado haijaingia akilini kwa wananchi wa Kagera. Wengi wanatoa tafsiri nyingi, nyingine huenda ni za kweli, nyingine huenda ni za uwongo, lakini ili kumaliza biashara hiyo na kuweza kuweka wigo vizuri, mimi binafsi nawasilisha kilio hicho cha wananchi wa Kagera, ni vema angefika. Kwa sababu kutofika kwake watu wengine wanafikiri yale majanga ni mepesi, kufika kwa Rais kutaweza kufunua macho watu wengine ambao wanataka kutusaidia sisi kama Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme majanga yale ya Mkoa wa Kagera yaliyotokea ya tetemeko, kama mtu hajafika kule hawezi kujua ukubwa wa tetemeko lile. Ndiyo maana katika mpango huu ninapozungumza hapa kwa niaba ya watu wa Bukoba Town na Mkoa wa Kagera kwa ujumla na hususan niliposoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba yatakayozingatiwa katika kukamilisha mpango na mwongozo ni pamoja na: nachukua kipengele cha kwanza: "Kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango na miradi ya maendeleo". Kipengele pia cha nne: "Kuchagua miradi michache ya kipaumbele kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huo mambo niliyojifunza katika janga la tetemeko la Kagera, ni kwamba kwa kweli mipango yetu haijajiandaa katika kukabiliana na majanga au maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia aibu kwamba majanga yanatokea kama lile tetemeko halafu Kitengo cha Maafa hakina hata senti tano, kinaanza kutegemea hela ya kuchangiwa na kutembeza kapu, matokeo yake shida haina mwenyewe, haingojei, ni kwamba watu wanatakiwa kupata msaada wa haraka hawapati. Kwa hiyo, ningepomba katika mpango huu nilichojifunza kwa tetemeko la Kagera ni kwamba Serikali ilikuwa haijajipanga na bado haijajipanga kwa sababu matatizo bado ni makubwa kweli. Tuone kwamba janga hili linaweza likatokea wakati wowote na kwa bahati mbaya kama nilivyowahi kueleza huko nyuma na Naibu Waziri wa Fedha akanijibu Mkoa wa Kagera majanga makubwa ya Kimataifa na ya Kitaifa yamekuwa yanaanzia kule, sasa funga kazi imekuja kwenye hili la tetemeko!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Naibu Waziri wa Fedha alikiri kwamba Kagera ina matatizo na ile kuwa maskini kati ya mikoa mitano kuna sababu za kihistoria na tumezijata hapa. Sasa kumeongezeka tetemeko, kwa hiyo hapa kwa kweli hebu jaribuni kusaidia na mpango uje mahsus kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri yeye alinihakikishia kwamba watatuweka kwenye *Big Result Now (BRN)*, *Big Result Now* ianze kuonekana kwenye mpango wa kutunusu hili janga la tetemeko. Kwa wataalam ambao wamefika pale na namshukuru Mheshimiwa Mbatia alisema kabisa ili kurudisha uchumi wa Kagera katika mstari wake baada ya janga la tetemeko kunahitajika si chini ya shilingi trilioni mbili, sasa shilingi trilioni mbili siyo hela ya mchezo bila kuiweka katika mpango mahsus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imeelezwa na wataalam kwamba lile janga litachukua zaidi ya miaka 10 kurudi kwenye mstari kama kweli Serikali itakuwa ina mpango mahsus. Naomba wakati anapo-*windup* au wakati unapopanga mipango ya kuelekea huko mbele, basi Mkoa wa Kagera uainishiwe kabisa hatua za makusudi ambazo zitachukuliwa ili kutunusu katika umaskini ule uliopita kwa sababu zilizotajwa na hili janga la tetemeko ambalo limetupata hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningepomba kuzungumza ni kwamba, lile tetemeko linahitaji mipango ya *short term*, *medium term* na *long term*. Sasa *short term* ni hii ambayo imeanza kufanyika ingawa nayo haichukuliwi hatua kwa umakini. Hata hivyo, nianzie kusema kwamba, kuna mambo mengine ambayo nimejifunza yanayoleta matatizo. Kuna matamko yanayokinzana ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali baada ya kuzidiwa na suala la kuwahudumia watu walitoa tamko kwamba michango mingi ambayo ilikuwa inakusanywa chini ya Kamati ya Maafa, walieleza kwamba ile michango itaelekezwa zaidi kukarabati na kurejesha miundombinu pamoja na kukarabati taasisi za umma na wakatoa tamko na *clip* ninazo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya Bukoba wakasema watu waanze kusaidiana wenyewe katika kukabiliana na tatizo hili, Serikali haitakuwa na uwezo, tukulipokea. Baada ya siku mbili nyumbani kwangu kulijaa watu wanamililia Mbunge, kwamba Mbunge wewe ndiyo mtu wa kwanza kutusaidia zile kura walizonipa zaidi ya 25, 000 si mchezo! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge kwa umakini wake akaweka mipango ya kuanza kuwasaidia watu wake nikaandika barua na naiweka kwenye *table* naomba ije ichukuliwe iwasilishwe, nikaandikia marafiki zangu na sehemu ya wale walionichagua wanisaidie; nashukuru baadhi yao walionisaidia licha ya wapiga kura hata Wabunge bila kujali vyama vyao, hata wa CCM wakaanza kunisaidia na kwa kuogopa hela mimi nisizishike mkononi nikawaelekeza wanunue vitu vinavyohitajika, maturubai ambayo Serikali ilishindwa kuwapa watu wananyeshewa mvua, wanapigwa na baridi, nikawaomba wawape watu wangu mablanketi, wawanunulie kwenye maduka, wanipe vifaa

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu nilichojifunza watendaji wenu mmewatia nidhamu ya woga, watu wana woga sijawahi kuona na nakala ya barua hiyo nikampelekea Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa, Mkuu wa Mkoa kwa kumweleza utaratibu wangu mimi kama Mbunge ambaye nimeapishwa hapa ndani ya Bunge, kwamba utaratibu wangu wa kuwasaidia watu ni huu, marafiki zangu wanataka kunisaidia, lakini nilishangaa barua hii ikawa ni kigezo eti napelekwa Polisi Lwakatare atafutwe eti ananzisha utaratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge ambaye nimeapishwa ndani ya jengo hili kwa Katiba, Rais ameapishwa pale uwanja wa Taifa wote kwa Katiba, hivi kama siwezi kuaminika na kukimbiliwa na wananchi wangu nani awakimbilie? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kinacholeta matatizo ni watendaji wenu mmewajaza woga, mnawatumbua bila utaratibu matokeo yake wanashindwa kusimamia hata kazi mnazowapa matokeo yake tunakimbizana huku na huko. Sasa na mipango hii tunayoipanga hapa tusipowaondolea watendaji wetu woga, mipango ya Mheshimiwa Waziri itapwaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuleta maombi maalum kwenye mipango ambayo itapangwa na hili naomba niliwasilishe kupitia hapa, kwanza niseme kabisa nimeombwa na wananchi wangu niliwasilishe hili la kwanza tunaomba sisi kama Kagera tupewe *tax holiday* kwa kipindi maalum (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni miaka mitano, miaka kumi kwamba bidhaa za ujenzi zipunguzwe bei. Hili jambo si la kwanza, tunakumbuka enzi za Mwalimu wakati tukianza kujenga Makao Makuu Dodoma uliwekwa utaratibu kuwashawishi wafanyabiashara waweze kuja kuwekeza Dodoma na cement

ikawa imepunguzwa bei, vifaa vya ujenzi vikapunguzwa bei ili watu wajenge. Katika hili ili kuweka utaratibu mzuri na watu wasichakachue viwanda vilielekezwa kuwekwa alama maalum, nembo maalum. Sasa wananchi wa Kagera tunajua Serikali haiwezi kutujengea sisi wote na janga ni kubwa, tunaomba iwekwe *tax holiday* kwa bidhaa za ujenzi ili wananchi wajijengee badala ya kubaki ombaomba, hili ni janga kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili wafanyabiashara wameniomba, kuna wafanyabiashara wanaidai Serikali zaidi ya bilioni moja, wamewakopa wametoa huduma mbalimbali za ku-supply hawajalipwa zaidi ya miaka minne. Hawa ndiyo matajiri wetu wa Mji wa Bukoba, ndiyo wenye majumba yaliyoanguka, hawakopesheki tena na kwa bahati mbaya nyumba wanasema haziwekewi bima kwa suala la tetemeko, kwa sababu ni *natural disaster*. Sasa wamenituma katika suala la kulipa kwenye majanga na wafanyabiashara hao muwaweke kwenye *package* ya kuwalipa ili hawa watu warudi kwenye reli, vinginevyo wamefilisika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu kuna watu walikopa kwa kutumia nyumba ambazo zimeteketea tunaomba Mheshimiwa Waziri katika mpango wake alitolee tamko kuzielekeza taasisi na mabenki yaliyokuwa yanawadai wananchi wa Bukoba na Kagera kwa ujumla waliopata janga, nyumba walizoweka kama *security* zimebomoka, zimeanguka wanafanyaje au mnataka wajinyonge? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la misaada inayotolewa, tunaomba misaada inayotolewa kama Serikali imeamua misaada yote kuweka kapuni, hili suala linajaribu kuwazuia na kuwa na walakini kwa wachangiaji wengine, pale mnapochanga kwa mgongo wa waathirika lakini kapu lote linaelekezwa kwenye kujenga taasisi za umma bila kwenda kuwasaidia waathirika wenyewe. Kama mmeamua kufanya hivyo basi watu wasiendeleo kujitoa na kuingia mitini kutuchangia tuweke makapu mawili wanaochangia Serikali na wale wanaotangaza kuchangia waathirika wachangie waathirika kuliko kuweka kapu moja vinginevyo watu wanaona mmetumia matetemeko kama chanzo cha mapato ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, tunaomba bajeti ya maafa ieleweke, katika mpango wa Mheshimiwa Waziri suala la maafa ajaribu kulitengea fedha zinazoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la sita, wananchi wa Kagera wamenituma na bahati nzuri hili suala nilishafika hata kwa Waziri Lukuvi, wanasema mwaka kesho pale Luguruni kuna makampuni mbalimbali toka duniani kote yanakuja kuonesha nyumba za bei nafuu na ambazo ni *earthquake proof*, nyumba ambazo hazizidi milioni nne mpaka milioni tano.

Tunaomba zoezi hili lianzie Kagera ambako nyumba zaidi ya 3000 zimekwisha, tunaomba nyumba hizi zije na iwekwe mipango mahsusi ambayo inaweza ikazi-*attract* hizi taasisi mbalimbali kuweza kuanzisha mpango huu ukaonekane Kagera ambako zaidi ya nyumba 4000 zote zimeteketea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya suala la mwisho kabisa, ni kuhusu suala la njaa, Mheshimiwa Bashungwa amezungumzia suala la njaa; Karagwe wanalima na Kyerwa, Muleba wanalima na mikoa mingine wanalima, wanaonunua ni watoto wa Bukoba Town bidhaa zote zinaingia mjini sisi ndio wanunuzi, sasa huko wote wamepigwa na njaa tutanunua nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bukoba kuna njaa na Mkoa mzima wa Kagera una njaa, ukame unatumaliza. Tunaomba Mheshimiwa Waziri katika mipango yake na Waziri wa Kilimo nilisikitika alikwenda Karagwe tu, lakini janga la njaa liko mkoa mzima, tunaomba mipango kabisa ipangwe kabla ya wananchi hawajateketea na bahati mbaya wananchi wa Bukoba Mjini huwaga hatupendi kulialia.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Khatib Said Haji na baadaye Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Josephat Kandege wajiandae.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kusimama hapa na pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajalia Wabunge wenzangu wote ambao tuko hapa, tupo katika hali ya afya njema na salama kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kabla ya kutoa mchango wangu wa mpango huu kuitakia heri Kamati ya Uongozi ya Chama cha CUF chini ya Jenerali Julius Mtatiro. Pili nimtakie kheri kipenzi cha Wazanzibari, Maalim Seif Sharrif Hamad nikimwambia zidisha uzi huo huo na kwa niaba ya Wabunge wa Chama cha Upinzani cha CUF, wote wako pamoja na wewe na Kamati ya Uongozi wa CUF na hawatayumba na hawatayumbishwa, wale wote wenye dhana kwamba CUF itakufa, watakufa wao kabla CUF haijafa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Stanslaus Nyongo aliongelea suala la mdororo wa mizigo katika bandari yetu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Nyongo ni Mjumbe mwenzangu tuko katika Kamati moja inayoongozwa na Mwenyekiti shupavu Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango kama huu mwaka uliopita mimi ni miongoni mwa waliosimama hapa kwa mdomo huu huu, kiti hiki hiki, kipaza sauti hiki hiki nikatahadharisha juu ya mpango wa Serikali kuingia kwenye mfumo mmoja wa himaya hii ambao utawafanya Wakongo walipie mizigo yao kabla ya kuondoka katika bandari ya Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitahadharisha kwa kujua kwamba, athari zake wafanyabiashara wa Congo wana mbinu zao ambazo hazihusishi nchi yetu na nikatahadharisha sana kwamba, tutahadhari na mpango ule tusijiingize katika jambo lile ambalo limekuwa ni *source* moja kubwa ya mdororo wa mizigo katika bandari ya Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri sana tulipopata bahati ya kwenda katika Bandari ya Dar-es-Salaam Kamati yetu kutembelea na kuona uhalisia wa mambo ulivyo na taarifa tulizopewa na Watendaji wa Bandari, tuliporudi na kuiambia Serikali ukweli wa tulichokiona, zilikuja tafsiri tofauti tofauti ambazo tulionekana sisi ni waongo na hatuna ukweli katika tunayoyaeleza, au tumetumwa au tunatumiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge yenye mchanganyiko wa Vyama vyote inakwenda kufanya kazi kwa ajili ya maslahi ya kuisaidia nchi hii, leo tunapoeleza ukweli, tunapokuwa tofauti na Watendaji wa Serikali ambao wanaogopa kumwambia Rais ukweli, huu ni ukweli! Wanaogopa kumwambia Mheshimiwa Magufuli ukweli uko hivi, wakadharau na wakasema waliyoyasema, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kitu cha ukweli kitaonekana tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Waziri wa Biashara na Viwanda, Mheshimiwa Charles Mwijage, akikutana na Taasisi ya Wafanyabiashara Wasafirishaji (TATO), kauli aliyosema ni ushahidi Watanzania nyote mmeisikia. Amekaa na wenye *ma-truck* anawaambia kwa muda waliofikia mizigo katika bandari yetu imepungua na sasa kinachofuata ni malori yenu mtafute *parking* myaweke na ikiwezekana wekeni vilainishi (*grease*), ili msubiri, hatujui ni mwaka huu au mwaka ujao. Nani mkweli na nani mwongo? Kamati kweli au Waziri mwongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mhukumuni kwa matendo yake, msimhukumu kwa dhana hafifu. Tuliyasema yale, leo Waziri amekuja kumthibitisha Rais kwa mlango wa nyuma kama ni kweli Kamati iliyoyasema, mdororo wa mizigo Bandari ya Dar-es-Salaam umekithiri na umeathiri sekta nyingi sana. Umeathiri uuzaji wa mafuta katika ma-*truck*, umeathiri huduma za mahoteli, umeathiri hata wale madereva, dereva yule wa *truck* kutoka Tanzania hadi Congo ana vituo chungu nzima, humo si ajabu wengine wameshazaa na watoto! Watu wale leo hawapiti, mashaka yameongezeka, uchumi umedorora, mahoteli yamefungwa! Sisi tunasema ukweli, ule mpango haufai na tunaiomba Serikali izingatie hili na iuondoe mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi katika huduma za mizigo ya *transit* ni kigezo cha pili ambacho kimesababisha wafanyabiashara wa Congo wakimbie! Naomba Mheshimiwa Waziri, jambo hili pia walizingatie kwa makini ili bandari yetu irudi katika hali yake, wafanyabiashara warudi na sekta za uchumi za nchi hii ziweze kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani ndani ya siku 100 za utawala wao huwa wanatoa taswira ya hali za uchumi za nchi zao zinavyoendelea, leo tuna mwaka mmoja wa utawala huu wa Chama kizee bado hatujajua hasa Watanzania wanaelekea wapi katika mfumo wa uchumi wa nchi hii. Hili ni jambo la kusikitisha sana! Sasa tunapowaambia hapa siyo kwamba, tunawaambia tunawachukia, tunawaambia ili mjue kama ni wajibu wetu kuwawakilisha wananchi na kuwaambia yale yaliyo ya kweli na hakuna budi myafuate, kwa sababu, sisi pamoja na kwamba ni washauri, lakini mshauri anayemaliza na kuwa na azimio huyo ni mshauri tofauti na washauri wa ngoma za mtaani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizingumzie Kituo cha Uwekezaji ambacho kimeandikwa katika taarifa ya Kamati, Kituo cha Uwekezaji cha Biashara cha Kurasini; mradi huu mkubwa wa Kituo cha Uwekezaji cha Kurasini ni jambo lililoanza mwaka 2010 na Bunge lililopita kwa mara ya mwanzo walitakiwa kulipa bilioni 45 Tanzania *shillings* ili kuuwezesha mradi ule mkubwa wa uwekezaji uwepo ndani ya nchi yetu. Matokeo yake mradi ule ulisuasua kutoka shilingi 45 bilioni ukaenda mpaka shilingi bilioni 60 ni mwaka wa pili, ukaenda mpaka shilingi bilioni 90 mwaka wa tatu, ukaenda mpaka shilingi bilioni 120, ndiyo matokeo yake umemaliza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha leo katika taarifa hii nimeona wanasema kama wale wafadhili ambao walikusudia kuendeleza mradi ule kuutekeleza wameondoka na haijulikani hatima yake. Tukumbuke kwamba, pesa za Watanzania zilizotumika, Watanzania walioondolewa maeneo yale kupisha mradi ule ni gharama kubwa ambayo imepatikana na maslahi hayaonekani yako wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo ni nini? Tatizo ni kuchelewa kwetu kufanya maamuzi katika mambo ya msingi ya nchi hii. Tunachelewa, ni hodari sana wa kuandika kwenye karatasi, lakini ni wazito sana wa kutekeleza yale ambayo tunadhani yanaleta tija kwa nchi hii. Leo mradi ule ambao ulikuwa unagombaniwa na nchi zote za Kiafrika, Tanzania ikapata bahati ikachaguliwa na China kuletewa mradi ule mkubwa tumekaa hapa tumebabaika-babaika mpaka tayari mradi ule, leo nimeona kwenye taarifa umeondolewa wakati Tanzania ikiwa imeshalipa mabilioni ya shilingi kupata lile eneo na Watanzania waliokuwa wakiendesha maisha yao pale wametupwa hata hatujui wametupwa wapi! Leo matokeo yake tunakuja kuona hapa kwenye taarifa kama wafadhili wale wamejiiondoa. Hiyo ni hasara nyingine kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kusuasua kwa kutekeleza miradi ambayo ni fursa kwa nchi inatueletea shida sana. Leo ni mwaka karibu wa 10 tunazungumza ndani ya nchi hii kuna chuma pale Liganga na Mchuchuma na kwenye mpango huu, kila mpango unaokuja tunaambiwa, tunasadikishwa kwamba, mradi wa chuma Liganga na Mchuchuma utafanyika, lakini matokeo yake tunaishia kusoma vitabu! Laiti mradi ule ungekuwa uko Kenya au Uganda au Burundi, leo tayari nchi zile zingekuwa zinazalisha chuma kile kwa wingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana Mwenyezi Mungu akishawapa anawapa, lakini kwa ugoigoi ambao tuko nao hata kama ingekuwa Mwenyezi Mungu anafikiria kuuondoa, bora angeuondolea mbali kwa sababu anatupa riziki tuzitumie kwa niaba ya watu wetu, lakini hatuwezi kutumia zile fursa, badala yake tunaandika kwenye makaratasi tu hatuwezi kufanya chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu tena leo nimeona nia ya Serikali juu ya kufufua viwanda. Imezungumzwa hapa *General Tyre* ya Arusha na viwanda vingine, *TEMDO* na kadhalika. Mheshimiwa nyimbo hizi hebu sasa Waheshimiwa Mawaziri, Serikali, wawe tayari kile wanachotusadikisha kinaweza kufanyika waweze kukifanya kwa muda unaowezekana. Leo hakuna asiyejua kwamba nchi ina *demand* kubwa ya matairi ya magari, biashara ya matairi ya magari ni biashara kubwa sana duniani, leo fursa ipo, mipira ndani ya nchi hii inazalishwa, lakini bado tunaimba wimbo tunafufua *General Tyre* kwenye vitabu, kwenye utekelezaji hakuna kinachotekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Maprofesa wengi wabobezi wa uchumi, wabobezi wa uchumi chungu nzima kwenye nchi wa kuisaidia Serikali kuandaa mipango mizuri ya uchumi, leo badala yake kupata wachumi wakatoa ushauri wao na kukaa na Serikali, leo wachumi mnawapeleka kuzoa taka mkiwapiga picha na *wheelbarrow* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachumi wa kuisaidia nchi hii mnawapiga picha wakizoa taka na ma-wheel barrow! What? Tutakwenda wapi? Wachumi wetu tunawageuza vituko tukitegemea nchi itakwenda mbele! Hasara yao. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie lile Shirika la TEMDO. TEMDO ile taasisi imeanzishwa kwa ajili ya kusaidia uvumbuzi wa viwanda vidogovidogo na mashine ambazo zinaweza kuwasaidia Watanzania kuanzia wa viwango vya chini kabisa, lakini cha kusikitisha Mheshimiwa Serikali imeanzisha taasisi ile kwa kujua umuhimu na faida zake, lakini taasisi ile imetupwa kama yatima. Wamekuwa wakilazimisha waonekane wapo kwa kutenda mambo ambayo hata Serikali haiwasaidii hata senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafanyaje? tunaanzisha kitu kwa nia ya kusaidia Taifa, lakini leo mnakitelekeza mnakifanya yatima! Matatizo ni yapi, hakuna kinachofanyika pale wakati wana uwezo mkubwa wa kusaidia kama vile viwanda amesema mwenzangu, viwanda vidogo-vidogo vya soksi, viwanda vya juice, viwanda vya kuteketeza taka kwenye mahospitali, ni watu ambao wana ujuzi mkubwa na wamesomeshwa na Taifa hili, lakini badala yake wametelekezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri waiangalie hii taasisi, hakuna nchi zilizoendelea bila kuwa na taasisi za uvumbuzi kama hizi, taasisi za utafiti kama hizi ambazo zinaweza kusaidia nchi zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakuwa ni nchi ya ajabu sana kwamba, leo tunapozungumzia suala la uimarishaji wa viwanda, lakini wawekezaji wanapotoka nje ya nchi kuja hapa kutaka kuwezesha kuwekeza katika maeneo wanapata usumbufu sana kuanzia kwenye ardhi na watu wa NEMC wanakuwa ni vikwazo vikubwa vya uwekezaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko ushahidi wamekuja wawekezaji hapa, Mwekezaji anatumia mpaka mwaka mmoja kuhangaikia vibali vya kuweza kuwekeza miradi ambayo italeti tija kwa nchi hii, italeti ajira kwa nchi hii. Wako wawekezaji wamekuja na wamehangaika mwisho wameondoka kwa kuona kwamba sisi ni Taifa ambalo hatuko tayari. Hawakufanya kosa Rais Museveni na mwenzie Rais Kagame siku zile walipoamua wakasema katika *East Africa* kuna nchi zilizo tayari kimaendeleo na kuna nchi kama Tanzania tuziache kwa sababu wao hawako tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwanza tuwe tayari kusikiliza ushauri unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Pili, tuwe tayari kumshauri na kumwambia ukweli Mtukufu Rais kwamba, hali halisi ilivyo ni hii. Yule tunatakiwa ni Rais wetu tumheshimu na nawaahidi watu wa CCM tunamheshimu Rais Magufuli, lakini niwaambie hatutamwogopa katika kumwambia ukweli utakaosaidia kulijenga Taifa hili. Tutamheshimu ni Rais wa

Tanzania, ni Rais wetu, lakini muwe tayari kumweleza ukweli, mnapoendelea kumfichaficha hamumsaidii! Mficha maradhi kifo humuumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Tanzania ukikua kwa kumshauri na kumwambia ukweli Rais, sifa na maendeleo ya nchi yetu ndio itakayotufanya sisi tujione ni Wabunge bora ni Mawaziri bora ni Serikali bora, lakini kuendelea kuona kila mmoja aah! Bwana mkubwa hafikiki! Itatuletea dhara na sisi tunawaambia haya, kama sisi tungekuwa na nia mbaya sana na Chama cha Mapinduzi tusingeyasema haya, tungekaa tu kwa sababu tunajua mnaharibikiwa. Watanzania sasa hivi wote wanalia hali ilivyo! Watanzania walikuwa hawajawahi kulia kwa ukosefu wa dawa katika nchi hii, mara hii mnasikia kilio!

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wanalia na mabegi barabarani wanarudishwa makwao hawana pesa katika mikopo! Leo huduma nyingine zote zimedorora, lakini akishuka hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha atasema uchumi wetu umekua! Uchumi umekua mabenki yanaeleza kabisa, *draft* imetolewa mabenki yote yame-collapse! Hasara tupu ambayo ipo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwe pamoja katika hili, tumshauri Mheshimiwa Rais Magufuli. Mtukufu Rais sio Mungu ni mwanadamu akiambiwa atasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khatib. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Janet Mbene, baadaye Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Augustino Masele wajiandae.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba nichangie machache katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuiomba Serikali kuwa, mipango inayotuletea kwa kweli ni mizuri sana na imepangwa kwa utaratibu mzuri sana wa kimkakati, lakini nafikiri katika mapendekezo mengi na maoni mengi yanayotolewa na Wabunge ni dhahiri kuwa, tuna tatizo la utekelezaji kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi hasa ile ya kimkakati imekuwa katika majadiliano kwa muda mrefu, tungetegemea sasa tuanze kuwa tumeweka mpango wa kuanza kuitekeleza. Tunajua kuwa mengine hatua ambayo imefikiwa ni nzuri, lakini kuna mambo machache tu ambayo

yanatakiwa yakamilishwe ili miradi hii ianze kufanya kazi na ianze kutuletea faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie miradi mikubwa ya kielelezo ambayo tumeipitisha hapa na imeonekana kuwa ingesaidia sana nchi yetu hasa katika wakati huu ambao tunalenga kuingia katika uchumi wa viwanda. Nataka nitaje mradi kwa mfano wa Mchuchuma na Liganga. Huu ni mradi ambao kwa kweli ungeanza kutekelezwa ilivyoandikwa au ilivyopangwa ni mradi ambao ungeiondoa nchi yetu katika uzalishaji wa chini na kutuingiza katika viwanda kwa haraka zaidi, maana ingetuletea malighafi muhimu sana kwa ajili ya viwanda vingine, lakini nasikitika kuwa mpaka sasa hivi bado haujakamilishwa na tunaambiwa kuwa pengine ni masuala machache tu yaliyobakia kujadiliwa. Je, kwa nini Serikali isiharakishe majadiliano hayo ili sasa huu mradi uanze kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunapozungumzia mradi huu wa Liganga na Mchuchuma, huu mradi utashughulikia makaa ya mawe, tunajua ni bidhaa ambayo ni kubwa, nzito na kwa vyovyote vile inahitaji miundombinu muhimu ya kusafirishia. Kulikuwa kuna mpango wa kujenga reli kwa ajili ya kupitisha makaa ya mawe kutoka katika maeneo ya mradi hadi bandarini, tungependa kujua fedha imeshawekwa kwa ajili ya kufanyia kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo kwa kweli linawagusa wananchi moja kwa moja. Wenzangu wengine wamegusia ni suala la kilimo, ni suala la maji, ni suala la afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukaa hapa tunazungumzia uchumi, tunazungumzia kilimo chenye tija bila kuzungumzia maji kwa maana ya umwagiliaji kwa maana ya maji salama yatakayotumiwa na wananchi, vilevile maji ya kusindika mazao ya kilimo na mazao ya mifugo. Kwa hiyo, tungependa sana kuona mkakati unawekwa kuhakikisha kuwa fedha ya kutosha inawekwa katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kilimo, wananchi wengi wangependa kulima kisasa, mashamba makubwa kwa tija, lakini hawawezi kupata mikopo. Kwanza Benki ya Kilimo haina mtaji wa kutosha, pili mashamba yao hayajapimwa. Kwa hiyo, hata kama Benki ya Kilimo ingeweza kuwakopesha, hawatakopesha kwa sababu mashamba yao hayajapimwa, hivyo, tunajikuta bado tuna tatizo, tunazunguka palepale, tunazungumzia kilimo lakini hatuwezeshi kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali ije sasa ituambie kuhusiana na suala hili la kilimo ambalo ndilo linaloajiri wananchi wengi na ambalo linge-*absorb* vijana wetu wengi, wangelima kwa tija na kibiashara tusingekuwa

tunalia kuwa vijana wengi hawana ajira. Vijana wengi wangepuga, vijana wengi wangukuwa wanauza na kusindika na tungekuwa hatuna shida na uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji kama nilivyozungumzia, kuna mikakati iliwekwa hapa na Serikali, tukaipitisha Bungeni juu ya kuweka tozo maalum kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Mfuko wa Maji unaundwa na unafanya kazi. Hatujui lile limefikia wapi, lakini tungependa Serikali iangalie uwezekano hata wa kuongeza ile tozo ili miradi ya maji yote itosheleze, bila maji ndugu zangu tutaongea mambo yote hapa lakini tunafanya kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala vilevile la vituo vya afya na zahanati nchi nzima. Ndugu zangu tunapokuwa tuna matatizo ya maji ni rahisi sana wananchi kupata maradhi, wananchi wakipata maradhi tunazungumzia sasa kwenda hospitali ambako tena hakuna vifaa au huduma muhimu. Kwa hiyo, tunajikuta tunazunguka katika mzunguko wa umaskini na *inefficiency* ambayo kwa kweli hatuikubali kama Wabunge, maana sisi ndiyo tuko na wananchi kule tunasumbukanao sana juu ya masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tuliomba, mwaka huu wakati wa bajeti tuliyoipitisha ya mwaka huu na mwaka wa kesho tuliomba tuongezewe fungu fulani kwa ajili ya kujenga zahanati na vituo vya afya ili vikamilike na vingi wananchi tayari walishajitolea, vipo. Tunaomba Serikali itusaidie kwa hilo, ile miradi muhimu ambayo ni kichocheo cha uchumi, cha uzalishaji kwa wananchi, ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuisisitiza hii kwa sababu hiyo ndiyo miradi ambayo inawagusa wanawake wengi. Wanawake wengi ndio wazalishaji vijijini, wanawake wengi ndio wanaohangaika na maji, wanawake wengi ndio wanaohangaika na watoto wagonjwa na wao wenyewe wakiugua, lakini huduma zote ambazo zinawagusa akinamama ndio hizo ambazo tunazipigia kelele sasa. Tunaomba Serikali wakati mnaangalia mambo makubwa lakini na haya madogo msiyape kisogo kwa sababu yana umuhimu mkubwa sana kwa uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya miradi ya mikakati ya kielelezo, kwa mfano, *General Tyre*. Hakuna asiyejua umuhimu wa *General Tyre* ilipokuwa ikifanya kazi na tunaambiwa kabisa kuwa ilikuwa tayari ianze kufanya kazi. Tunajjuliza kimekwama nini sasa kwa *General Tyre* kuanza kazi? Tungependa kujua *General Tyre* kwa nini haijaanzishwa mpaka sasa hivi wakati kila kitu kilikuwa kiko tayari kuendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka vilevile kuzungumzia *NDC* - Shirika la Taifa la Maendeleo. Hili ni shirika ambalo limepewa majukumu maalum kusimamia au kuibua miradi ya maendeleo na limekuwa likifanya hivyo, lakini fedha linayopata ni kidogo mno kiasi kwamba unashindwa kuelewa watafanyaje kazi. Mradi huu tunaozungumza wa Liganga na Mchuchuma ni mradi ambao upo chini ya *NDC*, mradi wa magadi soda upo chini ya *NDC* na miradi mingine mingi ambayo tunategemea *NDC* waisimamie lakini bila kuwa na bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa sasa hivi kusikia kutoka Serikalini mipango mikakati yao ya kuhakikisha kuwa hii miradi sasa inaanza kufanya kazi. Tumekuwa tukiizungumza na imekuwa katika vitabu vyetu kwa miaka mingi sana sasa, tungependa tujue Serikali imeshatenga fedha ya kutosha kwa ajili hiyo? Lakini kama wao wenyewe hawana fedha tulishakubaliana kuwa tuna mpango wa *PPP* jamani siyo kila kitu lazima Serikali yetu yenyewe ifanye na uwezo huo bado hatuna. Kwa nini tusiachie huu mpango wa *PPP* sasa ufanye kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa na nitafurahi sana kusikia Serikali ikisema kuwa kuanzia mwaka huu wa fedha tunaouenda tutakuwa na miradi kadhaa hata kama ni mitatu tu mikubwa ambayo inaendeshwa kwa mpango wa *PPP* ili kuipunguzia Serikali adha ya kuhakikisha inatafuta fedha yenyewe. Nchi nyingi zinazoendelea au zilizoendelea zilitumia mfumo huo kupunguza ule mzigo kwa Serikali kwa ajili ya bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie masuala ya *Economic Processing Zones* na *Special Economic Zones*. Nchi nyingi kama China kwa mfano waliendelea haraka sana kiuchumi walipojiingiza katika mfumo huu wa maeneo maalum ya kiuchumi. Sisi tumesainisha maeneo mengi mengine tumeshalipa mpaka hata fidia, lakini hatufanyi chochote wakati huko ndio ambako tungehakikisha kuwa uwekezaji mkubwa unafanywa na sekta binafsi kwa ajili ya kuhakikisha kuwa tunaendeleza viwanda vyetu hasa vile vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vichache ambavyo tayari vimeshaanzishwa kwa mfano pale Dar es Salaam tunaona kabisa jinsi ambavyo vinazalisha na vimezalisha ajira nyingi sana, *imagine* kila mkoa ambako kulikuwa kumesainishwa maeneo hayo ingekuwa yanafanya kazi sasa hivi tungekuwa tunalalamikia ajira wapi? Kwa hiyo, nataka kusikia *EPZ* na *Special Economic Zones* sasa hivi Serikali inakwenda kufanya nini kwa maana ya utekelezaji, kwa maana ya nadharia na mipango tunayo tunajua muda mrefu. Tunaomba sasa ikafanyiwe kazi japo tuone mradi hata mmoja unaanza katika hii miradi mikubwa ambayo imewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la bandari; tumekuwa na mipango mizuri tuliyoiweka kwa ajili ya kupanua bandari zetu, magati yale ili kuhakikisha kuwa meli zinakuja kuweka nanga na kutoa mizigo na kuchukua mizigo, lakini yamekuwa ni mazungumzo ya muda mrefu. Mpaka wenzetu sasa wamestuka wao sasa wameshaendeleza bandari zao na tupo kwenye ushindani mkali sana. Nataka kusema hivi, haya mambo ya kusema ooh! wawekezaji wanatupenda jamani tuachane na hizo ndoto, anakupenda kwa sababu kuna kitu atakuja kunufaika na wewe, hakupendi kwa sababu wewe ni Mtanzania au kwa sababu sijui una sura nzuri au kwa sababu una amani. Naomba ndugu zetu Serikalini mtambue kuwa biashara ni mashindano, Kenya wakimaliza bandari zao, Kenya wakimaliza reli zao hao mnaowaita marafiki zenu hamtawaona na tukishapoteza wateja siyo rahisi kuwarudisha jamani yaani hiyo ni *economic sense* ya kawaida kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali yangu sikivu, hebu sikieni hili *for the last time*, hebu fanyeni hivi vitu sasa hivi viwe *reality*. Tunashindwa hata jinsi ya kuvitetea kwa wananchi kwa sababu ni kila mwaka wanaviona, vyote vipo vimeainishwa katika Ilani yetu lakini utekelezaji lini sasa? Na kama hatuna fedha viko vyanzo sasa *through* sekta binafsi ambavyo vinaweza vikafanya. Rahisisheni masharti kwa sekta binafsi wa-engage wasikilizeni sekta binafsi wana mawazo mazuri, wale ni wafanyabiashara na wanajua jinsi ya kuendesha biashara kwa faida na faida hiyo itapatikana kwa wote; ninyi Serikali na wao sekta binafsi. Ningependa sana kusisitiza kuwa hayo ni mambo ambayo lazima sasa hivi tuyawekee mikakati ya kufanya, yapo kwenye vitabu, yapo kwenye Ilani lakini sasa tuanze utekelezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wajasiriamali wadogo na wa kati, bila kuwawezesha hawa hata hao wakubwa ambao tunataka kufanya nao biashara itakuwa ni kazi bure, hawa wadogo ndio watakaosaidiana na wakubwa, watakuwa na mahusiano yanayoshihiana. Wakubwa watakuwa ndio wanunuzi wa huduma za hawa wadogo na wadogo ndiyo watakuwa wanapata ujuzi kutoka kwa wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukawa tuna sekta ya chini kabisa na ya juu kabisa katikati hapa hakuna kitu, hakuna kitu kama hicho! Kwa hiyo, lazima wajasiriamali wadogo na wa kati wawe na mkakati maalum wa kuwasaidia kwa maana ujuzi, urasimishaji, lakini vilevile tuhakikishe kuwa kodi wanazotozwa jamani wanakuwa *discouraged* na kodi. Wanaanza tu hivi tayari wana mzigo wa kodi, haitawezekana kama tunataka kuwawezesha tuwape muda wafike mahali ambapo wataweza sasa kusimama ndiyo tuanze sasa kuwatoza kodi. Lazima tuwalee, mbona tunalea wakubwa, hawa wadogo kwa nini tunashindwa kuwalea na ni wazalendo na ndio watu wetu? Huko ndiyo vijana wetu watakapoponea katika masuala ya kiuchumi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala lingine la mabenki. Yamezungumzwa mambo mengi sana kuhusiana na mabenki kuwa yamekosa mitaji sasa yatakosa kukopesha, nataka kusema mabenki yetu yalikuwa yamelemaa, yalilemazwa na Serikali kwa ajili yalikuwa yanapata pesa za bure. Asilimia 20 ya Watanzania ndio ambao wanatumia mabenki, hawa wengine wote pesa zao ziko wapi? Mabenki yaanze kutoka sasa maofisini waende vijijini huko wakatafute wateja wakaweke kama ni *agency*, kama ni *branches*, chochote kile lakini wahakikishe kuwa wanazitafuta, fedha zipo, siyo za Serikali tu ndiyo fedha zao, wao watafute vyanzo vingine vya *deposits*. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephat Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele na baadaye Mheshimiwa Sebastian Kapufi pamoja na Mheshimiwa Waitara wajiandae.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi jioni ya leo ili kuchangia. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam kwa ujumla, mengi nimechangia kupitia Kamati ya Bajeti. Kwa leo kuna machache ambayo nadhani iko haja ya kuongezea ili kumtengeneza ng'ombe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wachangiaji wengi ni kama vile dhana haieleweki kwamba Serikali inataka na sisi tujazie ya kwetu, badala yake watu wanakuja wanalalamika kama vile essence ya kuwepo wao kuchangia haina maana. Tungewasikia wapi kama fursa hii isingepatikana, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge ni fursa ya kuchangia ili tuwe na mpango mzuri kwa ajili ya kulivusha Taifa hili, Taifa ni la kwetu sote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma maoni ya Kambi ya Upinzani wanachokisema ni kama vile wana nchi ya kwao kiasi kwamba hata boti hili likienda vibaya wao wana *option* ya pili, haitujengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ambayo nimeyatoa kwa utangulizi naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee ukurasa wa saba wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri ambayo katika matazamio yake anatarajia kwamba bei ya mafuta itaendelea kuwa nzuri. Naomba tukumbushane OPEC walishakubaliana kwamba watapunguza uzalishaji wa mafuta, tafsiri yake ni nini? Kama uzalishaji

wa mafuta utapungua maana yake bei itapanda, sasa katika mipango yetu lazima tulijue hili na tukishalijua sasa tujiandae tunafanyaje kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri, ni manufaa yapi ambayo tulipata kama Taifa baada ya bei kushuka? Kwa sababu haiwezekani tuache liende kama linavyoenda bei ikishuka hakuna ambacho Serikali inafanya, bei ikipanda hakuna ambacho Serikali inafanya. Ni vizuri tukawa na mkakati maalum kwamba pale ambapo inatokea bei kushuka tuone faida moja kwa moja ambayo inapatikana kutokana na anguko la bei ya mafuta. Lakini ingependeza sana kama ungeanzishwa Mfuko Maalum ili kuweza ku-*stabilize* pale ambapo bei zikipanda sana basi kuwe na namna ya kuweza ku-*absolve shock* ambazo zinajitokeza wakati bei za mafuta zimepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashuhuda kwamba pale ambapo bei ikipanda hata siku moja tayari siku inayofuata tunaambiwa nauli zinapanda na kila kitu kinapanda. Sasa ni vizuri katika mipango yetu tukajiandaa tunaitumiaje fursa kama hiyo pale inapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mpango wa maandalizi ya bajeti kuna *prediction* kwamba hali ya chakula itakuwa nzuri. Naomba nipingane na hili kwasababu kwa taarifa tulizonazo ni kwamba kuna ukame unatarajiwa kuwepo. Kwahiyo, hatuwezi tukasema hali ya chakula itakuwa nzuri, sio sahihi. Kwa hiyo, kwenye mipango yetu lazima *factor* hiyo tuiweke na tuseme sasa hiki kinachotokea tunafanyaje ili hali ya uchumi wetu isije ikaharibika kwa kiasi kikubwa. Ni vizuri katika mipango ambayo inawekwa tukaweka hiyo *factor* kwa sababu ipo; kama jambo una uhakika litatokea ukajifanya kwamba hulijui utakuwa husaidii Taifa. Ni vizuri tukalijua, tukajiandaa kwamba tunafanyaje kama Taifa ili tusije tukapata tabu kutokana na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wenzangu kuhusiana na kupungua kwa mizigo bandarini. Ni kweli, lakini ambacho ningepomba kiingie na kionekane vizuri kwenye mipango yetu, sisi sote ni mashuhuda kwamba bandari ya Dar es Salaam haina uwezo wa kupokea meli kubwa za kuanzia 3G, 4G uwezo huo hatuna, nini kifanyike? Tumekuwa tukisikia muda mrefu kwamba bandari ambayo itajengwa Bagamoyo itakuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kupokea meli za ukubwa wa *fourth generation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipata fursa ya kutembelea bandari ya Mombasa ukaona uwekezaji uliofanywa na wenzetu na hawakuishia kwenye Bandari ya Mombasa wameenda sasa Bandari ya kule Lamu, kiasi kwamba tusitarajie. Hata kama tutafanya upanuzi wa geti namba 13, 14 bila kuanza *seriously* ujenzi wa bandari ya Bagamoyo hakika tunajiandaa kwenda kushindwa kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri katika mipango yetu tukajielekeza katika hilo kwamba hata ungepanua vipi Bandari ya Dar es Salaam imeshafika mwisho. Kwahiyo, ni vizuri katika mipango yetu tukajielekeza katika kuanza kujenga bandari ya kisasa ambayo itakuwa na uwezo wa kupokea meli za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia taarifa na hii pia tulikutana nayo hata wakati tumekutana na Wizara ya Fedha. Kuna fikra ndani ya Serikali kwamba mpango unaokuja sasa hivi juu ya *currency* yetu ni kuhama kutoka utaratibu wa *fluctuation floating* twende kwenye *fixed* na fikra iliyopo Serikalini ni kwamba tu-peg shilingi yetu kuibadilisha na dola kwa shilingi 2,193 kama sijakosea, ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tafsiri yake ni nini? Ni kwamba tayari tunajijandaa kwamba shilingi yetu inakwenda kuanguka, faida ya ku-*devalue* shilingi inakuwa ni rahisi kwa mtu ambaye anakuja kuwekeza kwetu kwa ile *direct foreign investment* lakini *disadvantage* ambayo tunakuwa nayo ni kwamba itakuwa ni gharama sana kwa mtu ambaye anataka kupeleka mizigo nje kutoka Tanzania akija kubadilisha na pesa yetu atakuta anapata hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri hii hali ya kuacha soko ndio liamue na tutafute namna nzuri ambayo itahakikisha kwamba shilingi yetu haiyumbi sana, ndiyo namna iliyokuwa nzuri kulikoni habari ya kwamba unasema *fixed*, ukishafanya *fixed* ikija kutokea kipindi uchumi umeanguka maana yake tutalazimika ku-*devalue* shilingi yetu kwa kiasi kikubwa sana. Ni vizuri ikafanyika tathmini na utafiti wa kutosha kabla hatujafikia hatua hiyo, tujue madhara ambayo tumekuwa nayo kwa kuachia bei ya soko ni yapi na hicho ambacho tunatarajia kukifanya faida yake ni ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendeza sana tukiwa na makampuni ya Kitaifa kwa ajili ya Watanzania, sioni katika mpango unaokuja nia thabiti ya kuhakikisha kwamba TPDC inawezeshwa kwa niaba ya Watanzania ili kuweza kushiriki katika *upstream* na *downstream* katika suala zima la mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba iliyopo mizuri kabisa inaonesha kwamba, wakiweka mtaji basi ushiriki wao na *share* ambayo watakuwa wanapata ni kubwa, lakini pale ambapo hawezeshwi kwa maana ya *capital*, kitabaki kugawanywa kile kidogo ambacho kimebaki. Sasa kwa Taifa ambalo tungependa kampuni ya Taifa kama zilivyo *State Oil*, *Petrolbras* ni kwamba Serikali zao ziliwekeza ndiyo maana makampuni haya yakawa na uwezo mkubwa. Ni vizuri na sisi tukahakikisha kwamba TPDC inawezeshwa kwa ajili ya Watanzania walio wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la uvuvi wa bahari kuu. Silioni hili likijitokeza dhahiri lakini limekuwa likisemwa siku nyingi. Nakumbuka katika bajeti iliyotangulia ya 2015/2016 ilikuja Wizara ya Uvuvi wakisema kwamba wanahitaji pesa kwa ajili ya kununua meli ya doria. Ikatengwa nadhani kama shilingi milioni 500 wakapewa, hadithi ya hiyo pesa imetumikaje mpaka leo haijulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, haiwezekani kile ambacho tunapata kwenye bahari kinazidiwa na maziwa ya *Victoria* na Tanganyika. Maana yake kuna tatizo kubwa ambalo hatujafanya kiasi kwamba wanakuja Wakorea kuvua samaki wengi sana wanatajirika kutoka katika maji ya kwetu lakini sisi kama Taifa tunapata nini? Ni vizuri sasa likajitokeza waziwazi kwamba kama Taifa tunafaidika vipi na bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusiana na *General Tyre*; sisi sote ni mashahidi, Wabunge wote tunatumia magari, kwa hiyo hatuna jinsi lazima tununue matairi kwa ajili ya magari, kwa hiyo soko lipo wazi hata kama mngokuwa na uhakika wa ku-service gari za Wabunge tu una uhakika wa kupata tairi ambazo zina ubora lakini soko lipo la kutosha nchi zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kasi ya kufufua *General Tyre* ni vizuri ikaonekana dhahiri; haipendezi tukaendelea kutazama tu kwenye makaratasi, inatosha tunataka utekelezaji. Kama imeshindikana tuambizane kwamba *idea* hii imeshindikana, labda tuanze *thinking* nyingine, lakini ukirejea kama miaka minne, mitano *General Tyre* inatajwa, Mchuchuma na Liganga inatajwa, kule Natron inatajwa, itoshe kutajwa tunataka kwenda kutenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini katika Serikali hii ya Awamu ya Tano ambayo tunataka maneno kidogo vitendo viwe vingi, vitendo vikiwa vingi huna haja ya kusema sana wenzako watakuwa wanatafuta namna gani ya kukosoa. Lakini pale unapotenda kama ambavyo tumetenda kuhusiana na suala zima la ndege, kuna wengi walibeza wengine wakasema ni ndege chakavu, lakini ukija hata asiyekuwa na macho atapapasa, atajua kwamba hii siyo ndege chakavu, ni ndege mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Augustino Masele.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na wewe kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Serikali yetu ya Awamu ya Tano imekuja na mipango kabambe kwa ajili ya kufufua uchumi wa nchi hii na kwa maana hiyo, sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndiyo tunahusika kwa namna zote kuisimamia Serikali kuhakikisha kwamba inafanikiwa katika mipango yake ya kila siku, basi tuwe mstari wa mbele kuhakikisha kwamba tunaiunga mkono Serikali yetu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utanza na suala zima la uhamishaji Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma. Ni wazo zuri na ni la kimaendeleo lakini limechelewa. Pamoja na kuchelewa huko, tunatakiwa tujipange sawasawa kuhakikisha kwamba hatushindwi njiani. Kwa maana hiyo, mipangilio iwe thabiti tusije tukajikuta kwamba sasa tunakwamisha Serikali katika utendaji kazi wake kwa sababu sasa watumishi watakuwa mguu mmoja nje, mguu mmoja ndani. Kwa hiyo, nishauri Serikali kwa kweli ijipange vizuri na Maafisa Masuuli kama Waziri wa Fedha alivyoainisha kwenye mpango wake kwamba jambo hili waliweke katika bajeti ili liveze kutekelezeka kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia niishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaweka katika mipango yake ya bajeti gharama za ujenzi wa Halmashauri katika Wilaya mpya kama Mbogwe na nyingine. Pia itenge bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mikoa mipya ambayo imeanzishwa kama Mikoa ya Geita, Songwe, Simiyu, Njombe na Katavi ili wananchi wa mikoa hii na wao waweze kupata huduma karibu zaidi kama Serikali ilivyojipanga kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la utaratibu wa Serikali kufuta *retention* na kuziagiza taasisi mbalimbali kupeleka pesa zao katika akaunti ya Benki Kuu. Jambo hili ni zuri kwa sababu linaongeza udhibiti wa mapato na matumizi ya Serikali ili kuweza kufahamu thamani halisi ya yale mapato ambayo yanapatikana. Hata hivyo, niishauri Serikali iwe makini kuhakikisha kwamba pesa ambazo zimepangwa kwa ajili ya taasisi hizi zinaenda kwa wakati ili miradi ya maendeleo ambayo imepangwa kwenye sekta hizo isikwame. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la miradi ya kielelezo. Miradi hii mingi imeainishwa lakini mradi mkubwa ambao unatakiwa tuufanye haraka ni mradi wa reli ya kati na ujenzi wa Bandari za Tanga, Dar es Salaam,

Mtwara na pia bandari zile za maziwa makuu kama Mwanza, Bukoba, Karema, Kigoma na nyingine nyingi. Nasema hivi kwa sababu tumepakana na nchi mbalimbali ambazo nyingi zinategemea sana Bandari ya Dar es Salaam ambayo inaunganishwa na maziwa makuu kwa kupitia njia ya reli. Sasa reli ya kati kutoka Dar es Salaam – Tabora – Kigoma - Mwanza na nyingine ambayo itaanzia Isaka - Kigali, zote hizi zina muunganiko mzuri wa kuweza kutumiwa na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naiomba Serikali ihakikishe inafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba mradi huu kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo ambao ni nchi ya China ambayo imekubali kufadhili mradi huu, ufanyike kwa umakini na kwa haraka ili kuweza kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda inafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Nikiwa mwanakamati wa Kamati ya Bajeti, tumeona kwamba ili Serikali iweze kufanikiwa katika lengo hili ni vema basi ikaongeze chagizo lake katika bajeti kutoka shilingi milioni 59 kwa mwaka mpaka kufikia shilingi bilioni 200 ili kwa miaka yake minne iliyosalia lengo la kukipatia kila kijiji shilingi milioni 50 liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la kubadilika kwetu kwa *mindset* kwa maana ya Watanzania. Imeonekana kwamba wakati mwingine Watanzania tunakuwa na matatizo ya kutengenezwa kwa kuwa na urasimu mkubwa ambapo wawekezaji wanapokuja hapa nchini hucheleweshwa, matokeo yake wanaamua kukimbilia katika nchi nyingine ambazo na zenyewe zina uhitaji wa wawekezaji kama sisi. Kama tusipobadilika tunaweza tukajikuta tunaachwa na wenzetu nchi zenye ushindani na sisi, wakupokea wawekezaji wa kutosha na matokeo yake nchi zao zitaneemeka kiuchumi kuliko sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema haya, ahsante kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masele. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Waitara ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu changamoto ambazo ziko mbele yetu na kimsingi maendeleo ni matokeo ya mgongano wa mambo mbalimbali. Kwa hiyo, tunapozungumzia habari ya maendeleo tusiogope kukumbana na

changamoto mbalimbali, la msingi ni tunafanyaje kwa maana ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kufuatilia taarifa ya Kamati lakini hotuba ya Waziri na taarifa ya wenzetu kwa maana ya Kambi ya Upinzani, nimefarijika kuona kwamba wote wazo letu ni moja, ni namna ya kumsaidia Waziri tutoke hapo tulipo twende kwenye hatua nyingine. Kwa hiyo, naendelea kusema tusiziogope changamoto, la msingi ni kukabiliana nazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa reli kwa maana ya miradi ya vielelezo. Nafahamu lengo zuri kwa maana ya uboreshaji wa reli ya kati kwa maana ya kuwa *standard gauge* ni jambo jema, lakini naomba twende mbali zaidi. Nitatoa mfano hai, leo hii pamoja na nia hiyo njema ya kuboresha reli lakini utakapoboresha reli mabehewa ikawa tatizo, suala zima la uboreshaji linakuwa limefanyika ndivyo sivyoy. Nalisema hilo kwa sababu gani? Nitawapa mfano hai. Leo hii ukienda Mpanda, Katavi, treni zinakwenda kule kwa reli hiyo ambayo ipo kwa sasa hivi lakini shida kubwa ni suala la mabehewa. Wananchi katika maeneo yale wanakabiliana na changamoto kubwa ya mabehewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme shirika letu linatakiwa litoke hapo liende kwenye hatua nyingine ya mbele zaidi. Litoke kwenye mfumo ambao ulikuwa ukitumika toka enzi hizo za ukoloni liende kufanya kazi kibiashara zaidi. Nashangaa ukifika sehemu unaambiwa hapa tunahitaji abiria 40 tu, kama kuna abiria 100 wanasema idadi ya abiria wanaohitaji ni 40. Sasa wewe kama unafanya kazi kibiashara niliamini ungefurahia kupata abiria 100 badala ya ku-*limit* kuwa na abiria 40 kwamba abiria 40 ndiyo unaohitaji, 100 siku nyingine, wafanye kazi kibiashara. Nalisema hilo nikitolea mfano hai katika mazingira ya Mpanda, mabehewa ni machache, abiria ni wengi na kama shirika linataka kufanya kazi kibiashara ni kuongeza mabehewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la njaa kama fursa. Nilisikia wakizungumza kwamba nchi za jirani kuna maeneo mengine wenzetu kutokana na hali mbaya ya hewa suala la njaa linawakabili. Sisi Tanzania habari ya chakula Mungu katusaidia, je, tunafanyaje kutumia nafasi hii ya njaa kwa wenzetu kuwa ni fursa kwetu sisi ambao tuna chakula? Wanasema adui mwombee njaa. Kwa hiyo, naomba katika mazingira haya ambapo wengine wanakabiliwa na njaa kwetu sisi iwe ni fursa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo niende kwenye suala la ongezeko la watu. Nilikuwa nikijaribu kufuatilia *data* hapa, zinaonesha ongezeko la idadi ya watu kwa maana ya 2016 ni milioni 50.1 lakini itakapofika mwaka 2025 kutakuwa na watu milioni 63, namshukuru Mungu lakini ongezeko hili la watu linakwenda sambamba na mipango mingine ya maendeleo?

Naomba hilo tuliangalie. Tunazungumzia habari ya watu kuongezeka lakini vipi kuhusu mipango ya uzazi bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani watu waongezeke lakini wakiongezeka katika mazingira ambapo mipango mingine iko nyuma ndiyo tunarudi kwenye matatizo haya ambayo tumeendelea kuyaona kama migogoro ya ardhi kwa maana watu wameongezeka lakini ardhi haiongezeki, migogoro kwenye maeneo ya hifadhi na maeneo mengine ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wakati tutakapokuwa tukiliongelea Taifa kwenda kwenye ongezeko hilo la watu liende sambamba na mipango mingine hiyo kama suala zima hilo nililolisema la uzazi bora, lakini tuangalie na masuala mengine kwamba tumejipanga vipi kwa maana ya matumizi bora ya ardhi ili kuepuka migongano tunayoiona sasa hivi ya wakulima na wafugaji na mambo mengine ya namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya Serikali kuhamia Dodoma ni jambo jema, ni jambo la maendeleo, lakini naomba niendeleo kushauri jambo moja na si kwa maana ya Dodoma tu ni kwa maana ya miji yote inayoendelea kukua Tanzania. Changamoto tulizoziona kwa Jiji la Dar es Salaam ni kwa kiwango gani changamoto hizo zimekuwa elimu kwetu kwa maana zisijirudie katika maeneo mengine ikiwa ni pamoja na Dodoma, Arusha, Mwanza na kwingineko? Yale yote tuliyoyaona ya kuhusu watu kubanana barabarani, wanashindwa kufika makazini kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia tija, unapokuwa na watu wamechelewa kufika katika vituo vya kazi, muda mwingi wako barabarani tija utaipataje? Kwa hiyo, naomba wakati mpango mzuri huu wa Serikali kuhamia Dodoma ukifanyika tutoke hapo twende tukachukue yale yaliyojitokeza katika maeneo mengine na kwetu tusiyaogope, hayo yawe ni fursa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari kuhusu makusanyo katika majengo. Jambo hilo ni jema lakini ukifuatilia hata katika taarifa ya Kamati inasema hivi:-

“...kuhusu majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini kukusanya viwango vya kodi vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Vilevile katika ufanyaji tathmini, Serikali iangalie hali ya uchumi wa eneo husika, thamani ya ardhi na thamani ya nyumba yenyewe katika eneo husika”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa sababu gani? Haki iende sambamba na wajibu, utakapotamani kupewa haki ya kodi na vitu vingine vya namna hiyo lakini ni kwa kiwango gani na wewe umetimiza wajibu wako? Kuna maeneo leo hii tunaweza tukatamani tupate kodi hiyo ya majengo lakini ni kwa kiwango gani Serikali hii imetimiza wajibu wake wa kuwapatia haki yao ya

kimsingi wananchi wa maeneo husika kwa maana ya kuwapa hati husika za maeneo hayo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa sababu gani? Kwa mfano, sehemu kubwa ya Mji wa Mpanda watu wanakaa katika majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini na hivyo hawana hati za kumiliki maeneo hayo. Kwa hiyo, wakati tukiwa tunakusudia kwenda kuwaomba wananchi hawa watulipe kodi, basi Serikali iendelee kutimiza wajibu wao wa kimsingi wa kuhakikisha watu hawa wanapewa hati zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niendelee kushauri, fursa alizotupa Mwenyezi Mungu, fursa ya kijiografia kwa maana ya bandari tusikosee na kama kuna sehemu tumekosea tujirekebishe, fursa hii ni adimu. Niliwahi kuzungumza siku za nyuma nikasema tumependelewa na Mwenyezi Mungu kwa maana kijiografia tumejikuta hapa tulipo. Sasa pamoja na zawadi ya jiografia aliyotupa Mwenyezi Mungu tunashindwa kuitumia! Naomba tuitumie fursa hii, changamoto zote zinazojitokeza kwa maana ya bandari tuzirekebishe na iwe ni fursa badala ya kuwa adha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu mapendekezo yakiendelea kujirudia mara kwa mara bila utekelezaji panakuwa na shida hapo. Naomba mapendekezo mbalimbali haya tunayoyatoa basi yaonekane katika taswira ya utekelezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niongelee suala la vipaumbele. Tukiwa na vipaumbele vingi mwisho wa siku tutajikuta tuna vipaumbele ambavyo havijafanyiwa kazi. Tunaweza tusiweze yote kwa wakati mmoja pamoja na nia njema, basi twende kwenye vichache ambavyo tutavifanya kwa kiwango kinachostahili na watu wakaona hili na hili limefanyiwa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji, niendelee kuishauri Serikali yangu. Nafurahi kuona wananchi wa Kanda ile ya Ziwa tukitumia chanzo muhimu cha Ziwa Victoria, maji yanaendelea kuwafikia watu katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, naomba tena, Ziwa Tanganyika ni chanzo muhimu ambacho ametupa Mwenyezi Mungu, tuna sababu gani ya kuendelea kuhangaika na visima virefu ambavyo vingine hata hupati maji wakati tuna ziwa na maji unayashangaa yale pale? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mipango ile ambayo inaendelea katika ukanda ule na siyo huko tu tukiangalia nchi yetu yote kwa ujumla wake, naomba mpango huu hata kama utakuwa ni wa muda mrefu tufike sehemu habari ya maji iwe ni historia. Kwa sisi ambao tuna *water bodies* zimetuzunguka, una Ziwa Victoria pale, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa,

sijazungumzia mito mikubwa habari ya maji iwe ni historia. Kupanga ni kuchagua, kama tumechagua kwamba sasa tunakwenda kupambana na habari ya maji, tupambane! Ndiyo maana nimetangulia kusema tuwe na vipaumbele vichache ambavyo tunaweza tukavifanyia kazi kwa kiwango kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulindaji wa bidhaa za ndani na walaji pia, napata tabu sana. Siku za hivi karibuni kupitia vyombo vya habari nimeendelea kuona hata bidhaa kama dawa sehemu ambapo pameandikwa muda wa matumizi wa dawa hiyo watu wachache wasiowapenda Watanzania hawa wanakwenda kufuta ili bidhaa hiyo iendelee kuwepo sokoni. Hata kama tutakuwa na mipango mizuri wakati afya ya wananchi wetu iko mashakani hiyo mipango ni akina nani watakwenda kuifanyia kazi? Kama hatutahakikisha tunalinda afya ya watu wetu, kama hatutahakikisha chakula wanachokula watu wetu ni kile ambacho kinastahili, mipango yote hii itakuwa haina maana kwa sababu mwisho wa siku wale ambao walikuwa ni walengwa watakuwa wameshazikwa wote na wamekwenda kaburini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nakuja eneo la changamoto, si kwamba Mheshimiwa Waziri haya yote tunayoyazungumza hayasikii au hayaoni, kuna sehemu nilifarijika kuona ameandika changamoto na namna ya kuzifanyia kazi. Kwa mfano, kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi, nimefarijika kuona Mheshimiwa Waziri kumbe anafahamu huko kwenye eneo la kodi kuna mwanja mkubwa na hata hizi mashine tunazozungumzia sasa hivi watu wengine wajanja wanaziharibu kwa makusudi. Ukiliacha hilo, kuna maeneo unaweza ukaenda mashine ipo lakini hupewi stakabadhi kutoka kwenye mashine unapewa ambayo imeandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani twende kwenye hatua moja zaidi, inawezekana hata tungekuwa na mashine nzuri namna gani, hata tungekuwa na mipango mizuri namna gani kuhusu suala zima la kodi, hebu turudi kwenye mioyo ya watu, turudi kwenye suala zima la elimu ikamfikie kila mmoja kuhusu umuhimu wa kodi. Kwa sababu leo tunapozungumza kuna sehemu fedha imekosekana, mtu ajue kabisa kwamba yeye ni sehemu ya kutukwamisha kufikia kule tulikokusudia kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, elimu hiyo ikiendelea kutolewa na watu wafike sehemu kama ni makanisani, mashuleni wawe pia na hofu ya Mungu. Kwa sababu mimi naamini hata hizo nchi nyingine ambazo tunaziona zimepiga hatua ni wakali katika suala zima linalogusa kodi. Kwa hiyo, nataka kusema hilo nalo la changamoto ambazo Mheshimiwa Waziri ameziona tuendelee kuzifanyia kazi kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nafahamu unaweza ukawa na bilauri ina maji yamefika katikati itategemea mtu anakusudia kuleta picha gani. Mtu mwingine anaweza akakwambia ameiona bilauri maji yako nusu lakini mwingine akakuambia ameiona bilauri imejaa maji lakini imejaa maji nusu. Kwa hiyo, yupo atakayekuambia haina maji nusu lakini yupo atakayekuambia ina maji nusu. Kwa hiyo, ni namna ya mtazamo tu kila mmoja anakusudia kulitazama jambo kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kapufi. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwenye kitabu hiki cha Mpango, ukurasa wa saba ambapo anasema, mwenendo wa uchumi unaashiria kuendelea kuimarika kwa uchumi na utoaji wa huduma za jamii unaboreka. Ndiyo maana kukawa na hoja kwamba ingelazimika tukapata tathmini ya kipindi kilichopita kwa muda huu tulionao ili tuweze kujua mwelekeo. Hii kauli inachanganya sana wananchi wa kawaida na hata mimi mwenyewe. Ukiangalia hali halisi ya kiuchumi ilivyo, ukitembelea maduka mitaani, wafanyabiashara mbalimbali wanalalamika na hata sisi wenyewe Wabunge tunalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana imeelezwa kwamba imefikia hatua hata kwenye Kamati za Bunge unapewa maji moja ndogo kuanzia asubuhi mpaka jioni. Pia ukipewa chakula kimepangwa unasimamiwa usije ukazidisha vipande vitatu ni viwili tu, maana yake inawezekana ukizidisha utashikwa mkono. Hiyo maana yake inaashiria hali ya kiuchumi ni ngumu lakini kwenye vitabu wataalam wetu Mheshimiwa Dkt. Mpango na wenzake wanasema hali inaimarika na huduma za kijamii zinaboreshwa. Kwa hiyo, naomba hata atakapokuja kuhitimisha hoja ambayo mimi siungi mkono, basi atueleze angalau kinaga ubaga na kwa lugha ambayo tutaweza kuelewa anamaanisha kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niunge mkono hotuba nzuri sana ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani Bungeni. Niseme Waziri yeyote makini tukitoka hotuba hapa ni muhimu akapitia kile tunachokisema kwa sababu takwimu ambazo zinatolewa na sisi upande wa Upinzani hatuzipiki sisi bali zinatoka kwenye nyaraka mbalimbali Serikalini humohumo. Kwa hiyo, tunapotoa hotuba hapa siyo kuibeza na mimi ningekuwa ninyi ningekuwa mjanja sana kwa sababu mngekuwa mkisema naenda kuyafanyia kazi ili *next time* mkose hoja. Badala yake mnaweza kukaa hapa miaka mitano mnaambiwa mambo yaleyale ukirudi unatoa siasa, unapiga story, unapiga porojo, miaka inaenda na

huboreshi. Kwa hiyo, kimsingi unakuwa hufanyi lolote lile. Hoja ikitolewa iangalie na kama ina ukweli ifanyie kazi na kwa kufanya hivyo utakuwa unalisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia hiki kitabu, mimi nitajikita kwenye kitabu hiki kilichoandikwa, ukurasa wa 66 – 67, Waziri mwenye dhamana amezungumzia utawala bora na utawala wa sheria, lakini nilipoangalia utawala bora alioandika hapa alikuwa anaandika kuboresha majengo na kuongeza polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoelewa utawala bora angeeleza hapa kwamba mpango wa Serikali ni pia kuheshimiana katika maeneo yetu ya kazi. Kwa sababu kwa utawala huu ambao mnauita utawala wa Awamu ya Tano na mnakwepa kusema utawala wa Chama cha Mapinduzi mnataka watu waamini kwamba miaka inatofautisha matendo yenu, ndiyo maana mnahimiza sana utawala wa Awamu ya Tano, sema Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Watanzania wajue ni ileile hakuna jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hali ya sasa ambayo unataka kuboresha elimu lakini Mwalimu huyu ambaye anadai na hapa katika kuboresha elimu sikuona unaboresha namna gani, wapo Walimu ambao wanadai madai yao tangu mwaka 2012 mpaka leo. Ili uboresha elimu lazima Walimu walipwe madai yao, wapandishwe vyeo, walipwe likizo na malimbikizo yao ili migogoro iishe. Huwezi kuboresha elimu kwa maana ya majengo wakati Walimu wanadai na Walimu haohao Wakurugenzi ambao mnawateua makada wa CCM wanawaambia wapige deki mbele ya wanafunzi halafu unasema unataka kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unazungumzia utawala bora mahali ambapo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu anaagiza eti kuanzia leo Walimu wote nimewashusha vyeo, huo ndiyo utawala bora kweli? Sasa hapa hamzungumzi, mnazungumza habari ya kujenga majengo, haya mambo lazima tuzungumze ukweli. Sasa mnapotuanjikia, sisi siyo wajinga, tunaweza kusoma mnachoandika na kuchanganua, lazima mtueleze utawala bora maana yake ni nini? Sasa hivi hali iliyofikia watu hawaheshimiani yaani unakuta Rais ameagiza kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watumie ile Sheria ya saa 48, kwa hiyo, Mbunge kwenye eneo lake, Diwani kwenye eneo lake, Mwenyekiti wa Halmashauri au Mstahiki Meya anaweza akaambiwa kamata weka ndani, unasema huu ndiyo utawala bora halafu unataka upewe ushirikiano katika eneo hilo. Kwa hiyo, nashauri wahusika wa haya mambo lazima waangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuhusu utawala wa sheria, sasa hivi kinachotawala Tanzania wala siyo sheria ni amri mbalimbali, sheria wala haifuatwi. Bahati nzuri Waziri wa Utawala Bora ndiyo alikuwa mpiga kura kule Kinondoni kwenye uchaguzi wa Meya, walikuwepo hawa. Katika hali ya

kawaida inawezekanaje unafanya uchaguzi ambapo unajua idadi ya UKAWA ni nyingi kuliko Chama cha Mapinduzi na Naibu Spika ambaye ni mwanasheria tena alikuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali amehusika kuchakachua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inasema wateule wa Rais hawatazidi watatu katika Halmashauri lakini mlichokifanya mlipoleka watu wanne pale Kinondoni. Sheria inasema ni lazima mahudhurio yaandikwe, akidi ni mbili ya tatu (2/3), haikutimia hakuna mahudhurio. Watu wa CCM mlikuwa 18, tena viongozi mmekaa pale mkapiga kura mkajiapisha halafu unaandika makaratasi hapa utawala bora wa kitu gani, unamdanganya nani hapa? Huu ndiyo utawala bora kweli, huu ndiyo utawala wa sheria? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wasomi, Mawaziri, Maprofesa, Wanasheria, Naibu Spika na wenzenu, Mawaziri wazima hata aibu hawana, tena Waziri wa Elimu ambapo Waziri wa Elimu alikuja kupiga kura Ilala. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Mheshimiwa Profesa Ndalichako mama yangu na mtani wangu ambaye namheshimu sana alikuwepo ameletwa kujiandikisha kupiga kura Ilala halafu tena akakubali kubebwa mzobemzobe anashinikizwa kuja kupiga tena kura Kinondoni, wewe unafanya kitu gani kweli? Hata aibu hamuoni?

MBUNGE FULANI: Aibu!

MHE. MWITA M. WAITARA: Aibu sana kwa Chama cha Mapinduzi, chama kongwe, ndiyo maana mnaitwa chama kizee. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Acha kulia.

MHE. MWITA M. WAITARA: Hata busara na hekima inapotea. Sasa hapa utawala bora mnaozungumzia ni kitu gani? Tangu mmeanza kufanya uhuni katika nchi hii mimi kwa kweli nimekuwa *confused*.

MBUNGE FULANI: Acha kulia.

MHE. MWITA M. WAITARA: Ndiyo maana mnachofanya hata hapa kwenye elimu ni maigizo, tumegundua mtaji wenu katika nchi hii ni ujinga.

MBUNGE FULANI: Unalia nini?

MHE. MWITA M. WAITARA: Ndiyo maana mnavuruga elimu makusudi. Rais amewaambia Watanzania yeye hatakubali mtoto wa maskini asiende chuo kikuu atawakopesha, Waziri anasema ataangalia bajeti ilivyo sasa nani mwenye kauli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza habari ya afya hapa, Makamu wa Rais anasema dawa hakuna Waziri anasema dawa zipo tele na jana Naibu Waziri amethibitisha, akasema tumwonyeshe, tumemwambia tumpelekee nyumbani kwake akakataa. Sasa haya mambo ukisoma kwa kweli, mimi vitabu vyenu huwa navisoma sana, nipo tayari nisilale usiku lakini navisoma sana, lakini mnatuchanganya sana, kwa nini msilandike ukweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akija hapa Waziri wa Viwanda atapiga ngonjera zake utamwona huyu ndiyo mwanaume ametoka Bukoba wengine hawapo kabisa. Akiimba hapa ngonjera zake utashangaa, sasa nenda kwenye hali halisi, yote haya hamna. Anafukuzwa na Kamati yake kwamba mzee umeandika makabrasha mengi, pesa hakuna, Kamati ya Viwanda inasema hujafanya lolote, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda acha kuimbia watu ngonjera. *General tyre* mpaka leo haijaanza, watu wanataka kuona mnaleta tena *story* zilezile. Kwa kweli hii habari inatusumbua sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kuhusu hii habari ya mifugo, Wabunge wengi wanakaa Jimbo la Ukonga na Dar es Salaam kwa ujumla, hata kama mtu hakai ana kibanda pale lakini Dar es Salaam hakuna machinjio ya kisasa. Kuna machinjio ndogo kweli kweli pale Vingunguti na yale mazizi ni ya mtu binafsi siyo ya Serikali. Pale Zingiziwa kuna ekari zaidi ya 120, kama mkiweka mifugo pale na kuna mnada wa Kimataifa wa Pugu ambao kimsingi na wenyewe ni jina, ni mnada lakini ni kijiwe cha ng'ombe, hakuna maji, hakuna chochote pale, ukiboreshwa utasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ndiyo kuna Mawaziri, ndiyo ipo Ikulu lakini hakuna nyama safi, watu wanaweza kuchinjia vichochochoni wakauza mitaani, sijui kwa nini hampangi haya na maeneo yapo, hapa sikuona chochote kwamba mnaboreshaje suala hili. Dar es Salaam kuna watu wengi na wageni pia lakini suala hili haliwekewi mipango. Mbona mmesema tupande miti ili Jiji lipendeze Wazungu wafurahi, tengenezeni basi na mazingira mazuri ya kuchinjia nyama kwa afya zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme habari ya maji. Watu mikoani wanalia, lakini nawaambia hata Dar es Salaam kule Jimbo la Ukonga katika kata 13 ni kata moja au mbili zinaweza zikawa na uhakika wa maji na visima vingi zaidi ya asilimia 90 ni watu wamechimba wenyewe. Mheshimiwa Dkt. Mpango anakaa Zingiziwa pale Nzasa, yeye ni mpiga kura wangu kule, tupange siku moja aende Zingiziwa aone wale watoto na wazazi wa pale maji ambayo wanakunywa, Dar es Salaam acha kule kwao Kigoma, Dar es Salaam, maana anavyoandika hivi vitu twende kwa ushahidi aende aone, hajaandika chochote hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; Jimbo la Ukonga lina wapiga kura zaidi ya laki sita na kata 13. Watu wote wale kutoka Zingiziwa, Chanika, Msongola, Mvuti, Uwanja wa Nyani wanakuja Amana. Tuna eneo kubwa ekari 45 kwa ajili ya kujenga hospitali na tangu mwaka jana niliwaambia kwamba ile hospitali ikijengwa itasaidia mpaka na Kisarawe mpaka Mkuranga. Halmashauri ina uwezo wa kutenga shilingi milioni moja kwa mwaka na gharama yake ni shilingi milioni 26 maana yake Halmashauri ikiachiwa ijenge itatumia miaka 26 watu wanasubiri huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda anapopanga zahanati, kituo cha afya na hospitali ataje majina ili Mbunge ajue zamu hii ni ya Msigwa, zamu ijayo itaenda labda Kwimba na sehemu nyingine, tuwatajje, asiweke kwenye *bracket* hapa. Aseme anataka kujenga hospitali ipi, zahanati ipi ili tujue kama siyo zamu yangu nisubiri mwaka ujao na akiandika atekeleze, aache kutuambia ngonjera hapa. Mlishatuambia tutaisoma namba, tutaisoma wote pamoja, bahati nzuri hatuisomi wenyewe na nyie mnaisoma sana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Shirika la Ndege amelizungumzia, nataka nihoji hapa, tuna taarifa kwamba Chato kwa Mheshimiwa Magufuli pale nyumbani kwao Chato unajengwa uwanja wa ndege, mbona kwenye mipango hapa hiyo hela haipo? Bajeti iliyopita haikutajwa na hii hapa haijatajwa lakini unajengwa uwanja wa ndege kule Chato. Tunaomba tujue hiyo bajeti ya kujenga uwanja huo iko wapi mbona hapa kwenye mipango hamuutaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mtuambie, hivi Chato kujenga uwanja wa ndege, sawa kweli wale ni watani na wakwe zangu, hivi kule Chato mtafanya biashara gani, *projection* ni nini pale? Yaani mnataka mjenge uwanja wa ndege ili Mheshimiwa Magufuli akitaka kupumzika aende na ndege nyumbani kwao? Kujenga uwanja wa ndege ni lazima kuangalia *economic zone* kwamba biashara itafanyika kwa sababu *population* ni kubwa na vitu vya namna hiyo. Haya hata hapa hamuonyeshi, sasa hiyo siyo siri tunajua. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Kama Mobutu.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kumekuwa na malalamiko ya ndege mlizonunua, mimi siyo mtaalam, ndege zenyewe ni *Bombardier*?

MBUNGE FULANI: *Bombardier*.

MHE. MWITA M. WAITARA: Wanasema mikataba duniani mnalipa kwa *advance* nyie mmeenda kulipa kwa bei ya jumla. Mmechukua hela zote mkaenda kununua ndege kwa mbwembwe, eti mnazindua kununua ndege, hivi kweli nyie mnaumwa, unazindua kununua ndege? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karne ya 21, Serikali ya Chama cha Mapinduzi zaidi ya miaka 50, umri wa mtu mzima yaani miaka ya chama chenu inanzidi mimi Waitara, Mbunge wa Ukonga hebu niangalie halafu mnasherehekea kununua ndege. Muangalieni mwenzenu Kagame, ndege ya kwanza aliyonunua na mambo anayofanya. Ameleta ndege ambayo inaendesha kwa mitambo, *shabash*, nyie mnapiga makofi hapa! Wabunge wanasimama hapa hoja ambazo hazina maana eti anaunga mkono ili asisahau maana wamezeeka halafu wandalamika, mambo gani haya bwana? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme. Mimi ni Mbunge wa Ukonga, ukienda Kata ya Msongola, robo tatu ya kata hakuna umeme. Kivule ina mitaa minne, mitaa miwili ndiyo ina umeme. Ukienda Zingiziwa kuna mitaa nane ni mtaa mmoja tu wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndiyo kuna umeme. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Chanika kuna mitaa nane, miwili ndiyo ina umeme. Ukienda Pugu kuna mitaa mitano, mitatu ndiyo ina umeme miwili haina umeme. Ni Dar es Salaam hiyo sikutaja majimbo mengine ya Kigamboni na kadhalika na mnasema ule ndiyo mji ambao una *population* kubwa, ndiyo mji wa kibiashara, ndiyo Rais yuko pale lakini umeme ni shida. Kule mnatoa matamko kushughulikia watu kwenye vikao, kupindishapindisha na kuiba kura za Kinondoni, mnatangaza Meya hewa, mmeleta Meya hewa pale wakati nyie mnatafuta wafanyakazi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Waziri anayehusika ashughulikie suala hili ili umeme isiwe wimbo Dar es Salaam. Watu wanakaa Dar es Salaam kwa maana ya majina lakini akimwambia mtu amtembelee anamzungusha mjini anamkimbia kwa sababu akienda nyumbani kwake hatafanana na mbwembwe alizokuwa anasema. Kwa hiyo, tunahitaji suala hilo lishughulikiwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mimi nimshauri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara muda wako umeisha tafadhali naomba tu ukae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Haya basi siungi mkono hoja mimi. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Flatei Massay akae tayari.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia. Jambo la kwanza, ningependa kumwomba Waziri wa Fedha asirudie aliyoyafanya wakati analeta Mpango wa Mwaka 2016/2017. Tutakayomshauri *a-take into consideration* kwa sababu hii nchi ni yetu sote. Nchi hii siyo *ya executive only*, ni nchi yetu sote Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nishauri, ndugu zangu wa UKAWA, nimesoma hotuba aliyoisoma dada yetu Mheshimiwa Halima, kuna *a lot of constructive issues*. Hii nchi ni yetu sote, mkisema viwanda kizungumkuti kwa maana ya zile *abusive language* mnatufanya na sisi tuwe *defensive* na kusahau *content* mliyoweka ambayo ina *substance* kwenye maendeleo ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii iki-*develop* wote tuna-*develop*. Kuna mambo mengine mnasema ni ya msingi sana lakini inatufanya tu-*defend* kwa sababu ya lugha inayotumika. Nimemwambia nje na nasema humu ndani ili iingie kwenye rekodi. Linapokuja suala la Mpango wa nchi tuweke siasa pembeni tujadili Mpango wa nchi. Waziri wa Fedha asipochukua yale tunayoamini ni kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu tuna jukumu la kuungana bila kuangalia vyama vyetu, hili ni jambo la pili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa masikitiko, *premises* alizoziweka Waziri wa Fedha kwa ajili ya msingi wa bajeti anayokuja nayo ni *premises* ambazo zinatujengea *failure*. Ukienda ukurasa wa 14, *item 2.3.10*, ametaja *item* kama saba ambazo ndiyo msingi wa Mpango na bajeti ya 2017/2018, hii ndiyo *pillar*. *Item* ya mwisho anasema, kuwepo kwa sheria na taratibu wezeshi kwa uwekezaji. Ukiangalia taarifa ya Kamati, *World Bank Report* inatu-*rank* ni wa 139, *doing business in Tanzania is very difficult*. Ni jukumu lake Mheshimiwa Waziri akaangalie sheria za nchi hii kama zina-*attract investment*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *item number five* anasema, hali ya hewa ya nchi na katika nchi jirani ni nzuri, *which is not right!* Hali ya hewa ya nchi kwa mwaka 2017/2018 tuna-project kuwepo kwa ukame. Nchi zilizotuzunguka zina hali mbaya ya chakula, taarifa ya TMA inaonesha kwamba kutakuwa na ukame, yeye anasema itakuwa nzuri, *we are failing!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea kusema, kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia, Mheshimiwa Waziri anatoa wapi hii *fact? Global trade* imeteremka by 0.08! Siyo maneno yangu, ni ya *World Bank*, ni ya *IMF* yanaonesha na uki-google report ya *World Bank* ya tarehe 20 Oktoba, 2016 inasema wazi kwamba bei ya mafuta duniani inapanda, Waziri anasema itaimarika. Tulivyopitisha bajeti iliyopita na bajeti hii mafuta yamepanda kwa zaidi ya *dollar 10!* Kaka yangu anasema unaimarika, *this is very bad!* Hii nchi ni yetu sote, tulisema kwenye mpango wa mwezi Februari, tukasema sana kwenye bajeti, yale yote tuliyomshauri humu ndani akaja akatuona humu ndani Wabunge wote hatuna akili, leo tunaathirika kama nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii ya Waziri ya Mapendekezo ya Mpango inazungumzia *growth* ya biashara yetu ya nje by 7.4, *very good!* Kataja mazao, katani, tumbaku na nyuzi, nimechukua hii *document*, nimeangalia kwenye *agro sector*, hakuna sehemu anapanga kuongeza uzalishaji na ku-invest kwenye hizi bidhaa ambazo zimetuingizia fedha, *what is this?* Anachosema huku na Mpango wake havifanani! Kaka sisi Chama cha Mapinduzi tumewachidi wananchi, au kwa sababu kaka yangu hajaenda kuomba kura? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CEO wa Nokia wakati imekuwa *taken* na *Microsoft* alisema, *we did not do anything wrong but somehow we lost*, sisi tuko excited na *historical fact*, *the world is changing!* Tusipobadilika *we are going to perish*. Soma Mipango, Liganga na Mchuchuma mimi sijaja Bungeni naisikia, iko chini ya NDC, hebu jiulizeni kwenye Mipango, NDC toka lini inapelekewa fedha na nchi hii na mnitajie *subsidiary* moja iliyo-succeed NDC, *nothing!* Hakuna *subsidiary* iliyo succeed! Nashindwa kuelewa *what are we thinking?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anazungumzia, Mungu huyu! Waziri anazungumzia 32, 33 *trillion shilling budget*, area ya kwanza ni makusanyo ya kodi kuongezeka kwa 16%, maana yake tuna mpango wa kwenda kuongeza kodi na mzigo kwa wananchi by 16%. Tuliwaambia msiweke kodi kwenye *money transfer* hamkutusikiliza, tuliwaambia msiweke kodi kwenye *tourism* hamkutusikiliza, tuliwaambia msiweke kodi kwenye maeneo mengi, mnajua matokeo yake? *Quarter* iliyopita *commercial banks* zimeshuka *profitability* by 94%. *Implication* yake ni moja, *income tax* itakuwa chini, *excise duty* zitaporomoka, *there is no hope!* (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ninachotaka kushauri? Moja, Dkt. Mpango kaka yangu, *I respect your academic background; kodi should not be your target* kwenye kila jambo. Haina maana kuweka kodi kwenye kila kitu, kwenye maeneo yale yale *we are killing the business*. Tutumie *strategic location* ya nchi, nataka nitoe mfano mdogo, *it's not a rocket science*, Dubai ime-grow because *of airport*, tuna *best location* hapa lakini *one of the expensive landing* katika dunia hii ni Tanzania, futeni kodi kwenye viwanja vya ndege, fanyeni *this is the hub, we will grow!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnaleta *issue* ya Kurasini kutengeneza gulio la Wachina mnaua Kariakoo. Maana yake Wachina waje pale waweke bidhaa zao halafu iwe ni *free tax* kuziweka pale halafu ikitoka ndiyo tuchukue kodi, hatuna hizo *control mechanism!* *If you want to establish a free market with zero tax* fungueni soko la Kariakoo waacheni Waswahili wale wauze pale ikitoka tukusanye kodi! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumekuwa wakusanya ushuru wa Kongo...

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Muda umekwisha?

MBUNGE FULANI: Bado endelea.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uwezo wa kutengeneza fedha sana, alisema kaka yangu kwenye Bunge lililopita, Mbunge wa Kahama tuanzisheni soko la madini, yeyote atakayeleta madini yake hapa Tanzania aingize bure, yakiuzwa yakitoka tutapata kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu *agro sector*. Nataka niwaambie, tunazungumzia kwamba tunataka kuondoa umaskini, kama hatufikiri sawasawa kwenye kuwekeza zaidi kwenye sekta za kilimo na uwekezaji wetu wa viwanda ukagusa maeneo ya kilimo *there is no way* tutapambana na umaskini wa nchi hii. Hapa nimesikia Wabunge wanalalamika dawa hamna, Wabunge wanalalamika kuhusu mikopo, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mimi natoka Kamati ya Huduma za Jamii, Kamati ya Guantanamo, ndiyo inayosimamia Sekta ya Elimu na Afya, mtamtoa roho Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla bure, mtamtoa roho Mheshimiwa Ummu, mtamtoa roho Mheshimiwa Profesa Ndalichako, *MSD, if we will not rectify our economy* hatuwezi kuondoa matatizo ya afya. Sasa kama Wabunge tunataka kweli kusaidia Serikali tu-deal na Wizara ya Fedha. *That is the only solution!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Fedha ha-cherish *private sector*, wanasheria wanajua kuna kitu kinaitwa *law of negligence*, huwezi kwenda Kariakoo umeshika burungutu la shilingi milioni 10 unatembea halafu watu wakichukua ulalamike. Tuliacha milango yetu wazi muda mrefu, wafanyabiashara wakatumia *opportunity*, wakavuta, leo kwa uzembe wetu uliowa-attract wao kukwepa kodi na wizi mwingine ulikuwa *masterminded from the Government, it is true!*

MBUNGE FULANI: Sema.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: *This is the naked truth.* Kwa nini mpaka leo *mindset* ya Serikali na Wizara ya Fedha ni kwamba *business community* ni wezi? *No one will come to our market.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwape mfano mwingine, Waziri anasema uchumi umekua kwa asilimia 6.7 katika kipindi cha miezi sita ya kwanza na moja ya eneo ambalo limechangia kukua huko ni *minerals*. Mimi najjuliza sana na nashangaa taarifa zake, najjuliza kuna tatizo Serikalini? *Production* ya *Tanzanite* imeshuka by 50% toka tumewauzia wale wahuni ule mgodi, hiyo *growth* inatoka wapi? Tunasema fedha imekua, imekua kutoka wapi wakati wana-*register losses*, *private sector can not access loans from the financial institution* na siyo kwa sababu hawana hela ni kwa sababu hakuna *security* sokoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo biashara zina-*collapse* nchi hii, leo mabenki yanapata hasara. Nataka niitahadharishe Serikali, *if we will not be careful* na Waziri wa Fedha usipofanya *intervention* kwenye *financial institution*, *real estate is going down* na wengi waliokopa watahondwa kulipa, tutaingia kwenye matatizo. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Bashe muda wako umemalizika.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum na baadaye Mheshimiwa Balozzi Dkt. Kamala ajiandae.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendeleza pale alipoishia Mheshimiwa Bashe, Waheshimiwa Wabunge wa CCM tusipokuwa wakweli hii ni Serikali yetu, ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tusipomwambia ukweli Waziri wa Fedha tunakwenda kugonga mwamba. Leo tunapoongelea uchumi kuna tatizo la mzunguko wa fedha ndani ya nchi yetu, unajiuliza fedha zimekwenda wapi? Halafu unakuja hapa unasema uchumi mzuri, sijui nini, *how!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mabenki yanaanza kufilisika, Twiga tayari imeshakuwa *taken over*, CRDB tayari imeshapata hasara, TIB tayari imeshapata hasara maana yake nini? Maana yake ni kwamba hizo benki *projection* ya mbele kule miaka miwili, mitatu zinakwenda kufungwa, inakuwa *another crisis of Tanzania*. Waziri wa Fedha amekaa tu anatazama hali hii! Waheshimiwa Wabunge, mabenki yakifungwa na huku yametoa mkopo *businesses* hazirudishi mikopo, hebu angalia *crisis* na tatizo la uchumi wa ndani ya nchi litakavyokuwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mheshimiwa Bashe inawezekana hawa hawakwenda kuomba kura hawaelewi joto la wananchi kule. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. AHMED A. SALUM: Sisi ndiyo tunakwenda, ndiyo *frontline*. Tatizo lingine unaweza kuwa umeteuliwa na Mheshimiwa Rais, basi kule kuteuliwa tu unajiona wewe bora kweli, hapa lazima useme kweli! (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Jimbo la Solwa, tuna ahadi tumeahidi na kesho nina swali hapa tutabanana tu na TAMISEMI, unakwenda unaongea, unadanganya mpaka unachoka, yapo mambo unachoka kudanganya! Ameahidi Kikwete ameondoka, amekuja Pinda ameondoka, anakuja Magufuli ataondoka na baadhi ya miradi haitawezekana kufanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri, fedha ambazo mmezichukua za hizi *parastatals companies*, haya Mashirika ya Hifadhi ya Jamii mmekwenda kuziweka kabatini BOT, warudishieni wenyewe wazifungulie akaunti kwenye *commercial banks*, waachie wenyewe iwe ni kama *another income of their source*. Zile fedha wao watapata, benki zitaendelea kuzitumia ku-lend kwa *customers*, uchumi kidogo utaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipe madeni ya ndani ili fedha zianze kuzunguka sasa hivi kuna joto. Leo Wabunge si mnaona hapa, jana mlikuwa mnaongea sijui nini, hata Bunge hapa ukata mtupu kwa kwenda mbele. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa CCM. Tukienda kwenye *party caucus* tukafanye maamuzi kweli kwa sababu ya nchi yetu na Serikali yetu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine, wakati ule niliwahi kumshauri Waziri wa Fedha nikasema Mawaziri watakuwa wanafanya kazi kwa matukio, unasubiri tukio likitokea unaenda ku-*deal* nalo kwa sababu hatuna *Department ya Research and Development*. Tunaweza tukaanzia na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Miundombinu ili *research* zile zijulikane kwenye sekta ya viwanda na Serikali kwa ujumla wake. Ukiweka juu ya meza unakuja hapa na mpango wako yako mambo ya kubadilisha sheria, ya kurekebisha sera matatizo haya yote yatapungua na wananchi watapata ahueni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Japan mwaka 1980 waliweka 2% ya bajeti yake kwenye *R&D* yaani unafanya utafiti wa sehemu gani tumekosea, tufanye nini, tuboresha nini ili uwekezaji ukipita pale uweze kunufaika. Australia 1.5 mwaka 1982 ya bajeti yake na ndiyo iliyowapeleka mpaka leo nchi zile zimeweza kuendelea. Leo unakuja na Mpango umeutoa wapi, umefanya *research* gani? Tutabaki tunahangaika na tunalalamika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikwenda kwenye Kamati ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara walikuja wawekezaji wa nchi nzima, wawakilishi kutoka Bakhresa, Mohammed *Enterprises*, wafanyabiashara wengi walikuja na kila aliyesimama analalamika, halafu unasema Tanzania ya viwanda, halafu unasema Magufuli ataweza kuleta viwanda, ukiwasikiliza wale wanavyolalamika, ukiona sera na sheria zimepitwa na wakati hatuwezi kufika. Kama ni viwanda kwa *style* hii hatuwezi kufika kwa sababu kuna mambo ya kurekebisha kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIC, One Stop Center*, ukienda pale hakuna cha *One Stop Center* kuna *Many Stop Centers*, unaweka *document* yako pale hakuna maamuzi, *documents* zinachukuliwa zinaenda *TRA, TRA* pale wiki mbili tatu, mwezi irudi, unangoja *certificate* umalize pale, maamuzi yanachelewa, kila mtu hana maamuzi. Tatizo ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu viwanda. Tukitaka tu-*win* kwenye viwanda sheria lazima ibadilishwe baada ya kufanya utafiti wa kina. Kuna tatizo kubwa sana *TBS*, kuna tatizo kubwa sana *NEMC* na siyo

kwamba wao ni tatizo, tumechukua sheria za nje, tumezi-copy tukazi-paste kwetu, imekuja kwenda tofauti na uhalisia wa wawekezaji ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii wawekezaji watakaoweza ku-win vizuri wale wanaotoka nje, wakubwa, anakuja na dola milioni 50, milioni 200, wale ndiyo watakuja kuimeza nchi hii. Mkitaka Watanzania waweze kuinuka kwa sheria tulizokuwa nazo, kwa watendaji ambao wanafanya kazi kwa mazoea bila kuwa na mfumo rasmi, bila kubadilisha mfumo na sera ya nchi nzima, hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikimwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha alete taarifa ya kodi wanazokusanya kuachana na *arrears*, kama mtu alikuwa ameuzua gari nane au kumi, unamwambia bwana kuna gari 10 uliuzua lipa hizo hela, sisi tunakutambua wewe kwa sababu hiyo gari ulinunua kwa jina lako na *TIN number* yako, unabebeshwa mzigo siyo wako. Sasa ile itafika mahali itakwisha, itafika mahali *arrears* zitakwisha utabaki na *cash revenue* ya siku hiyo, hapo ndipo utakapoona kutoka 1.5 trilioni inashuka inakuja mpaka kwenye bilioni 800 ambapo Rais Kikwete ameichacha hiyo. Rais Kikwete ameichacha bilioni 850 nchi ilikuwa nzuri mambo yanaenda raha kwa kwenda mbele. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magufuli ana *vision* kubwa ya nchi hii anatamani nchi hii itoke tufanane kama Thailand walivyotoka. Hata hivyo, ninavyoona tatizo ni wasaidizi wake ama mnamwogopa au hamumwambii ukweli, mnaogopa kufukuzwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magufuli tumefanya naye kazi hapa miaka kumi, mimi nimefanya naye kazi namfahamu, ukienda na *data* vizuri ukamwambia Mheshimiwa Magufuli kwa tatizo la bandari kuna mambo mawili, mimi nataka niongelee kukimbiwa na wafanyabiashara wa nchi jirani sitaki kuongelea mizigo ya ndani ya nchi, kuna vitu viwili pale...

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniongezee muda. *(Kicheko/Makofi)*

WABUNGE FULANI: Endelea.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa muda bado.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni kengele ya kwanza hiyo.

MBUNGE FULANI: Endelea na ongeza kasi sasa.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kukimbiwa na wafanyabiashara kutoka Zaire, jana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu anajibu kana kwamba yeye ni Waziri wa Zaire ndani ya Bunge la nchi hii. Anasema sisi tumeweka ofisi pale ili Wazaire wawe wanalipa ushuru pale kwa sababu wao wanakwepa ushuru inatuhusu nini mambo ya Zaire sisi humu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwawekea ofisi Wazaire walipe ushuru pale ndiyo iliyowakimbiza. Rais Kabila amekuja hapa kwa Magufuli kama alikuwa anataka Wazaire walipie ushuru hapa angeshindwa? Wangeweka sheria pale Bungeni kwamba mizigo yote isipotoka bandari ya Dar es Salaam haingii Zaire lakini yeye ndiyo amewa-encourage akasema nendeni Mombasa, nendeni kule Beira halafu hamuelewi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaambia bandari yetu inakufa kwa sababu ya mambo manne, naongelea mizigo ya *transit* siongelei mizigo ya ndani naomba mnielewe hivyo, tunapoteza *revenue billions of money*. Sababu ya kwanza ni hiyo *Single Custom Territory*, toa hiyo! Ya pili ni *VAT on transit goods*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongelea kontena moja moja huwezi kuipata kuna meli kama Impala analeta meli tano mpaka sita, akishusha meli yake pale malori 10,000 yanapakia miezi mitatu yanakwenda lakini leo tunamweleza haelewi. Kenya hawana VAT wamesoma sheria zetu, Mozambique wamesoma sheria zetu wameona Watanzania hawa hawaelewi kitu wapo hivi, wao wakaondoa VAT, sisi siku saba tunawapa *free* wao wameweka siku 90, sijui *Single Custom Territory* wametoa, *check point* sisi tunazo sita wao wameweka mbili, tayari wao wamekuwa kwenye *advantage*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakosa mapato, hoja hapa tunakosa nini?

WABUNGE FULANI: Mapato.

MHE. AHMED A. SALUM: *Billions of billions* zinapotea. Bandari hii ingefanyiwa kazi vizuri ina uwezo wa kuingiza shilingi trilioni tano kwa mwaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Singapore in and out containers* milioni 30 kwa mwaka, Dubai milioni 27 sisi 500,000 aibu! Jiografia yetu imekaa vizuri tu, jamani bandari muifanye kama *private sector*, *one of the objective of the business is to make profit*, bandari ibadilishwe mfumo ikae pale kama *private sector* kwa ajili

ya kuleta mapato kwa Serikali yetu. Sasa leo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaenda anawabana watu mpaka hawa wenye bodaboda anaenda anawabana anaacha mapato yale, mapato bandarini shilingi trilionni tano anaacha anaenda kubana bodaboda kwa Sh. 50,000 au Sh.100,000 ni nini hii? Waheshimiwa Wabunge tuna vikodi vidogo vidogo vingi sana na ni kero katika nchi hii sasa hivi. Leo hapa *traffic* wanakamata magari kama kuna vita, ukikamatwa Sh. 30,000, kundi la madereva ni hatari kwenye kura za CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba inajiri zaidi ya watu milioni 16. Mimi natoka kwenye Mkoa wa Shinyanga, nimeongea nadhani nimeelewewa, Waziri wa Fedha asiponelewa safari hii itakula kwake baadaye. Sisi ni Wabunge wa CCM kule tutafanya maamuzi magumu tu, hatuwezi kuiacha nchi hii inayumba, nchi imeyumba tuseme ukweli. Kwa sababu tukianza kufichaficha hivi tunamficha nani? Sisi ndiyo tunajua 2020 tutashinda, hatuna tatizo lakini lazima sisi wenyewe turekebishe humu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamba leo inajiri watu milioni 16, mimi natoka kwenye Mkoa wa Shinyanga, tumeongea viwanda, Serikali itafute wawekezaji, sasa hivi Mheshimiwa Magufuli kwa nia njema tu ametaka haya mashirika yetu ya umma yaingie huko, sasa kama kuna mpango huo, niombe mashirika hayo yalete viwanda kwenye Mkoa wa Shinyanga, viwanda vya nguo vikubwa. China na India kiwanda kimoja cha nguo kinanunua pamba yote ya nchi hii, tunataka viwanda vya aina hiyo. Kiwanda kimoja kiweze kununua pamba yote ya nchi hii na kiweze kutengeneza uzi na nguo na ku-add value ili sasa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahmed muda wako umemalizika.

MHE. AHMED A. SALUM: Ili sasa kutengeneza soko la uhakika kwa wakulima wa pamba wa Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ahmed kengele ya pili hiyo muda wako umemalizika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa namkaribisha Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami ningeungana na wenzangu kuzungumza kama walivyozungumza. Hata hivyo, kwa kuwa tetemeko lililoanzia jimboni kwangu

bado linatetemesha na bado linamtetemesha na Mbunge mwenyewe kwa hiyo naomba nijikite kwenye tetemeko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu tarehe 10/9/2016 saa tisa na dakika 27 mchana katika eneo lililo kilometa 27 Kaskazini Mashariki mwa Nsunga kulitokea tetemeko kubwa la ardhi. Eneo hilo si pengine bali ni Wilaya ya Misenyi katika Kata ya Minziro, Kitongoji cha Murungu B. Tetemeko hilo lilileta madhara makubwa na madhara hayo yameelezwa na Waheshimiwa mbalimbali waliochangia katika Bunge hili na viongozi mbalimbali walitembelea eneo hilo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda niseme machache kwamba katika Mpango wa maendeleo tunaoupanga niungane na wale ambao wameshauri ingekuwa vizuri basi katika mpango huo tujipange pia jinsi ya kukabiliana na madhara hayo. Kwa mfano, katika Kitongoji cha Murungu pale tetemeko la ardhi lilipoanzia karibu nyumba zote zilienda chini. Kwa hiyo, matarajio ya wananchi makubwa waliyonayo ni kwamba, Serikali itaweka utaratibu mzuri na kuchukua hatua za kibajeti za kuwawezesha kuweza kujenga nyumba zao upya. Sasa linaweza kufanyika vipi, Waziri wa Fedha anafahamu Serikali inaweza ikatumia mbinu mbalimbali lakini hayo ndiyo matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya tetemeko la ardhi kutokea lazima tujifunze. Jambo la kwanza ambalo ni muhimu tujifunze, tujipange kwa changamoto kama hizo zitakazotokea baadaye. Kwa sababu kubwa lililojitokeza ni kwamba tulikuwa hatujajipanga vizuri kwa sababu hakuna aliyejua kwamba tunaweza kupata tetemeko la ardhi, sasa limejitokea ni vizuri tujipange kwa siku zijazo likitokea tuwe tumejipanga vizuri. Inapochukua zaidi ya wiki tatu kufanya tathmini ya tetemeko la ardhi inakuwa ni majanga ndani ya majanga. Kwa sababu hata yule ambaye angependa kukusaidia haji kukusaidia kwa sababu wewe mwenyewe hujui tatizo lililokukuta ni lipi na hujui unatakiwa kufanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tetemeko la ardhi kutokea ilitolewa taarifa kwamba utaratibu wa kukusanya michango utaratibiwa, ni jambo jema. Pia utaratibu wa kutoa matamko baada ya kutokea tetemeko la ardhi na wenyewe unahitaji kuratibiwa kwa sababu kila mtu anapokuwa anasema analofikiri linaenda kwa wananchi walewale, tunapeleka taarifa za kuchanganya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi mmoja mzito baada ya tetemeko kutokea alisema kwamba wananchi wasiwe na wasiwasi watawezesha kupata vifaa kama cement pamoja na mabati ili waweze kujenga, wakafurahia. Baadaye likatoka tamko lingine zito kwamba hakuna atakayetoa

vifaa vya ujenzi bali wenye uwezo waanze kujenga na wananchi wakaanza kutuuliza Mheshimiwa Mbunge mnasema wenye uwezo tuanze na je, wasiokuwa na uwezo mnawafanyaje, sikuwa na majibu kwa kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na mtaalam mmoja kiongozi akatoa kauli akasema tetemeko hili ni kubwa, tunafanya uchunguzi wa miamba, kwa hiyo msianze kujenga msubiri mpaka tukishajua miamba imekaaje huko chini ya ardhi. Mpaka leo nazungumza taarifa ya miamba ikoje chini ya ardhi haijatoka. Nayasema mambo haya kwa sababu tusipojipanga vizuri mbele ya safari yatatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia hata jinsi tulivyokuwa tukijitahidi kusaidia wananchi, nilienda kwa mfano upande wa Minziro kule nikakuta wananchi wengi walikuwa wanasaidiwa na wataalam wetu wa maafa kwa kupewa kitu kinaitwa *sheeting*. Wanasema nimefika pale nimekuta watu hawana nyumba, wataalam wanaeleza, tumetoa *sheeting*, *sheeting* ni turubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye kutembeatembea nikakuta maeneo mengine wana *tents* zimetengenezwa vizuri, nikawauliza nyie hizi mmetoa wapi? Wakasema jirani zetu hapa ambao ni ndugu zetu wametutolea hapa wanatusaidia kujenga na kila *tent* linajengwa kwa Sh. 70,000 na linakuwa limejengwa vizuri. Nikagundua kwamba wataalam wa maafa wa Tanzania wao wanachojua inapotokea maafa ni kugawa *sheeting* tu lakini hawachukui hatua kuangalia kidogo kwa wenzao wanafanya nini inapotokea matatizo kama yale. Si lengo langu kumlaumu mtu yeyote, lakini ni vizuri kujifunza ili siku zijazo tusirudie katika matatizo yale yale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia humu kwenye kitabu cha mapendekezo ya Mipango tunafikiri kwamba hali ya hewa itakuwa nzuri Afrika Mashariki lakini ukweli hali ya hewa si nzuri hata huko Kagera kwenyewe ninakozungumzia, kila mahali unapopita agenda kubwa ni ukame, kule Karagwe ni ukame, Misenye ni ukame na kila sehemu ni ukame. Kwa hiyo, matarajio yetu katika Mpango huu basi changamoto hizi za ukame zizingatiwe ili tuone tunaweza kufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yote mingi tuliyonayo katika kitabu hiki yako mambo mengi, wengi wetu huwa tunazungumzia fedha lakini tunalo tatizo lingine. Miradi mingi haitelezeki si kwa sababu ya fedha kutokuwepo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha alielewe hili, wakati mwingine fedha za kutosha zinakuwepo, lakini uwezo mdogo wa wale wataalam wetu tuliowapa majukumu kushindwa kusimamia hii miradi ni tatizo kubwa kuliko hata tatizo la ukosefu wa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili nitatumia mifano miwili, kwa mfano tunao mpango wa *SEDP* unaeleweka Wizara husika ilitoa zaidi ya shilingi milioni 790 za kuweza kujenga nyumba za Walimu katika shule za Sekondari za Kashenye, Bwanja, Nsunga na Kakunyu. Wakandarasi wamefanya kazi yao vizuri, shilingi milioni 709 zilishatolewa, lakini juzijuzi nilikuwa kwenye ziara nimefuatilia kwenye Halmashauri yangu wakandarasi waliojenga nyumba katika sekondari nilizotaja wamelipwa tu shilingi milioni 600 zaidi ya shilingi milioni 200 hazijulikani ziko wapi, viongozi wote hawajui lakini kazi imefanyika, sasa hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna tatizo la mradi wa maji katika Wilaya yangu. Kwa mfano, tuna mradi ya maji mikubwa, kule Ruzinga tuna mradi mmoja wa maji wa shilingi milioni 567, Rukurungo, Igurugati shilingi milioni 400, Bugango, Kenyana, Kakunyu ni mabilioni ya fedha lakini mradi yote hii ukitembelea unachokiona ni mabomba ambayo yanatoa hewa badala ya kutoa maji. Mabilioni ya fedha yametumika lakini hakuna maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano mmoja wa hadhara mtaalam mmoja akaniambia Mheshimiwa tumepata maji mpaka mabomba yamepasuka. Nikamwambia hongera nitakuja unioneshe mabomba yalivyopasuka. Nikamuuliza mabomba mliyotumia yakapasuka yako wapi? Akasema Mheshimiwa ni haya hapa. Nikamwambia bomba hili haliwezi kupasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mkutano tukachimba pale nikakuta bomba lililo ndani ya ardhi siyo kama lile alilionyesha kwamba walitumia. Nikamwambia mbona bomba ni tofauti, akasema Mheshimiwa unajua sikuelewa swali ulilouliza. Kwa hiyo, umefanyaje? Akasema tumetumia mabomba yaleyale ya zamani yaliyokuwepo. Kwa maneno mengine wale wana Ruzinga hadi leo hawajapata maji na zaidi ya shilingi bilioni 2.7 zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Waziri wa Fedha na kwa Serikali ni kwamba, tatizo siyo fedha tu, tatizo pia ni kuwa na wataalam ambao uwezo wao ni mdogo. Lazima jambo hili tuliangalie, Serikali itupe wataalam wenye uwezo, kama hawajaenda shule sawasawa wapelekwe shuleni, hata kama ni kuazima popote pale tuazime tunachotaka ni utekelezaji wa yale mambo tuliyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilijibiwa hapa kwamba siku za karibuni kule *Kajunguti International Airport* wananchi wataanza kulipwa fidia na niliambiwa hapa kwamba kabla ya mwezi Oktoba watakuwa wamelipwa. Naomba nieleze masikitiko yangu kwamba hadi leo hii hakuna aliyelipwa hata shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi, sasa Bunge linarudia.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mwongozo Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hakuna mwongozo nimeshasima tayari, kwa hiyo, naomba mstahimili hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuwashukuru wote ambao mmetoa michango yenu kwa siku ya leo, Mungu awabariki sana, lakini pia Mwenyezi Mungu aibariki Serikali yetu iweze kuyapokea na kuyafanyia kazi yale yote yenye tija kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo kwa vile shughuli yetu imefikia mwisho kwa siku hii ya leo, basi nalihakirisha Bunge hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 2 Novemba, 2016, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.39 Usiku Bunge lilihakirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 2 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*